Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Thelathini na Tano - Tarehe 28 Julai, 2004**

*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza ningependa kuwatambulisha wageni Wabunge kutoka Uingereza ambao wamekuja kututembelea katika ziara rasmi. Nitasema hivyo kwa Kingereza ili na wao wajue kwamba wanatambulishwa.

*I wish to recognize the presence in the gallery of a British Parliamentary CPA Delegation visiting Tanzania. (Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 325

**Michango ya Halmashauri kwa Ajili ya *LAPF***

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa hadi sasa zipo Halmashauri nyingi ambazo bado zinadaiwa fedha nyingi za michango ya kisheria ya *LAPF* kwa watumishi wengi wakiwemo wale waliofariki, wastaafu na waliopo kazini bado na kwa kuwa makato/michango hiyo inakatwa moja kwa moja huko Hazina.

Je, Serikali ina mikakati gani ya haraka ya kuhakikisha kwamba watumishi wanalipwa mafao yao hasa ndugu wa marehemu na wastaafu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa zipo Halmashauri nyingi ambazo bado zinadaiwa fedha nyingi za michango ya kisheria ya akiba ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa. Aidha, wapo pia watumishi waliofariki au kustaafu wanaodai malipo yao kutokana na Halmashauri husika kutowasilisha michango ya watumishi hao wakati wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, michango ya *LAPF* inatokana na makato ya asilimia 5 ya mishahara ya watumishi na asilimia 15 ya mishahara iliyochangwa na mwajiri. Fedha hizo zinatakiwa kuwasilishwa Mfuko wa *LAPF* siku 30 baada ya tarehe ya mwisho ya mwezi unaofuata. Kwa miaka ya nyuma hadi mwaka 2001 Halmashauri nyingi hazikuwa zinatuma fedha hizi na kujikuta zina malimbikizo makubwa ya fedha ambazo hazijawalishwa kwenye Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi. Kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha sheria Na. 6 ya mwaka 2000 ya Mfuko wa *LAPF,* mtumishi anayestaafu au kuachishwa kazi na hata kufariki dunia, mrithi wake anaweza tu kulipwa mafao yangu kama itathibitika kwamba michango yake imewasilishwa *LAPF.*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Julai, 2002 malimbikizo ya makato ya watumishi kutoka Halmashauri mbalimbali nchini yalikuwa yamefikia jumla ya shilingi bilioni 9.0. Ili kudhibiti malimbikizo haya yasiendelee kukua na pia kuhakikisha malimbikizo ya nyuma yanalipwa *LAPF* na Ofisi yangu imechukua hatua mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(a) Kuanzia mwezi Septemba, 2002 makato ya kisheria sasa yanakatwa na Hazina na kuwasilishwa *LAPF* moja kwa moja. Tangu wakati huo hatuna malimbikizo mapya ya makato hayo ya kisheria. *(Makofi)*

(b) Katika mwaka wa fedha 2002/2003, ofisi yangu iliingia mkataba na Halmashauri 85 zenye malimbikizo makubwa ya michango na kuzitaka kulipa madeni yao ifikapo tarehe 31 Desemba, 2003.

(c) Kuzitembelea Halmashauri mara kwa mara kwa lengo la kukusanya madeni na kuwaelimisha viongozi wa Halmashauri kuhusu umuhimu wa kulipa michango ya wafanyakazi kwa wakati ili kuwaondolea usumbufu wakati wa kudai mafao.

(d) Kuwachukua hatua za kinidhamu Wakurugenzi ili kuimarisha utendaji na udhibiti wa matumizi ya fedha za Halmashauri ukiwemo udhaifu katika uwasilishaji wa makato ya kisheria ya *LAPF.*

(e) Kufungua ofisi za Kanda za *LAPF* ili kurahisisha shughuli za Mfuko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchukuliwa kwa hatua hizo nilizozitaja, ukaguzi wa kina uliofanyika kwenye Halmashauri zote nchini hivi karibuni umethibitisha kuwepo bado kwa malimbikizo makubwa ya michango ya zamani katika Halmashauri mbalimbali yenye jumla ya shilingi bilioni 6.9 ilipofika tarehe 30 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii isiyoridhisha ofisi yangu iliwasilisha maombi maalum Wizara ya Fedha, ili kiasi hicho chote kikatwe moja kwa moja kutoka katika ruzuku wanazopewa Halmashauri zinazodaiwa. Lengo la ombi hili ni kuhakikisha kwamba tatizo hili kubwa linapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ofisi yangu imedhamiria kwa dhati kulimaliza kabisa tatizo la malimbikizo ya michango katika muda mfupi ujao ili mafao ya wanachama yaweze kulipwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kuwa kutokana na tatizo hili kupatiwa ufumbuzi watumishi wa Serikali za Mitaa wanaochangia Mfuko wa *LAPF* sasa wataweza kulipwa mafao yao bila matatizo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba sasa Halmashauri zimewekeana mkataba na Hazina ili makato haya yaanze kukatwa moja kwa moja na kwa kuwa Serikali sasa hivi inatoa ruzuku kwa Halmashauri kwa ajili ya upungufu wa vyanzo vya mapato ambavyo vilifutwa.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba ni wakati muafaka sasa kutamka rasmi kwamba mwezi fulani makato haya yote yatakuwa yamelipwa na Hazina ili kuondoka na madai haya ambayo sasa hivi ni kero kwa wafanyakazi wengi na kwa wasimamizi wa mirathi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kuanzia mwezi Septemba, 2002, Hazina imekuwa ikikata moja kwa moja makato ya watumishi na kuyapeleka moja kwa moja kwenye Mfuko wa *LAPF.* Kwa hiyo, kuanzia wakati huo hakuna nyongeza ya madeni.

Mheshimiwa Spika, pili, nikaeleza kwamba sasa tuko katika mazungumzo na Hazina na kwamba madeni hayo ya miaka ya nyuma yatakatwa mara moja yapelekwe *LAPF* kwa hiyo, hakutakuwa na suala madeni tena.

Na. 326

**Kufungua Ofisi za *LAPF* Kikanda**

**MHE. BERNARD K. MEMBE (k.n.y. MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* sasa hivi una wateja wengi kutokana na kuimarishwa kwa Serikali za Mitaa na kwa kuwa kutokana na wingi wa wateja hao taratibu za malipo kwa wastaafu wakati mwingine zimekuwa zikichelewa sana na kuwaathiri wastaafu.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufungua Ofisi za *LAPF* kikanda ili kupunguza msongamano wa wastaafu wa kuwasilisha madai yao kwenye Makao Makuu ya Ofisi hiyo?

(b) Kama Serikali imeona umuhimu huo, je, itaanzisha ofisi hizo lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa *(Local Authorities Provident Fund),* umeanzishwa kwa dhumuni moja kuu la kutoa malipo kwa wafanyakazi walioko kwenye utumishi wa Serikali za Mitaa na hususan baada ya mtumishi ama kustaafu, kuacha kazi, kuachishwa kazi au kufariki. Mfuko huu kwa sasa una wanachama zaidi ya 54,200. Kutokana na juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali za kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuongeza watumishi wa ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuboresha utendaji kazi wao, tunatarajia idadi ya wanachama wa Mfuko kuendelea kuongezeka.

Kutokana na mahitaji ya huduma unazozitoa na pia ongezeko la wanachama wake, Mfuko umeanza kuchukua hatua za kuimarisha taratibu za utoaji wa huduma zake ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi zake kikanda ambazo zitafanya shughuli zifuatazo:-

(i) Kuandikisha na kuweka orodha na kumbukumbu mbalimbali za wanachama wa Mfuko.

(ii) Kuandikisha waajiri wa wanachama na kuwaingiza katika mpango wa kuwalipia michango ya wafanyakazi wao.

(iii) Kukusanya michango ya wanachama.

(iv) Kulipa mafao kwa wanachama wa mfuko.

(v) Kuandaa na kutekeleza taratibu na mikakati mbalimbali zinazohusu uboreshaji wa huduma zitolewazo na Mfuko.

(b) Mheshimiwa Spika, mfuko utafungua ofisi zake katika kanda tano zifuatazo, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Kanda ya Mashariki ambayo ipo katika jengo la Kitega Uchumi la Mfuko lililopo Kijitonyama Jijini Dar es Salaam, imekwishafunguliwa na imekuwa ikitoa huduma zake kwa wanachama waliomo katika Kanda hiyo kuanzia Januari, 2004. Ofisi za Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini zitafunguliwa kati ya robo ya kwanza na ya pili ya mwaka wa fedha wa 2004/2005. Taratibu zinafanywa ili mfuko uweze kufungua ofisi za Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati katika mwaka wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na waajiri wa wanachama wa mfuko kuhakikisha kuwa makato na michango ya wanachama inawasilishwa kikamilifu na kwa wakati. Hatua hiyo itauwezesha mfuko kufikia malengo yake iliyojiwekea ya kutoa huduma zinazotarajiwa na wanachama wake na hivyo kujenga imani ya wanachama kuhusu umuhimu wa mfuko huu.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa hii mifuko inaonekana inaleta matatizo sana ya kuwahudumia wateja wake, ningependa Mheshimiwa Waziri, atueleze tatizo hasa liko wapi linalofanya mfuko kama wa *LAPF* ushindwe kutoa huduma kwa wateja wanaostaafu ikizingatiwa kwamba orodha ya wastaafu hawa wanajulikana, mishahara yao inajulikana, muda wao wa kustaafu unajulikana na taratibu za kuandaa malipo haya zinajulikana, ni kitu gani hasa kinachofanya mfuko huu ushindwe kutoa huduma? *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba Kanda tano ndiyo zitakazopata huduma hizi. Sasa Lindi na Mtwara kwa kweli kuwaambia waende kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, maana ni kuwapeleka Iringa. Mheshimiwa Waziri haioni umuhimu wa kuanzisha Kanda pale Lindi ili wananchi wa Mtwara, Lindi na Tunduru wapate huduma pale badala ya kutupeleka Iringa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bernard Membe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli yamekuwepo matatizo, kama nilivyosema matatizo mengi yamekuwa yakitokea kwa sababu waajiri kwa maana ya Halmashauri, walikuwa wanashindwa kutoa michango ya makato ambayo wamekata kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi kupeleka kwenye mfuko.

Kwa hiyo, hatua ya kwanza tuliyochukua ni kuhakikisha kwamba makato ya wanachama wa mfuko huu yanakwenda kule yanakotakiwa. Tumekwishachukua hatua, Hazina sasa inakata fedha hizo moja kwa moja. Tumekwishachukua hatua, madeni yote ya huko nyuma sasa yatakatwa moja kwa moja. Tunaamini kwamba baada ya kukamilisha hatua hiyo, hakutakuwa na matatizo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, Mikoa ya Lindi na Mtwara kuwa katika Nyanda ya Juu Kusini, Mikoa ya Lindi na Mtwara haitakuwa kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, itakuwa kwenye Kanda ya Pwani, maana yake Dar es Salaam. Kwa hiyo, kwa sasa hivi tumeangalia urahisi wa mawasiliano. Wakati tukiwa tayari, mfuko ukiwa na uwezo naamini kwamba ofisi za Kanda kwa ajili ya Mikoa hiyo, itafunguliwa. *(Makofi)*

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri nyingi hapa nchini wamekuwa wazembe kwa kutowasilisha makato hayo *LAPF* kama ilivyo ada na uzembe huu ni wa makusudi kwa sababu wanajua sheria na kanuni, je, ni Wakurugenzi wangapi ambao wamewajibishwa kwa kutopeleka fedha za wafanyakazi *LAPF?* Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli na kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kuwa wapo Wakurugenzi ambao walizembea na nikasema wamechukuliwa hatua, kwa bahati mbaya sasa hivi siwezi kutoa takwimu ila tutawasiliana baadaye nitampa takwimu hizo.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Lakini kabla maswali hayo hayajaulizwa niwajulishe Waheshimiwa Wabunge, kwamba kuna ratiba imetolewa asubuhi hii kwa makosa inayoonyesha kwamba tutajadili hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nasema

imetolewa kwa makosa kwa sababu nilikwisha idhinisha mabadiliko kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, amesafiri nje ya nchi kikazi. Kwa hiyo, tuliwabadilisha na Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Kwa hiyo, hoja ya kesho ni ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, wale waliokwisha kupata orodha tafadhali msizijali zilitolewa kwa makosa. Sasa maswali kwa Wizara hiyo.

Na. 327

**Wapiganaji wa Vita Kuu ya Pili**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Siha wapo wananchi ambao walipigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1939 hadi 1945 chini ya *King's African Rifles* akiwemo Mzee Elirehema Ngowo pamoja na wazee wenzake ambao wamekuwa wakilalamikia *pension* zao ambazo ziliahidiwa na Serikali ya Kikoloni ya Kiingereza ya kwamba watalipwa mpaka kufa.

(a) Je, Serikali ya Tanzania inalitambua tatizo hilo?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isiwalipe wananchi hao *pension* hizo kama ilivyoahidiwa hasa ikizingatiwa utumishi wao na kuwa wengi wao ni wazee na hali zao za maisha ni duni sana?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, swali lake, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu swali lake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafahamu kwamba baada ya kumalizika kwa Vita Kuu ya Pili ya Dunia na wapiganaji kurejea nyumbani, Serikali ya Uingereza iliunda chombo kinachoitwa *British Commonwealth Ex-Services League.*

Mheshimiwa Spika, chombo hiki pamoja na mambo mengine kilikuwa na jukumu la kuwaunganisha askari waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia, katika nchi mbalimbali zilizokua chini ya himaya ya Uingereza.

Mheshimiwa Spika, askari waliorejea vitani walianzisha chama chao cha *Tanganyika Legion* nacho kikawa wanachama wa *British Commonwealth Ex-Services League.* Serikali ya Uingereza imekuwa inatoa posho ya kujikimu kwa askari wa Tanzania. Posho hiyo ilikuwa inatumwa *Tanzania Legion and Clubs* na yenyewe ndiyo yenye utaratibu wa kuwatambua askari hao na kuwapatia posho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utaratibu huu pamekuwapo na matatizo mawili yafuatayo:-

(i) Chama cha *Tanzania Legion and Clubs* kimekumbwa na mgogoro wa uongozi uliotokana na madai ya ubadhirifu na uongozi mbaya uliodumu kwa miaka minne sasa.

(ii) Kutokana na mgogoro huo, *British Commonwealth Ex-Services League* imevunja uhusiano na *Tanzania Legion and Clubs* na wamesimamisha utoaji wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua matatizo yanayowapata wazee waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia na ndiyo maana Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tumekuwa tunafanya mazungumzo na *Tanzania Legion and Clubs* kwa lengo la kutatua mgogoro wa uongozi na pia kurejesha mahusiano na *British Commonwealth Ex-Services League.*

Mheshimiwa Spika, Wizara haina taarifa kuhusu pensheni ambayo inadaiwa kuahidiwa na Serikali ya Uingereza. Endapo pensheni hiyo iliahidiwa, mwenye wajibu wa kulipa ni Serikali ya Uingereza. Endapo Mheshimiwa Mbunge ama *Tanzania Legion and Clubs* wanayo hoja timilifu kuhusu pensheni hiyo, Serikali itakuwa tayari kuisilikiliza na kuiwasilisha kwa wahusika.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali na namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa hapa.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba Serikali imetambua kuhusu matatizo haya ya wastaafu ambao walipigana katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia na kwa kuwa Serikali ya Tanzania, ndiyo sasa inayowajibika kwa wananchi wa Tanzania na hasa tukizingatia kwamba hawa ni wazee ambao kwa kweli maisha yao sasa ni magumu hawajiwezi. Je, ni kwa nini Serikali isisaidie kama anavyosema kuingilia kati na kuhakikisha kwamba hao wananchi ambao wanataabika na wamekuwa wanauliziwa maswali mara kwa mara na Wabunge wenzangu hapa ndani, kwamba wanasaidia ili hali yao ya maisha walau iweze kuendelea vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kwamba inawajibika kwa wananchi wake ilichukua hatua za kuingilia kati mgogoro unaendelea kufukuta ndani ya *Tanzania Legion and Clubs* kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ilizikutanisha pande zote mbili upande wa Mzee Sykes na upande wa Mzee Lyatuu na kutafuta suluhu na tulifikia uamuzi wa kufanya ukaguzi wa mahesabu yote yametufanya tayari na hatua inayofuata ni mwezi ujazo wa nane kufanya mkutano wa kupata suluhu na kuchagua viongozi watakaokubalika na pande zote mbili ili kwa pamoja tuweze kuwasiliana na wenzetu kule Uingereza, kuwaza kurudisha mahusiano ili wapiganaji hawa waendelee hizi posho zao kama kawaida. Ni posho wala siyo pensheni. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES A. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa sababu wazee wengi ambao wanatakiwa kulipwa wengi wamekufa, je, mafao yatakapopatikana familia zao zitapewa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, kama ifuatavyo:-

Kwa kweli makubaliano ya *British Commonwealth Ex-Services League* na *Tanzania Legion and Clubs* na wengine katika nchi mbalimbali hayakuwa kulipa pensheni ambayo ingeweza kwenda kwenye urithi. Hii ni posho ili mradi yule askari wa zamani anaendelea kuishi basi katika hiyo *center* alipo aweze kuweza kucheza karata vizuri, kunywa soda yake vizuri kusahau machungu ya vita.

Kwa hiyo, ukishakufa ndiyo na kila kitu kimekufa. Kwa hiyo, hakuna atakayerithi ndiyo makubaliano hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 328

**Vijana wenye Vipaji vya Ufundi**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa hapa Tanzania wapo vijana mbalimbali wenye vipaji vya ubunifu wa kutengeneza *toys* za vifaa mbalimbali kama vile redio, *television,* trekta, *caterpillars* na kadhalika na kwa kuwa kutokana na ujuzi mzuri walionao ungeweza kuisaidia sekta husika kupata watalaam wazuri kutoka hapa hapa nchini kama vijana hao wangepewa kila msaada hasa wa kielimu ili kuendeleza vipaji hivyo na tukapata watalaamu wa hali ya juu kuliko kutafuta watalaam kutoka nje ambao hugharamiwa kwa fedha nyingi.

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo hilo?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwatafuta na kuwaweka pamoja kwa lengo la kuwaelimisha zaidi ili ujuzi na utaalamu huo usipotee?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inatambua na inayo taarifa ya vijana wengi wenye vipaji vya ubunifu katika maeneo mbalimbali na umuhimu wa kuwaendeleza vijana hao ili kuwa watalaamu wazuri na kulipunguzia Taifa gharama za kuajiri watalaam toka nje.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijitahidi kuwafahamu vijana wenye vipaji mbalimbali na uwezo wao kunzia mashuleni. Zipo shule zinazochukua vijana wenye vipaji maalum kwa lengo la kuendelea vipaji vyao. Aidha, kimeanzishwa kituo cha vijana wenye vipaji maalum eneo la Segerea, Wilaya ya Ilala kiitwacho *Tanzania Children Playing Centre* ambacho kina lengo la kuwaendeleza watoto na vijana kulingana na vipaji vyao ili waweze kutumia vizuri utaalam wao hapo baadaye. Hadi hivi sasa kituo hicho kimeandikisha na kinawaendeleza vijana 85. *(Makofi)*

Aidha, hivi sasa Serikali inaandaa programu ya vijana ya uzalishaji mali, uhamasishaji pamoja na kuwaelimisha vijana kuunda taasisi zao kisheria kwa lengo la kuhakikisha kwamba vijana wenye vipaji maalum wanakaa pamoja na kutumia vipaji vyao katika kujiletea maendeleo yao na ya Taifa kwa ujumla.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunipatia majibu mazuri. Lakini kuna swali moja naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Je, ni lini watoto hawa watapatiwa na wao nafasi ya kupelekwa nchi za nje kama vile China na nchi tofauti ambazo watoto wenzao kama hawa wako ili kuonana na wenzao na kubadilishana mawazo na kuweza kujifunza zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali zuri la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali, imeshaanza kuwakutanisha vijana wetu na vijana wa mataifa mengine na wiki ya pili ya mwezi ujao tunapeleka vijana Barcelona ambako watakutana na wenzao katika tamasha, tumefanya hivyo Algeria, Korea, Urusi, Ureno na hivi karibuni tunategemea baada ya Barcelona litafanyika hilo Namibia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kufanya hilo na si jambo geni na tupochagua, hatuchagui tu wa Bara, tunachukua pamoja na wa Visiwani ikiwemo na Zanzibar na Pemba. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa niliwahi kumletea picha Mheshimiwa Naibu Waziri za kijana mbunifu aliyetengeneza gari kwa kutumia mashine ya kukatia majani na hivi sasa ametengeneza puto kwa kutumia mashine hiyo hiyo, amekwama na turubai tu, je, Mheshimiwa Waziri atasaidia vipi vijana kama hao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mhehsimiwa Spika, ni kweli aliniletea picha hizo na mimi mwenyewe nilijitahidi kufika jimboni kwake Jang'ombe kumwona kijana yule kwa bahati mbaya hakuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara zetu za vijana kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tuna ushirikiano wa karibu mno. Ili tusionekane kwamba tunavuka mipaka basi alipitishie kule na sisi *Inshallah* tutashirikiana na wenzetu kumsaidia. *(Makofi)*

Na. 329

**Fedha za Mpango wa Maendeleo Mkoa wa Shinyanga**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2003/2004 Mkoa wa Shinyanga ulipewa mgao mdogo wa fedha za Mpango wa Maendeleo ikilinganishwa na Mikoa mingine.

(a) Je, utaratibu wa mgao wa fedha hizo unazingatia vigezo gani?

(b) Je, Mkoa wa Shinyanga unachangia kiasi gani katika Pato la Taifa *(GDP)?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 Serikali ilizingatia mambo yafuatayo wakati wa kugawa fedha za maendeleo kwenda Mikoani.

(i) Miradi inayoendelea ilipewa kipaumbele katika ugawaji wa fedha za maendeleo ili iweze kukamilishwa.

(ii) Miradi mipya ya maendeleo iliyoanzishwa na Serikali kwa kushirikiana na wafadhili ilichangiwa fedha *(counterpart funds)* na Serikali kulingana na makubaliano ya mikataba ya kuanzisha miradi hiyo.

(iii) Serikali Kuu ilitenga fedha kwa ajili ya baadhi ya shughuli za maendeleo ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja za Wabunge wakati wa Kikao cha Bajeti cha mwaka 2003/2004, Serikali katika mwaka 2003/2004 ilikamilisha utafiti *(study)* wa mfumo bora utakaotumika wa kugawa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa Halmashauri za Miji na Wilaya nchini. Matokeo ya utafiti huu yameiwezesha Serikali kuwa na utaratibu bora wa kugawa fedha za maendeleo na pia fedha za kawaida. Utaratibu huu umeanza kutumika kwa awamu katika mwaka huu wa fedha 2004/2005 kwa kuanza na sekta za elimu na sekta ya Afya. Vigezo vilivyotumika kugawa fedha za ruzuku katika sekta hizo ni elimu ya msingi, idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule na sekta ya afya, vigezo vilivyotumika ni idadi ya watu ambayo ilipewa uzito wa 70%, viashiria vya umaskini ilipewa uzito wa 10%, kiwango cha vifo vya watoto chini ya miaka 5 ilipewa uzito wa 10% na umbali kutoka hospitali ya Wilaya hadi Wilayani ilipewa uzito wa 10%.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilitumia mfumo huu kugawa fedha za ruzuku za maendeleo kwenda Wilayani kuanzia mwaka 2004/2004. Mfumo huu mpya wa kugawa ruzuku kwa Halmashauri za Miji na Wilaya ni bora na wa uwazi zaidi kama unavyotumika katika nchi mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na Uganda, Kenya, India, Brazil, Philippines na Indonesia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Mkoa wa Shinyanga ulitengewa jumla ya shilingi milioni 500 fedha za ndani kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kiasi cha fedha za kutoka nje hakikuonyeshwa katika kitabu cha Bajeti kwa sababu wakati wa maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2003/2004 kumbukumbu za misaada ya Wahisani hazikuwepo. Kwa sasa inafahamika kwamba baadhi ya wahisani hupeleka fedha zao moja kwa moja kwenye Halmashauri kwa utekelezaji wa miradi yao bila kufuata utaratibu wa mfumo wa Bajeti ya Serikali. Aidha, Serikali inaendelea kuwasiliana na Wafadhili na Wahisani kuhakikisha kwamba misaada yao inapitia katika mfumo wa Bajeti ya Serikali.

Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida mwaka 2003/2004, Mkoa wa Shinyanga ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 19.1. Kiasi hiki kiliufanya Mkoa wa Shinyanga uwa wa nne Kitaifa kwa mgao wa Fedha za Matumizi ya Kawaida baada ya Mikoa ya Mwanza, Mbeya na Kilimanjaro. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu takwimu za Pato la Taifa yaani *GDP,* Mkoa wa Shinyanga ulichangia asilimia 7.79 katika Pato la Taifa mwaka 2002. Aidha, Mikoa ambayo ilichangia asilimia kubwa zaidi ya Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa wa Dar es Salaam ambao ulichangia asilimia 16.93 na Mkoa wa Mwanza ambao ulichangia asilimia 9.74.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Pamoja na mfumo mpya ambao ameutaja Mheshimiwa Naibu Waziri, je, anakumbuka kwamba kwa mwaka huu Mkoa wa Shinyanga katika mgao wa fedha umepewa shilingi bilioni 1.9, Mkoa wa Mwanza shilingi bilioni tano, Morogoro shilingi bilioni 3.5, je, huu ndio mgao wa mfumo mpya ambao ameutaja? Kama ni hivyo, haoni kwamba baadhi ya Mikoa itaendelea kubaki nyuma na mingine itapiga hatua haraka zaidi kimaendeleo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli takwimu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge ni kama zilivyoandikwa ukurasa wa 17 katika Kitabu cha Nne ukurasa wa 17 namba za kirumi ambayo ni kiambatanisho Na.2.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga ulipata shilingi milioni 527 mwaka 2003/2004 na mwaka 2004/2005 imetengewa shilingi bilioni 1.6. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 1.38 ambalo ni ongezeko la asilimia 260. Kwa hiyo, kutokana na utaratibu huu mpya ndio maana Shinyanga imepata ongezeko la fedha kiasi cha asilimia 260. Kuna Wilaya ambazo zilikuwa zimepata hela nyingi zaidi mwaka jana, zimepunguzwa. Ukiangalia kwenye jedwali hili, Mkoa wa Arusha ulikuwa unapata shilingi bilioni 1.6, lakini mwaka 2004/2005 umepata shilingi bilioni 1.4. Kwa hiyo, kutokana na utaratibu huu mpya ndio maana Shinyanga imepata fedha nyingi zaidi. Ukiangalia hata katika Matumizi ya Kawaida Shinyanga imepata hela nyingi zaidi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea jibu zuri la Naibu Waziri kwa kusisitiza kwamba Serikali kimsingi na kwa utendaji wa mwaka huu wa fedha, imetekeleza matakwa ya Bunge hapa kwamba tuangalie uwiano katika kugawa *resources* za Taifa katika Mikoa. Ndivyo tulivyofanya mwaka huu.

Mwaka huu Wizara zilizokuwa zinapata zaidi zimepunguziwa, kwa mara ya kwanza. Lakini kwa sababu huwezi kupunguza ghafla, kwa sababu kuna miradi ilikuwa inaendelea, huwezi kuisimamisha kwa sababu tu umeanza *formula.* Lazima ufanye kwa mtiririko ambao miradi iliyokuwa inachukua fedha nyingi zaidi inakuwa *phased out,* taratibu inakwisha. La sivyo, tutasimamisha maendeleo kwenye Mikoa mingine na kusababisha tena malalamiko upya. Kwa hiyo, nia yangu ni kwamba ili utaratibu huu uweze kutumika vizuri kabisa mia kwa mia, itachukua miaka miwili, mitatu. Tunakwenda *in phases.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza kabisa kwamba *formula* hii ndiyo pekee tutakayoweza kuitumia. Kwa Shinyanga ningependa ieleweke kwamba fedha zilizoingia Shinyanga mwaka 2003 na mwaka 2004, sio hizo zilizoko kwenye vitabu tu, zipo fedha kwa mfano kwenye vitabu, ziko fedha hazionyeshwi fedha za barabara zinazotengenezwa kwenye Mkoa ule. Kwa mfano, mwaka 2003 Japan walipeleka zaidi

ya shilingi bilioni moja katika Mkoa wa Shinyanga katika elimu licha ya zile ambazo ziko kwenye kitabu cha Bajeti cha Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kuna nyingine *over one billion* zilikwenda kule kusaidia Elimu ya Msingi na Barabara na Maji na mambo mengine mengi ambayo hayako kwenye vitabu. Kwa hiyo, ningependa mtuamini kwa mara ya mwisho, msirudie tena kwamba tuko kazini, tupeni muda wa kukamilisha hii kazi mliyotupa. *(Makofi)*

Na. 330

**Malipo ya Uzeeni**

**MHE. MUTTAMWEGA P. MGAYWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wazee ni hazina ya Taifa kwa busara zao na kwa kuwa Wazee wastaafu wanahitaji matunzo kutokana na uwajibikaji wao kwa Taifa:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwalipa wastaafu malipo mazuri ya uzeeni ili waweze kuishi maisha bora yasiyo ya kujutia uwajibikaji wao kwa Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, kuwa wazee ni hazina kubwa ya Taifa kwa busara zao na kwamba wanahitaji matunzo kutokana na uwajibikaji wao kwa Taifa. Ndio maana Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwaenzi, mfano kuwasilisha Bungeni Miswada mbalimbali ya kurekebisha sheria ya pensheni.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma yaani *Public Service Retirement Benefit Act No.2* ambayo Watumishi wa Serikali walianza kuchangia mafao yao ya kustaafu katika Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma. Mfuko huo licha ya kuwapa haki zaidi watumishi wastaafu, utawawezesha kuongeza pensheni zao kutokana na michango yao na ya waajiri wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya marekebisho ya viinua mgongo na pensheni kama ifuatavyo:-

Kwanza, mwaka 1998 Bunge lilikubaliana na Serikali Kurekebisha kiwango cha limbikizo la pensheni kutoka 1/600 na kuwa 1/540 ya mishahara ya mtumishi katika utumishi wake. Hatua hii ina maana kwamba mtumishi aliyestaafu badala ya kupata 1/600 ya mishahara ya utumishi wake wote, sasa atapata 1/540 ya mishahara yake yote aliyopata katika utumishi wake.

Pili, kima cha chini cha pensheni kiliongezwa kwa awamu kutoka shilingi 2,000/= kwa mwezi mwaka 1994 na kuwa shilingi 20,077/= kwa mwezi mwaka 2003/2004.

Tatu, wastaafu wote ambao walichukua pensheni zao kwa mkupuo wamerejeshwa katika daftari la wanaolipwa pensheni na hivyo kurejeshwa tena katika malipo ya pensheni ya kila mwezi. Kama nilivyosema katika hotuba ya Bajeti ya Serikali, wastaafu hawa wataanza kulipwa pensheni mwezi Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yote haya yamelenga kuboresha maisha ya wastaafu kufuatia uwajibikaji wao kwa Taifa. Pamoja na hayo, kwa kutambua umuhimu wa wazee, Serikali na asasi zake zimekuwa zikiwatumia baadhi ya wazee katika shughuli za ushauri popote walipo na kwa masuala waliyo na ujuzi nayo. Serikali itaendelea kuwathamini wazee kadri itakavyowahitaji. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Katiba yetu inataja wazi kwamba nchi yetu ni ya wakulima na wafanyakazi na kwa kuwa sekta ya kilimo inachangia pato kubwa sana katika Taifa letu.

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kufanya utaratibu maalum ya kuwalipa wakulima wanapozeeka na kushindwa kufanya kazi na wao waingizwe katika utaratibu wa kupata malipo ya uzeeni? *(Kicheko/Makofi)*

Pili, kama tunaona ni busara kufanya hivyo, tutaanza lini? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna nchi duniani ambazo zinalipa pensheni kwa kila mtu. Zinalipa wakulima na hata wachungaji. Lakini kwa bahati mbaya sana Tanzania haijafika hatua hiyo kiuchumi ya kuweza kulipa kila mtu. Kwa sasa tunajitahidi kulipa wafanyakazi, lakini *inshallah,* mbele ya safari labda wajukuu wetu wanaweza wakafanya hilo analotaka Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa. *(Kicheko)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa wote wanatakiwa kuenziwa katika uzee, wakulima, wafanyakazi na wafugaji na kila mtu kwa aina yake na kwa kuwa kuna mifuko mingi ya pensheni kwa ajili ya wafanyakazi wa Mashirika mbalimbali.

Je, Serikali inaonaje kuanzisha mfuko wa namna hiyo kwa ajili ya wakulima na wafugaji na watu wengine ili wanapokosa nguvu waweze kupata pensheni yao katika mifuko hiyo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imechukua hatua ya kwanza kwa Mfuko wa Afya ambao umeanza kuenea katika Wilaya nyingi. Lakini mifuko ya namna hii, iwe ni huo wa Afya au aina hiyo anayotaja Mheshimiwa Mbunge, ni mifuko ambayo inachangiwa na wahusika. Kwa hiyo, kwa sababu wakulima wengi wetu hawana hela za kuchangia kila mwezi, hela zao ni za msimu kutokana na ahadi yetu ya kilimo, basi tumeanza na hilo la afya tuone angalau wapone, wawe na afya tukifikiria

hayo mengine. Mpaka sasa hivi hatujafanikiwa, kwa hiyo, tunaendelea, tuko mbioni. *(Kicheko)*

Na.331

***The Land Bank of Tanzania***

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1948 Serikali ilianzisha Benki ya kuwasaidia wakulima iliyojulikana kama *The Land Bank of Tanzania* na kwa kuwa Benki hiyo ilikuwa ikitoa mikopo kwa wananchi wa Tanganyika wakati huo na kwa kuwa dhamana ya mikopo hiyo ilikuwa ni Hati ya Ardhi na muda wa kulipa deni hilo ulikuwa ni miaka isiyozidi thelathini:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa muda wa miaka mitatu uliowekwa na Serikali wa kurejesha mikopo na riba toka mfuko wa pembejeo hautoshi, hasa kwa mazao kama Chai, Kahawa, Miti ya Mbao, Ufugaji na kadhalika?

(b) Kwa kuwa Serikali wakati huo ilianzisha Benki hiyo ili kutekeleza malengo yake na kwa kuwa si rahisi kwa wakulima wadogo Vijijini kupata mikopo toka kwenye Benki kubwa za nje pamoja na ukweli kuwa wanayo ardhi, je, ni lini Serikali itaanzisha tena *The Land Bank of Tanzania* au chombo kama hicho kitakachowasaidia wakulima wadogo kwa kuwapa mikopo ya muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba katika mwaka 1948, Serikali ya Kikoloni ilianzisha *The Land Bank of Tanganyika* chini ya Sheria ya *The Land Bank Ordinance 1947.* Benki hiyo ilikuwa ikitoa mikopo kwa wakulima wakubwa, wengi wao walikuwa walowezi kwa dhamana ya ardhi. Mikopo iliyotolewa ilikuwa kwa ajili ya kununulia ardhi, mazao na pembejeo kwa ajili ya kujengea nyumba. Kati ya mwaka 1947 na mwaka 1960 asilimia 40 ya mikopo ya shilingi milioni 60 ilitolewa na ilitumiwa kuendeleza ardhi. Masharti ya Benki hiyo yalikuwa magumu na yalisahau kabisa wakulima wadogo wa Kiafrika. Benki hiyo ilivunjwa mwaka 1961.

Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ulioanzishwa kwa sheria ya mwaka 1994, unatoa mikopo kwa shughuli zinazofanyika katika msimu mmoja na mkopaji anatakiwa kurejesha mkopo aliochukua katika miezi 12.

Mikopo kwa ajili ya kukarabati matrekta ilitakiwa irejeshwe katika miezi 18 wakati mikopo ya kununulia matrekta mapya inatakiwa irejeshwe katika miezi 36. Muda huo umewekwa kwa kuzingatia urefu wa maisha ya matrekta yaani *economic life* na

uwezo wa matrekta hayo kuzalisha mapato ya kumwezesha mkopaji kurejesha mkopo na kuhudumia trekta ipasavyo. Mfuko wa Pembejeo hautoi mikopo kwa ajili ya kilimo cha mazao yakiwemo Chai, Kahawa, Miti ya Mbao au kwa ajili ya ufugaji. Kwa hali hiyo, muda wa miezi 12 hadi 36 unatosha kurejesha mikopo inayotakiwa kutolewe na Mfuko wa Pembejeo wa Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji katika hotuba yake ya Bajeti mwaka 2004/2005, mipango ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo inashughulikiwa na Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania na itaanzishwa mara maandalizi yatakapokamilika.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaonyesha kwamba mpaka sasa hatuna Benki inayoweza kuwakopesha wakulima hasa wa mazao ya biashara kama Chai, Kahawa na kadhalika, ningependa Mheshimiwa Naibu Waziri anieleze kwamba hiyo Benki inayotarajiwa kuanza inaanza lini ili kusaidia wakulima ambao kwa kweli kwa sasa hawana namna yoyote ile ya kuwasaidia kupata mikopo?

Pili, nataka kuuliza kwamba kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha Benki hii na kwa kuwa tayari ipo Benki ndani ya nchi hii inayoitwa *NMB,* ni juhudi gani ambazo zinafanywa ili kuziunganisha Benki hizi ziweze kufanyakazi kwa pamoja ukizingatia kwamba *NMB* tayari ina mtandao katika nchi nzima? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli hatuna Benki sasa inayowasaidia wakulima wadogo wadogo. Lakini mipango inafanywa na tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, itakapokamilika, Benki itaanza kazi mara moja.

Pili, Benki ya *NMB* haikuanzishwa kwa lengo hasa la kutekeleza shughuli za *Land Bank,* ndiyo maana mkazo uko katika kuanza kitu kipya badala ya kubadilisha *NMB* ifanye kazi ya *Land Bank.* Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira mpaka hapo utakapopatikana ufumbuzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo, kuna nafasi ya swali moja. Nampa nafasi Mheshimiwa Venance Mwamoto, nilikuona mwanzo.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa zoezi la kutoa ruzuku katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini lilifanyika na lilileta matatizo na kwa kuwa pamoja na Serikali kuwa na nia nzuri ya kuanzisha Benki ya Wakulima bado kuna uwezekano tukafanya vibaya, je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuzunguka na kuongea na wadau na hata kwenda nchi za jirani kuona wenzetu wanafanya nini ili tusifanye makosa ya kuendelea kuwatesa wakulima ili waweze kupata mkopo na kuweza kulima?

**SPIKA:** Dhamana ya Mabenki iko Wizara ya Fedha. Ningependa swali hili lijibiwe na Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, maandalizi yanafanywa na hatutaki kufanya makosa kama Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri. Kati ya maandalizi hayo ni kujifunza wenzetu wenye Benki za namna hiyo wanafanya nini. Hivi karibuni mwenzangu jirani yangu hapa Waziri wa Ushirika na Masoko, alikwenda Afrika ya Kusini kujifunza kwa mfano Benki yao kule inayoitwa *Land Bank* ambayo inakopesha kilimo.

Mheshimiwa Spika, siri kubwa katika ukopeshaji wa kilimo ni kwamba kilimo hakikopeshwi kama biashara nyingine. Kwa kawaida kinakopeshwa kwa masharti maalum kwa sababu biashara ya kilimo hailipi kwa kulipua, inachukua muda mrefu kulipa. Kwa hiyo, inakopesha kwa utaratibu maalum na ndio maana swali lililokuwa limeulizwa mapema na Mheshimiwa Benito Malangalila, ni kwamba *NMB* ya sasa hata ijayo hata kama itakuwa na nia ya kukopesha kilimo, haitawezekana kwa ufanisi sana. wa sababu *NMB* itaendeshwa Kibiashara ingawa itakuwa ni Benki ya wanyonge.

Kwa hiyo, naomba mtupe muda, jambo hili tumeshalizungumza wakati wa Bajeti hapa, tunalifanyia kazi *seriously* kabisa na tumaini langu ni kwamba tutafika mahali tutaleta mapendekezo namna tunavyodhani kazi hiyo ingefanywa.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Lydia Boma.

Na. 332

**Bei ya Korosho**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na hali ya kupanda na kushuka kwa bei ya korosho na kwa kuwa bei inaposhuka ni hasara kwa mkulima na kupanda kwa bei ni faida kwao na Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, kwa wale wakulima wanaozalisha korosho bora kwa nini wasifidiwe na mfuko maalum pale bei ya korosho inaposhuka?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula alipokuwa akijibu Swali Na.393 hapo tarehe 6 Agosti, 2003 alinishauri niulize upya suala linalohusiana na *STABEX* ili lipatiwe majibu sahihi, je, Serikali italeta lini kwa upendeleo Mfuko wa *STABEX* kwa ajili ya zao la korosho kama ilivyo kwa mazao mengine ya Pamba, Chai na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wakulima wanaozalisha korosho bora hawafidiwi pale bei ya korosho inaposhuka kwa sababu Serikali haina mfuko maalum uliowekwa kwa madhumuni hayo. Hata hivyo tathmini ya bei ya zao la korosho nchini katika miaka ya hivi karibuni inaweza kuwa bei hizo zinaimarika zikilinganishwa na zilivyokuwa miaka ya nyuma. Kwa mfano, katika msimu wa mwaka 2002/2003 bei ya kilo moja ya korosho Daraja la Kwanza iliongezeka kutoka shilingi 300/= kwa kilo mwaka 2001/2002 hadi shilingi 425/=. Katika msimu wa mwaka 2003/2004 bei iliendelea kuongezeka hadi shilingi 650/= kwa kilo moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, bei ya korosho Daraja la Pili iliongezeka kutoka shilingi 250/= hadi shilingi 300/= kwa kilo moja katika msimu wa mwaka 2002/2003 na kuongezeka hadi shilingi 450/= katika msimu wa mwaka 2003/2004.

(b) Serikali haina mpango wa kuleta Mfuko wa *STABEX* kwa ajili ya zao la korosho au zao lingine lolote kwa sababu zifuatazo:-

(i) Utaratibu wa Mfuko wa *STABEX* ulianzishwa na nchi za Jumuiya ya Ulaya *(EU)* kwa ajili ya kupunguza athari zinazotokana na kushuka kwa mapato ya fedha za kigeni katika nchi za *Africa Caribean Pacific* kwa baadhi ya mazao yaliyokuwa yakiuzwa katika Jumuiya hiyo.

Kwa kuwa korosho iliyokuwa inazalishwa nchini ilikuwa haiuzwi kwenye Jumuiya ya Ulaya, zao la Korosho halikuingizwa katika utaratibu wa *STABEX.*

(ii) Zao la Korosho haliwezi kufaidika na Mfuko wa *STABEX* kwa sababu Jumuiya ya Ulaya ilikwishafuta utaratibu wa *STABEX* kwa mazao yote kuanzia mwaka 2002.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Mkoa wa Mtwara zao la korosho lilishuka kutokana na ukame kwa misimu mitatu mfululizo, je, Serikali inawasaidiaje wakulima hawa?

Pili, kwa kuwa Serikali mara nyingi imekuwa inasema ziko fedha kwa ajili ya wakulima na kwamba fedha hizo zipo, wakulima hawa wadogo wadogo wakiwemo wanawake na vijana, wafanye nini sasa ili waweze kuzipata fedha hizo kirahisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na ukame katika Mkoa wa Mtwara, lakini haujakuwa kwa kiasi cha kuwa hapakuwepo na korosho kabisa. Korosho zipo ingawa zimepungua na kama nilivyosema

katika jibu langu, ni kuwa bei nayo imepanda na hiyo haikuwa kizuizi kwa watu wengine kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, tulipowasaidia watu hawa ni kuwasaidia huduma za ugani, vile vile kuwasaidia watu hawa mipango ya kusindika zao hili, badala ya kuuza *raw* au isiyobanguliwa maganda, tunawasaidia kuwapa utaalam wa kuanzisha shughuli za kusindika mazao badala ya kuuza kwa maganda.

Pili, fedha za wakulima wadogo wadogo zipo kwa vijana. Kwanza kupitia Halmashauri za Wilaya zina mifuko hiyo ya *ten percent* kwa vijana na wanawake na vile vile Wizara ya Vijana nayo inatoa misaada hii. Ninachoomba turudi kwenye Halmashauri zetu kuhamasisha matumizi ya fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya vijana wadogo. Bado zaidi ya hapo kuna Mfuko wa Pembejeo. Kuna *Stockist* wamekopeshwa na kwa kutumia fedha hiyo, pembejeo zimewafikia wakulima wa korosho.

**SPIKA:** Bado nina maswali mawili ya msingi, kwa hiyo, maswali ya nyongeza hayawezi kupata nafasi. Maswali kwa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Henry Shekiffu.

Na. 333

**Umeme Makao Makuu ya Tarafa ya Mlola**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2002 Serikali kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* lilifanya tathmini ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Tarafa ya Mlola Wilayani Lushoto na kwa kuwa tathmini hiyo imeshakamilika na gharama za kazi hiyo sasa inafahamika:-

Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa Serikali itatekeleza azma yake ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Tarafa hiyo vikiwemo Vijiji vya Lwandai, Kihitu, Kigurunde, Mazashai, Ungo, Makole, Kwekanga na Kilole?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kufikisha umeme Vijijini ili kuharakisha maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo uhaba wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Umeme ndio kikwazo kikubwa cha azma hii njema ya Serikali. Hivyo Serikali itatekeleza azma yake ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Tarafa ya Mlola ikiwemo Vijiji vya Lwandai, Kihutu, Kigurunde, Mazashai, Ungo, Makole, Kwekanga na Kilole pindi itakapopata fedha kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Spika, tathmini aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, ndiyo imebaini kuwa gharama za mradi anazozungumzia zinakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi milioni 490. Serikali inafanya jitihada ya kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza kazi hii.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Ninalo swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa umeme ni kichocheo muhimu kwa maendeleo ya nchi na wananchi wengi wanaishi Vijijini, ni asilimia kumi tu ya wananchi wetu ndio wanapata umeme na kwa bahati mbaya umeme haukuwekwa katika sekta muhimu katika mpango wa kupambana na umaskini, je, Serikali inakubaliana nami kwamba umefika wakati sekta ya umeme iwekwe katika vipaumbele muhimu vya kupambana na umaskini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba umeme ni kichocheo kikubwa cha maendeleo na umeme unahitajika Vijijini ambapo wananchi wengi wanahitaji kusukuma maendeleo yao wenyewe. Serikali sasa hivi inaangalia ule mpango wa kupunguza umasikini *PSRP* na kuona ni sekta gani nyingine ziongezwe pale, kwa mfano kuna sekta yetu ya Madini ambayo nayo inagusia wananchi walio wengi na sekta hiyo ya umeme vile vile ni namna gani inaweza kuingizwa katika kundi la zile sekta ambazo zimepewa kipaumbele katika kupambana na umaskini.

Na.334

**Fidia kwa Wananchi wa Maeneo ya Mgodi wa *Geita Gold Mining***

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa bado wapo wananchi wachache ambao nyumba, mazao na mashamba yao yalichukuliwa na wamiliki/wawekezaji wa mgodi wa *Geita Gold Mine Limited* lakini jambo la kushangaza ni kwamba hadi leo wananchi hao hawajalipwa fidia pamoja na Serikali kuunda Tume mbalimbali:-

Je, Serikali inasema nini juu ya fidia ya wananchi hao ambao wanapata taabu ya kusubiri malipo yao ambayo hatma yake hawaijui?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa muda mrefu baadhi ya wananchi waliokuwa wakikaa kwenye maeneo ya mgodi wa *Geita Gold Mining Limited* walikuwa hawajalipwa fidia kwa mali zao. Hata hivyo kwa kuzingatia kilio cha wananchi hao, kwa kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge wao, kikao cha wazee wa Geita na Mheshimiwa

Waziri Mkuu kilifanyika mwezi Novemba, 2003 na ziara ya Waziri Mkuu, Geita ilifanyika mwezi Januari, 2004. Serikali imetoa fedha na fidia zimelipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malipo yamefanyika kama ifuatavyo:-

Wananchi 106 walikuwa hawajalipwa kabisa fidia, hivi sasa wamelipwa jumla ya shilingi 89,607,901.75. Wananchi 257 walikuwa hawajalipwa malipo ya kutakiana kheri, wananchi hao wamelipwa jumla ya shilingi 344,761,303.80. Wananchi 164 wamebainika kwamba walipunjwa fidia za mali zao, nao wamelipwa jumla ya shilingi 130,356,978.90. Wananchi 36 walikuwa na hundi za Halmashauri ya Wilaya ya Geita ambazo baadaye zilichacha. Hundi mpya zenye jumla ya shilingi 9,943,038.25 zimetolewa na kulipwa.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuweza kujali matatizo ya wananchi wake na kuyafuatilia kwa karibu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuishukuru Serikali na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pili kwa kuwa mgodi wa Geita unakuwa siku hadi siku na umepanua shughuli zake kiasi kwamba vijiji vya Magema, Katoma, Katumaini na Namalembo, Nyakabare na Malimpya zimekuwa katika tatizo la kupata vumbi ambalo linatokana na mgodi huo na wananchi wake kuwa wanapanja kila siku, je, Serikali inasemaje kuwafidia hawa wananchi wa vijiji hivi ili waondokane na vumbi hilo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kazi ya kuchimba madini inagusa mazingira na katika kupanua migodi tunaangalia sana *environmental impact* ya shughuli hiyo. Imetokea Bulyanhulu na tumekwenda kuangalia, tumepeleka wataalam kuona ni athari gani zinatokea na tukashauriana na wenye mgodi ni njia gani tuzichukue ili kupunguza athari kwa wale wanaoishi sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili tupeleke wataalamu wetu wakapime ni kiasi gani au kiwango gani cha athari inatokana na upanuzi wa mgodi huo ili tupate maendeleo lakini vile vile tulinde mazingira yetu na afya za wananchi wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Sasa matangazo ya vikao vya leo.

Kamati mbili za Kudumu zimepangiwa kufanya vikao vyake. Ya kwanza ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dr. John Malecela, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5.00 asubuhi kwenye Ukumbi Namba 231 ghorofa ya pili, Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Kamati nyingine ni ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anaomba Wajumbe wakutane saa 5.00 asubuhi hii kwenye chumba cha Kamati Namba 227 ghorofa hiyo hiyo ya pili.

Vikao vingine ni cha Umoja wa Wabunge Wanawake, Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake anaomba Wabunge Wanawake wote wakutane leo saa 7.00 mchana katika viwanja tunavyofanyia burudani kwa kawaida pale nyuma ya jengo la Utawala.

Halafu kikao cha mwisho ni cha Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 11.00 jioni leo ili kukutana na Wabunge wa Afrika Mashariki katika Ukumbi Namba 227 ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo, Katibu tunaendelea na *Order Paper.*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Kuhusu unafuu wa Kodi unaotolewa chini ya Sheria ya Kodi ya Mwaka 2004 Kipengele Kihusucho Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, niliahidi kutoa ufafanuzi rasmi hapa Bungeni kuhusu unafuu wa kodi unaotolewa chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwa wale wanaochangia mfuko wa elimu ulio chini ya Wizara hiyo na shughuli nyinginezo za maendeleo ya wananchi. Naomba sasa nitimize ahadi hiyo, kwa kuelezea utaratibu wa kisheria kuhusu unafuu wa kodi kwa watu binafsi, makampuni na asasi zitakazochangia shughuli za uendeshaji wa elimu nchini na maelezo yangu yatagusa pia unafuu unaotolewa kwa kuchangia shughuli nyingine za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kinatoa unafuu wa kodi kwa michango itakayotolewa kwa assasi za hisani. Yaani *Charitable Organizations,* miradi ya maendeleo ya jamii, au uendelezaji wa elimu kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001.

Kwa mujibu wa kifungu hiki cha Sheria ya Kodi ya Mapato mtu, kampuni au assasi itapata unafuu wa kodi wa hadi asilimia 2 kwa mwaka wa mapato husika akichangia shughuli za maendeleo ya elimu au miradi mingine ya maendeleo ya wananchi wakati wa kukokotoa mapato yake yanayostahili kutozwa kodi. Lakini akichangia mfuko wa elimu ulioanzishwa na Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001 atapata unafuu unaozidi hata hiyo asilimia mbili ya mapato.

Mheshimiwa Spika, unafuu huu unatolewa kwa michango iliyotolewa kwa assasi ambazo zinakidhi masharti ya kifungu cha 64 kifungu kidogo cha 8 cha Sheria hiyo. Masharti hayo ni asasi hiyo iwe na madhumuni ya kupunguza umaskini na hali ngumu ya maisha kwa jamii, kuendeleza elimu, kutoa huduma za afya, elimu, maji na barabara.

Aidha, asasi husika budi iwe na hati ya Kamishna wa Kodi ya Mapato inayotolewa chini ya kifungu cha 131 cha Sheria ya Kodi ya Mapato inayothibitisha kuwa hiyo ni assasi hisani au ya kidini.

Mheshimiwa Spika, ili mchangiaji wa maendeleo ya jamii kwa kupitia assasi hisani, assasi za kidini, mfuko wa elimu ulioanzishwa chini ya Sheria ya Mfuko wa elimu ya mwaka 2001 au maendeleo ya jamii kwa ujumla hawezi kupata unafuu wa kodi kutokana na michango aliyochangia, mhisani mwenye azma hiyo ni muhimu kuhakikisha kuwa anapata ushahidi wa kati wa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ushahidi huo waweza kuwa *receipt* ya kupokea fedha iliyotolewa na mfuko aliyouchangia au hati ya kupokea mizigo iliyotolewa na mfuko aliouchangia kwa mfano saruji yaani hiyo ni *delivery note of goods received note.*

Ushahidi wa kupokewa kwa mchango utategemea hali halisi ya mahali mchango ulipofanywa mfano muhtasari wa kikao cha kuchangisha michango ambao unaonyesha pamoja na mambo mengine, maendeleo ya mradi husika na majina ya watu waliochangia na kiasi alichochangia kila mmoja wao, au barua toka kwa Kamati inayosimamia mradi. Kitu cha msingi ni mhisani aliyechangia maendeleo ya jamii atatakiwa kutoa ushahidi wa kumridhisha Kamishna wa Kodi ya Mapato kuwa ni kweli alichangia mradi husika ili nafasi hiyo isitumike vibaya na wale wanaotaka kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, natumaini kuwa kwa kauli hii wenye nia na moyo wa ukarimu watatumia ufafanuzi huu kutoa misaada kwa mfuko wa elimu wa taifa kama inavyotegemewa na Serikali na pia kwa miradi mingine ya maendeleo ya wananchi hasa katika sekta ya elimu, maji, afya na barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kueleza kuwa unafuu unaotolewa chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 ni haki ya aliyetoa mchango. Hata hivyo, mfadhili halazimiki kudai unafuu huo. Kwa hiyo, ni hiari yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, kauli imetolewa, haina mjadala, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2004/2005

### Ofisi ya Makamu wa Rais

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likae kama Kamati lipokee, lijadili na likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Kwanza kabisa naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani, Zanzibar na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Nawapongeza pia Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge na Mheshimiwa Danhi Makanga, kurejea tena kwenye Bunge hili baada ya uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bariadi Mashariki uliofanyika tarehe 30 Mei 2004. *(Makofi)*

Niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Yete Mwalyego na Mheshimiwa Kapteni Thadeus Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Aidha, nawapa pole Dr. Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge Viti Maalum, kwa msiba wa kufiwa na baba yao mzazi. Pia tunawapa pole Mheshimiwa Dr. Lawrnce Gama, Mbunge wa Songea Mjini na Mheshimiwa Parmukh Sigh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, tangu tumeanza Bunge hili la Bajeti baadhi ya Wabunge wenzetu wamepata mikasa mbalimbali. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, alivamiwa na majambazi akiwa njiani kuja Dodoma Bungeni, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, alipata ajali eneo la Morogoro akiwa njiani kuja Dodoma Bungeni na Mheshimiwa Estherina Kilasi, naye alipata ajali mbaya ya gari hapa hapa Dodoma. Wote hawa nawapa pole kwa mikasa hiyo iliyowafika.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba zao mwanzoni mwa Mkutano wa Bunge la Bajeti. Hotuba hizo zimefafanua sera za jumla za uchumi na bajeti na kuweka mwelekeo na hatua ambazo Serikali inachukua kuimarisha uchumi pamoja na utoaji wa huduma muhimu za jamii. Aidha, ningependa kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa hotuba yake ambayo imetoa malengo yatakayowezesha usimamizi thabiti katika kutekeleza shughuli mbali mbali za Serikali kwa mwaka wa fedha 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini. Kamati hii ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais na maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kukamilisha makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi kilichopita.

Ofisi ya Makamu wa Rais ina majukumu ya kusimamia na kuratibu shughuli za Muungano, kuratibu juhudi za kuondoa umaskini nchini, kusimamia sera ya mazingira na kuratibu utekelezaji wake, pamoja na kuratibu shughuli zinazofanywa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na jumuiya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, tukiwa tumetimiza miaka 40 ya Muungano, nchi yetu inakabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko makubwa ikiwa ni pamoja na ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pamoja na wananchi wa pande zote kuwa na ari kubwa ya kisiasa, utekelezaji wa baadhi ya masuala ya Muungano umepata vikwazo mbalimbali. Kuwepo kwa vikwazo katika muundo wa Muungano wetu si jambo la ajabu. Ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilizungumzia jambo hili.

Naomba kunukuu maneno ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aliyosema katika hotuba aliyoitoa kwenye kilele cha sherehe za miaka 40 ya Muungano katika viwanja vya Amani, Zanzibar, tarehe 26 Aprili, 2004: "Ni kweli na wala si ajabu kuwa Muungano wowote unaweza kuwa na matatizo ya hapa na pale. Wajibu wetu ni kuimarisha Muungano hata katika mazingira hayo, badala ya kuzikuza mno kasoro ndogo. Tukumbuke kuwa Muungano wa kisiasa, umoja peke yake, hata bila faida nyingine, ni maendeleo na manufaa makubwa..." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa masuala yanayoleta vikwazo katika Muungano yanashughulikiwa, Serikali imeendelea na utaratibu uliowekwa wa wataalamu kukutana na kujadili masuala yanayoonekana kuwa ni vikwazo na kutoa ushauri. Serikali inayafanyia kazi siku hadi siku masuala haya kwa matarajio ya kupata ufumbuzi wa kudumu. Katika kutafuta ufumbuzi huo pamoja na juhudi nyingine, Serikali inawapa wananchi wake fursa mbalimbali kushiriki katika kubuni na kutathmini njia za kuboresha Muungano.

Mheshimiwa Spika, sera ya kuimarisha Muungano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni mojawapo ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Ilani ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000. Ilani hiyo imetamka nanukuu: "...muundo wa Muungano ambao umeendelea kukubaliwa na Chama cha Mapinduzi ni Muungano wenye Serikali mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar," Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo yenye dola *(sovereignity)* ambayo haigawiki.

Mfumo wetu ni wa nchi moja yenye Serikali mbili. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye mamlaka kamili juu ya masuala yanayohusu Tanzania Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye madaraka kamili juu ya masuala ya Muungano na yale yanayohusu Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, sheria ya Uraia namba 6 ya mwaka 1995 imetungwa na hivyo kufuta Sheria zilizokuwa na utata. Kwa mantiki hiyo mwananchi yoyote wa Tanzania ana haki ya kuishi au kwenda sehemu yoyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuhusu Utumishi katika Serikali ya Muungano, suala la sifa linazingatiwa bila ubaguzi wa aina yo yote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililopatiwa ufumbuzi ni lile la Serikali kutoa tafsiri ya neno utafiti kumaanisha *research* na hivyo kufanyika Kimuungano. Aidha, kituo cha utafiti wa viumbe wa bahari cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichopo Zanzibar kinapanuliwa ili kuweza kupanua wigo wa shughuli hizi nchini.

Nafurahi kuliarifu Bunge hili kuwa kituo cha utafiti wa viumbe wa bahari cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania ni moja kati ya vituo vinne duniani - Mexico, Australia na Phillipines vilivyoteuliwa na Benki ya Dunia kuwa *Centres of Excellence."* Aidha, hatua zimechukuliwa kuimarisha sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na ile ya usafiri wa anga kwa kuboresha uwanja wa ndege wa Zanzibar hivyo ndege kubwa kuruhusiwa kutua, kuruhusu mashirika ya watu binafsi kuendesha biashara ya usafiri na usafirishaji wa anga na kubinafsisha Shirika la Ndege Tanzania ili huduma iboreshwe. Sekta nyingine zilizoboreshwa ni zile za Mawasiliano, Posta na Simu.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza uchumi wa Taifa taratibu za utafutaji gesi asilia na petroli zinafanyika Kimuungano. Utaratibu wa kuvuna rasilimali katika eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu unatakiwa kufanyika kwa pamoja. Muundo wa Benki Kuu sasa una sura ya Muungano kwa Benki Kuu kufungua Tawi Zanzibar na ujenzi wa jengo la Benki Kuu Zanzibar kuanza katika kiwanja cha Gulioni.

Aidha, SMZ imefungua akaunti yake Benki Kuu na inaendelea kupata huduma toka benki hii pamoja na kupata mgao wa 4.5% ya faida ya Benki Kuu inayopatikana kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa kodi ya mapato unafanyika kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizokubalika na pande zote. Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Na. 14 ya mwaka 1996 inatekelezwa. Wajumbe wa Tume waliteuliwa mwaka 2003 na kuanza kazi chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo. Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinatakiwa kuchangia katika akaunti ya pamoja ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Muungano. Utaratibu huu unatakiwa kuwekwa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Aidha, hivi sasa Benki ya Dunia, *ADB* na *UNDP* zimeanza kuisaidia Zanzibar katika vita dhidi ya umaskini *(ZPRP).*

Mheshimiwa Spika, katika kurahisisha huduma ya Vyama vya Siasa nchini, Msajili wa Vyama vya Siasa nchini amefungua ofisi zake mjini Zanzibar, hivyo kusogeza huduma zake karibu zaidi kwa wanachi waishio katika visiwa vya Unguja na Pemba. Masuala mengine yanayoendelea kujitokeza ni pamoja na yanayohusu Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu *(Exclusive Economic Zone).* Suala hili ni la Muungano na sheria ya *Exclusive Economic Zone* ya mwaka 1989 inazungumzia kuhusu uvunaji wa rasilimali katika ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuratibu na kufuatilia maamuzi mbalimbali yanayohusu Muungano, kipaumbele kitakuwa kuhakikisha kuwa maamuzi ya Serikali yanatekelezwa ili kuondoa vikwazo na kudumisha Muungano wetu. Aidha, mawasiliano na wadau katika maeneo ambayo ni ya Muungano na yasiyo ya Muungano yatafanyika, ikiwa ni pamoja na elimu kuhusu Muungano kutolewa na kuweka mikakati ya ushirikiano kwa maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya Serikali zetu katika sekta zisizo za Muungano umezidi kukua kuanzia ngazi ya viongozi wa kitaifa hadi wananchi wa kawaida. Kwa mfano, maadhimisho ya miaka 40 ya Muungano yalifanyika mjini Zanzibar na kufana sana. Kudumisha Muungano na ushirikiano kunasaidia maendeleo ya kiuchumi na ya wananchi kwa ujumla. Ni wajibu wetu kuulinda Muungano huu ambao kama nilivyosema hapo awali, umedumu kwa miaka 40 hivi sasa. Ni haki yetu kujivunia Muungano huu na kumshukuru Mola wetu.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii na matumizi ya maliasili sharti kuzingatia athari zake kwa binadamu na kwa mazingira. Suala la kuhifadhi mazingira ni miongoni mwa mambo yanayopewa kipaumbele na Serikali ya awamu ya tatu. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kulinda mazingira nchini ikiwa ni pamoja na kupitisha programu na miradi ya utekelezaji na kuweka sera madhubuti za kusimamia hifadhi ya mazingira.

Kwa vile matatizo ya uharibifu wa mazingira hayana mpaka kati ya nchi na nchi au bara na bara, Tanzania inashirikiana na nchi jirani na nyinginezo kupitia mikataba mbalimbali ya Kimataifa, katika kudhibiti matatizo haya kwa pamoja. Matatizo ya namna hii ni kama vile upotevu wa bioanuwai, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, mabadiliko ya tabianchi *(Climate Change),* uharibifu wa ukanda wa Ozoni angani na udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi. Kwa lengo hili, Tanzania imeridhia mikataba kadhaa ya Kimataifa kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, ziko programu na miradi iliyoandaliwa na sekta mbalimbali kuhusu hifadhi ya ardhi na upandaji miti kwenye maeneo yaliyoathirika na yaliyo katika hatari ya kugeuka jangwa, hifadhi ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, hasa misitu ya asili na milima yenye miti ya asili, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya makazi na viwanda, hifadhi ya mazingira katika maeneo ya pwani ya bahari, na programu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Programu na miradi hii inalenga kuboresha mazingira ili kuleta maendeleo endelevu kuiwezesha nchi yetu kuondoa umaskini uliokithiri ifikapo 2010 na kuwa na uchumi imara ifikapo 2025, sambamba na dira ya maendeleo ya Taifa. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikisha taasisi mbalimbali na wananchi inaratibu programu za aina hii, inatoa miongozo ya kisera, mikakati na mipango na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, inayotekelezwa na nchi za Afrika ya Mashariki yaani Kenya, Tanzania na

Uganda kwa kushirikiana. Programu hii inalenga katika kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria na inatoa kipaumbele katika kuimarisha shughuli endelevu za uvuvi, kudhibiti uchafuzi wa maji na utupaji taka za majumbani na viwandani, kuhifadhi ardhi, misitu, vyanzo vya maji na maeneo owevu *(wetlands)* na kudhibiti magugu maji. Programu pia inafadhili miradi midogo midogo ambayo inatekelezwa na wananchi inayolenga katika kuboresha hali yao ya maisha na kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria katika sekta za afya, elimu na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu iliendelea kudhibiti magugumaji katika kipindi cha 2003/2004. Mbawakavu wapatao milioni 52.6 walizalishwa na kusambazwa katika maeneo korofi *(hot spots)* ya Ziwa Victoria. Udhibiti kwa sasa umefikia zaidi ya asilimia 80. Mialo ipatayo 500 haina gugumaji kwa sasa. Tafiti kuhusu uchafuzi wa maji na utupaji taka za majumbani na viwandani uliendelea katika kipindi chote cha mwaka 2003/2004.

Utafiti huu umezidi kuthibitisha kuwa uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria umeathiri kwa kiasi maji yaliyoko kando kando ya Ziwa hili na hasa maji yaliyo karibu na miji na viwanda kama vile jiji la Mwanza, Musoma na kadhalika. Mapendekezo ya kupunguza uchafuzi huo yametolewa. Aidha, viwanda 12 vilivyoshiriki katika mafunzo ya mbinu za kupunguza uchafuzi vimeendeleza hatua za kupunguza uchafuzi wa maji na mafanikio yanaendelea kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu imeendelea kuboresha uvuvi endelevu kwa kuwasaidia baadhi ya wananchi wa wilaya za Bukoba, Muleba na Tarime kufuga samaki. Programu imesaidia kutoa mafunzo kwa wananchi 29 wanaopenda kufuga samaki katika wilaya hizo. Programu imesaidia pia ujenzi wa vituo vya kuzalishia vifaranga vya samaki katika kijiji cha Magoma wilaya ya Tarime. Tayari kituo hiki kimekwishazalisha vifaranga 1,800 na kuvisambaza kwa wafugaji. Ufugaji wa samaki utawaongezea kipato na lishe wafugaji na jamii kwa ujumla. Mwaka 2002 programu ilifanya sensa ya wavuvi Ziwani katika nchi zote tatu. Matokeo ya sensa yamebainisha, pamoja na mambo mengine, kwamba kwa upande wa Tanzania kuna wavuvi 80,053 na mitumbwi 21,658. Taarifa hizi zitawezesha kuweka mikakati ya uvuvi endelevu na makadirio ya uvunaji wa samaki katika Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu iliendelea kushauri baadhi ya vijiji vya Mkoa wa Mara kuhusu kuhifadhi misitu hasa misitu ya asili ili kupunguza kasi ya kutoweka kwa misitu. Aidha, kitengo cha Misitu cha Programu kimepanda miche ya miti milioni moja na kusambazwa. Kupitia Programu hii kitabu cha Uanzishaji wa Bustani na Upandaji Miti, kimetayarishwa. Nakala 2000 zimechapishwa na kusambazwa. Kitabu kinaeleza faida za kupanda miti.

Programu pia imesaidia utekelezaji wa miradi midogo midogo saba katika sekta za elimu, afya na barabara. Katika kuhakikisha matumizi bora ya ardhi, wakulima wapatao 58 wamepata mafunzo ya kilimo endelevu katika lindimaji la Tarafa ya Kalemera, Wilaya ya Magu. Mafunzo hayo pia yalihusu kilimo cha Makinga maji kwenye miteremko. Makinga maji yenye urefu wa kilometa 15 yalitengenezwa katika

lindimaji hili. Kutokana na baadhi ya wakulima kufuata ushauri huu, uzalishaji wa mazao yao umeongezeka.

Kwa mfano, baadhi ya wakulima wa pamba wameongeza uzalishaji kutoka kilo 880 kwa hekta hadi kilo 2380 kwa hekta, mpunga kutoka kilo 300 hadi 1200 na mahindi toka kilo 450 kwa hekta hadi kilo 2060 kwa hekta. Aidha, programu imetayarisha vijitabu viwili kuhusu (a) njia bora za matumizi ya madawa ya kilimo na (b) njia muafaka ya kuhifadhi udongo na maji.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1997 tafiti mbali mbali za kisayansi zimefanyika. Matokeo ya tafiti hizi yamechapishwa katika kitabu cha *Proceedings of the LVEMP-Tanzania 2001 Scientific Conference.* Nakala 200 za kitabu hiki zimesambazwa kwa wadau mbali mbali ikiwemo Ofisi ya Bunge. Programu pia iliendelea kushauri vijiji na wilaya katika Mkoa wa Mara, Kagera na Mwanza kuhusu matumizi bora ya maeneo owevu. Baadhi ya vijiji vimesaidiwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya maeneo haya. Programu iliendelea kujenga uwezo wa vyombo vinavyotekeleza mradi kwa kununua vifaa kama vile madawa na kemikali za maabara na kuendelea kufadhili watumishi wanaosoma vyuoni kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika kutekeleza shughuli zote zilizofanyika mwaka 2003/2004 Programu imetumia shilingi bilioni 2.3.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria ambayo iligharimiwa na Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia *(IDA)* na Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(Global Environment Facility)* imemalizika mwezi Juni, 2004.

Pamoja na mafanikio mengi na mazuri yaliyopatikana katika miaka saba ya utekelezaji wa programu hii, matatizo ya Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria na Bonde lake bado hayajamalizika. Aidha, Serikali za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeona umuhimu wa kuandaa Awamu ya Pili ya Programu *(LVEMP-2)* itakayotekelezwa kwa muda mrefu zaidi wa miaka 10 hadi 15. Programu inayoandaliwa italenga katika masuala ya utafiti wa kisayansi wa mazingira, ukuzaji wa uchumi na usimamizi wa maliasili katika bonde la Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Japan kupitia Mfuko wake wa *Policy and Human Resources Development* na Mfuko wa Dunia wa Mazingira wamekubali kutoa Dola za Marekani 719,689 na Dola 186,600 sawia, zitakazotumika kuandaa programu hii. Maandalizi ya Awamu hii yameanza na yatakamilika Desemba 2005. Ili kuunganisha Awamu ya Kwanza iliyomalizika mwezi Juni 2004 na Awamu ya Pili itakayoanza mwaka 2006, kipindi cha miezi 18 kimeongezwa. Hii ni kufuatia maafikiano kati ya Serikali na Benki ya Dunia na tayari kiasi cha Dola za Marekani milioni 3.5 kimeombwa kuendeleza kazi za Programu hadi Awamu ya Pili itakapoanza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 shughuli zifuatazo zitafanyika: -

(a) Kudhibiti magugumaji kwa kuzalisha na kusambaza mbawakavu wapatao milioni 75 katika Ziwa Victoria, Maziwa madogo madogo *(Satttellite lakes),* mito, mabwawa na kwenye maeneo korofi *(hot spots)* na kufuatilia matukio ya magugumaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, programu itaweka mikakati mipya ya kudhibiti magugumaji katika Mto Kagera kwa kushirikiana na Kenya na Uganda na kuzishirikisha nchi za Rwanda na Burundi kufanya utafiti wa kina katika mto huu ili kubaini sababu zinazofanya mbawakavu kushindwa kushamiri katika eneo hili.

(b) Kuendeleza shughuli za uvuvi kwa kutoa mbinu za uvuvi kwa wavuvi, kuimarisha ulinzi dhidi ya uvuvi haramu na kuhifadhi mazalio ya samaki katika Ziwa Victoria kwa kushirikisha wananchi na vikundi vya ulinzi wa rasilimali *(Beach Management Units).*

Aidha, programu itaendeleza utafiti juu ya biolojia ya viumbe katika Ziwa Victoria, mabwawa na mito na kukamilisha shughuli za kuandika vitabu viwili vinavyoelezea aina ya samaki na viumbe wengine katika Ziwa hili.

(c) Kuendelea na utafiti kuhusu ubora wa maji katika vituo 126 vilivyojengwa katika Bonde la Ziwa Victoria na katika maeneo yaliyo karibu na makazi ya watu na mahali palipojengwa viwanda ili kubaini uchafuzi utokao katika maeneo haya. Kufuatilia utekelezaji wa *Cleaner Production* viwandani ili kubaini punguzo katika viwango vya uchafu unaoingia Ziwani kutokana na viwanda husika na kuvihamasisha viwanda kutekeleza programu hii.

(d) Kuendelea kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuhifadhi misitu asilia, ardhi owevu na kuzuia mmomonyoko wa ardhi na kukuza miche ya miti ipatayo 400,000 na kuisambaza kwa wakulima. Aidha, Programu itaendeleza shughuli za hifadhi ya udongo na maji katika lindimaji la Kwibuse-Kuruya (Tarime) na Kalemela (Magu).

(e) Kukamilisha miradi midogo midogo minne inayoendelea katika sekta za elimu mitatu na afya mmoja na kuanzisha mipya sita katika Wilaya za Biharamulo mitatu, Magu miwili na Musoma mmoja.

(f) Kuendelea na uchunguzi wa kina katika maeneo owevu ya Nyashishi na Mabubi juu ya uwezo wa ardhi owevu wa kuchuja uchafu unaoingia ziwani. Kutayarisha ramani zinazoonesha maeneo owevu katika bonde la Ziwa Victoria.

(g) Kuendeleza mafunzo ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya shahada ya pili na Falsafa.

(h) Kuelimisha na kuhamasisha wananchi na wadau wengine wa Kanda ya Ziwa Victoria juu ya uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Victoria kwa njia ya redio, luninga, warsha, magazeti na vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu maandalizi ya miradi ya utekelezaji wa programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika *(Strategic Action Programme)* kwa ushirikiano na nchi jirani za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia. Miradi miwili iliandaliwa kuhusu hifadhi ya bonde la ziwa na udhibiti wa maji machafu katika mji wa Kigoma na ilifanyiwa upembuzi yakinifu na kutafutiwa fedha. Ninayo furaha kulielezea Bunge lako Tukufu kwamba wafadhili wafuatao walijitokeza kushiriki katika kutekeleza miradi ya programu hii Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF)* kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Kimataifa lisilo la kiserikali la Hifadhi ya Maliasili *(IUCN).*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hii miwili utaanza katika kipindi cha mwaka 2004/2005 na shughuli zifuatazo zitafanyika:-

Kuajiri watumishi na wataalamu wa miradi, kununua vifaa vya miradi, kutoa mafunzo kwa wataalamu wa serikali za mitaa na wa vijiji, kukuza weledi kuhusu masuala ya mazingira ya ziwa na bonde lake na maandalizi ya mipango ya ardhi kwa lengo la kuhifadhi mazingira. Ofisi ya Makamu wa Rais itakamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa Hifadhi ya Mazingira na Uendelezaji wa bonde la Ziwa Tanganyika.

Aidha, Ofisi itaendelea kufanya majadiliano na wafadhili wengine walioonyesha nia ya kugharamia shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu kwenye ziwa na bonde lake. Wafadhili hao ni Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB), Nordic Development Fund,* Jumuia ya Ulaya *(EU), FAO* na *FINNIDA*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza Bunge lako Tukufu mwaka 2003, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kupitia Kituo cha Teknolojia na Uendeshaji Endelevu wa Viwanda *(Cleaner Production Centre of Tanzania -CPCT)* inasimamia utekelezaji wa mradi wa usafi wa mazingira katika shughuli za viwanda. Mradi huu wa miaka mitano ulianza mwezi Desemba, 1999 na una madhumuni ya kujenga uwezo wa viwanda na wadau wengine nchini katika teknolojia na mbinu za uzalishaji za kupunguza au kuzuia uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Kituo kiliendelea kukusanya na kusambaza taarifa mbalimbali za uzalishaji bora kwa walengwa kupitia vyombo vya habari, vipeperushi na jarida la Kituo kwa lengo la kukuza dhana ya uzalishaji bora na shughuli za Kituo. Vile vile Kituo, kwa kushirikiana na programu endelevu ya Manispaa ya Tanga, kiliandaa na kuendesha semina tatu za kukuza ufahamu juu ya dhana ya uzalishaji bora kwa washiriki wapatao 75 kutoka idara za serikali, manispaa, viwanda na makampuni kutoka sekta rasmi na wafanyabiashara ndogo ndogo zilizo katika sekta isiyo rasmi. Kituo kilifanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati katika kiwanda kimoja kinachotengeneza sabuni na kingine cha kusindika samaki vilivyoko mjini Tanga kwa ajili ya kusafirisha nje.

Pia, Kituo kilifuatilia na kuhamasisha utekelezaji wa dhana ya uzalishaji bora katika viwanda vya Manispaa ya Arusha *(Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd, A to Z*

*Textile Mills Ltd, Chemipack (T) Ltd.* na *Continental General Tyre East Africa Ltd.)* na Jiji la Mwanza *(Vic Fish Ltd., Mwanza Fishing Industries Ltd., Nyanza Bottling Co. Ltd., Mwanza City Abattoir, Vegetable Oil Industries Ltd (VOIL), Birchand Oil Mill* na *Nyakato Steel Mill Ltd.).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Kituo kitatekeleza majukumu yafuatayo:-

Kuanzisha kitengo cha kuratibu usambazaji wa taarifa kuhusu teknolojia zenye kupunguza uzalishaji wa taka, kupokea, kukusanya, kutayarisha taarifa kuhusu dhana ya uzalishaji bora na utekelezaji wake na kuzisambaza kwa walengwa kupitia vyombo vya habari na jarida la Kituo na kutayarisha na kusambaza majarida na vipeperushi kwa wadau mbali mbali kwa lengo la kueneza taarifa ya shughuli za Kituo.

Majukumu mengine yatakayotekelezwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati viwandani, kuelimisha viwanda kuhusu kuandaa maombi ya mikopo ya kuwekeza katika miradi inayopunguza uzalishaji wa taka na kuiwasilisha kwenye taasisi za fedha na kwenye mfuko wa uendelezaji wa mazingira *(Environmental Development Fund)* ulio chini ya programu ya miji endelevu, kufuatilia uanzishwaji wa mfumo wa kugharamia uwekezaji katika mbinu za kupunguza uzalishaji wa taka *(Financing Mechanism for Cleaner Production Investments)* na kuendesha semina na warsha za kukuza ufahamu wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu kwa wadau mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Kituo kiliendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya Kitaifa ya kuzuia matumizi ya madawa yanayomomonyoa ukanda wa hewa ya ozoni angani. Kituo kilipokea vifaa vya kufundishia mafundi mchundo wa majokofu na viyoyozi na vifaa vya kukusanya na kusafisha gesi aina ya *Chlorofluorocarbons (CFCs)* itumikayo kwenye majokofu na viyoyozi. Vifaa hivyo vimekwisha kabidhiwa Chuo cha Ufundi Stadi - *VETA,* Moshi na vingine vimehifadhiwa Kituoni.

Vile vile Kituo kiliandaa warsha tatu kwa ajili ya mafunzo ya mafundi mchundo wa majokofu na viyoyozi, warsha mbili juu ya usimamizi wakati wa matengenezo madogo madogo na ukarabati wa majokofu na viyoyozi na warsha moja juu ya njia bora za kusafisha, kuhifadhi na kurejesha gesi *(CFCs)* kwenye majokofu na viyoyozi. Washiriki 22 kutoka katika baadhi ya miji mikuu ya mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani walinufaika na mafunzo haya. Mafunzo hayo yalifanyika katika Chuo cha Ufundi Stadi - *VETA,* Moshi.

Kituo kiliendelea pia kuratibu miradi ya uwekezaji katika teknolojia zisizotumia gesi zinazoharibu ukanda wa Ozoni kwenye viwanda vya *Pan Africa Enterprises* na *Plyfoam* vinavyotengeneza bidhaa za sponji. Aidha, Kituo kilikusanya takwimu kuhusu matumizi ya kemikali hizi nchini na kuwasilisha Sekretarieti ya Itifaki ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya nchi wanachama wa Itifaki ya Montreal.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikamilisha taratibu za kukipa Kituo cha Teknolojia na Uendeshaji Endelevu wa Viwanda *(CPCT)* hadhi ya kisheria chini ya sheria ya Udhamini *(Trustees Incorporation Ordinance, Cap. 375).*

Mheshimiwa Spika, mwezi Aprili, 2004 Baraza la Mawaziri lilipitisha uamuzi wa kukipa Kituo hadhi ya kisheria. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Ofisi ya Makamu wa Rais itafuatilia upatikanaji wa ofisi ya kudumu ya Kituo.

Mheshimiwa Spika, pia nchi yetu, kupitia Kituo cha *CPCT,* imetunukiwa heshima ya kuwa mwenyeji wa Taasisi ya Afrika ya Matumizi na Uzalishaji Endelevu *(African Roundtable on Sustainable Consumption and Production - ARSCP)* ambayo ilizinduliwa rasmi kama taasisi ya kimataifa ya Afrika isiyo ya kiserikali huko Casablanca, Morocco tarehe 18 Mei, 2004. Katika mkutano huo Kituo cha *CPCT* kilichaguliwa kuwa Sekretariati ya mpito *(Interim Secretariat)* kikiwa na jukumu la kushughulikia usajili wa Taasisi hiyo kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia maendeleo endelevu na kwa kupitia Kituo cha Teknolojia na Uendeshaji Endelevu wa Viwanda *(CPCT),* inatekeleza mradi unaohusu Mkakati wa Kitaifa wa Teknolojia bora zenye uwezo wa kudhibiti madhara kwa mazingira na afya.

Madhumuni ya mradi huu ni kuimarisha uwezo wa Serikali katika kuboresha uwekezaji katika teknolojia mbadala viwandani na hivyo kuleta maendeleo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mradi huu wa mwaka mmoja, umeanza mwezi Aprili, 2004 na unatarajiwa kukamilika Machi, 2005. Tanzania ni moja ya nchi nne duniani zinazonufaika na msaada huu. Nchi nyingine ni Argentina, Nicaragua na Vietnam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kazi zifuatazo zilifanyika chini ya mradi huu:-

Kamati ya Wataalamu ambayo ina majukumu ya kufanya mapitio ya ripoti zote za mradi iliundwa, Mikutano miwili ya kamati ya wataalamu iliitishwa na Mwongozo na Hadidu za rejea kwa ajili ya tathmini ya uwezo na nafasi ya kutekeleza tekinolojia bora viliandaliwa. Aidha, takwimu zilikusanywa kwa ajili ya kuandaa vigezo vitakavyotumika kwenye tathmini hiyo.

Mheshimiwa Spika, shughuli zitakazofanyika katika kipindi cha mwaka 2004/05 ni pamoja na uchunguzi wa kina wa aina ya teknolojia bora zilizopo nchini na upatikanaji wake, tathmini ya teknolojia zinazopunguza taka katika viwanda teule, kuandaa mipango ya uwekezaji na usambazaji wa teknolojia bora katika viwanda hivyo na kuitisha mikutano ya kamati ya wataalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mwaka jana Serikali iliweka kodi *(excise duty)* ya mifuko ya plastiki inayotengenezwa nchini na inayoagizwa kwa kiwango cha asilimia 15 kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa mazingira kutokana na matumizi ya bidhaa hii. Katika juhudi za kutafuta ufumbuzi wa kudumu, Ofisi ya Makamu wa Rais iliitisha kikao cha wadau wa bidhaa hii, mwaka 2003. Kutokana na majadiliano, wadau walitoa mapendekezo ya kina ya kushughulikia tatizo la uchafuzi wa mazingira utokanao na bidhaa hii. *(Makofi)*

Aidha, ilidhihirika kwamba suala la mifuko ya plastiki linagusa sekta ya uwekezaji, ajira, shughuli za sekta isiyo rasmi, usimamizi wa taka mijini, mahitaji ya watumiaji na biashara ya Kimataifa. Ofisi ya Makamu wa Rais inafanya uchambuzi wa mapendekezo ya wadau na itawasilisha Serikalini kwa hatua zaidi katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Lengo ni kupiga marufuku kisayansi uingizaji kutoka nje ya nchi na utengenezaji ndani ya nchi mifuko yote ya plastiki isiyorejelezeka ambayo siyo tu inachafua mazingira na kuhatarisha maisha ya binadamu na hata mifugo, bali pia mifuko hiyo imekuwa ni kero kubwa mijini na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Bunge hili Tukufu katika Kikao chake cha 14 kilichofanyika mwezi Februari, 2004 liliuridhia Mkataba wa Stockholm unaohusu udhibiti wa kemikali zinazochukua muda mrefu sana kuoza katika mazingira *(Persistent Organic Pollutants - POPs).* Madhumuni ya Mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara ya kemikali zinazochukua muda mrefu sana kuoza katika mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza Bunge lako Tukufu mwaka 2003, Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza mradi unaohusu kuandaa Mpango wa Taifa wa kutekeleza Mkataba huu. Mradi ni wa miaka miwili na ulizinduliwa mwezi Juni, 2002.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

Uchambuzi kuhusu maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm ulifanywa na wataalamu wa sekta za Afya, Viwanda, Kilimo, Mazingira na Elimu ya Juu kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Warsha moja ya wadau ilifanyika Dar es Salaam kujadili na kuboresha ripoti ya maeneo ya kipaumbele. Aidha, mkutano wa pili wa Kamati ya Usimamizi wa mradi ulifanyika kujadili utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaundwa na wajumbe 12 kutoka sekta za Kilimo, Afya, Viwanda, Serikali za Mitaa, Fedha, Usafirishaji na Nishati na Sekta binafsi. Pia katika kipindi hiki rasimu ya Mpango wa Taifa wa kutekeleza Mkataba wa Stockholm iliandaliwa. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 kazi zifuatazo zitafanyika chini ya mradi huu:-

Rasimu ya Mpango itaboreshwa na warsha ya wadau ya kujadili rasimu ya Mpango itafanyika. Aidha, maandalizi ya miradi na programu mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Taifa yatafanyika ikiwa ni pamoja na kutafuta wafadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu mwaka 2003, Ofisi ya Makamu wa Rais inasimamia utekelezaji wa mradi wa kutayarisha takwimu za kemikali zinazochukua muda mrefu kuoza aina ya *Polychlorinated Biphenyls (PCBs)* na vifaa vinavyotumia kemikali hizo. Mradi huu unatekelezwa katika nchi wanachama 14 wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC). (Makofi)*

Utekelezaji wa mradi umeanza mwezi Machi, 2004 na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi sita. Lengo la mradi ni kuhamasisha jitihada zinazofanywa na Mikataba ya Stockholm, Basel na Rotterdam katika kukuza uwezo wa kusimamia kemikali na vifaa vinavyotumia kemikali aina ya *PCBs* ili kuweka mikakati ya pamoja ya kulinda mazingira na afya ya binadamu dhidi ya athari ya kemikali hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, shughuli zifuatazo zilifanyika chini ya mradi huu:-

Mafunzo yametolewa kwa wataalam 32 mwezi Machi, 2004 watakaohusika na ukusanyaji takwimu za kemikali aina ya *PCBs* na vifaa vinavyotumia kemikali hiyo. Washiriki walitoka *TANESCO,* Shirika la Umeme la Zanzibar *(SFPC),* Sekta za Afya na Mazingira na vile vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *NGOs. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayotembelewa na wataalam katika zoezi hili yametambuliwa na vigezo vya kutambua mafuta ya mitambo na vifaa vyenye kutumia kemikali aina ya *PCB* viliandaliwa. Aidha, uchunguzi wa kikemia ulifanywa na wataalam wa Ofisi ya Makamu wa Rais, *TANESCO, SFPC* na Chuo Kikuu ili kutambua viwango vya *PCBs* kwenye mafuta ya mitambo ya kusambaza umeme inayotumika na isiyotumika ambayo kwa vigezo vya utambuzi yanaweza kuwa na kemikali hizi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, ripoti itaandaliwa kuhusu kiasi cha *PCBs* nchini na Mpango wa Taifa wa usimamizi wake utaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka 2003, nchi zilizoridhia Mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa utupaji na usafirishaji wa taka sumu baina ya nchi na nchi *(The Basel Convention on the Control of Transboundary Movements of Hazardous Wastes and their Disposal)* ziliamua kuanzisha Vituo vya Kanda vya Mafunzo na usambazaji wa teknolojia. Katika bara la Afrika, vimeanzishwa vituo vitatu. Kituo kwa ajili ya nchi zinazozungumza kiingereza kiko Pretoria, Afrika ya Kusini. Kituo kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kifaransa kiko Senegal na kwa nchi zinazozungumza Kiarabu kiko Misri. Tanzania ni mjumbe wa Kamati ya wataalamu inayoratibu uanzishaji wa Kituo kilichoko Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Afrika ya Kusini, Nigeria, Uganda na Zambia. Kamati ilianza kazi yake mwezi Septemba, 1999. Katika mkutano wa sita wa nchi wanachama wa mkataba wa Basel uliofanyika Geneva, Switzerland mwaka 2002 ilikubalika kuwa Kituo hiki kisajiliwe chini ya sheria za Kimataifa *(Inter-Govenmental Organizations - IGO)* ili kiwe na hadhi ya kimataifa.

Katika kipindi cha 2003/2004 Sekretarieti ya Mkataba wa Basel iliandaa rasimu ya Katiba *(statute)* ya kuanzisha kituo hiki rasmi na kuisambaza kwa nchi wanachama wanaohudumiwa na kituo hiki ili watoe maoni. Hapa nchini wizara na wadau mbalimbali walishirikishwa kutoa maoni ya kuboresha rasimu ya Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kikao maalum cha nane cha Baraza la Usimamizi la Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP Governing Council),* kilichofanyika katika kisiwa cha Jeju, Korea ya kusini, mwezi Machi, 2004 nchi 10 zinazohudumiwa na Kituo hiki zilitia saini Katiba hiyo. Nchi hizo ni Afrika Kusini, Ghana, Kenya, Msumbiji, Nigeria, Rwanda, Swaziland, Tanzania, Uganda na Zambia. Hapa nchini tumeanza taratibu za kuridhia Katiba hii ili Kituo kiweze kuandikishwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 kazi zilizofanywa kuhusiana na Kituo cha Pretoria ni pamoja na kuandaa programu ya mafunzo kwa wadau mbali mbali juu ya usimamizi wa taka zenye sumu katika sekta za Afya, Viwanda na Usafiri, kuandaa mkakati kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za kituo, kuandaa mapendekezo ya miradi na kuiwasilisha kwa wahisani, kuchambua rasimu ya Katiba ya Kituo, kuendesha mafunzo juu ya kuimarisha ushirikiano na programu za kimataifa na za kikanda zinazotekelezwa chini ya mikataba mbalimbali ya mazingira *(Multilateral Environmental Agreements Programs),* kuendesha warsha ya mafunzo kuhusu usimamizi wa taka zenye sumu kwa maofisa wa Idara na Taasisi za Serikali na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa taka za hospitalini na jinsi ya kuandaa miradi inayoweza kuvutia uwekezaji katika tekinolojia zenye kudhibiti athari za taka zenye sumu. Nchi mbalimbali za Afrika zimenufaika na mafunzo hayo. Nchi hizo ni Afrika Kusini, Eritrea, Ethiopia, Gambia, Ghana, Kenya, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Sychelles, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, shughuli zitakazofanyika ni kuendesha mafunzo juu ya Itifaki ya Mkataba wa Basel inayohusu fidia kutokana na ajali au madhara yanayoweza kutokea wakati wa usafirishaji wa taka zenye sumu kati ya nchi na nchi na utupaji wake, kuendesha mafunzo kuhusu usimamizi na usafirishaji wa mabati ya *Asbestos,* kuendesha semina ya kuhamasisha viongozi wa ngazi za juu Serikalini kuhusiana na usimamizi wa taka zenye sumu, kuendesha mafunzo mafupi kwa maofisa wa kati wa Serikali na taasisi zinazojitegemea juu ya uandaaji na usimamizi wa miradi ya mazingira hasa ya taka za sumu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu programu ya Kuimarisha Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira na Maliasili. Programu hii inafadhiliwa na Serikali ya Marekani. Madhumuni ya programu hii ni kukuza ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za usimamizi wa hifadhi ya Mazingira ili kujenga uwezo wa Serikali za Mitaa na Vijiji, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kupanga na kutekeleza shughuli za hifadhi na uendelezaji wa mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya siku mbili yaliendeshwa kwa lengo la kuwaelimisha, kuwahamasisha na kujenga uwezo wa utendaji wa Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa sera ya Taifa ya Mazingira, matatizo ya mazingira na wajibu wao. Warsha hii ilihusisha washiriki 94 wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mameya, Wakurugenzi wa Manispaa na Miji, Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi Watendaji kutoka Wilaya 31 zilizoko kwenye awamu ya 3 ya utekelezaji wa programu ya uboreshaji wa shughuli za Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Programme).* Shughuli nyingine zilizofanyika ni ukamilishaji wa Ujenzi wa Vituo vya kupokea wageni *(visitors centre*) vya hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara na usambazaji wa maji vimeendelea kuimarishwa na tafiti mbalimbali za ekolojia kufanyika katika Hifadhi za Tarangire na Manyara. Mafunzo yanaendeshwa kwa wafanyakazi wa *TANAPA* na jamii zinazozunguka Hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara na Hifadhi ya Akiba ya Ugalla, kuhusu masuala mbalimbali ya hifadhi ya maliasili na Mazingira, ushirikishwaji wa wananchi katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na matumizi ya majiko sanifu vilizingatiwa.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizofanyika ni kukamilisha maandalizi ya mapendekezo ya Mbinu za Kiuchumi *(Economic Instruments)* kwa ajili ya usimamizi wa hifadhi ya Mazingira, kukamilisha uanzishaji wa hifadhi za wanyamapori za jamii *(Wildlife Management Areas)* ya Muwada Wilayani Babati na Makame Wilayani Kiteto katika Mkoa wa Manyara na ujenzi wa boma la asili *(Cultural Boma)* kwa ajili ya Kikundi cha akinamama wa Kijiji cha Esilalei wilayani Monduli.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka 2003, Ofisi ya Makamu wa Rais ilifanikisha ziara ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira katika Mikoa ya Tanga, Arusha na Manyara, ambapo walijionea shughuli mbalimbali za hifadhi ya Mazingira na kutoa maelekezo juu ya athari za uharibifu wa mazingira katika msitu wa Hifadhi ya Amani *(Amani Nature Reserve),* Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na machimbo ya madini katika eneo la Mererani. Ofisi ya Makamu wa Rais inakubaliana na maoni ya Kamati ya Bunge na kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, TAMISEMI na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tanga inaendelea kuyashughulikia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05, chini ya Programu ya Mazingira na Maliasili, miundombinu ya hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara itaendelea kuimarishwa, mafunzo pia yataendeshwa juu ya matumizi bora ya vituo vya kupokea wageni *(visitors centres)* katika hifadhi hizo. Aidha, Ofisi itaendesha warsha mbili kwa wataalam wa maliasili na mazingira wa ngazi ya Wilaya, itaandaa taratibu na kanuni kwa ajili ya Sheria mama ya mazingira pindi itakapokamilika na pia itaandaa ziara kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Maliasili, Mazingira na Kuondoa Umaskini Mikoani, ili kuona, kujifunza na kushauri juu ya masuala yanayohusu mazingira na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililieleza Bunge lako Tukufu juu ya tatizo la magugu maji katika Ziwa Jipe lililoko Wilayani Mwanga. Katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa mradi wa kukabiliana na tatizo hili ambao unatafutiwa wafadhili. Aidha, kwa sasa, Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kushirikiana na serikali za vijiji wilayani Mwanga kupitia mradi wa *Mixed Farming Improvement Project (Mifpro),* inaandaa mpango wa usimamizi wa uhifadhi wa miteremko mikali katika bonde la Ziwa Jipe, ili kukabiliana na tatizo la ukataji miti holela, uchomaji moto ovyo na ufugaji usio endelevu. Wanavijiji wanashauriwa kufuga kitaalamu mifugo michache ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaoathiri Ziwa Jipe na bonde lake.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Bunge lako Tukufu kupitisha na hatimaye Tanzania kuridhia Itifaki ya Cartagena, Ofisi ya Makamu wa Rais ilianza kuratibu mradi wa kitaifa kuhusu usalama kwa mazingira na afya ya binadamu katika matumizi ya mazao ya biotekinolojia kwa ufadhili wa *UNEP.* Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, chini ya mradi huu, Ofisi ya Makamu wa Rais ilifanya tafiti sita juu ya sheria na sera za sekta mbalimbali ili kujua ni kwa kiasi gani zinasimamia matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa.

Katika Kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa taarifa za tafiti hizo ambazo zitatumika katika kuanzisha kituo cha utunzaji na ubadilishanaji taarifa. Rasimu ya awali ya mfumo na mikakati ya matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa imeandaliwa na inatarajiwa kujadiliwa katika kanda mbalimbali nchini ili kupata maoni zaidi ya wadau kwa nia ya kuiboresha. *(Makofi)*

Aidha, matokeo ya tafiti hizi yalichangia katika maandalizi ya rasimu ya sheria ya mazingira. Pia warsha mbili za mafunzo kwa wataalamu na wadau zilifanyika na zilihusisha washiriki 120 kutoka Idara mbalimbali za Serikali, vyuo vikuu na mashirika binafsi. Warsha hizo zilihusu tathmini na udhibiti wa athari za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa kwa mazingira. Vile vile, vitabu na vipeperushi mbalimbali vilisambazwa kwa wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

Kukamilisha uanzishaji wa kituo cha utunzaji na ubadilishanaji taarifa *(creation of a database),* kuendeleza zoezi la utayarishaji na usambazaji wa vipeperushi na njia nyingine za kukuza weledi kwa umma, kuendesha mafunzo kuhusu matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa kwa wataalamu na wadau mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari; na kupokea na kuchambua maoni kuhusu rasimu ya awali kuhusu muundo na mikakati ya matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa Kimataifa wa matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa kwa nchi 25 toka Afrika na ulifunguliwa na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkutano huu ulisisitiza ushirikiano katika ubadilishanaji habari, uandaaji wa mikakati ya matumizi salama ya

bioteknolojia ya kisasa na mbinu zote za kuhakikisha usalama wa hifadhi ya bioanuwai na afya ya wakazi wa bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Tanzania ilishiriki kwenye mkutano wa kwanza wa nchi zilizoridhia Itifaki ya Cartagena kuhusu matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa *(The first Meeting of the Parties to the Cartagena Protocol on Biosafety - MOP1),* uliofanyika Kuala Lumpur, Malaysia mwezi Februari, 2004. Jumla ya washiriki 750 kutoka nchi 160, mashirika ya kimataifa na taasisi mbalimbali walihudhuria mkutano huo.

Mheshimiwa Spika, mkutano uliweka taratibu na miongozo ya kufanya maamuzi ya kukubali au kukataa uingizaji nchini wa viumbe, mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na utambulisho wake *(labelling),* kabla ya kusafirishwa toka nchi moja hadi nyingine, taratibu za nyaraka mbalimbali zinazohusu bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki wakati wa uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi na ufungaji wake; na masuala ya kubadilishana taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, mkutano huo pia uliweka taratibu na miongozo ya kufuatwa katika kujenga uwezo wa Taasisi na mafunzo kwa wataalamu na elimu kwa umma, tathmini na udhibiti wa athari za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa kwa mazingira na afya ya binadamu, utambuzi wa bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na utafiti na uendelezaji wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa.

Aidha, Mkutano ulipitisha mwongozo na kuunda kamati ya wataalamu kuhusu bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki; utaratibu wa fidia *(Liability and Redress)* kwa nchi itakayoathirika na uingizaji na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa ulikubalika, programu ya utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena na taratibu za kudhibiti bidhaa ziliainishwa.

Kwa kuwa Tanzania imeridhia Itifaki ya Cartagena, itaendelea kunufaika na misaada katika nyanja zote zilizokubalika, hususani utaalamu na fedha katika kutekeleza Itifaki kupitia Mfuko wa Dunia wa Mazingira. Aidha, katika mkutano huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa Mkutano wa nchi zilizoridhia Itifaki ya Cartagena. Kwa sababu hii, Tanzania sasa ni mjumbe wa Kamati Kuu *(Bureau)* inayosimamia mwenendo wa utekelezaji wa Itifaki hii, ikiwakilisha bara la Afrika, pamoja na Burkina Faso, kwa kipindi cha sasa hadi mwezi Juni mwaka kesho utakapofanyika mkutano wa pili.

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ulitanguliwa na kikao cha saba cha nchi zilizoridhia Mkataba wa Bioanuwai. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni suala la jinsi nchi zenye bioanuwai kubwa, hususan nchi zinazoendelea, zinavyoweza kunufaika kwa haki na usawa, kutokana na bioteknolojia ya kisasa, katika ushirikiano wa kimataifa na nchi zilizoendelea *(The fair and equitable sharing of the benefits arising out of the utilisation of genetic resources).* Kikao kiliamua kuanzisha majadiliano kwa lengo la kuunda chombo cha kimataifa kitakachoshughulikia suala hili.

Aidha, iliamuliwa kukuza ushirikiano wa kimataifa katika kupambana na magugumaji na viumbe vingine vinavyoweza kuenea kwa haraka na kuathiri mazingira. Ushirikiano huo ni katika kupashana habari, kupeana teknolojia na maarifa na kusaidia nchi maskini kifedha na kujenga uwezo wao katika kukabiliana na tatizo hili. Pia, programu mbalimbali zenye malengo, shughuli, na mbinu za utekelezaji, zilipitishwa kuhusu hifadhi ya bioanuwai ya milimani, maeneo ya hifadhi, na ubadilishanaji wa teknolojia na maarifa katika matumizi endelevu ya bioanuwai.

Vile vile kikao kilitoa mwongozo kwa Mfuko wa Dunia wa Mazingira, kuhusu misaada kwa nchi zinazoendelea katika maeneo mbalimbali ya Mkataba na Itifaki ya Cartagena.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 niliarifu Bunge lako Tukufu juu ya kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa pamoja wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa ushirikiano wa nchi za Malawi na Msumbiji. Mradi huu haukutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2003. Hii ni kutokana na Benki ya Dunia kusimamisha kufadhili miradi yote ya mazingira katika nchi ya Malawi. Tunafanya mawasiliano na *GEF* ambao ndio wafadhili wa mradi kuona kama tunaweza kutumia wakala wengine badala ya Benki ya Dunia katika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Mapitio ya miradi saba iliyowasilishwa na Taasisi za serikali, Vyuo vya Utafiti na Mafunzo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* yalifanyika. Miradi hiyo iliwasilishwa kwenye Mfuko wa Dunia wa Mazingira na wahisani wengine kwa ajili ya ufadhili. Miradi ilihusu matumizi ya nishati jadidifu *(renewable energy),* nishati mbadala na nishati itokanayo na mionzi ya jua. Baadhi ya miradi hiyo tayari imepatiwa fedha na iko katika hatua ya utekelezaji. Mojawapo ya mradi huo ni wa Kujenga Uwezo wa Matumizi ya Nishati ya Jua na soko lake katika Mkoa wa Mwanza *(Transformation of the Rural PV Market in Tanzania).* Mradi huu unafadhiliwa na *GEF* kupitia *UNDP* na unasimamiwa na Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ilibuni mradi wa Dola za Marekani 200,000 ili kuandaa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(National Adaptation Programme of Action- NAPA)* kwa ufadhili wa *GEF* kupitia *UNEP.* Utekelezaji wa mradi huu umeanza, timu ya watalaam 20 kutoka Wizara na Asasi mbalimbali, Vyuo Vikuu na Vyuo vya Utafiti pamoja na sekta binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali imeundwa ili kuandaa Mpango huo. Timu hii ya wataalam inajumuisha pia wajumbe kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika maandalizi ya miradi ya kupunguza hewajoto chini ya makubaliano ya Itifaki ya Kyoto ya kushirikisha nchi zinazoendelea katika kupambana na ongezeko la mabadiliko ya tabianchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na asasi za hapa nchini na *UNCTAD,* imeandaa mwongozo wa Taifa *(Clean Development Mechanism Investors Guide)* kuhusu jinsi ya kushiriki katika miradi ya *CDM.*

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais iliendesha mafunzo kwa zaidi ya watalaam 50 kutoka sekta mbalimbali kuhusu uandaaji na utekelezaji wa miradi ya *CDM.* Mafunzo haya yalidhaminiwa na kufadhiliwa na *UNCTAD* na yalifanyika kwa njia ya mtandao wa *internet.* Baadhi ya wataalam waliopewa mafunzo hayo ni wajumbe wa timu ya Taifa inayoandaa *NAPA.* Tayari yapo makampuni ya Ulaya na Marekani ambayo yameonyesha nia ya kuwekeza katika shughuli zenye kulenga kupunguza uzalishaji wa hewa-joto chini ya *CDM* na majadiliano na Makampuni hayo yameanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

Kukamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(NAPA),* kuendelea na uhamasishaji na kufanya warsha mbalimbali kwa ajili ya kukuza weledi kuhusu miradi ya *CDM* na Mkataba kwa ujumla na kuanza maandalizi ya Ripoti ya pili ya kitaifa kuhusu utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais ilipata kiasi cha Dola za Marekani 80,000 kutoka Shirika la Kimataifa la Kilimo *(IFAD)* na Dola za Marekani 17,000 kutoka *Global Mechanism* kupitia Sekretarieti ya *SADC* kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame. Mashirika sita yasiyo ya Kiserikali kutoka mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Kagera, Morogoro na Pwani yalipatiwa fedha kutoka *IFAD* kwa ajili ya kusaidia shughuli zinazohusu kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame katika maeneo yao.

Aidha, Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania *(JET)* kilipatiwa fedha na *IFAD* ili kuwawezesha kuandika na kusambaza Gazeti lao la Mazingira, maarufu kwa jina la Kasuku, kuendesha warsha juu ya masuala ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame kwa *NGOs* nyingine na kuendesha vipindi maalum na midahalo inayohusu kuenea kwa hali ya jangwa na ukame redioni. Aidha, Ofisi imepitia upya Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame ili kujumuisha masuala mapya yaliyojitokeza tangu mpango huu ulipoandaliwa mwaka 1999. *(Makofi)*

Vilevile Ofisi kwa kutumia shirika lisilo la kiserikali liitwalo *DONET* imeandaa na kugharamia ziara za mafunzo kwa wakulima kutoka mkoa wa Dodoma kwenda katika chuo cha Mipango na Maendeleo Vijini, Dodoma ili waweze kujifunza masuala ya kilimo bora na jinsi ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uamuzi wa Baraza la Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF Assembly)* wa kukubali kufadhili miradi ya kukabiliana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Katika kipindi cha mwaka 2003/04 Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa na kuendesha warsha ya uhamasishaji kwa taasisi za kiserikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu maeneo hayo mapya yanayofadhiliwa na Mfuko huo. Kufuatia warsha hiyo mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yameitikia wito wa kuandaa miradi ya kupambana na kuenea kwa hali ya

jangwa na ukame na miradi hii imewasilishwa kwenye Sekretariati ya Mfuko kwa ufadhili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Ofisi ya Makamu wa Rais inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kuendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za miradi tuliyoiwasilisha na tutakayoandaa, kuandaa ripoti ya utekelezaji wa shughuli za Mkataba na kuiwasilisha kwenye Sekretariati na kuendelea kuwahamasisha wadau mbalimbali ili kutekeleza shughuli za Mkataba.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu kukamilika na kupitishwa na Serikali kwa muundo husishi wa kitaasisi wa usimamizi wa Mazingira nchini. Kufuatia hatua hii maandalizi ya sheria ya mazingira yalianza. *(Makofi)*

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maandalizi ya muswada wa sheria hii ya mazingira yalikamilika. Muswada huu unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni katika kipindi cha mwaka huu wa fedha na *Inshallah* mategemeo yetu ni muswada huu muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu kusomwa mara ya kwanza katika mkutano huu wa 16 wa Bunge unaoendelea ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuupata na kwenda kuwashirikisha wadau kuuchambua kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya maazimio ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu *(World Summit on Sustainable Development-WSSD)* uliofanyika mwishoni mwa mwaka 2002, Afrika Kusini. Mkutano huu pamoja na kufanya tathimini ya utekelezaji wa makubaliano ya wakuu wa nchi na serikali kuhusu mazingira na maendeleo yaliyofanyika Rio mwaka 1992, uliandaa mpango wa utekelezaji wa *WSSD (WSSD Plan of Implementation).*

Katika kipindi cha mwaka 2003, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na mambo mengine iliendelea kuratibu maandalizi ya Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa *WSSD Plan of Implementation.* Kazi hii itakamilishwa katika kipindi cha mwaka huu, kutegemea upatikanaji wa fedha. Aidha, mpango wa Taifa wa Mazingira *(NEAP)* unapitiwa upya ili kujumuisha mpango wa utekelezaji wa *WSSD* na masuala ya *PRSP.*

Vile vile mwaka 2003 Tanzania ilishiriki katika mkutano wa 12 wa *Commission for Sustainable Development-CSD* uliofanyika huko New York, Marekani ambao ulijadili hatua za kuchukua ili kufikia malengo ya milenia *(Millenium Development Goals)* katika maeneo ya Maji, Maji Taka na Maendeleo ya Makazi. Ofisi ya Makamu wa Rais itaratibu hatua za utekelezaji wake Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, masuala ya mazingira ni *agenda* pana inayogusa sekta na shughuli nyingi za watu binafsi, vikundi mbalimbali, taasisi, makampuni na mashirika mbalimbali ya Serikali na yasiyo ya Serikali. Serikali inatiwa moyo na mwamko wa wananchi kushiriki katika shughuli za

hifadhi ya mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2003, vikundi 22 vinavyojishughulisha na hifadhi ya mazingira vilipata huduma ya ushauri ili kuboresha shughuli zao za uhifadhi, na vingine kupendekezwa kusajiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuhamasisha wananchi kuhusu hifadhi ya mazingira, Taifa letu huadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kila mwaka tarehe 5 Juni. Katika kuadhimisha siku hiyo kwa mwaka 2004, Ofisi ya Makamu wa Rais iliratibu shughuli mbalimbali za uhamasishaji nchini. Shughuli zilizofanyika kwa kushirikisha wananchi ni:-

Kuzibua na kusafisha mifereji ya maji machafu na yale ya mvua, kusafisha maeneo mbalimbali yakiwemo yale ya mijini, kupanda na kupalilia miti; kuendesha mashindano ya kata na shule mbalimbali kuhusu usafi na hifadhi ya mazingira na kuzindua kamati za mazingira za Wilaya. Maadhimisho haya yalifanyika kitaifa, mjini Kasulu, Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wote walioshiriki na kufanikisha maadhimisho haya. Vile vile napenda kuipongeza Wizara ya Afya kwa kuendelea na mashindano ya usafi wa mazingira mijini, na kampuni za *Sunflag Arusha* na *TTCL,* kwa msaada wao wa *T-shirts* kwa ajili ya kufanikisha maadhimisho haya na vyombo vya habari kwa jinsi walivyohamasisha maadhimisho hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa vyombo vyote vinavyojihusisha na shughuli za hifadhi ya mazingira nchini kuendelea kukuza elimu ya mazingira mikoani, wilayani, na vijijini ili kuboresha ufahamu wa wananchi kuhusu masuala ya usafi na hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira linaendelea kufanya shughuli zake chini ya Sheria ya Bunge Na. 19 ya mwaka 1983. Sheria hiyo inaainisha majukumu ya Baraza ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu, kuratibu na kukuza uhusiano kati ya taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali na kutoa hamasa juu ya hifadhi ya mazingira hususan uandaaji na utekelezaji wa mipango ya kuhifadhi mazingira, utafiti na kukuza weledi katika masuala ya mazingira, na tathimini za athari ya shughuli za maendeleo kwa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004 Baraza liliendelea kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa maeneo owevu kanda ya Ziwa Victoria. Aidha, Baraza likishirikiana na wanavijiji wa wilaya za Bunda na Magu limetayarisha mikakati ya kuhifadhi maeneo owevu ya mito ya Simiyu na Rubana. Baraza limemaliza kutayarisha ramani za maeneo owevu ya Ziwa Victoria zionyeshazo mito, aina ya udongo, matumizi ya ardhi, aina mbali mbali za uoto zinazolizunguka Ziwa Victoria *(land use/land cover maps).*

Aidha, Baraza liliendelea kukusanya takwimu na kufanya utafiti wa uchujaji maji machafu katika mito ya Nyashishi (Mwanza na Misungwi), Mabubi (Geita) na Kagondo

na Ngono (Bukoba). Baraza liliendelea kushirikiana na wananchi katika kubuni mikakati ya kukarabati maeneo yaliyoathirika hususan katika mito ya Simiyu na Rubana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Baraza linatarajia kuendelea kuziwezesha wilaya zinazozunguka mwambao wa Ziwa kutayarisha mikakati ya uhifadhi wa maeneo ya mito hasa mito ya wilaya za Geita, Bukoba, Muleba, Bunda na Musoma. Vile vile Baraza likishirikiana na wilaya, linatarajia kutenga sehemu maalum kwa ajili ya uhifadhi wa Bioanuwai katika maeneo mbalimbali yenye raslimali za pekee za bioanuwai. Aidha, Baraza lina mpango wa kuwafundisha wasusi wa bidhaa za ukindu kwa kutumia watalaam kutoka Kenya na Uganda ili kuboresha bidhaa zao. Vile vile shamba la majaribio la kuotesha ukindu lililoko Bubinza (Magu) litaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza shughuli na malengo yaliyokuwa yamepangwa na kutekelezwa na mradi wa kuhifadhi bioanuwai za mipakani ambao umemalizika na kufungwa rasmi, Baraza kwa kushirikiana na taasisi isiyo kuwa ya kiserikali ya *TaTEDO* kupitia mradi wa kuendeleza mikakati endelevu ya nishati katika ngazi ya Wilaya *(Developing Sustainable Rural Energy Strategies at the District level),* liliandaa na kutoa mafunzo ya utengenezaji wa majiko sanifu kwa vikundi vidogo vidogo pamoja na kamati za mazingira katika wilaya za Monduli, Same na Bukoba.

Mheshimiwa Spika, Baraza pia liliwezesha na kufanikisha kuanzishwa kwa vitalu vya miti aina ya Jatropha katika maeneo ya mradi. Baraza pia kwa kushirikiana na *TaTEDO* lilitayarisha na kusambaza taarifa na habari juu ya miti aina ya Jatropha pamoja na tekinolojia ya nishati ya samadi ya mifugo *(Biodigesters).*

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005, Baraza kwa kupitia mradi huu limepanga kutoa mafunzo zaidi juu ya uanzishaji na utunzaji bora wa vitalu kwa kamati za mazingira za Wilaya na vijiji pamoja na watu binafsi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004 Baraza kwa kupitia Mradi huu wa kuhifadhi maeneo ya pwani limetoa makala mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ya Pwani, pamoja na Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Pwani *(State of the Coastal Environment Report)* na rasilimali zake. *(Makofi)*

Pia Baraza limeendelea kutoa jarida liitwalo Pwani Yetu ambalo hutolewa kila baada ya miezi mitatu kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Jarida hili hutoa taarifa mbalimbali za hifadhi ya mazingira ya Pwani ikiwa ni pamoja na faida zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza mpango wa Tuzo ya Hifadhi ya Mazingira ya Pwani *(Coastal Environmental Award Scheme),* ambayo imeleta hamasa kubwa katika kuelimisha juu ya hifadhi ya mazingira ya pwani. Baraza pia limetoa mafunzo ya utumiaji wa mwongozo wa uwekezaji katika viumbe bahari *(mariculture)* kama vile kilimo cha mwani, ufugaji wa samaki na uwekezaji katika sekta ya utalii Pwani.

Mheshimiwa Spika, pia Baraza limetoa mafunzo katika utumiaji wa mwongozo wa uandaaji wa mipango na kanuni za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira ya pwani kwa njia kamilifu *(Integrated Coastal Management action planning guidelines).* Baraza pia linaendelea kutoa mafunzo ya jinsi ya kutumia mwongozo wa kufuatilia mwenendo wa mazingira ya pwani *(Ecological Monitoring Guidelines).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Baraza linakusudia kuwashirikisha wadau wa sekta binafsi katika kuchangia kuelimisha juu ya umuhimu wa kuwa na fukwe safi kwa kujenga vyoo katika mashule na sehemu za jumuiya kama vile sokoni na kwenye ufukwe. Baraza pia litaandaa na kutoa mafunzo ya kutumia rasilimali kwa njia endelevu ili kupunguza umaskini, hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha ufugaji wa nyuki, samaki na kilimo cha mwani kwa kushirikiana na Wilaya husika ili kuongeza kipato na wakati huohuo kupunguza uharibifu wa mazingira.

heshimiwa Spika, aidha, Baraza litaendelea na mpango wake wa kuandaa na kutoa makala kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watafiti, wanafunzi, idara za serikali na watu binafsi, zinazohusu hifadhi ya mazingira ya Pwani. Baraza limepanga kufadhili wadau wa pwani katika masomo ya muda mfupi, kuhudhuria mikutano mbalimbali ndani na nje ya nchi inayolenga katika kujenga na kuongeza ufanisi wa kiutendaji, na pia kujifunza kwa wadau wengine walio na shughuli kama zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara za Maliasili na Utalii kwa upande wa Tanzania Bara na ile ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika kwa upande wa Tanzania Zanzibar, tunaandaa mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Pwani *(Marine and Coastal Environment Management Project - MACEMP)* utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unalenga kutekeleza sera na mikakati yetu mbali mbali tuliyojiwekea inayohusu, pamoja na mambo mengine, hifadhi ya mazingira hususan usimamizi wa maliasili za bahari na pwani na kuondoa umasikini kwa pande zote mbili za Muungano. Mradi huu utalenga pia kushirikiana na mradi wa utafiti wa matumbawe *(Coral Reefs)* ambao unatekelezwa na nchi nne duniani, Tanzania ni kupitia taasisi ya utafiti wa Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu iliyopo Zanzibar *(Institute of Marine Science - IMS). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine ni Phillipines, Australia na Mexico. Jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuchochea ushirikiano baina ya Wizara na taasisi husika nilizozitaja hapo juu kwa kuhakikisha ufuatiliaji na tathmini *(Monitoring and Evaluation)* ya shughuli za mradi huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Baraza lilishirikishwa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam, katika maandalizi ya mkakati na mpango wa kuboresha huduma ya maji na kuhifadhi mazingira katika jiji la Dar es Salaam. Mradi huu wa miaka miwili unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Makazi ya Binadamu *(United Nations Human Settlements Progamme)* unalenga

kuboresha upatikanaji wa maji na uhifadhi wa mazingira katika baadhi ya miji mikubwa barani Afrika, ambapo Serikali ya Tanzania imelichagua jiji la Dar es Salaam kuwa mwakilishi wake katika utekelezaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mikakati iliyopangwa kutekelezwa na mradi huu ni pamoja na kuongeza uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa maji, uhifadhi wa vyanzo vya maji pamoja mazingira. Katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Baraza kwa kushirikiana na wadau wanahohusika na mradi huu, limepanga kutekeleza mipango na mikakati ambayo imeandaliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, kama ilivyobainishwa.

Mheshimiwa Spika, Baraza limeshiriki katika mradi wa kujumuisha masuala ya mazingira katika Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini *(PRSP).* Mradi huu umelenga kuainisha kwa mapana uhusiano kati ya umaskini na mazingira na pia kuongeza uelewa juu ya umuhimu wa kupitia upya mipango ya maendeleo na bajeti za taasisi mbalimbali ili kuweza kuyapa kipaumbele masuala ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/04, Baraza kwa kupitia mradi kwa ushirikiano na wadau wengine limeweza kuingiza masuala ya kuondoa umaskini katika rasimu ya mkakati wa kitaifa wa elimu ya mazingira, kuandaa rasimu ya mwongozo wa mafunzo kuhusu tathmini ya athari kwa mazingira. Baraza limeshiriki katika majadiliano ya kuongeza uelewa wa mazingira na umaskini katika Wilaya za Muheza, Magu na Urambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 Baraza litaendeleza shughuli za kujumuisha masuala ya mazingira katika mkakati wa kuondoa umaskini katika wilaya ya Newala, kushiriki katika kuunda viashiria na/au vionyeshi vya umaskini na mazingira *(poverty-environment indicators),* Kushirikiana na serikali za mitaa katika kuingiza masuala ya mazingira katika mipango yao ya maendeleo na pia kuandaa vipeperushi vya tathmini ya athari za mazingira.

Aidha, Baraza litaandaa mkutano wa kitaalamu utakaobaini uhusiano uliopo baina ya mazingira, kilimo na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa Mpango Mpya wa hifadhi ya bioanuwai Kihansi *(updated Environmental Management Plan)* umekamilika kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali kama vile Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Maliasili na Utalii, *TANESCO* pamoja na wananchi wanaoishi karibu na maeneo husika.

Aidha, mradi umeshawezesha utayarishaji wa Hati ya Kudumu ya kutumia maji kuendesha mtambo wa Umeme wa Kihansi chini ya *TANESCO (TANESCO's Final Water Right)* na unaendelea kusaidia katika kujenga na kuongeza uwezo wa kitaasisi wa sekta zinazohusika na Uhifadhi wa rasilimali ya mazingira na maji Kitaifa. *(Makofi)*

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 mradi utatekeleza huo mpango mpya wa uhifadhi, utatengeneza mkakati madhubuti wa kuhifadhi bioanuwai na raslimali nyingine katika bonde la Kihansi *(Landscape-Wide Conservation Plan)* na kuendelea kutekeleza shughuli zinazolenga kujenga uwezo wa kitaasisi katika kuhifadhi na kusimamia mazingira kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Baraza lilitekeleza yafuatayo:-

Lilifanya mapitio ya ripoti kumi na tano za tathmini ya athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assessment - EIA)* ya miradi ya maendeleo na kutoa ushauri pamoja na vibali vyenye masharti ya kuboresha mazingira *(Conditional Environmental Clearance)* kwa miradi hiyo hapa nchini. Lengo kuu la zoezi hili ni kuhakikisha kwamba masuala ya mazingira yameainishwa barabara katika hatua zote za uhai wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa hapa nchini.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* pia lilitoa ushauri wa kitaalam kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu uhifadhi wa mazingira kwa Taasisi na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa taasisi/asasi zilizopewa ushauri huo ni pamoja na *Tanzania Social Action Fund (TASAF)* kuhusu utaratibu wa namna ya kufanya tathmini ya athari ya miradi midogo ya jamii *(Social micro-projects)* kwa mazingira. Lengo ni kuhakikisha kuwa suala zima la kuhifadhi na kuboresha mazingira linatiliwa maanani wakati wa kubuni, kutekeleza na kuhitimisha shughuli za miradi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza lilitoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi ya *African Centre for Technological Studies (ACTS, Nairobi)* kuhusu taratibu za kufanya tathmini za athari kwa mazingira *(EIA)* kwa maliasili zilizopo mipakani mwa nchi za Afrika ya Mashariki. Ushauri wa kitaalam ulitolewa pia kwa wananchi wa kawaida, mashirika yasiyo ya kiserikali *(NGOs)* kuhusu masuala mbali mbali yanayohusu matumizi ya rasilimali za asili na mazingira kwa ujumla.

Pia, Baraza lilishiriki katika juhudi za taifa za kuondoa umasikini ikiwa ni pamoja na kushiriki moja kwa moja kwenye miradi ya mazingira inayolenga katika kuondoa umasikini. Mfano, Baraza linashirikiana na *World Wide Fund for Nature (WWF)* katika kutayarisha mpango shirikishi wa matumizi endelevu ya raslimali za pwani na bahari *(Rufiji-Mafia-Kilwa Eco-region-Seascape Programme). (Makofi)*

Baraza lilikagua shughuli za uchimbaji wa madini ya *bauxite* huko Lushoto na pia shughuli za ukanda wa uzalishaji wa bidhaa za kuuzwa katika soko la nje *(Economic Processing Zone-EPZ)* katika maeneo ya viwanda Ubungo *(Ubungo Millenium Park)* na Vingunguti.

Pia, Baraza lilifanya mapitio ya mipango ya kusimamia mazingira *(Environmental Management Plan, EMP)* ya miradi ifuatayo:-

*Lower Kihansi Environmental Management Project (LKEMP), Geita Gold Mine* na *Afrika Mashariki Gold Mining.*

Pamoja na kutekeleza shughuli zilizotajwa, Baraza lilishiriki katika semina, warsha na mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, ikiwa ni pamoja na ile ya kutayarisha Sheria Mama ya Mazingira *(ILFEMP),* mapitio ya matumizi ya umeme, *(Public Expenditure Review - PER)* na ya mkutano wa uhusiano baina ya umasikini na mazingira *(Poverty Environment Partnership)* uliofanyika Uholanzi kutathmini na kuweka mikakati ya namna ya kujumuisha *(mainstream)* suala la mazingira katika mikakati ya kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Baraza litaendelea na utekelezaji wa shughuli zilizoanzishwa katika kipindi cha 2003/2004 kama ifuatavyo:-

- Kushiriki katika uandaaji wa miongozo ya mazingira katika sekta mbalimbali *(Environmental Sectoral Guidelines).*

- Kutoa ushauri kuhusu masuala ya taratibu za kufanya tathmini ya mazingira katika ngazi za sera, mipango na mikakati *(Strategic Environmental Assessment-SEA).*

- Kukuza weledi kwa watumishi wa Halmashauri za Wilaya, na Miji ili kuwajengea uwezo wa kufanya tathmini ya athari ya miradi kwa mazingira, kwa miradi ya maendeleo iliyoko katika halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, Baraza limepewa jukumu la kuhamasisha wadau wote juu ya umuhimu na jukumu lao katika kuyatumia na kuhifadhi mazingira. Katika kipindi cha 2003/2004 Baraza limetekeleza jukumu hili kwa kuanza maandalizi ya mkakati wa Taifa wa Elimu ya Mazingira na uhamasishaji ambao ukikamilika utatoa miongozo na maelekezo kwa wadau na watoa elimu na wahamasishaji.

Aidha, mkakati huu unapendekeza kuundwa kwa mtandao wa wahamasishaji mazingira ili waweze kubadilishana uzoefu na kushirikiana ili kufanikisha uhamasishaji na ushirikishwaji umma katika matumizi bora na utunzaji wa mazingira na maliasili zetu. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine limeandaa mradi unaolenga kuanzisha kozi fupi ambayo itatolewa kwa watoa elimu ya mazingira ili kukuza weledi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutoa taarifa za mazingira kwa wadau wake kwa kupitia maktaba yake na kwa kuandaa makala katika vyombo vya habari, warsha, makongamano na mikutano. Maktaba ya Baraza ilihudumia zaidi ya watumiaji mia tano kwa mwaka huu. Aidha, Baraza liliendelea kushirikiana na wadau mbali mbali kuelimisha umma ili kukuza uelewa na ushiriki wake katika maamuzi yanayozingatia hifadhi ya mazingira na kuchangia kuleta maendeleo endelevu.

Kwa mwaka ujao wa fedha Baraza litajihusisha zaidi na kukamilisha kupitishwa, kusambaza na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa Elimu ya Mazingira. Mkazo zaidi

utawekwa katika kukuza weledi wa wanahabari ili waweze kuandika kwa wingi na kwa ufasaha habari za mazingira, hasa za vijijini. Pia Baraza linashirikiana na wadau wa elimu kuandaa miongozo na makala za kushauri na kuelimisha juu ya majukumu yao katika suala zima la matumizi endelevu na utunzaji mazingira. Aidha Baraza litaendelea kuboresha huduma za maktaba ili iweze kuhudumia wateja wake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, pamoja na ukaguzi wa maeneo mbalimbali ya miji na viwanda ili kushauri juu ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, Baraza linakamilisha taratitbu za kuanza kutekeleza programu ya ukusanyaji na uteketezaji wa madawa chakavu *(ASP)* kwa mikoa yote ya Tanzania Bara.

Aidha, Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* limesaidia Serikali yetu kuboresha maeneo matano yaliyoathirika zaidi na madawa chakavu huko Arusha *(TPRI),* Korogwe (Tanga), Morogoro na Mbarali (Mbeya). Uboreshaji huo ni pamoja na kuezeka kwa bati stoo ya madawa iliyokuwa wazi (Korogwe), kuhamisha madawa kutoka kwenye mapipa yaliyooza na kuyahifadhi kwenye mapipa mapya na kwenye ghala bora (Arusha), kupakia madawa yaliyomwagwa kiholela sakafuni na kuyaingiza kwenye mapipa mapya na kuyahamisha kutoka ghala iliyovunjika na kuyapeleka kwenye ghala bora zaidi (Mbarali na Morogoro).

Aidha, Baraza linategemea kutekeleza mradi wa kudhibiti uchafuzi wa bonde la Mto Msimbazi kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kusimamia Mazingira *(UNEP/GPA).*

Lengo kuu la mradi huu ni kudhibiti mtiririko wa majitaka yanaouingia baharini kwa kutumia nyasi za *vetiver,* zenye sifa kuhusiana na ubora wake katika kukinga mmomonyoko wa ardhi pamoja na kuchuja majitaka hata kufikia viwango vinavyoruhusiwa kuingia baharini bila kuleta madhara kwa viumbe majini na mazingira kwa ujumla. Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano na Vyuo Vikuu, Manispaa zetu na *NGOs* za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vipengele muhimu vya Mradi huu ni:

- Kukusanya takwimu muhimu za bonde la Mto Msimbazi *(Baseline data).*

- Kuitisha kikao cha wadau mbalimbali ili kujenga uelewa wa mradi huu na kuwashirikisha kuhusu utekelezaji *(awareness).*
- Kuandaa eneo Owevu la ekari moja kwa kutumia nyasi za *Vetiver.*

- Kuandaa kanda *(zone)* ya kuzuia mmomonyoko wa urefu wa meta 100 kwa kutumia nyasi za *vetiver.*

- Kuanzisha shughuli za biashara kwa bidhaa zitokanazo na nyasi za *vetiver.*

- Kuandaa programu ya mafunzo ihusuyo udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na mmomonyoko wa ardhi kwa kutumia teknolojia ya nyasi za *vetiver.*

Mheshimiwa Spika, mradi wa Udhibiti wa Bonde la Mto Msimbazi unategemewa kugharimu Dola za Kimarekani 200,000.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kusimamia na kuratibu jitihada za Serikali za kupambana na umaskini chini ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini *(PRSP)* na kutathmini jitihada hizo kama zinakuza uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi walio wengi na hasa wale waishio vijijini. Lengo la Serikali kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, ni kuwa na Taifa lenye jamii iliyoondokana na umaskini uliokithiri, yenye maisha bora na mazuri, amani, utulivu na umoja, utawala na uongozi bora, jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi na uchumi wenye uwezo wa ushindani kujiletea ukuaji wa kudumu kwa maslahi ya watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta za Serikali zinazohusika zimeendelea kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kisekta iliyoandaliwa kwa kushirikiana na wananchi wenyewe, vyama vya hiari, taasisi za kijamii, taasisi za taaluma mbalimbali na wahisani, ili kwa pamoja tuweze kufikia malengo.

Mheshimiwa Spika, mengi yaliyotekelezwa kukuza uchumi na kuboresha huduma za jamii katika kipindi kilichopita yamejitokeza katika hotuba mbalimbali zilizosomwa na Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia. Hotuba za Waheshimiwa Mawaziri, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha na zile zilizosomwa na Mawaziri wa sekta mbalimbali, zimefafanua kwa kina utekelezaji wa mikakati mbalimbali pamoja na mafanikio na matatizo yaliyopo. Aidha, hali ya mwelekeo wa uchumi na fedha nchini pamoja na matumizi kwa kipindi kilichopita na kinachokuja vimewekwa bayana.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali bado ni nyenzo muhimu katika juhudi zetu za kupambana na umaskini. Mafanikio yaliyopatikana katika uchumi wetu yameendelea kutumika kuboresha bajeti yetu yenye lengo la kuongeza ufanisi katika sekta za kipaumbele. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la fedha zinazotengwa katika sekta za kipaumbele ili kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Serikali imeweka mkazo mkubwa katika kufanya mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini ulioandaliwa mwaka 2000, kama hatua mojawapo ya kutathmini jitihada za kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kufanya mapitio ya Mkakati huo baada ya miaka mitatu ya utekelezaji kwa lengo la kubaini mapungufu na kuboresha Mkakati ili uweze kuleta mafanikio zaidi kwa wananchi na uchumi kuendelea kukua kwa kasi zaidi, ili kufikia lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mapitio yamepewa muda mrefu zaidi ukilinganisha na maandalizi ya mkakati wa awali ili kupanua ushiriki wa wananchi, kupanua maeneo ya kipaumbele na kuboresha utekelezaji. *(Makofi)*

Katika mapitio hayo, masuala makuu matatu yamezingatiwa: kuchambua uzoefu wa nyuma kwa kupitia taarifa na ripoti za tafiti mbalimbali zilizopo, ushirikishwaji wa wananchi ili kupata maoni yao na kufanya tafiti pale penye hitaji kubwa kwa nia ya kupanua uelewa kwa yale yanayohitaji uchambuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya utekelezaji na mafanikio ni kama ifuatavyo:-

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliandaa na kutoa miongozo inayotumika ili kufanikisha zoezi hili. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini kwa ujumla na Mwongozo wa mashauriano ya wadau katika kupunguza umaskini.

Aidha, Serikali iliweka wazi ratiba ya zoezi hili katika hatua muhimu, ambazo ni: uzinduzi wa mapitio yenyewe, Mashauriano ya wadau katika ngazi zote kuanzia taifa hadi kwenye jumuia/vijiji, uandikaji wa Rasimu ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini (awamu ya pili), mashauriano katika ngazi ya Taifa, kujadiliwa na kupitishwa na Serikali, kutafsiriwa kwa lugha nyepesi na uchapishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wananchi umefanyika katika hatua mbalimbali. Vipeperushi vilichapishwa na kusambazwa Wilayani ili vigawanywe kwa wadau mbalimbali mijini na vijijini ili kupata maoni ya wengi. Serikali kwa makusudi kabisa iliamua mashauriano hayo yaongozwe na wadau wenyewe na Serikali ibakie kufanya uratibu wa zoezi hili kwa ujumla, kuwezesha wadau kuendesha mashauriano na kukusanya maoni. Wadau wakuu ambao wanashirikishwa kwenye mashauriano ni pamoja na Serikali kuu yenyewe, Serikali za mitaa, washirika, sekta binafsi, sekta isiyo rasmi, wakulima, asasi zisizo za kiserikali, vijana, wazee, walemavu, taasisi za kidini, waheshimiwa wabunge, taasisi za taaluma na utafiti, vyombo vya habari na vyama vya wafanyakazi. Miongozo iliyokwisha tolewa imeweka wazi nafasi ya kila mdau katika mchakato mzima wa mapitio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipenda isikie kutoka kwa wananchi wenyewe mambo makuu matatu yafuatayo:-

(a) Mabadiliko makuu yaonekanayo katika jitihada za kupunguza umaskini katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita;

(b) Matatizo makuu wananchi wanayokumbana nayo ambayo ni kikwazo katika kupata maisha bora na ukiukwaji wa haki za binadamu; na

(c) Mambo gani lazima yawepo katika mkakati wa kupunguza umaskini (awamu ya pili) unaoandaliwa ili kupunguza umaskini na kuinua ubora wa maisha.

Mheshimiwa Spika, kupitia vipeperushi hivi maoni yamekusanywa kutoka kwa wadau wengi, wadau wakuu wakiwa wananchi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, jitihada nyingine ya kukusanya maoni ni kupitia mikusanyiko ya watu katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi za jamii hadi Taifa. Aidha, maoni

mbalimbali yameibuliwa kutoka taarifa za utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini ziandaliwazo kila mwaka, Taarifa ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu *(Poverty and Human Development Report -PHDR)* na Ripoti za Warsha za Kitaifa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, maoni kutoka kwenye ripoti hizi yamejumuishwa na maoni yaliyokusanywa katika mashauriano mbalimbali, maoni kutoka kwenye vipeperushi pamoja na uzoefu Serikali iliyopata katika utekelezaji wa awamu ya kwanza yamewekwa pamoja. Mchakato huu unafanyiwa uchambuzi wa kitaalam ili kuandaa Rasimu ya Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Rasimu itajadiliwa na wadau mbalimbali na inatarajiwa mkakati wa awamu ya pili kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2004. Utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Pili, unatarajiwa kuwa wa miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006 hadi 2009/2010. Utekelezaji huu utaendana na malengo yaliyobainindhwa kwenye Dira ya Taifa ya 2025 ya kupunguza umaskini uliokithiri kwa asilimia hamsini ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliandaa hapo mwaka 2001 utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini uliobainishwa kwenye Mfumo wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mkakata wa Kupunguza Umaskini.

Katika mwaka 2003/2004 kazi ya ufuatiliaji na tathmini ya hali ya umaskini iliendelea kufanyika kama ilivyopangwa. Ripoti ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini (2002/2003) iliandaliwa kwa kushirikisha sekta za kipaumbele na wadau wengine. Ripoti inatoa maelezo ya utekelezaji katika maeneo yanayogusa moja kwa moja maisha ya wananchi walio wengi ambayo ni: kilimo, elimu, afya, maji, barabara za vijijini, janga la Ukimwi, jinsia, ajira, mazingira na utawala bora. Taarifa hii kama ilivyokuwa ile ya Kwanza (2000/2001) na ya Pili (2001/2002) imeelezea utekelezaji wa malengo yaliyopangwa kwa kila sekta kila mwaka, matatizo yanayokwamisha utekelezaji, na malengo ya kipindi kinachofuata. Ripoti hii inapatikana katika tovuti ya Taifa, ya mfumo wa kufuatilia hali ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, ripoti hiyo inaonesha kuwa hali ya uchumi kwa ujumla imeimarika, na kuwa Tanzania ni moja ya nchi maskini zenye mazingira ya uchumi tulivu *(Stable Macroeconomic Environment).* Hata hivyo, taarifa inatambua kuwa mafanikio haya hayajaweza kujionyesha kikamilifu katika hali ya maisha ya wananchi. Hii bado ni changamoto ya maendeleo kwa nchi yetu. Kwa ujumla, kiwango cha umaskini bado ni kikubwa hasa vijijini na kinapungua kwa kasi ndogo sana vijijini ukilinganisha na mijini na hasa katika jiji la Dar es Salaam ambapo idadi ya watu walio chini ya ulingo wa umaskini inapungua kwa kasi kubwa zaidi. Changamoto ni jinsi ya kuongeza tija katika sekta ya kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao ili kuboresha maisha ya watu. Mkakati wa Maendeleo Vijijini na Programu ya Maendeleo ya Kilimo inayolenga kuweka msisitizo katika mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Serikali za Mitaa vitaendelea kupewa umuhimu unaostahili.

Aidha, hatua za makusudi za kuboresha sekta mbali mbali zinaendelea, ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu, huduma za jamii na ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi yanayogusa maisha na maendeleo yao. Serikali inachukua hatua mbalimbali kuhakikisha masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo yanapatikana. Hatua ya awali iliyokwishachukuliwa ni kupitishwa kwa Sera ya Maendeleo ya Ushirika (2002) ambayo pamoja na masuala mengine inalenga kuimarisha vyama vya ushirika ili kurahisisha upatikanaji wa masoko kwa wakulima. Mkazo unawekwa pia katika kuendeleza shughuli ndogondogo na za kati *(Small and Medium Enterprises - SMEs)* na kupatikana kwa mikopo nafuu kwa wawekezaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine iliyofanyika ni kuandaa mwongozo wa usimamizi wa fedha *(Accounting and Operational Manual).* Kukamilika kwa kazi hii kumewezesha vikundi vinne vya utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji kupata fedha za utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji. Kazi kubwa zilizofanywa na vikundi hivi ni pamoja na Savei ya Kilimo na Mifugo *(Agriculture Sample Survey 2003/2004)* ambapo ukusanyaji wa takwimu ulianza Novemba, 2003 na kukamilika Januari, 2004, maandalizi ya kufanya Savei ya masuala ya Afya na Uzazi *(Demographic and Health Survey-2004/2005)* pia yalifanyika, chambuzi za takwimu za sensa ya 2002 na uandaaji wa ripoti za mikoa na ripoti nyingine muhimu zinazotokana na takwimu za sensa na savei.

Mheshimiwa Spika, vikundi viliandaa pia Ripoti ya tatu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na Ripoti ya pili kuhusu Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu *(Poverty and Human Development Report -PHDR)* ya 2003. Ripoti hizo zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali, ikiwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ripoti hizi zinajumuisha matokeo ya ufuatiliaji ya mfumo mzima na kupendekeza mwelekeo wa sera ili kuleta ufanisi zaidi katika jitihada za kupambana na umaskini. Kazi nyingine ni kusimamia mapitio ya mkakati, kuelimisha jamii kuhusu matokeo ya mfumo wa ufuatiliaji na jitihada za serikali katika kutekeleza sera na mikakati mbalimbali ya kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali za kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya jitihada zinazofanywa na serikali zilifanyika. Hii ilijumuisha wiki ya Sera na Mikakati ya Kuondoa Umaskini iliyofanyika kwa mara ya pili mwezi Oktoba mwaka 2003. Wiki hii ilizunduliwa na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wiki ya Sera za Kuondoa Umaskini inatoa fursa ya kubadilishana mawazo na kuibua mijadala ya kitaifa inayosaidia kuboresha jitihada za kupambana na umaskini. Wananchi walifahamishwa hatua iliyofikiwa katika jitihada za kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Ili kupanua wigo wa washiriki, baadhi ya sekta/taasisi kwa uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, ziliendesha majadiliano yaliyojumuisha wadau wengi na kwa karibu zaidi, tofauti na ilivyofanyika mwaka 2002. Mfano Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana (Idara ya Ustawi wa Jamii) iliendesha warsha kuhusu masuala ya vijana, wazee na

watu wenye ulemavu ambapo pia Sera ya Wazee ilijadiliwa na kuzinduliwa rasmi. *(Makofi)*

Aidha, katika wiki hii ya sera za kuondoa umaskini mwongozo wa mapitio ya mkakati ulijadiliwa na kuzinduliwa rasmi. Wadau walijadili pia ripoti ya Uchambuzi Shirikishi wa Hali ya Umaskini *(Participatory Poverty Assessment - PPA)* iliyofanyika mwaka 2002/2003. Maoni yote yaliyotolewa ambayo yamechapishwa na kusambazwa kwa wadau yatasaidia kuboresha sera na mikakati ya kupunguza umaskini na hasa katika kipindi cha mapitio ya mkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira walielimishwa kuhusu: Mapitio ya Mkakati wa kupambana na Umaskini, Malengo ya Milenia, mfumo wa ufuatiliaji unavyofanya kazi, na matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 na namna ya kutumia takwimu zake katika kupanga mipango bora na kuandaa bajeti kwa shughuli za maendeleo kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa. *(Makofi)*

Aidha, kwa kushirikiana na wataalamu kutoka *Canadian Parliamentary Centre* na taasisi ya *Research on Poverty Alleviation-REPOA* Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo walifanyiwa semina kuhusu umuhimu wa Wabunge katika kuharakisha mapambano dhidi ya umaskini. Ilielezwa kuwa Bunge na Wabunge wanayo nafasi kubwa katika mkakati mzima wa kupunguza umaskini.

Kwa kutambua hili Serikali ya Canada ilitenga dola za Marekani milioni 9 ili kuimarisha baadhi ya Mabunge Afrika katika kupambana na umaskini, masuala ya jinsia na kupambana na rushwa.

Mnamo mwezi Novemba, 2003 mtandao wa kuondoa umaskini *(poverty network)* Afrika uliundwa huko Ghana na ulizihusisha nchi tatu ambazo tayari zilikuwa na kamati za kudumu za Bunge ambazo hushughulikia masuala ya kupambana na umaskini. Nchi hizo ni Ghana, Malawi na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaendelea kushiriki kikamilifu katika mtandao huo. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Anne Makinda, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira kwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Uendeshaji *(Steering Committee of Poverty Network)* akiwakilisha Ukanda wa Mashariki wa nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, kufanyika kwa warsha katika mikoa ya Lindi na Mtwara kulitoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge kuona hali halisi ya umaskini na hasa vijijini, na jinsi wananchi katika vikundi mbalimbali na watu binafsi wanavyojishughulisha na kazi za kuwaletea maendeleo. Matatizo makuu yaliyobainishwa kuwa kero katika kuleta maendeleo ya vikundi na watu binafsi ni: ukosefu wa masoko, ukosefu wa vitendea kazi, ukosefu wa mitaji na urasimu mwingi wanaopambana nao wanapofuatilia mambo yao.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya ushirikishwaji wa wananchi katika maandalizi ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini lilipewa uzito mkubwa. Aidha, vyombo mbali mbali vya habari yakiwemo magazeti, redio na televisheni zilitoa habari zenye kuhamasisha na kuelimisha wananchi. Ni nia ya Serikali kuona kuwa kila mwananchi anashiriki kikamilifu katika hatua zote za kuandaa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na kuutekeleza. Jitihada hizi ziliwataka wadau katika maeneo yao wahakikishe kuwa mchakato shirikishi wa mapitio ya mkakati unazingatia mambo manne - uwazi, uwakilishi, ujumuishi na mjadala usioegemea siasa za upande wowote.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine ni pamoja na uhamasishaji na uelimishaji umma kupitia redio, majarida, vipeperushi na tovuti ziliendelea vizuri. Uelimishaji wa wananchi kuhusu jitihada mbalimbali za kupambana na umaskini ulifanyika kupitia kipindi cha redio cha Tujikomboe kinachorushwa na Redio Tanzania kila wiki Jumatano saa 10.30 jioni. Kadhalika, Gazeti la Mapambano linalochapishwa mara mbili kwa mwaka (Januari - Juni na Julai - Desemba) zilichapishwa na nakala kusambazwa kwa wadau katika ngazi mbalimbali. Kupitia jarida hili jamii huelimishwa kuhusu jitihada za kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Aidha, taarifa na vitabu mbalimbali vimekusanywa kwa ajili ya kuanzisha *Documentation Center* ambayo inakusudia kutoa nafasi kwa wadau na hasa kwa watumishi kupata taarifa mbalimbali kwa urahisi kwa lengo la kuongeza ujuzi katika maeneo, hasa jitihada za kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kutekeleza mradi wa *Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF)* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kwa lengo kubwa la kupunguza umaskini. Kupitia asasi za kifedha, mikopo na mafunzo hutolewa kwa walengwa ambao ni wananchi wenye kipato cha chini ili waweze kufanya biashara ndogo ndogo za kuwapatia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita kiasi cha shilingi 825,800,000/= kilitolewa kwa asasi za kifedha 25 kama ifuatavyo:-

*SIDO* Lindi, *SELFINA* - Kibaha, *Changamoto LPF* Zanzibar, *UMHJ* Dodoma, *Juhudi Afya SACCOS; Savings and Credit Co-operative Union League of Tanzania (SCCULT), SIDO* Morogoro, *SIDO* Mtwara, *MWASHITA SACCOS, NYUMBU SACCOS, Dodoma Rural SACCOS, CAVI, USHIRIKIANO SACCOS, Lindi Rural SACCOS, Mzumbe SEC SACCOS, SHIVU* Singida, *KIFISACCOS, Kilombero Teachers SACCOS, CHAMWAI, Mpwapwa Utafiti SACCOS, Nachingwea Teachers SACCOS, SIDO Singida, CISP, Newala Teachers SACCOS* na *Mzumbe University SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2004, jumla kuu ya mikopo iliyoidhinishwa tangu mradi uanze kutoa huduma hii imefikia shillingi bilioni 1.769 na kuwanufaisha walengwa wapatao 11,025 ambao kati yao asilimia 58 ni wanawake. Marejesho ya mikopo kutoka asasi zilizokopa kwa ujumla yaliendelea vizuri na kufikia

takriban asilimia 97. Orodha ya asasi zilizopata mikopo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2004 zimeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 1 katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ili walengwa waweze kuuelewa mradi na kufaidika nao jitihada mbalimbali za uhamasishaji zilifanyika katika wilaya zote ambako mradi unatekelezwa. Njia mojawapo iliyotumika ni kupitia kipindi cha Redio Kopa Ujiendeleze. Mkazo ulikuwa kuihamasisha jamii juu ya matumizi sahihi ya huduma za fedha na umuhimu wa kuanzisha asasi za Kifedha. Jumla ya vipindi 24 vilirushwa hewani na Redio Tanzania Dar es Salaam *(RTD), RTD* Kanda ya Kati na Kanda ya Kusini na Redio Sauti ya Tanzania Zanzibar. Uhamasishaji vile vile ulifanyika kwa kutembelea Wilaya mbali mbali na kukutana na viongozi wa Asasi, hususani *SACCOS.* Vyombo vingine vya habari pia vilitumika kutangaza shughuli za mradi kama vile televisheni, redio na magazeti. *(Makofi)*

Aidha, machapisho mbali mbali yaliyobeba ujumbe kwa lengo la kutangaza shughuli za mradi zinavyotekelezwa na jinsi wanavyoweza kufaidika yaliandaliwa na kusambazwa katika eneo la mradi. Machapisho haya ni vipeperushi nakala 3000, kalenda ya mwaka 2004 nakala 2000, dayari nakala 500 na mifuniko ya magurudumu *(wheel covers)* yenye matangazo nakala 300. Mradi uligharamia pia ushiriki wa wateja wa asasi za kifedha katika maonyesho ya wazalishaji wadogo na wajasiriamali yaliyofanyika katika mikoa ya Morogoro na Ruvuma. Lengo lilikuwa kuwawezesha wazalishaji wadogo na wajasiriamali kupata masoko ya bidhaa zao na kujifunza mbinu mpya za kibiashara toka kwa wenzao wenye uzoefu.

Mheshimiwa Spika, kupima kama mradi unasaidia kuboresha maisha ya watu wenye kipato cha chini (walengwa) utafiti ulifanyika, kujua hali halisi za kiuchumi katika jamii husika ili kupima ni kwa kiasi gani mradi umechangia kuboresha maisha ya walengwa. Mradi vile vile uliweza kufanya zoezi la tathmini ya walengwa walionufaika na huduma za mikopo ambalo lilihusisha asasi 16 na walengwa wa huduma za mikopo wapatao 191. Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Iramba, Singida, Kongwa, Dodoma, Kilosa, Morogoro, Masasi, Tandahimba, Mtwara na Lindi. Taarifa ya awali ya utafiti huu imekwisha tayarishwa. Uchambuzi unaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Aidha, mradi ulikusanya takwimu za awali kutoka wilaya 11 ambapo jumla ya watu 550 walihojiwa. Takwimu hizi zitasaidia kupima mafanikio wakati mradi ukitekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ujuzi katika utoaji na udhibiti wa mikopo, mafunzo yalitolewa kwa watendaji 271 wa Asasi za fedha zilizosajiliwa vikiwemo vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(SACCOS)* pamoja na wateja 718 wa Asasi hizo. Aidha, watendaji 40 kutoka Asasi 17 zisizo na uwezo, na uzoefu wa kutoa mikopo midogo midogo, walizitembelea asasi tatu zenye uzoefu wa muda mrefu ili watendaji hao waweze kujifunza kwa vitendo kutoka kwa wenzao. Mradi pia umeziwezesha asasi tisa kwa kuzifadhili Kompyuta 30 kwa *SIDO,* baiskeli mbili kwa *Kibaigwa SACCOS,* Kasiki za kuhifadhia fedha 3 kwa Changamoto ya Zanzibar, Utafiti Mifugo *SACCOS* na *Ushirikiano SACCOS* pia kukarabati Ofisi moja ya *Mnenia SACCOS. (Makofi)*

Vile vile wafanyakazi wa Mradi 11 walihudhuria mafunzo mbalimbali ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, Mradi uliwasilisha hesabu zake za mwaka ulioishia Juni, 2003 kwa Mkaguzi wa mahesabu kutoka Ofisi ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa ajili ya ukaguzi. Ukaguzi huo umekamilika na tayari ripoti ya ukaguzi huo imekwisha wasilishwa katika kamati ya Uongozi wa Mradi *(Project Steering Committee - PSC)* na *ADB.*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokwishaelezwa siku za nyuma, Mfuko huu ulizinduliwa Novemba 2000 na umekuwa ukitekelezwa katika Wilaya arobaini Tanzania Bara na Zanzibar, ukiendelea kuchangia juhudi za wananchi katika kupambana na umaskini na kujiletea maendeleo. Katika mwaka wa Fedha 2002/2003 jumla ya miradi 302 ya jamii ilianzishwa yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 6.8 na kufanya jumla ya miradi ya jamii kufikia 1,338 hadi tarehe 30 Juni. Miradi hii ina thamani ya shilingi bilioni 27.2. Miradi ya kujinusuru (Miradi ya Ujenzi - *PWP*) iliyoanzishwa mwaka 2002/2003 ni 120 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.62.

Mheshimiwa Spika, hadi Juni, 2004 jumla ya miradi yote ya kujinusuru (Ujenzi) imefikia 305 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 12.4. Pia majaribio *(pilot)* yamefanywa katika miradi inayolenga makundi maalum *(vulnerable and disadvantaged groups)* ambayo hadi Juni, 2004 miradi 61 ya majaribio ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Jedwali Na. 2 linaonyesha miradi iliyotekelezwa katika Wilaya za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfuko unaendelea kugharamia miradi yote inayoendelea na utekelezaji kwa lengo la kuikamilisha ifikapo Desemba ,2004, mwisho wa awamu ya kwanza ya *TASAF*. Kufuatia mafanikio yaliyopatikana Serikali na Benki ya Dunia zimekubaliana kuandaa awamu ya pili ya *TASAF* inayotegemewa kuanza rasmi Januari, 2005 katika wilaya zote Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato *(NIGP)* ilikamilisha awamu ya kwanza mwaka 2000. Tangu wakati huo, *NIGP* imekuwa ikifuatilia usimamizi wa miradi inayoendelea pamoja na kufuatilia marejesho ya mikopo. *(Makofi)*

Kwa mwaka huu wa fedha 2004/2005, *NIGP* itaendelea kusimamia rasilimali za miradi iliyokamilika pamoja na kubuni sera ya kutekeleza miradi mipya wakati jitihada za kuitafutia fedha za utekelezaji zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi kijacho itaweka mkazo katika mambo makuu yafuatayo: kukamilisha mapitio ya Mkakati wa awali wa Kupunguza Umaskini kwa kuandaa na kuchapisha Mkakati wa Kupunguza Umaskini Awamu ya Pili. Mkakati huu utakuwa ni mkakati ulioboreka zaidi kuliko wa nyuma na pia utatafsiriwa kwa lugha nyepesi na kusambazwa kwa wadau ili wauelewe na washiriki kuutekeleza.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Mkakati wa mwaka 2004 ni kupanua wigo wa jitihada za kupambana na umaskini na kuhakikisha kwamba mafanikio yaliyopatikana kitaifa yanawanufaisha wananchi wengi na hasa vijijini. Juhudi za pekee zitaelekezwa katika makundi yanayoathirika zaidi na hali ya umaskini kwa kutilia maanani maoni yaliyotolewa na makundi haya pamoja na mapendekezo ya uchambuzi shirikishi jamii wa hali ya umaskini *(PPA)*. *(Makofi)*

Aidha, shughuli za kawaida za uratibu wa utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya umaskini zitaendelea kutiliwa mkazo, zikiwemo jitihada za kujenga uwezo katika kuandaa mipango shirikishi na bora zaidi katika kupambana na umaskini uliokithiri. Ili kutoa fursa kwa wananchi kujadili na kubadilishana mawazo kuhusu harakati za kupambana na umaskini, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuandaa na kuadhimisha Wiki ya Sera na Mikakati ya Kuondoa Umaskini mwezi Oktoba, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwasiliana na wafadhili wa miradi ya *SELF* na *TASAF* ambao ni *ADB* na Benki ya Dunia ili kupata fedha za kutosha kupanua miradi katika maeneo mengine na ikiwezekana mikoa yote. Tayari mafanikio yamepatikana kama vile, *ADB* kuidhinisha upanuzi wa mradi wa *SELF* katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mwanza na Mara. Pamoja na mikoa ya awali ambayo ni Singida, Dodoma, Morogoro, Pwani, Lindi na Mtwara, jumla inafikia mikoa 14 itakayotekeleza mradi wa *SELF* kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005. Mazungumzo kati ya Serikali na Benki ya Dunia yanaendelea kufanyika ili kupanua miradi ya *TASAF* katika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kukumbusha kuwa Waheshimiwa Wabunge ni chachu kubwa katika kuleta maendeleo ya wananchi, hasa kwa kuunga mkono nguvu zao kwa kuwaelimisha, kuhamasisha na kuwashirikisha katika kutoa maamuzi na kuandaa mipango shirikishi na kuitekeleza na kufuatilia matokeo. Bado kazi ya Serikali inabakia kuandaa mazingira bora yatakayowawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti yenye mwelekeo wa kuboresha hali ya maisha ya wananchi kupitia sekta husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu la kutoa huduma kwa wananchi ili washiriki kikamilifu kwenye jitihada za kujenga uchumi wa Taifa letu siyo la Serikali tu bali hata na sekta nyingine nchini. Mojawapo ya sekta hizo muhimu ni Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo uratibu wake uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. *NGOs* ni washirika wenza katika maendeleo na Serikali inatambua na kuthamini mchango wao katika maendeleo ya Taifa. Ni kwa kutambua umuhimu wao ndiyo maana Serikali imekuwa ikijitahidi kuweka mazingira muafaka kwa *NGOs* kutenda kazi zao kikamilifu. Jitihada hizo za Serikali ni pamoja na kuandaa na kupitisha Sera ya Taifa ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kwa muda huu nikagusia kwa ufupi mambo muhimu yaliyofanyika katika mwaka wa 2003/2004. Katika kuhakikisha kwamba sekta ya *NGOs* inaendesha shughuli zake kwa ukamilifu, kanuni za kusimamia utekelezaji wa

Sheria ya *NGOs* ziliidhinishwa na Mwandishi Mkuu wa Sheria. Baadaye Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002 ilitangazwa rasmi kwenye gazeti la Serikali tarehe 12 Desemba, 2003 kwa Notisi Na. 405. Kutangazwa kwa sheria hii ambayo ilikuwa inasubiriwa sana na wadau kulisaidia sana kuweka changamoto ya kuanzisha mkakati wa pamoja kati ya Serikali na *NGOs* wa utekelezaji wake. Itakumbukwa kwamba Bodi ya Taifa ya Uratibu wa Shughuli za *NGOs* inaundwa na wajumbe toka Serikalini na wawakilishi wa *NGOs. (Makofi)*

Aidha, wadau katika sekta ya *NGOs* walipata fursa ya kukutana na kuunda Baraza la Taifa la *NGOs (The National NGOs Council)* kwa kushirikisha wawakilishi wa *NGOs* nchi nzima kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Mkoa na kitaifa, kuchagua viongozi wao na wawakilishi wa *NGOs* kwenye Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs.* Uzinduzi wa Bodi hii na Baraza la Taifa la *NGOs* ulifanyika rasmi tarehe 20 hadi 21 Mei, 2004 huko Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa Tanzania ni kubwa hivyo uratibu wa *NGOs* unahitaji mtandao makini na imara wenye kuhimiza mawasiliano ya uwazi na ushirikishwaji wadau. Hivyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005, utekelezaji wa Sheria ya *NGOs* utasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, japokuwa vyombo vingine kama vile Baraza la Taifa la *NGOs* na Mitandao ya Kimkoa na Kiwilaya vitashirikishwa ili kurahisisha utendaji kazi na uratibu. Katika suala la usajili wa *NGOs,* kulingana na Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002, kutakuwa na maofisa wa Serikali watakaoteuliwa kusajili *NGOs* katika ngazi ya Wilaya na Mkoa. Maofisa hawa watapewa mafunzo ya weledi kuhusu Sheria ya *NGOs* na Kanuni za Usajili wa *NGOs.*

Mheshimiwa Spika, usajili huu unalenga hasa kufanya mambo makuu mawili, kwanza kuwapunguzia wanachi muda wa kusafiri hadi Dar es Salaam kufuata usajili, pili, kuleta mahusiano mazuri ya kazi kati ya Serikali za Mitaa na *NGOs* kwa kuongeza nafasi ya ushiriki wa *NGOs* katika mipango ya maendeleo ya Halmashauri. Hii ni kutokana na matakwa ya Sera ya Taifa ya *NGOs* ambayo inahimiza ushiriki wa watendaji wote katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishasema awali si nia ya Serikali kuzibana *NGOs* bali kutoa nafasi kwa kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maendeleo nchini na hivyo kutenda kazi zao kwa ufanisi zaidi. Natumaini Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba pamoja na jitihada za Serikali kuweka mazingira bora kwa *NGOs* kuendesha shughuli zao nchini, pia *NGOs* wenyewe wanapaswa kujiwekea misingi ya kujiendesha wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza suala hili, Baraza la Taifa la *NGOs* kwa kushirikiana na wadau litaandaa Kanuni za Maadili *(code of conduct)* zitakazosimamia uendeshaji wa *NGOs* katika sekta hii *(self-regulation).* Uandaaji wake pia utahusisha Mitandao ya Kiwilaya, Mitandao ya Kimkoa na Kitaifa. Serikali iko tayari kushirikiana na Baraza la Taifa la *NGOs* na Mitandao hii ili kuhakikisha kwamba mahusiano kati ya Serikali na *NGOs* yanakuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuratibu shughuli za *NGOs* nchini Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa utaratibu wa kujenga kumbukumbu madhubuti wa kutunza orodha ya *NGOs* na shughuli zao kote nchini. Utaratibu huu utarahisisha ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za *NGOs* (Benki ya Takwimu). Benki hii ya takwimu itakuwa inafanyiwa marekebisho kila mwaka na kuingiza taarifa hizi kwenye Tovuti ya Taifa ili iwe rahisi kwa wananchi kuweza kupata taarifa za *NGOs* kwa kutambua ni zipi, anuani zao, ziko wapi, zinafanya nini na katika maeneo gani. Hii itasaidia sana kutandaa kwa *NGOs* na kubadilishana taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 jumla ya wafanyakazi wanne wamethibitishwa kazini baada ya kukidhi masharti ya miundo ya Utumishi na mmoja ameajiriwa kazi. Aidha, watumishi 43 wamehudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi ili kuongeza uwezo wa kufanyakazi, ufanisi, ujuzi na uwajibikaji. Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuchukua hatua za kuwathibitisha na kuwapandisha vyeo watumishi wake na kuwapatia mafunzo wanayostahili ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, teknolojia na kijamii yanayoendelea hapa nchini na duniani kote kwa kuzingatia suala zima la utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuwashirikisha watumishi, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Baraza la wafanyakazi lilifanya kikao chake cha pili tarehe 18 Machi, 2004 katika Manispaa ya Dodoma ambako masuala mbalimbali ya watumishi pamoja na mapendekezo ya bajeti hii yalijadiliwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2003/2004 imekamilisha mpango wa mkakati *(strategic plan)* wa uboreshaji wa huduma zitolewazo na idara katika hatua yake ya kutekeleza mfumo wa utendaji kazi serikalini wa kupima matokeo ya kazi *(Result Oriented Management)* watumishi wa ngazi mbalimbali wameelimishwa juu ya utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la kusambaa Jijini ofisi za kufanyia kazi lililokuwa linazikabili idara mbalimbali chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, tumeweza kutatua baada ya kupewa kwa muda jengo lililokuwa linatumiwa na Wizara za Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Nishati na Madini lililoko Mtaa wa Sokoine/Mkwepu. Ofisi imelifanyia ukarabati ili kukidhi mahitaji ya Idara hizo.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Idara za Utawala, Kuondoa Umaskini, Sekretarieti ya Muungano na Idara inayoratibu Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* zimekwishahamia kwenye jengo hilo. Ni matumaini yangu kuwa ifikapo mwishoni mwa mwezi Agosti, 2004 Idara zilizobakia zitakuwa zimehamia kwenye jengo la muda tulilopewa. Hii itapunguza gharama kwa Serikali hususan gharama za pango la Ofisi tulizokuwa tunalipa kwenye Ofisi za Idara zilizokuwa kwenye majengo ya kupanga na pia utaongeza ufanisi kwa Idara kufanyia kazi katika jengo moja. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 Ofisi ya Makamu wa Rais itajenga jengo la kudumu lenye hadhi inayostahili. Hii ni kufuatia kukamilika kwa michoro na uchunguzi wa udongo *(Soil analysis)*.

Mheshimiwa Spika, kama wote tunavyojua janga la UKIMWI limeendelea kutupunguzia nguvukazi sio tu kwenye ofisi bali hata kwa jamii kwa ujumla. Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na jitihada za kupigana na ugonjwa huu hatari kwa kuelimisha watumishi wake athari zitokanazo na kuenea virusi vya Ukimwi.

Kwa mwaka huu wa fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na *TACAIDS* itaimarisha Kamati ya Ukimwi *(Technical Aids Committee)* ili kufanya *survey* ya kutambua kiasi cha maambukizi kwa watumishi wake kwenye vituo vya Dar es Salaam, Dodoma, Pemba na Unguja kwa lengo la kuendelea kuwashawishi na kushauri waathirika kupimwa afya zao na hatimaye kupewa ushauri nasaha ya namna ya kujikinga na kutosambaza virusi kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini, ushauri, maelekezo na maagizo yake katika kufanikisha utekelezaji wa kazi na majukumu ya sekta zilizo chini ya ofisi yake kwa mwaka uliopita. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Makamu wa Rais ameendelea kutekeleza majukumu yake aliyopewa akiwa Msaidizi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, tuna kauli mbiu ya kufanya kazi kama wanafamilia na kwa kweli tuna haki ya kujivunia uongozi adilifu, madhubuti, makini, thabiti na uliosheheni hekima na busara wa kiongozi mkuu wa familia iitwayo Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wanafamilia hiyo, tunamwomba Mwenyezi Mungu amzidishie kila la kheri na kwa Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa, kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa kiongozi wetu huyo. Pia tunamshukuru yeye mwenyewe binafsi na kumpongeza Rais wetu kwa kuwa na Makamu wa Rais mwenye sifa nilizozitaja hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu ya Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wafanyakazi wenzangu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, nikianzia na kaka yangu, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mbunge wa Nachingwea na wengine chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Mwandamizi, Raphael Mollel, Katibu Mkuu Bibi Mary Issa Mushi, Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, Bwana Raymond Moshi, Wakurugenzi na Wataalamu wote ambao wameshiriki katika kuandaa hotuba hii na kukamilisha makadirio haya. Nazishukuru pia Wizara na taasisi mbalimbali ambazo kwa njia moja au nyingine zimechangia katika kukamilisha hotuba hii.

Aidha, namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapa maelezo haya kwa unadhifu wa hali ya juu kabisa. Pia nawashukuru wanahabari wote makini kwa kuwafikishia Watanzania yale tunayoyatekeleza katika kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, naomba kutoa shukrani zangu za dhati. Kipindi cha Mkutano wa 15 na Mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge mbalimbali kwa jina au kwa tukio, wamenipongeza kwa kuchaguliwa kuwa *President of the Governing Council of the United Nations Environment Programme* (Rais wa Baraza la Mazingira Duniani). Nimepokea barua na kadi za pongezi. Nawashukuru wote hao bila kusahau Kamati ya Waheshimiwa Wabunge Wanawake kwa zawadi walizonitunukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowaambia wana taaluma ya habari niliporejea kutoka Jeju, Korea ya Kusini, shukrani haswa zimrudie Mwenyezi Mungu, wazazi wangu, Chama changu cha CCM, wapiga kura wa Jimbo la Muhambwe na Watanzania wote wenye nia njema na wenye kuthamini mchango wa utumishi wetu sisi viongozi watumishi kwa nchi na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutoa shukrani nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumshukuru kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa barua yake ya kunipongeza kwa kuchaguliwa kwangu. Barua ya Mheshimiwa Makamu wa Rais imenitia moyo wa kuzidi kujitahidi kuitumikia nchi yangu kwa kila hali na mali kwa majaliwa ya Mwenyezi Mungu. Barua hiyo nitaienzi, nitaitunza na kuihifadhi kama mwongozo wa kudumu katika utumishi wangu kwa Taifa langu na kwa maisha yangu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya maswali niliyoulizwa baada ya kuchaguliwa ilikuwa Tanzania itanufaika vipi kwa kuchaguliwa kwako? Katika sala kabla ya kuanza kila kikao cha kila siku ya Mkutano wa Bunge tunakiri kuwa Mwenyezi Mungu ameweka mabaraza ya Kimataifa ili haki itendeke kama apendavyo yeye. Tanzania tunashiriki katika mabaraza hayo kwa mfano Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa na mashirika yake kama vile Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira.

Tarehe 29 Juni, 2004 mjini Sirte nchini Libya, kwa niaba ya Tanzania, niliweka sahihi mkataba wa kutekeleza mradi wa kujenga uwezo *(capacity building)* kwa Watanzania. Mradi wenyewe ingawa si wa fedha nyingi, dola za Marekani 358,000 kwa kipindi cha miaka minne, ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa Ushirikiano Mpya kwa Maendeleo ya Afrika katika nyanja ya mazingira *(NEPAD Environmental Initiative).* Mwisho wa mradi huo naamini kwa kiasi fulani Tanzania tutakuwa tumejenga uwezo wa kutatua baadhi ya matatizo ya masuala ya mazingira kwa manufaa na ustawi wa watu wetu wote kama inavyosema sehemu ya dua, kila asubuhi kabla ya kuanza shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa wahisani mbalimbali ambao wamekubali na wameendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kugharamia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Wahisani hao ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO),* Shirika la Misaada na Maendeleo la Norway *(NORAD), Nordic Development Fund, FINNIDA,* Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* Serikali ya Finland, Serikali ya Japan,

Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DFID),* Shirika la Maendeleo la Uswisi *(SDC),* Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF),* Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira *(UNEP),* Sekretariati za Mikataba mbalimbali ya Mazingira na wengineo. Tunawashukuru kwa kuchangia kwa hali na mali juhudi zetu za kujiletea maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26, Makamu wa Rais, katika mwaka huu wa fedha 2004/2005, kiasi cha shilingi 1,485,900,700/ = kinaombwa kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida ya Makamu wa Rais *(Private Office).* Kati ya fedha hizi shilingi 184,829,800/= ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi na shilingi 1,299,070,900/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengine ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mwaka 2004/2005, Ofisi ya Makamu wa Rais inaomba kiasi cha shilingi 17,315,112,700/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 378,045,500/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 16,383,186,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges).* Ruzuku kwa *NEMC* ni shilingi 553,881,200/= ambazo kiasi cha shilingi 357,625,500/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 196,255,700/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kiasi cha shilingi 11,977,915,500/= kitapelekwa Zanzibar kwa ajili ya shughuli za Muungano *(Union Government Contribution).* Kiasi cha shilingi 11,043,071,400/= kinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kati ya hizo shilingi 671,699,700/= ni fedha za ndani na shilingi 10,371,371,700/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nakushukuru sana kwa kunisikiliza, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kifungu Na. 81(1) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2003/2004 pamoja na maoni juu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii kwa masikitiko makubwa kuwapa pole za dhati familia na wananchi wa Jimbo la

Mbeya Vijijini, Mkoani Mbeya, kwa kufiwa na Mbunge wao Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, tarehe 24 Juni, 2004 hapa mjini Dodoma. Pia nachukua nafasi hii kuwapa pole familia na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, Mkoani Morogoro, kwa kufiwa na Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, usiku wa kuamkia tarehe 22 Julai, 2004 hapa mjini Dodoma. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki kupitia Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati yangu ikipitia na kuchambua taarifa husika zilizowasilishwa mbele ya Kamati na Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam tarehe 27 Mei, 2004 masuala yaliyojadiliwa ni dira na Mwelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Rais, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mwaka 2003/2004, mwelekeo kuhusu Mapato na Matumizi kwa kipindi kilichopita (2003/2004), mafanikio na matatizo ya utekelezaji katika kipindi kilichopita (2003/2004), kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati na maombi ya fedha za matumizi katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, dira ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni kuona kwamba Tanzania inaondokana na umaskini uliokithiri, mazingira bora, Muungano imara na kuona kuwa kuna ushiriki makini katika maendeleo ya asasi zisizokuwa za Kiserikali *(NGOs)*.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais ina jukumu la kumsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majukumu yake kama Msaidizi Mkuu wa Rais. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais ina majukumu yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia shughuli zote za Muungano;
- Kuratibu shughuli za kuondoa umaskini;
- Kuratibu masuala ya mazingira; na
- Kuratibu shughuli za Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata bahati ya kutembelea na kuona shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Kamati imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Makamu wa Rais inavyotekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais ni kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mawaziri wenye dhamana ya ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imeweza kuyatekeleza maagizo yote ya Kamati kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa Matumizi ya Kawaida katika kipindi cha mwaka 2003/2004 unaridhisha kwani Ofisi ya Makamu wa Rais hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili, 2004 ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 16,476,692,317/= kati ya shilingi 16,754,633,950/= ilizopangiwa kwa kipindi cha mwaka mzima. Kiasi hicho kilichotumika ni sawa na asilimia 98.7 ya makadirio yote.

Hata hivyo, Kamati haikuelezwa jinsi Ofisi ya Makamu wa Rais ilivyotumia fedha za maendeleo katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kutokana na kwamba taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati hazikutoa mchanganuo ulio wazi wa matumizi hayo. Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa inatoa mchanganuo unaoeleweka wa Mapato na Matumizi ya fedha za maendeleo kama ilivyofanya kwa shughuli za matumizi ya fedha za kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo ya Muungano, gawio la 4.5% liliendelea kutolewa na Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha, tulielezwa kuwa vikao vya Mashirikiano kati ya Serikali hizi mbili kwa Wizara zisizo za Muungano, vilifanyika Dar es Salaam na Zanzibar chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaendelea na matayarisho ya Sheria Mama ya Mazingira, tunaamini kuwa Baraza la Mazingira *(NEMC)* limepewa nafasi yake ndani ya sheria hii. Hivi sasa bajeti inayotengwa kwa ajili ya *NEMC* ni ndogo sana hivyo kusababisha majukumu mengi ambayo yanapaswa kufanywa na Baraza hili kutofanyika kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kutosha. Kazi nyingi za udhibiti wa mazingira zimekuwa zinafanyika Dar es Salaam zaidi kuliko sehemu nyingine za nchi kutokana na upungufu huo huo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *TASAF* uenezwe nchi nzima kwani Wilaya ambazo *TASAF* ipo maendeleo ya jamii yanafanyika kwa uhakika na ushiriki wa wananchi unakuwa hauna mashaka. Kamati inashauri jitihada hizi za kueneza mfuko huu nchi nzima zifanyike. Hii ni njia mojawapo ya kupambana na umaskini na ni njia ya kutekeleza mkakati wa maendeleo ya *millennium.*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais pia imekuwa ikiratibu Mfuko wa *SELF.* Mfuko huu umekuwa ukitoa mikopo kwenye asasi zenye uzoefu wa kutoa mikopo kwa walengwa. Asasi hizo sehemu nyingine hazipo ama hazina uzoefu wa kutosha. Hivyo ni vizuri *SELF* ifanye tathmini ya utekelezaji wake na ione ni vipi changamoto kubwa ya kutoa mikopo kwa walengwa inafanyika haraka na kwa matarajio ya kufanikiwa kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Msitu wa Amani huko Tanga na Hifadhi ya Ngorongoro. Huko tuliona dhahiri uharibifu wa mazingira. Kwenye Msitu wa Amani, wachimbaji wadogo wadogo wa madini wameharibu sana vyanzo vya maji na kuharibu kabisa Msitu wa Amani. Huko *Ngorongoro National Park* wako watu wanaojiingiza na kulima ndani ya hifadhi na hivyo kuharibu mazingira.

Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwa mratibu wa shughuli za hifadhi ya mazingira ikae na wadau wote ili ufumbuzi upatikane na hatimaye kuondokana na uharibifu huu isiachiwe Wizara moja moja kutoa kauli ambazo zinagongana na hali halisi au zinasababisha utekelezaji kukwama.

Mfano mzuri ni uchimbaji haramu wa madini katika Msitu wa Amani. Wizara ya Nishati na Madini wamekwenda kule na kuwaahidi wananchi kuwa watapimiwa maeneo wakati huo huo maeneo hayo ni sehemu ya vyanzo vikuu vya maji kwa mji wa Tanga. Sera ya Maji inasema: "Vyanzo vya maji visiharibiwe, vihifadhiwe." Huku kuna msitu wa Taifa lakini wachimbaji hawa wanakwenda kuchimba hadi ndani ya msitu na kung'oa kabisa miti yake iliyotunzwa kwa miaka mingi. Ndio maana Kamati inapendekeza wadau wote yaani Wizara ya Nishati na Madini, Maliasili na Utalii, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Makamu wa Rais wakae chini na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la Msitu wa Amani na maeneo mengine Mkoani Tanga. Yafaa hatua za haraka sana zifanyike vinginevyo tutakuwa tunatafuta majibu kwa hali ambayo imekwishaharibika kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo tunapenda lipewe uzito wa pekee ni matumizi ya mifuko ya *plastic.* Kamati toka muda mrefu imekuwa ikifuatilia suala hili la mifuko ya plastic ambayo imezagaa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mategemeo yetu yalikuwa kwamba mapendekezo yetu kwa Serikali yangekuwa yanapunguza kuenea ovyo kwa mifuko hii kinyume chake nchi nzima imejaa mifuko hii. Madhara yake ni makubwa sana. Nchi nzima inaonekana imejaa uchafu huu kila mahali kisha ardhi yetu inakufa kwani mahali pale ambapo mifuko hii imefukiwa hapaoti kitu, wanyama kama ng'ombe na mbuzi wanakula mifuko hii na kufa. Kwa kuwa mifuko hii haiozi ndio kusema kadri miaka inavyopita basi ardhi inakuwa mifuko ya plastic tu. Hatima ya nchi hii ni nini?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Serikali imesema ndani ya Bunge lako kuwa itatoza kodi wale wote wanaoingiza mifuko hii. Kwa uhakika kodi haikupunguza mifuko hii badala yake mifuko imeongezeka sana. Serikali haikueleza ni fedha kiasi gani ilipata kutokana na kodi hiyo. Je, mafanikio ya uamuzi huu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeitaka Serikali kutamka bayana kufutwa kwa matumizi ya mifuko hiyo. Muda utolewe kwa wafanyabiashara kutengeneza mifuko ambayo inaweza kuoza. Aidha, wananchi waendeleze ufundi wao wa kutengeneza mifuko na vikapu vizuri ili kujipatia mapato huku wakihifadhi mazingira aya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kufikiri kuwa ipo hujuma inayofanywa dhidi ya nchi yetu. Kwa mfano, vile vimfuko vyembamba vya plastic havirejerezeki, hupatikana bure hata vijijini kwani hutengenezwa kwa mabaki ya mazao ya petroli. Wakikosa mahali pa kutupa mabaki hayo basi hutengeneza mifuko hiyo. Je, Tanzania haitumiki kama jalala la uchafu wa nchi nyingine katika umbile la bidhaa kama hii ya *plastic?* Wakati umefika wa kukataa hujuma kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Julai, 2004, tulikutana na Chama cha Watengenezaji wa Bidhaa za *Plastic* hapa nchini. Waliomba kukutana na Kamati kutokana na Kamati kuagiza Serikali kutoa tamko la kuzuia utengenezaji na uingizaji wa mifuko nchini ile membamba ya plastic ambayo imezagaa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipotoa tamko hilo kwa Serikali, ukweli wa mifuko ulikuwa haufahamiki vizuri. Kila pendekezo la kutokomeza mifuko hii lilikuwa halifanyiwa kazi. *NEMC* iliahidi kufanya uchambuzi wa kitaalam ili kupata njia ya kutokomeza uchafu huu wa mifuko hii ya *plastic* hata uchambuzi huu haukuweza kutekelezeka. Baada ya kuagiza Serikali kupiga marufuku mifuko hii, ndipo wahusika wamejitokeza. Hata hivyo, bado tunaamini kuwa ukweli wa ndani haujapatikana.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho, tuliwakaribisha Mawaziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais na kuwahoji kwa kutokuona kuzagaa kwa mifuko hiyo kama ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, tulishangazwa kupita kiasi na Wizara ya Viwanda na Biashara ambapo wenyewe hutoa leseni za kujenga viwanda hivyo pamoja na leseni za kuingiza bidhaa hizo kutoka nje, Wizara ya Fedha haikuleta hata mwakilishi wake kwenye mkutano huo. Hivyo tulielewa kwa nini suala hili la kusambaa kwa mifuko hii limekuwa gumu kupata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hicho Chama cha Watengenezaji wa Bidhaa za *Plastic* kinasema kuwa hakuna haja ya kuzuia uzalishaji au uingizaji wa mifuko hii kwani uchafu uliopo si kitu cha kutisha ukilinganisha na nchi kama Kenya, Ujerumani, Ufaransa na kadhalika. Wakati huo huo wanasema vipo viwanda 50 vinavyotengeneza bidhaa hii ya *plastic.* Kiwanda ambacho kinaweza kurejereza *plastic* hadi sasa ni kimoja tu ambacho kimefadhiliwa na *UNIDO* ambacho kimekamilika hivi karibuni na kipo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, fikiria Dar es Salaam peke yake mifuko imezagaa kila mahali sembuse Mikoani ambapo hata ukifanya nini haiwezekani kukusanya *plastic* hizo kutoka huko na kuzifikisha Dar es Salaam. Wao wanadai kuwa ajira na kipato kitapatikana kwa wananchi ambao watakuwa wanakusanya mifuko na *plastic* nyingine. Tunakubali lakini mnunuzi ni nani?

Mheshimiwa Spika, mfumo wa shughuli hii hata Chama hiki hakijauanza. Mbaya zaidi uko ubishi iwapo hiyo mifuko membamba ya *plastic* inaweza kurejerezwa au la. Kamati imeelewa kuwa watengenezaji na waagizaji wa mifuko hii wanapata nguvu kutokana na Serikali kutokuwa na msimamo wa pamoja juu ya taka hizi za mifuko ya *plastic. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali itakuja na msimamo wa pamoja kuhusu tatizo hili vinginevyo nchi yetu na ardhi vitaathirika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati ya Maliasili na Mazingira imeyapitia makadirio na matumizi kwa kipindi cha 2004/005 na inakubaliana na ombi la Ofisi hii, hivyo basi tunashauri Bunge lako Tukufu kuyapitisha Makadirio haya. Kiasi kinachoomba ni jumla ya shilingi 29,842,084,800/=. Kati ya kiasi hiki shilingi 1,483,900,700/= ni kwa ajili ya Fungu Na. 26 la Makamu wa Rais na shilingi 28,358,184,100/= ni kwa ajili ya Fungu Na. 31 la Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha taarifa hii, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi wote wawili walioshughulikia masuala ya Muungano, Mazingira na Kuondoa Umaskini, Mheshimiwa Arcado Ntangazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Katibu Mkuu Mwandamizi Bwana Raphael Mollel, Katibu Mkuu, Bibi Mary Mushi pamoja na wataalam na watendaji wengine wa Ofisi hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa kwa makini Mpango na Bajeti hii. Ubora wa taarifa zao ndio uliotuwezesha kukamilisha kwa ufanisi mkubwa wa zoezi zima la kupitia na kuchambua Makadirio ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa ushirikiano walionipa hadi kuniwezesha kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Kipenka Mussa na Katibu wa Kamati hii, Bwana Sam Manamba kwa kazi nzuri walizozifanya za kuratibu shughuli za Kamati hii katika kipindi chote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, mimi nimepangiwa kufanya mazungumzo na wageni niliowatambulisha asubuhi, Wabunge wa Uingereza. Sasa nitamwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda, aje apokee kiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anne Makinda, ataongoza Bunge mpaka kipindi cha jioni wakati wa kuahirisha Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. KARIM SAID OTHMAN (k.n.y. MHE. ALI SAID JUMA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naomba nami kujadili hotuba ya ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Kuondoa Umaskini, nasimama hapa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kutoa maoni kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu Na. 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia za Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, waliofariki ghafla tukiwa hapa Dodoma kwenye kikao hiki cha Bajeti. Misiba hii hakika imegonga mioyoni mwetu na

kwa kweli ni lazima niseme na nikiri kwamba haijapata kutokea. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali zinapostahili. *Amin.*

Aidha, natoa pole kwa Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mbunge wa Pandani, kwa kifo cha baba yake mpendwa. Pia nawapa pole Waheshimiwa Wabunge wote waliopata matatizo kwa namna yeyote ile, Mwenyezi Mungu awape subira. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo na wataalam wao kuleta hapa Bungeni bajeti yao ya kuliomba Bunge kutoa idhini ya kupata shilingi 29,842,084,800/= kwa nia ya kutekeleza na kusimamia mipango iliyopangwa chini ya ofisi hii kwa kipindi cha fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawapongeza Mheshimiwa Mbunge wa Chambani, Pemba ambae pia ni Msemaji Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais Kuondoa Umaskini pamoja na wananchi wa Jimbo lake la Chambani kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika matayarisho ya hotuba hii. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile kwa mchango wake mkubwa alionipa katika kuandaa na kuiboresha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini ni neno ambalo limezoeleka sana kutajwa miongoni mwa viongozi wetu wakuu wa nchi kama vile ni jambo la kawaida tu na kinachofanyika ni kuunda Kamati za kuondoa huo umaskini kama vile ni kitu kimekaa sehemu fulani na inatakiwa kiondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa umaskini mkubwa wa mtu ni ule wa kutokufahamu haki yake ya msingi. Hata kama Wizara zote zitakuwa ni za kuondoa umaskini bila wao wananchi kuelewa haki zao na wanatakiwa wazilinde vipi bado ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini wa nchi au wa mtu hautaondoka kwa kumpa pesa za kufanyia biashara bila ya kumwelekeza na kumwongoza kwa kile anachokifanya ili kimpatie pesa. Mfano, kama ni mkulima jaribu kumtafutia soko na bei ya kuuzia iwe nzuri kama ni mfanyabiashara mwonyeshe mbinu zitakazomfanya aweze kuuza zaidi na kupata faida zaidi ili mzunguko wa biashara yake uongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini wa mtu maana yake ni umaskini wa nchi na umaskini wa nchi maana yake ni umaskini wa Viongozi watendaji *(Planners)* kushindwa kuyashinda na kunufaika na mazingira yanayoizunguka nchi husika. Kwa upande wa nchi kama yetu ambayo Mwenyezi Mungu ametupa kila aina ya utajiri kuanzia Madini Maziwa, Mbuga za Wanyama, Mito mikubwa na ardhi yenye rutuba. Hivyo umaskini kwa maana ya Wazungu na Wawekezaji wanaokuja Tanzania ni Ufinyu wa kuweza kufikiri na kupanga na *to take advantage of natural resources* na maana nyingine ni wao kutumia *Principle* za biashara za *minimize cost maximize profit* kutoa kitu kidogo na kupewa haki ya kumiliki kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye anaweza kumwonea huruma mwenzake na kumpa pesa bila ya kazi ili zimsaidie tu, bila ya kutegemea au kuwa na njia zingine za uficho za kulipwa pesa zake. Hivyo kutegemea wafadhili watupe pesa za kuondoa umaskini ni kiini macho ambacho bado hatujagundua, kuna nini ndani yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mission* na *Vision* za viongozi wetu katika kupambana na kushinda mazingira yaliyotuzunguka ndio njia pekee ya kushinda na kuikomboa nchi yetu kwenye lindi la umaskini uliokithiri, ni kuwaonyesha njia mbadala na yenye mwelekeo kwa wananchi, kama ni wafanyabiashara wahamasishwe wafanye biashara ambayo upatikanaji wake kwenye eneo walilonalo au wanaloishi na soko lake liandaliwe badala ya kuwapa mikopo kwa proposal hewa isiyokuwa na mradi halisi. Badala ya kumsaidia inazidisha ubadhirifu kwenye kitengo husika. Mifano ipo mingi ni wangapi wamekopa mpaka kufilisi iliyokuwa Benki ya Nyumba na umaskini uko pale pale! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu katika kupambana na umaskini ni kitu cha umuhimu. Hali halisi ya takwimu zetu zinazotumiwa na Serikali zina walakini mkubwa kwani vyanzo vyake vinafanywa kwa ajili ya kuwafurahisha watu fulani badala ya kutoa hal halisi ya agenda inayohusika, mfano mzuri ni takwimu zilizokuwa zinatolewa na Wakuu wa Wilaya kwa Serikali kuhusu hali ya njaa kwa kipindi kilichopita. Sasa huu ni mfano tu wa takwimu zisizo sahihi kuhusu mipango na mikakati ya kuondoa umaskini.

Takwimu za chakula na mazao mengine mara nyingi huwa ni za Manzese na Tandale Uzuri tu bado tunahitaji takwimu za Handeni, Tandahimba, Kibondo, Pemba Newala, Unguja, Nzega, Singa Chini, Babati, Hanang na pengine pengi ili wigo ukue na utupe hali iliyokaribu na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali wanakusanya taarifa muhimu kuhusiana na umaskini, kwenye nyanja za makazi, mapato na matumizi kwa familia ziishizo Mijini na Vijijini, takwimu juu ya idadi ya watoto wanaoshindwa kumaliza elimu ya msingi, nguvu kazi iliyo Vijijini na Mijini lakini haitumiwi. Taarifa au takwimu hizi haziwi za kutoa mwanga kwani wakusanyaji huwa na vigezo ambavyo huwa ni kulingana na mtu au shirika lililotoa fedha za utafiti limetaka nini na takwimu ni za matumizi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini wa Taifa letu hauwezi kumalizwa kwa misaada toka kwa wafadhili au sera na mipango ambayo hutengenezwa katika ngazi ya Kitaifa.

Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa baada ya kumkomboa mwananchi kifikra kuelewa haki zake na nchi yake na baadae wananchi wenyewe washirikishwe kuchagua mbinu mbadala katika uendeshaji wa maisha yao ya kila siku, kwa kuzingatia kipindi cha Dira ya Kuondoa Umaskini 2025, Watanzania tunaweza kabisa kujiondolea umaskini kwa kuelewa jinsi ya kumiliki na kutumia vizuri maliasili iliyo kwenye mazingira tunamoishi. *(Makofi)*

Naomba nikumbushe kidogo maneno ya Muasisi wa Tanzania na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere ambapo aliuliza kuwa ninanukuu: "... *a development process is Nationally owned or externally imposed"? "In 1988, Tanzania's per capita income was $280, in 1998, it is $140, so what went wrong?"* Mwisho wa kunukuu.

Maneno haya ni kwamba Tanzania haina mkakati wake wa kuondokana na umaskini ila mkakati tunaoambiwa tumeletewa na washauri toka nje ambao hali halisi ya Mtanzania hawaijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa mkakati wa kweli wa kuondoa umaskini na kuiendeleza nchi yetu, mhusika mkuu ni mwananchi mwenyewe, yakishatengenezwa mazingira ya kuelewa haki yake na jinsi ya kuidai na kuitetea, hii italeta heri ya uwajibikaji, kuthamini na kuheshimu chochote atakachokuwa anakifanya yeye au mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi kama Tanzania ambayo zaidi ya 80% ya wananchi wake wanaishi kwa kutegemea kilimo na sera ya Taifa ya mkakati wa kuondoa umaskini *(PRSP)* haionyeshi na kusema chochote juu ya kulinda masoko ya ndani, kutoa ruzuku kwa wakulima na kuimarisha viwanda vyetu vya ndani kitu ambacho ni msingi katika uondoaji wa umaskini.

Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuwa umaskini utaondolewa na sisi wenyewe na sio Mataifa ya nje. Wahisani na Serikali zao wanashauri Serikali kupiga marufuku kutoa ruzuku katika Sekta ya Kilimo wakati wakulima wao wanapewa ruzuku. Hapa kweli si wanatunywesha sumu badala ya kutupa tiba ya kuondoa umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kwa dhati kabisa inampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Rashid Mfaume Kawawa, kwa mkakati wake aliokuwa ameuanzisha wa Kilimo cha Uyoga na kutoa ushauri kwa wananchi juu ya kilimo hicho.

Sasa tunaomba kumuuliza Waziri mwenye dhamana ya kuondoa umaskini ni juhudi gani na Msaada upi alioutoa kwa Mheshimiwa Rashid Kawawa, kuhakikisha kilimo cha Uyoga kinakua kwani uzalishaji wake ni wa muda mfupi na soko lake likoje kwa ujumla? Sio hilo tu kilimo cha mwani baharini ni zao linalozalishwa kwa muda mfupi tu.

Mheshimiwa Edward Lowassa akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, alizishauri jamii zote ziishizo kwenye ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi kujishughulisha na kilimo cha zao hilo badala ya kutegemea uvuvi tu. Mheshimiwa Edward Lowassa alionyesha nia yake katika kuwaondolea umaskini wananchi wa maeneo hayo kwa kutoa motisha kwa vikundi vya miradi ya akina mama inayolima zao la Mwani.

Takwimu zinaonyesha kuwa wastani wa pato kwa mwaka la mkulima wa kawaida wa kilimo cha mwani Zanzibar ni *USD 1,000.* Wakati kwa mvuvi wa kawaida ni *USD 600.* Serikali inafanya nini kueneza zao hilo kwani halina cha msimu, Mwambao wote wa pwani kuanzia Tanga mpaka Mtwara na visiwa vya Unguja na Pemba. Hiki ni Kilimo ambacho kama kikielimishwa vizuri na Wizara yenye dhamana ya kuondoa umaskini tunaamini lengo la kuondoa umaskini linaweza kufikiwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa kama juhudi zilizokuwa zimeanzishwa na Mheshimiwa Edward Lowassa zitatiliwa mkazo, wananchi waishio mwambao wa Bahari ya Hindi wangeweza kuliingizia Taifa kipato na wao watakuwa na uhakika wa wastani wa pato lisilopungua *USD 2,000* kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na hivyo ili kuwa na kipimo sahihi cha kupambana na umaskini ni lazima tuangalie kwa wenzetu nao vipi? Kwa kufanya hivyo ni lazima tuwe na kipimo kimoja, *(Common denominator)* ambacho ni dola ya Kimarekani au *Euro Currency.* Vinginevyo tutakuwa tunashindana bila kuwa na mwamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani baada ya kupitia takwimu za mipango na matumizi, uendeshaji Serikali na Huduma nyingine, inaonyesha kuwa toka 1997 mpaka 2003 kumekuwepo na badiliko la kushuka katika *percentage* baada ya kutumia *Exchange rates* za miaka husika kwenda kwenye *USD,* ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1997 ni asilimia 44, mwaka 1998 ni asilimia 16, mwaka 1999 ni asilimia 0.4, mwaka 2000 ni asilimia 0.3, mwaka 2001 ni asilimia 0.3, mwaka 2002 ni asilimia 0.2 na mwaka 2003 ni asilimia 0.4. Hii inaashiria kuwa bado Sekta za Elimu, Afya na Huduma nyingine bado hazijawezeshwa sawasawa ili kuwa katika mwelekeo wa kumwondolea Mtanzania umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa tutumie vizuri na tuwe na Sera nzuri ya wahitimu wa vyuo vyetu kwani, *SUA* tuna wataalam wa kilimo, Mzumbe wataalam wa uongozi na utawala, *IFM,* tuna watu wa Fedha, *UDSM* watu wa uchumi na kila mwaka wahitimu wanakuwepo. Kinachotakiwa ni kuweka pamoja hizo taaluma katika makundi na Serikali kuwa mdhamini wao kwenye vyombo vya fedha baada ya kuwatengenezea miundombinu na wao waendelee. Kwa njia hii nguvu kazi iliyokuwa Vijijini itatumika na ujuzi wa wahitimu na maana halisi ya Serikali kusomesha wataalam Chuo Kikuu itaonekana. Kambi inaamini kwa mkakati huu punguzo la umaskini halitakuwa kwenye makaratasi tu kama ilivyo sasa na wananchi wataweza kupima hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni dhana pana inayohusisha Wizara zote kwa upana wake. Juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais bado hazijaweza kuhakikisha usalama na usafi wa mazingira kwa upana wake, kwani mazingira yanahatarishwa na pande mbili yaani matajiri na maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kwanza wa matajiri, huwa ni uharibifu wa mazingira katika utumiaji wa kemikali ambazo huathiri mazingira pindi ziingiapo kwenye ardhi, kwenye mito na mabonde yatumiwayo kwa kilimo cha mboga mboga kama vile bonde la Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na takwimu zilizotolewa na *Senior Industrial Engineer, Vice President Office, Ms.* Angelina Madete, kuwa Kemikali zinazoingizwa nchini kwa mwaka kwa matumizi ya viwandani ni tani 210,250 na tani 81,500 kama dawa za kuulia wadudu waharibifu wa mazao na mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki cha kemikali ni kikubwa na uhifadhi wake na matumizi yake ni kitu ambacho kinataka udhibiti wa kitaalam, lakini kutokana na sababu zisizoweza kuzuilika kutokana na uwezo mdogo wa kifedha na kitaaluma udhibiti wake huwa na matatizo ambayo husababisha uchafuzi mkubwa na wa hatari kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uharibifu wa mazingira ni suala la kijamii na kiuchumi. Kiuchumi suala hili linaendana na mfumo wa uzalishaji moja kwa moja. Mfano ni vumbi na moshi mzito unaotakana na uzalishaji wa *cement (Air Pollution),* hii inahatarisha afya za wakazi katika maeneo husika na mimea inayooteshwa jirani, sio hilo tu na madhara makubwa pindi moshi huo unapochanganyika na mvua na kurudi kwenye udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila eneo la uzalishaji ambapo kwa njia moja ama nyingine kemikali inatumika lazima *waste products* yake iwe ni hatari kwa mazingira, matatizo makubwa ni jinsi ya kukabiliana na hizi *waste products* zitokanazo na uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili unahusu umaskini ambapo uharibifu unakuwa mkubwa kadri idadi ya watu inavyoongezeka Vijijini. Hii inatokana na kutokuwa na shughuli mbadala ya kuongeza kipato kwa haraka zaidi mbali na kutumia maliasili iliyomzunguka. Ukali wa maisha ni suala linaloleta kasi kubwa ya uharibifu wa mazingira katika nyanja zote za maliasili; misitu, uvuvi na uchimbaji madini. Suala hili ni la hatari kubwa kwa nchi yetu, hivyo umaskini ni kitu kinachoendana moja kwa moja na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu hafifu zinazotumika katika kilimo husababisha uharibifu wa mazingira katika maeneo ya kando kando mwa mito na barabara, aidha uharibifu mwingine wa mazingira ni hasa kwenye udongo kutokana na matumizi ya mara kwa mara na yasiyo na kipimo ya madawa ya kuulia wadudu, magugu na mbolea ya chumvi chumvi. Mkusanyiko wa hayo yote kwa kiasi kikubwa kwenye udongo husababisha udongo kuwa sumu na mimea kushindwa kustawi kama ilivyotarajiwa kitu kinachopelekea kufanyika juhudi kubwa ili ardhi irudie hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri matumizi ya madawa na mbolea za chumvi chumvi wauzaji wawe na elimu ya kutosha ili wawaelekeze wakulima

viwango sahihi vya matumizi yake badala ya wakulima kutumia madawa hayo na mbolea bila ushauri wa wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu kama unavyoendeshwa na wakazi wa Kijiji cha Nalingu-Mkoa wa Mtwara na kutotii amri na sheria kupingana na mpango wa Wizara ya Maliasili na Utalii juu ya Uanzishwaji wa *Marine Park* katika eneo hilo.

Kambi ya Upinzani inaliona hilo kama dalili mbaya zaidi kwa jamii katika kutetea na kulinda njia za kujipatia riziki yao, hivyo wako tayari kuua au kuuawa kama ambavyo ilivyojitokeza wakati wa Kamati ya Maliasili na Mazingira walipotembelea Mkoa wa Mtwara na kufika Kijijini hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondokana na tatizo hilo si kugombana nao kwa nguvu za dola bali ni kuwaonyesha njia mbadala ya kuongeza kipato chao ili kukabiliana na ukali wa maisha kama nilivyokwisha pendekeza kwenye uondoaji umaskini kwa jamii ziishizo mwambao mwa bahari. Kilimo cha mwani ndio njia mbadala ya kutunza mazingira ya bahari na wakati huo pato lao na la Taifa linaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* utendaji kazi wake haupewi kipaumbele katika kupatiwa vifaa vya kuiwezesha kutenda kazi zake za msingi *to set International safe environmental standards* katika maeneo yote yanayohusu uzalishaji. Hili la kuweka viwango sio jambo la kuangalia kwa macho tu, inatakiwa iwezeshwe kuwa na maabara ya kisasa ambayo itashughulika na mambo yote yahusuyo mazingira na kuweka miongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii hata tafiti zinazofanywa na Baraza hili zitakuwa na umuhimu na kuheshimiwa na watu na makampuni yanayowekeza nchini ambayo yanashindwa kutekeleza mambo yaliyomo kwenye Mikataba yao kuhusiana na utunzaji wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inategemea *NEMC* kuwa imeishatoa taarifa kuhusu shughuli za uchimbaji madini zinazofanyika Mkuyuni na Matombo Mkoani Morogoro na wachimbaji wadogo wadogo ambao hutumia *mercury* na maji yanayotumiwa na wakazi wa Dar es Salaam vyanzo vyake ni huko, hatujui Serikali inalionaje tatizo hili ambalo madhara yake yatakuwa ni makubwa kwa miaka ya mbeleni kwa wananchi watumiao maji ya mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa Madini unaofanywa na wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo mbalimbali kwa kutumia vifaa duni na vya hatari sio tu kwa maisha yao bali pia kwa mazingira husika.

Aidha, wafanyabiashara wanaofyeka Misitu ya hifadhi kama vile Msitu wa asili wa Amani kwa ajili ya kusafirisha magogo na mbao na kuharibu kabisa vyanzo vya maji na mazingira ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu, Baraza la Mazingira linatakiwa litoe *Air Pollution Acceptable Standard* sio kukuta wanapochomea takataka za Mijini, moshi umezingira makazi ya watu kitu ambacho ni hatari kwa afya za wananchi. Aidha, *Management disposal standards* ya kuchoma taka Mijini ieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa yote hayo, elimu ya kutosha itolewe jinsi ya matumizi endelevu kwenye sekta husika, ili na wao wapate faida ya hiyo maliasili isiwe tu kwa wachimbaji au wafanyabiashara wakubwa tu kwani kila Mtanzania ana haki na utajiri wetu wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo namalizia kwa kusema, nampongeza tena Mheshimiwa Ntagazwa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Mazingira Duniani, hivyo basi dosari za uharibifu wa mazingira Tanzania zitatoweka kama sio kwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Ofisi hii ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijafanya hayo kwanza nami niungane na Waheshimiwa Wabunge kutoa mkono wa pole kwa jamaa, marafiki pamoja na wapiga kura wote na familia ya Waheshimiwa ambao tulikuwa nao hapa Bungeni nikianza na Mheshimiwa Kasapira na Mheshimiwa Mwalyego. Mungu azilaze roho hizo za marehemu peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau ni juzi tu Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mbunge wa Pandani, naye alifiwa na baba yake, pia naye nimpe mkono wa pole nikimwambia kwamba mauti ni barabara kila mtu ataikanyaga, ama mauti ni maji kila mtu atakunywa na sote tupo katika foleni, tutafika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikimsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati akisoma hotuba yake na nilikuwa nikimsikiliza kwa makini mno. Kwa kweli moja ambalo nataka nilinukuu katika hotuba yake ni suala la kuondoa umaskini na hasa vijijini.

Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa namna ambavyo aliweza kuwasilisha hotuba yake na mambo kadhaa ambayo ameyaorodhesha katika kitabu hiki, mimi niseme kwamba sina pingamizi nalo sana hotuba hii. Isipokuwa inataka kuboreshwa na kwa kweli yaliyotajwa kufanikishwa na siyo kuandikwa na badala yake yakasahaulika yaliyozungumzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Wizara hii hasa *TANAPA* kwa kuanzisha Mfuko unaoitwa Mfuko wa Ujirani Mwema. Huu Mfuko ni kama alivyoeleza Mheshimiwa Wanyancha. Umebadilisha mtazamo wa wananchi kwa wanyamapori kwamba sasa wanafaidi kuwa na wanyamapori kuliko wakati ule ambapo wakiwa nao

wanaona ni balaa. Lakini pamoja na pongezi na shukrani hizo kwa kifupi kwa sababu nimepewa muda mfupi nina yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Nyerere aliwahi kusema hivi: "Wizi mbaya kupita wote na mkubwa kupita wote ni kumwibia mwanao ambaye hajazaliwa". Kuharibu mazingira na kumaliza wanyamapori ni kuwaibia watoto ambao hawajazaliwa. Nasema hivyo kwa sababu Wizara hii inajitahidi kwa hali ngumu sana kuhifadhi mazingira kwa ajili ya watoto ambao hawajazaliwa, lakini Watanzania wengine wao wenyewe ama kwa kutumiwa na wageni wanamaliza misitu na wanamaliza wanyamapori. Najua Wizara hii itakuwa na kazi ngumu ya kufanya kazi hii peke yake hasa kwa sababu mbili, pamoja na jitihada zao. Kwanza hawana askari wanyamapori wa kutosha, ni wachache sana. Kwa hiyo leo anayemsaidia Waziri wa Wizara hii ni Waziri anayehusika na Utumishi, nimwombe kabisa akumbuke Wizara hii waajiriwe askari wanyamapori ili na sisi tusije kuhesabiwa kwamba tulishiriki kuwaibia watoto ambao hawajazaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika tatizo lingine kubwa ni suala la silaha, hawa askari wanafanya kazi katika hali ngumu. Kwa askari wa hifadhi ya Taifa *TANAPA* na hifadhi ya Ngorongoro wao wanatumia silaha za zamani, lakini majangili wanaopambana nao wanatumia silaha za kisasa. Mimi nafikiri Wizara inayohusika na kutoa leseni za silaha ifikirie kuwapatia silaha kwa mfano *AK 47,* hiyo ingeweza kutumika kulinda hazina hii ambayo ndiyo hazina pekee ambayo tunaweza kupambana ua kushindana na nchi zingine za dunia hii ya sasa. Naomba pia Sheria ya Wanyamapori inayoandaliwa sasa kuletwa Bungeni, kwa kweli ilenge kabisa kukabidhi uhifadhi kwa wananchi na wananchi waone kweli hifadhi ni yao ndipo wataweza kushiriki vizuri katika kuhifadhi mali yetu hii tuliyonayo.

Mwisho, kwa kweli narudia hili la silaha kwa sababu bado nina dakika moja. Niliwahi kuuliza swali hili hapa Bungeni ikasemekana hii *AK 47* ni silaha za kivita, lakini benki tunalinda kwa silaha kubwa kubwa. Sisemi silaha za kuwapa hawa askari zilingane na zile za kulinda benki, lakini zikaribiane kwa sababu wanyama watakapotoweka sijui sisi tunaweza kushindana na nini kingine katika dunia hii. Viwanda hatuna wala hatuna chochote kingine, lakini uhifadhi na utalii ungeweza kufidia pengo hilo la viwanda ambavyo hatuna. Naipongeza Wizara kwa hali inayojitahidi kuwalinda wanyama. Faru hawajawahi kupotea na sasa wanaongezeka pamoja na hali hiyo ngumu ya kutokuwa na uwezo wa vifaa na askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa niaba ya wananchi wa Babati Mashariki, naomba niungane na wananchi wa Ulanga Mashariki katika kuomboleza kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Theodos Kasapira ambaye tumekuwa naye hapa kwa muda mrefu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mfupi nataka niseme hoja yangu kwa sentensi kama mbili, tatu au nne tu. Nitaielekeza kwenye kifungu Na. 25, ukurasa wa 14, pale Waziri aliposema sentensi ya mwisho kwenye *paragraph* hiyo kwamba: "Mashamba Na. 1 mpaka Na. 3 ya Manyara kuwa sehemu za hifadhi na kwamba Wizara itawasilisha Muswada kwa ajili ya kuanzisha maeneo hayo". Kwa ufupi wa maneno yale yaliyokuwepo pale ambayo hayakuzingatia maslahi ya wananchi wa Wilaya ya Babati, wananchi wa Jimbo la Babati Mashariki na wala maslahi ya wananchi wa Kijiji cha Mayoka. Nataka nitamke rasmi kwamba tulikubaliana kuanzisha majadiliano juu ya maeneo hayo kwa sababu ya migogoro iliyokuwepo na Mheshimiwa Waziri aliwahi kuleta hapa Azimio la kutaka kupanua hifadhi hiyo. Mimi nikaomba kwamba sehemu hiyo ina migogoro, turudi kwanza tutatue na tushirikiane na *TANAPA*. Ushirikiano ule uliishia mahali na haujaendelea mpaka jana. Sasa leo nilipoona kuna sentensi inayoonyesha kwamba mashamba Na. 1 mpaka Na. 3 ya Manyara yatakuwa sehemu ya hifadhi ya Ziwa Manyara bila mawasiliano zaidi na Waziri anafahamu kwamba Jimbo la Babati Mashariki ndiyo *custodian* wa Hifadhi ya Tarangire kwa sehemu kubwa vile vile na sehemu ya Manyara, nashangaa. Kwa hali hiyo basi natamka wazi kabisa kwamba siungi mkono hoja hii na nitataka kupata maelezo ya kina kwa sababu yanahusu maslahi ya wananchi wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mmoja wa wale watakaochangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niungane na wengi hapa Bungeni. Maana siku zote tunakutetateta hapa, tunasema Mheshimiwa Mwenyekiti anapokalia kile kiti wakati wote mama huyo anatumia busara, muadilifu na kwa kweli ni mzoefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakutakia kila la kheri na fanaka na maisha marefu. Mwenyezi Mungu akujalie, lile ambalo liko rohoni mwako ulipate na kwa kuwa ni mwaka wetu tuko mwaka wa mwisho mwisho niwaombee na Wabunge wote na wao awapatie ndani ya roho yao yale ambayo wameyakusudia wafanikiwe na awaondoshee balaa za kila namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wote wawili waliofariki na kumuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya katika Taifa letu. Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano amekuwa anatembea nchi hii usiku na mchana na wakati wote amekuwa anahimiza maendeleo na kuujenga umoja na mshikamano wa Taifa letu. Mwenyezi Mungu amjalie afya njema na kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Kaka Yangu Arcado Ntagazwa naambiwa amekuwa Rais wa Mambo ya Kimataifa, Mwenyezi Mungu amjalie aendelee. Lakini kaka yangu Maokola-Majogo huyu Mbunge wa zamani kidogo katika hili Bunge. Katibu Mkuu wa hii Wizara, namheshimu sana, kazi anazofanya nzuri, wataalam wake na hata hiyo hotuba iliyokuja leo hapa imeandikwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza haya sasa naomba na mimi nichangie. Mchango wangu eneo la kwanza kabisa nitaanza kuzungumzia kuhusu *TASAF.* Naomba niishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuanzisha huu Mfuko wa *TASAF.* Nia yake ni njema, nzuri sana na matokeo yake tumeanza kuyaona, lakini bado ziko kasoro na hizi kasoro zinasababishwa na watendaji.

Nataka niseme mradi wa *TASAF* asilimia kubwa ya fedha hizi zinatoka Benki ya Dunia. Ni deni la Watanzania wote tutalipa sote. Nashangazwa sana nimeomba taarifa kutoka *TASAF* nikaambiwa Zanzibar kuna miradi 76, lakini imehudumia Majimbo 38 haya Majimbo 12 kwa nini yasiwekwe. Miradi 76 ingekwenda kila jimbo mradi mmoja mmoja ingebakia bado mna miradi 26. Ni dhahiri kuna Majimbo mengine yameongezewa miradi kabla ya mengine hayana hata mmoja. Kitendo hicho sio kizuri. Afadhali tuwe na chakula kidogo tugawane kidogo kidogo au kuna Majimbo mengine ya wakubwa na mengine ya wadogo. Tuwe tunaambizana hapa. Hili ni deni watalipa wale kwanza waliokuwa na miradi mitatu hawa wengine mradi mmoja hawatolipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa hapa naambiwa kwamba *TASAF* awamu ya pili inaanza mwaka 2005 maana yake nini. Maana yake mimi nisubiri jimbo langu la Dole mpaka mwaka 2005, hatuelewani hayo katika suala la jimbo. Kama mradi huu wanabeba Watanzania wote ni lazima tuhakikishe Watanzania wote wanafaidika. Wakiwa Watumbatu, ikiwa wa Dar es Salaam, ikiwa Kagera, Shinyanga twende na uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikupata maelezo mazuri nitaliomba Bunge liunde Kamati ya kuangalia uwiano wa fedha hizi. Tumechoka na kubabaishwa na mambo mengine. Tanzania ni ya Watanzania wote bila ya kujali kabila, rangi, dini ya mtu au chama cha siasa. Inakuwaje leo mtu anabeba. Kuna miradi sita ya *TASAF* eneo moja, eneo moja hakuna hata mmoja kwa sababu wana wajomba, wana shangazi wana nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nivumilie sana nimewaambia watu wa *TASAF* nikamfuata Mkurugenzi nikazungumza naye hakuna alichofanya, nikawaeleza naambiwa tu maana yake, mimi mwanamume mzima nadanganywa. Mimi nimekuja hapa nimechaguliwa na wananchi wa Dole kuja kuwasimamia shughuli zao. Sheiya yangu ama Kijiji changu wamekamilisha *process* zote mradi wa kwanza, wa pili wa tatu kila siku napigwa Kiswahili. Aah maana yake nini na nini, maana yake nini? Kama mimi nimeingia hapa Mbunge kipindi cha nne nadanganywa aliyeingia kipindi cha kwanza atakuwaje? *(Makofi)*

Wao pale *TASAF* wana Mashangingi makubwa linazunguuka huu huu. Watu wana matatizo. Hatuwezi tukaendesha Serikali namna hiyo. Hatuwezi tukabeba mikopo tukawatisha Watanzania wao bado wasifaidike. Ningeliomba wale Viongozi wa *TASAF* wakajirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukavumiliana hali hii. Hatuwezi hata siku moja katika nchi hii tukavumiliana wengine wanakwenda wanajiwekea nusu pepo, wengine wanabakia wako katika moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa hapa ambayo imeandikwa na wenyewe watu wa *TASAF* sikuandika mimi. Inaonekana katika Majimbo mengine kuna miradi zaidi ya mmoja, miwili, mitatu lingine bado, ukiambiwa utaambiwa *procedure* na kila kitu, masemina mengi, uwiano, tathmini, tunataka tathmini sisi. Katika fedha za madeni unataka tathmini. Tathmini baada ya kufanya watu watatu wataalamu inafanywa na watu mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama sikupata majibu mazuri kipindi hiki nitaliomba Bunge liniunge mkono tuangalie uwiano na hayo masharti yaliyoandikwa humu. Nimesema haya kwa hasira kwa sababu sikufurahishwa na utendaji wa *TASAF.* Sina sababu Zanzibar yote ni sawa sawa na Wilaya moja ya Tanzania Bara. Leo naambiwa kuna Majimbo mengine yamepata mengine hayakupata. Watu wa Zanzibar wote ni milioni moja hawafiki hata mkoa mmoja kwa nini kusiwe na uwiano ile kazi ikafanywa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hiyo kuhusu *TASAF* nataka pia nichangie kuhusu Muungano kidogo tu. Wala sikusudii kusema sana. Muungano wa Watanzania ni Muungano wa damu. Sijui kama kuna mtu anapinga hilo. Watanzania wote ni ndugu inabakia mtu kwa bahati mbaya amezaliwa Zanzibar, mwingine amezaliwa Pemba, na mwingine amezaliwa Makunduchi. Lakini tangu asili na jadi Watanzania wote ni wamoja. Nawashukuru sana waasisi wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere walioliasisi suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema na kuliomba Bunge na kuiomba Serikali na kuwaomba wananchi kwamba Muungano uliokuwepo uheshimiwe na uendelee. Toka mwaka 1964 tulikubaliana kwamba Muungano wa Tanzania uendelee na mwelekeo wa Serikali mbili. Kwa maana hiyo mimi sizungumzii tatu, nne, tano maana kuna watu wanaongeza Serikali wapate nafasi za kazi. Maana ikiongezwa Serikali ya tatu mimi nitakuwa Waziri Mkuu, nitakuwa Rais mdogo, nitakuwa Mkuu wa Mkoa katika Serikali hiyo. Hamna, Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachosema ndani ya Muungano ziko kasoro. Hizi kasoro za Muungano ni vizuri zikafanyiwa kazi zikaondoshwa pale. Sasa hivi tunazungumzia Jamhuri ya Muungano ambayo ina miaka 40. Leo tunazungumzia Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Muungano bado una matatizo yake tunaingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hiki kisiwa au visiwa vya Zanzibar katika huu Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki utafaidikaje? Nazungumzia Watanzania sizungumzii

vyeo. Maana watu wanaanza kuzungumzia vyeo. Mimi sina haja ya vyeo. Haja yangu Watanzania waboreke katika maisha yao. Watanzania wanazungumza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Waziri wa Elimu hapa akaileta hotuba yake nzuri tu lakini haizungumzii chochote wananchi wa Zanzibar watakavyoboreka kielimu. Sijui kuna MMEM kuna nini na kadhalika anasema aah huku hakunihusu. Mwingine anazungumzia mambo mengine anasema huko hakunihusu. Tunafanya nini. Lazima Serikali ya Jamhuri ya Muungano iangalie vizuri Zanzibar kwa sababu Zanzibar kama haitosaidiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado itaendelea kuwa imetupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ndugu zangu tunachozungumzia dunia nzima haizungumzii ukubwa wa Serikali inazungumzia uwezo wa kiuchumi. Hali ya uwezo wa kiuchumi ya Zanzibar hakuna asiyeelewa. Hali si nzuri hata kidogo, hali zao ngumu. Wananchi wale wa Zanzibar hasa milioni moja hawana biashara ya kufanya, hakuna mazao yoyote hawa wataishi ishije katika huu Muungano na katika hii Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Soko lao hawa litakuwa lipi? Serikali yao itaendeshwa vipi? Ndiyo mambo sisi tunataka yazungumzwe hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naiomba Serikali ikae kutatua haraka iwezekanavyo kasoro zote za Muungano. Maandalizi mazuri yafanywe Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwemo Zanzibar itaingiaje katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine kiuchumi. Leo hii Mzanzibar anakuja na televisheni Tanzania Bara anaambiwa lipa kodi, nalipa kodi katika nchi moja. Nchi moja, baba mmoja, mama mmoja kule ameshalipa maana yake nini ananyanyasika pale. Hali zao za uchumi ndugu zetu mishahara shida mambo mengine shida na kila kitu sisi huku tumenyamaza kimya mtu anaagiza shilingi 80,000,000 na kila kitu hamna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapokuwa nyumba yako moja katika chumba chako kimoja kina matatizo bado uhuru huna. Kama Zanzibar hali yake ya uchumi itakuwa si nzuri basi na Mtanzania Bara hali ya uchumi si nzuri. Lazima Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikae izungumze kasoro hizo ili tuhakikishe uchumi wote sehemu mbili unaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kisiasa tukubali, tukatae pengine hali ya Zanzibar si nzuri. Serikali ya Jamhuri ya Muungano inasaidiaje. Inaacha watu waendelee kuishi kwa wasi wasi, inajenga kitu gani kule, inaweka nini, inaacha mambo, matisho yaendelee. Hayo ndiyo mambo ya kuzungumzia. La sivyo tutaendelea kuandaa tena baada ya muda matatizo ambayo hatuyataki yarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hilo suala la Muungano naomba pia nichangie katika ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Muungano huu umekaa kama watoto kule Zanzibar wanachezea kile kinachoruka angani nini kile?

**WABUNGE FULANI:** Kishada.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Kishada eeh !!!

Unakiona tu kishada kumbe uzi uliopita hapa huuoni. Maana kule Zanzibar hakuna jengo lolote la Muungano linalojulikana liwepo. Unaambiwa Ofisi ya Makamu wa Rais tumehangaika hapa miaka mitano ikaundwa Kamati ya kutafuta viwanja na kila kitu umezungushwa uzio kwa shilingi milioni 200. Tunataka ofisi ijengwe sio uzio. Benki Kuu tumesema imetafutwa zaidi ya miaka 20 umezungushwa uzio sijui kwa milioni ngapi, mpaka leo ofisi haijajengwa maana yake nini? Tunataniana, tunajaribishana au kuna nini au kuna kidudu mtu anazunguka zunguka.

Ningeiomba Wizara hii ya Makamu wa Rais ikasimamie ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais ikaharakisha ujenzi wa Benki Kuu iliyokuwepo Zanzibar na taasisi nyingine za Muungano zijenge majengo yake haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu. Imetosha eeh?

**MWENYEKITI:** Mmmhh!!!

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono. Ahsante sana.

**MHE. ABDALLAH KHAMIS FERUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa sina budi kutoa mkono wangu wa rambirambi kwa wafiwa na jamaa wa Marehemu Kasapira, Mbunge wa jimbo la Ulanga Mashariki. Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *(Amin)*

Kwa kuwa hii ni mara yangu ya pili kuchangia wengine tayari nilishatoa mkono wa rambirambi na kuwapa pole jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuiunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais asilimia mia moja. Nawapongeza sana watayarishaji wa hotuba hii nzuri, hotuba iliyotayarishwa kisayansi kabisa. Nawapongeza Mawaziri pamoja na watendaji wao wote waliokaa usiku na mchana kutayarisha kitu kama hiki walichotuletea ambacho kina mantiki nzuri sana kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitoacha kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa miradi aliyoichangia katika jimbo langu baada ya mwaka jana wakati kama huu kuomba huyu Makamu na sisi kule Zanzibar afanye ziara, apite katika Majimbo yetu ili na sisi tupate michango yake. Nashukuru katika ziara aliyoifanya mpaka Jimboni kweli alikuja na alifika mpaka kwenye jimbo langu la Chake Chake vile vile na nilipata misaada kama miwili hivi ambayo karibu kwenye shilingi 3,000,000 mpaka 4,000,000.

Kwa hivyo ndugu Mawaziri salamu hizi kupitia Mwenyekiti naomba zimfikie Makamu wa Rais. Hii tabia ya kutembelea katika Majimbo yetu mbalimbali, Wilaya na

Mikoa aendelee nayo. Kwa hivyo naomba salamu hizo zifike na wananchi wa kule jimbo la Chake Chake wanampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumzia sana kuhusu makazi na jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar. Kwa bahati kilio kile kiliitikiwa na tukaambiwa zimetengwa fedha mwaka jana zimo katika kitabu hiki shilingi 454,699,700. Tukaingia matumaini makubwa sana kuwa sasa Ofisi ya Makamu wa Rais itajengwa kule Visiwani pamoja na sehemu yake ya malazi na wananchi sasa watakuwa hawana matatizo tena kwenda kuonana naye wakati maalum au kama kuna matatizo yoyote yanayohusu Serikali ya Muungano kwenda kuyapeleka mahali panapohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matokeo yake ule ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais haikujengwa mpaka leo bado hapajajengwa kitu na badala yake pana ukuta kama mwenzangu aliyemaliza kuzungumzia kabla yangu mimi alivyosema. Ni ukuta mtupu.

Sasa tukaanza kujiuliza mbona muda mrefu ukuta tu kuna nini. Tukaanza kulifuatilia hili suala. Tumepata tetesi ukweli nafikiri mkiufuatilia zaidi mtaujua kuwa lile eneo limefeli. Sababu mimi sizijui itakuwa nyie mnazijua. Lakini mimi naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* anijibu hili suala langu nitakalomwuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kutokana na tetesi zile ikiwa lile eneo limefeli kweli basi atupe sababu za msingi za kufeli kwake. Ilikuwaje hata likafeli na tayari fedha nyingi sana zilishatumiwa pale. Hilo la kwanza. La ikiwa halijafeli kwa nini mpaka leo likawa lile eneo limekaa hivi hivi wakati mwaka jana tulishatenga fedha 454,000,000 ziko wapi hizi fedha mtuambie zilipo.

Sasa kuna shilingi 4.1 bilioni kwa hivyo Mheshimiwa Waziri utatumbia za mwaka jana mmezipeleka wapi na za mwaka huu pia. Ikiwa kumefeli kile kiwanja utueleze, je mmeshapata kiwanja kingine kiko wapi na hiyo kazi itaanza lini? Ikiwa si hivyo tutakutana katika mahesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea na Idara za Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika utafiti wangu au wetu kwa Idara za Ofisi ya Makamu wa Rais za Zanzibar tumegundua yafuatayo. La kwanza, kumbe kule Zanzibar iliyopo ni Idara moja tu ya *Private Officer* ambaye mkubwa wake ni yule siku hizi ameshakuwa Naibu Katibu Mkuu Mama Faharia. Basi hakuna lingine. Peke yake kama roho.

La pili hakuna taarifa yoyote iwapo ipo azma ya kufungua ofisi nyingine katika Idara za Ofisi hii ya Makamu wa Rais kule Zanzibar. La tatu tulililogundua labda tunategemea kimawazo yetu sisi kama binadamu kuwa pengine baada ya kukamilika huo ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar mwakani hatujui ni lini, labda hizo Idara za Ofisi ya Makamu wa Rais pengine huenda zikapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua kuwa Ofisi iliyopo hivi sasa kale ka - *Private Office* kusaidia Idara za Ofisi ya Makamu zinapokuwa na kazi zake kule Zanzibar kutoka huku Bara. Hii husaidia saidia yule mtoto anasaidia saidia kule.

Kwa mfano kuna ziara au mambo mengine haya madogo madogo. Lakini Idara ile haina mamlaka yoyote kiutendaji na kimaamuzi zaidi ya hizo dharura zinazojitokeza, huo ni utu. Huko ni kazi, hiyo ni kuaminiana. Sasa yule mmemweka pale anafanya nini hizi Idara huko zinafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yule kijana mnampa kazi nzito sana kule. Kuna matatizo tumegundua kuwa Ofisi ile ya Makamu kule Zanzibar huwa inapokea malalamiko na matatizo mbalimbali ya wafanyakazi na wastaafu wa SMT na Mashirika yake katika madai ya maslahi yao mbalimbali.

Lakini pamoja na kuwa pale tuna Kiongozi, yule kijana wetu, Kiongozi yule tumegundua hujaribu kufanya mawasiliano mazuri, anajitahidi na taasisi mbalimbali za huku SMT lakini mafanikio yamekuwa madogo sana kwa vile hana uwezo wa kisheria wala mamlaka ya kiutendaji katika kazi hizo bali hufanya hivyo kibinadamu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusisitiza kuwa kuwapo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar ni muhimu sana na ni lazima kwani kutawezesha kutanzua matatizo mengi yanayowakabili wananchi, watumishi na wastaafu wa SMT na Mashirika yake yaliyopo Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti. nitatoa mfano, wafanyakazi wote wa SMT na Mashirika yake wanakatwa Bima katika mishahara yao kwa muda mrefu sasa. Lakini huduma hiyo kwa upande wa Zanzibar imeanza hivi karibuni tu na hiyo ni kwa Unguja Mjini tu. Upo hapo. Ni kwa Unguja Mjini tu.

Kwa hiyo, wafanyakazi walioko Pemba na nje ya mji wa Unguja wanaendelea kuchangia bila ya kufaidika na michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ninaiomba Serikali na hii Wizara iyashughulikie masuala hayo. Ukiwa na watoto wawili basi jitahidi kwa njia yoyote pamoja na kuwa huna uwezo ukija na ndizi moja mkatie huyu kipande na huyu kipande. Lakini wengine unawaweka katika Bima wengine huwaweki, hawa watajisikia vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kidogo katika masuala mazima ya *TASAF*. Huyu mwenzangu aliyepita amezungumzia kwa urefu, kwa jazba lakini sisi yeye anatetea wananchi wa jimbo lake na wananchi wengine ambao bado miradi hii haijafika katika Wilaya na maeneo yao. Lakini kwa bahati nzuri kwangu mimi namshukuru Mwenyezi Mungu, nashukuru *TASAF* nimepata miradi. Kwa hivyo, naipongeza. Mimi naipongeza kwa awamu ile iliyopita, tumefanikiwa na tuna matumaini ya awamu inayofuata maeneo mengine nayo yataendelea kupata. *(Makofi)*

Nafikiri katika dunia si kama nyote mnaweza mkapata kitu kwa wakati mmoja. Hata mvua ikinyesha inaweza kunyesha hapa lakini ukifika hapo ikawa haipo. Ukienda

pengine ipo, ukienda kwingine ikawa haipo.  Ukienda Morogoro ipo. Sasa haya ni ya kidunia ilivyo.

Sasa mimi naona tungeliendelea kustahimili tuangalie hii awamu ya pili. Nataka niwashauri wenzangu tungelisubiri hii awamu ya pili tukaona je, awamu ya mwanzo imekwisha, hii awamu ya pili watatufanyia nini si bado tunao.

Mungu atuweke, Mungu azidishe ishara kwa rehema zake tutakuja kukutana tena hapa hapa.  Tutaelezana kuwa hili 2005 mambo yataanza na bado tuna Januari mpaka Juni tutakutana hapa. Kwa hiyo wanaohusika na *TASAF* nafikiri wapo pale wanatuona. Rafiki yangu yule basi tujitahidi mwaka 2005 hii miradi tuitekeleze.  Nina imani kwa imani ya nchi yetu na jinsi ya kutekeleza Ilani yetu ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi tutayatekeleza yote hayo.  Hiyo nina imani kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi naiunga mkono tena hotuba hii mia kwa mia.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jirani yangu na mwalimu wangu hapa, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwapa pole waliopatwa na matatizo yote.  Wale waliofariki Mungu awajaalie waingie peponi na sisi tutakapofika huko Mungu atujaalie tuingie peponi hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia kwa ufupi sana tu, wala sina matatizo makubwa na napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja na wala sina tatizo, lakini nina machache.   *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, machache yenyewe ni kwamba, neno Tanzania kwa kweli maana yake ni Tanganyika na Zanzibar.  Hiyo ndiyo maana yake na sote tunaelewa.  Si Mbeya na Ukerewe, wala si Njombe na Dodoma   Kwa maana hiyo, naomba kumuuliza Waziri, kweli tunayo Ofisi ya Muungano?   Kama ipo, iko wapi? Kama yeye ni Waziri anayeshughulika na Muungano na mazingira, wapi na wapi Muungano na mazingira!  Yeye kama Waziri anashughulika na uendeshaji, Muungano ni kitu peke yake ulimwenguni bwana, inatakiwa iwe Wizara peke yake na Waziri peke yake anayeshughulika na kitu hicho tu.  Lakini mnaweka pamoja na mazingira, si mngepeleka kilimo huko bwana!  Wapi na wapi?  Kwanza tafsiri iwe mbalimbali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua yeye siye anayepanga, lakini anayepanga abadilishe, aweke Wizara ya Muungano peke yake kwa sababu kuna matatizo mengi na ya muda mrefu na watu yamewakaa hapa kifuani.  Hatuna njia, hatuna pa kwenda na wala hatujui, kwa sababu hakuna Ofisi ya Muungano ati, hakuna!  Tunataka Waziri atakayeshughulika na Muungano awepo Bara na Naibu wake awe Zanzibar, ama Waziri awepo Zanzibar na Naibu wake awepo Bara.  *(Makofi)*

Tunashughulika na Muungano, lakini sasa hapana, tumekuwa kama nini sijui. Tunachangia tu kwa sababu tupo ndani ya Bunge, lakini ukitaka kuuliza matatizo ya nchi za nje hujui uende wapi, ukienda kwa mambo ya nchi za nje wanakwambia: "Aah, haya mambo ya Muungano." Hatujui, kwa kweli tumo tu! Kama sasa hivi tumechelewa, huyo Rais atakayekuja basi aweke Ofisi ya Muungano peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka kulizungumza ni kwamba, kule Zanzibar hakuna hata ofisi inayoshughulikia na Muungano, hata idara moja hakuna. Kuna *Private Officer* anapokuja Makamu wa Rais ajue wapi atapata chakula chake, wapi atapata chai yake, basi! Sasa ni heshima gani hiyo, ofisi iko wapi hapo! Hivi kweli ni utaratibu huo, akija kule Zanzibar anakaa katika nyumba ya *lord* mmoja wa zamani pale Mnazi Mmoja ndiyo anaishi Makamu na yule karani au sijui *Private Officer.* Huyo ni Ofisa mwenzangu tulikuwa pamoja Ofisi ya Waziri Kiongozi na yeye anakwenda kuuliza: "Leo bwana utakula nini?" Ni hilo tu. Sisi tukiwa na matatizo yetu twende wapi, hakuna. Sasa jama hapa pana Muungano kweli? Naomba hilo lishughulikiwe kabisa kabisa. Kero za Muungano mojawapo ni kutokuwa na mahali pa kupeleka kero zenyewe, ndiyo maana zinakua, hakuna utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kwamba, hivi sasa kuna hiyo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Utatusamehe kwa sababu ni lazima turudie kwa kuwa ndiyo kero tulizonazo. Hatuwezi kusema mambo ya mazingira au nini, hatuwezi kwa sababu hizi ni Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi zetu tatu zimekutana zote zimo, lakini Zanzibar hamna hata mmoja. Siyo vibaya kuomba. Sasa hivi ndugu yangu, shemeji yetu yule Ali Mchumo kapata nafasi Ulaya huko, Mungu amjaalie, lakini tupeni na sisi angalau tuwemo. Mchagueni mtu kule wasomi wapo wazuri tu, asije akachaguliwa tena huku huku. Zanzibar hatumo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatuna Ofisa. Wanasema kuna Mhasibu, kakimbia kule sijui miaka mingapi. Kwa hiyo, tunaomba hilo mliangalie sana. Nasema kwa nia nzuri kabisa, labda usemaji wangu ndiyo wa jazba kwa sababu mnene. Lakini nasema kwa nia nzuri sana, kwa sababu mnene tu labda ndiyo maana sauti yangu kubwa, lakini ndiyo ninavyosema hivi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, tunaomba hili ulishughulikie, kama hapa ni mahali pako au si mahali pako nimeishakueleza mapema hatujui tupeleke wapi. Tukipata nafasi hii sisi tunaizungumza hapa hapa. Tusaidie angalau na sisi tuwe na mtu wetu kule Zanzibar katika Muungano. Ali Mchumo Mungu amjaalie anafanya kazi vizuri kwa niaba yetu, lakini nafasi ile tupewe sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu asilimia 4.5. Hii bwana tunaisema kila siku, lakini nani anasikiliza, nani anaweza kuamua, hatumjui. Kila siku hapa tunapiga kelele Zanzibar wanapewa msaada 4.5. Kabla ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyokufa katika Benki ya Afrika Mashariki Zanzibar walikuwa na asilimia 11.1. Angalieni nyuma Zanzibar asilimia 11.1 na

Tanganyika walikuwa wana asilimia 22. Sasa imekuwaje sisi tukarudi katika 4.5? Ni kwa nini tusiache pale pale katika 11.1 na sisi tulikuwemo katika benki ile? Nyingine zinakwenda wapi na nani kwenye uwezo wa kuamua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika, natanguliza hilo kwamba sina uhakika na ninaomba radhi. Ninasikia kwamba Mheshimiwa Malecela alipokuwa Waziri Mkuu ndiye aliamua hii 4.5 alisema: "Tutafikiria mbele." Hakuna mahali palipoandikwa, kama hakuna mahali ilipoandikwa, tuna tatizo gani? Tuna kigugumizi gani kuwasaidia wale kuwapa angalau ile waliyokuwa wanapata Afrika Mashariki ambayo ni 11.1?

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya nimejaribu kutafuta katika kumbukumbu zangu, Mheshimiwa Mwalimu Nyerere, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, alisema kwamba: "Tunaanza na Muungano huu kwa kanzu hii ndogo, lakini kila tukikua tutashona kanzu nyingine." Ina maana bado hatujakua tu tukavaa joho, bado tuko katika kanzu ile ile, eeh! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walisema hayo Waheshimiwa Marais wetu wa kwanza ambao ndiyo waliunganisha Muungano wote wawili, Mheshimiwa Karume na Mheshimiwa Nyerere. Sasa tumeishakua bwana, tumeshapita katika kanzu tuko katika joho, miaka 40 tupeni tutoke hapa katika 4.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuongelea kuhusu Katiba. Katiba inatuambia kwamba kuna vitu vya nishati ni vya Muungano. Ni kikatiba, siyo kwa mazungumzo ya mtu, mfano mafuta na gesi. Mungu katujaalia tumeanza na gesi, sasa inaingia Dar es Salaam na inafanya kazi huko, Zanzibar sehemu yao iko wapi? Hili ni jambo la kikatiba, ni kwa nini mtu anashindwa kutimiza Katiba? Ikiwa Zanzibar imeandikwa kikatiba kwamba mafuta na gesi ni vya Muungano na tayari gesi ipo, sasa sehemu ya Zanzibar iko wapi? Ikiwa hawawezi kupelekewa gesi, ni kwa nini? Fedha yao wanayopata Zanzibar si isaidie kulipia ili mambo mengine wapewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini hatupewi, au Katiba haisemi hivyo, au nani anaweza kuvunja Katiba? Katiba imesema hivyo na gesi imetajwa. Sasa gesi ipo Dar es Salaam, Zanzibar wanapata nini, wanafaidika nini! Tunaomba ile sehemu yetu ya gesi zile pesa zinazopatikana tupewe kiasi chetu, tusing'ang'anie mafuta tu ambayo hayapo Zanzibar, yanasemwa tu kama yatakuwepo, tusing'ang'anie. Vile vile, dhahabu na Zanzibar tupewe, haya ni madini. Tupewe Zanzibar dhahabu, almasi, sijui tanzanite hiyo inayopatikana, pamoja na manyangarika gani yanayopatika katika ardhi tupewe ili tuondolewe umaskini. Tunataka kuondoa umaskini isifikiriwe tu mafuta, tupewe na gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia, tupewe gesi, kama gesi haiwezi kusafirishwa kwa utaratibu mahali ilipo, tupewe mapato ya gesi kwa sababu ni haki yetu kikatiba. Kwa nini tunawapa nafasi wengine waseme? Mambo mengine hatuwezi kusema sisi. Sisi ni Chama kimoja, usiwape nafasi hao kusema, tekeleza usingojee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Wabunge, sijui kama ni mahali pale au si mahali pake, utaniwia radhi. Sisi ni Wabunge wa Muungano wa Tanzania, sote humu ni Wabunge wa Tanzania, lakini ni jambo la aibu, ni jambo la fedheha kwamba Wabunge wa Bara wamepata Ofisi, lakini sisi hatuna ofisi, wala hakuna mtu aliyewaza. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema : "Ooh, nitazungumza na Waziri Kiongozi." Muda wote huo hujazungumza naye! Huyo Waziri Kiongozi afanye nini? Hana hata pesa za kulipa mshahara wafanyakazi wake kule, halafu atupe sisi pesa za ofisi, kwa nini tunabaguliwa na sisi ni Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha kama yupo tukiondoka atupe cheki zetu na sisi tukatengeneze ofisi, sisi ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, si Wawakilishi. Wawakilishi watapewa huko na Waziri Kiongozi, hana kitu yule, atawapa wao. Sisi tupewe hapa, sisi niWabunge, kama alivyo Mbunge wa Mbeya ndivyo nilivyo Mbunge mie. Mbona tunapewa mshahara mmoja, mbona tunakaa pamoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja Mheshimiwa fulani aliuliza swali na ndiyo hayo mambo magumu mnayotupatisha. Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani aliuliza swali na Mheshimiwa mmoja alijibu hapa, lakini sipendi kumtaja. Jibu likawa: "Ooh sisi mbona hatuchangii katika Polisi? Mbona hatuchangii katika Majeshi?" Kweli hiyo ni jibu la kumjibu mtu! Mheshimiwa Waziri alijibu swali hilo hapa. Hatuchangii vipi? Mbona tunachangia tu, hatukwenda Kagera siye, hatukwenda? Zanzibar haikwenda? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mlikwenda.

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Si majibu mazuri ya kujibu hayo. Mheshimiwa Waziri fulani alijibu hivyo. Hayo ni mambo magumu mnatupatisha, maswali haya hayatakiwi kuulizwa hapa. Wenzetu wana nafasi ya kuuliza, lakini sisi hatuna! Hatuna kutokana na taratibu za Chama chetu. Sisi Chama chetu ni kimoja tunafanya kazi moja, tunapendana na tunataka tutawale milele. Kama nilivyosema CCM itatawala milele, basi tutatawala tu, wala msiwe na hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, nimeona pesa kidogo hapa zimetengwa. Nakuomba Mheshimiwa Waziri usimamie suala hili ili ofisi ile angalau msingi uwepo na tuwe tunaonyeshwa kwamba ule pale. Miaka 40 sasa hatuna Ofisi ya Makamu wa Rais! Ukienda kule na ukawa na matatizo ya kuonana na Makamu wa Rais unakwenda Ikulu ya Zanzibar, unakwenda chumba kidogo pale karibu na chooni ndiyo alipo yule mtoto ...

**WABUNGE FULANI:** Aaah! *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED ABDULY ALLY:** Ndiyo. Siyo siri, ni kwa sababu hakuna ofisi. Unakwenda pale unamwona ndugu yangu Ofisa wa pale Faharia, maskini ana chumba kimoja pale kama saloon. Haitakiwi hivyo, tunataka tuwe na ofisi ili akija mgeni ajue hizi ni nchi mbili zilizoungana. Bara ofisi yake iko huko, Zanzibar ofisi yake

iko hapa. Kila mtu anakwenda kwa kuji-*proud*. Sisi hatuna ofisi jama, msituone hivi. Hatuna Ofisi za Wabunge, hatuna Ofisi ya Makamu wa Rais wala hatuna Ofisi ya Muungano, twende wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kitu kilichotuunganisha ni Bunge, Bunge linatuunganisha vipi! Bunge tuko hapa kwa sababu ya kikatiba tu, hatuwezi kusema matatizo yetu, hatuwezi. Mimi siwezi kuja hapa nikasema nina tatizo hili, siwezi. Ni lazima pawe na ofisi niende nikamuone Waziri anayehusika. Rafiki yangu Ntagazwa wanakusema kwamba ulikuwa katika *G.55*, kwa hiyo sipendi upate tatizo hilo. Wewe rafiki yangu sana, najua unaipenda Zanzibar, unaishughulikia Zanzibar. Saidia Zanzibar katika mambo magumu. Ndivyo wanavyosema, mimi sijakuwepo wakati huo katika Bunge hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuzungumzia kuhusu UKIMWI. UKIMWI utatumaliza kwa sababu palipo na UKIMWI ni mahali pabaya. Ni pabaya kwa sababu si rahisi kumwambia mtu asiende. Kama tutanyoosha mikono humu jana tumekwenda wangapi itakuwa aibu! Kama tukisema kila aliyekwenda jana anyooshe mkono, itakuwa aibu. Siyo rahisi kuacha kwa sababu hata sisi Waislam tunatakiwa tufanye mambo mazuri hapa duniani ili tutakapofika mbele ya haki, mbele ya Mwenyezi Mungu kitu ambacho tutapewa, tutapewa wanawake kule, kwa hiyo si rahisi kuacha. Tutapewa wanawake tu kule, hakuna atakayepata *Jet,* hakuna atakayepata ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MWANAMKUU MAKAME KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mie niweze kuchangia machache niliyonayo juu ya hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo inashughulika na mambo ya kuondoa umaskini, mambo ya mazingira na vile vile mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia naanza kwa kuwapongeza wote waliohusika na kuandaa hotuba hii na pia kuisoma katika Bunge hili Tukufu leo hii tarehe 28/07/2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nawapongeza sana kwa juhudi zao za kumsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais. Nawapongeza sana kwa kazi zao nzuri na juhudi zao. Pia, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kazi yake nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuchangia na mie nitazungumzia kidogo kuhusu mambo ya Muungano. Tulielezwa hapa kwenye hotuba kwamba Muungano wetu sasa hivi na ndivyo ilivyo umetimiza miaka 40 tayari. Jambo hili ni jambo la kujivunia na ni jambo la kusema tujipongeze sisi wenyewe hasa kwa Muungano wetu kukaa ukiwa

katika hali ya salama toka kipindi hicho chote mpaka kufikia miaka 40 na *Inshallah* tuombe dua Mwenyezi Mungu atujaalie udumu milele na milele. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi kero mbalimbali ambazo sasa ni za muda mrefu sana na bado hazijatafutiwa namna ya kuziondoa. Tunashukuru kwa zile kero ambazo tayari sasa hivi ziliishatafutiwa namna ya kutatuliwa, lakini basi hizi kero zilizobaki zipatiwe ufumbuzi ili zizidi kuung'arisha Muungano wetu. Ingawa Mheshimiwa Waziri katueleza kuwa Serikali sasa hivi inafanya kazi siku hadi siku kutafuta namna ya kuweza kutatua kero hizi, tunaipongeza sana. Lakini sasa siku zimeishakuwa nyingi sana, si siku tena wala siyo miezi isipokuwa ni miaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri ametueleza kuwa, siku zote Wananchi wanapewa fursa ya kubuni au ya kutafuta mbinu mbalimbali za kuweza kuimarisha huu Muungano wetu. Lakini pia ni lazima tujiulize, hivi kero zilizokwisha ainishwa ambazo zitadumishwa na kuimarisha ni lini zitatafutiwa ufumbuzi? Kama ilivyosema, Serikali inajitahidi, lakini kuna umuhimu wa kuzipa kipaumbele kuzitafutia namna ya kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nieleze kero zote hapa isipokuwa nataka nitoe mfano tu. Kwa kuwa Serikali yetu ni ya Muungano, ingependeza kwa zile Wizara za Muungano, Wizara ikiwa huku na kule Zanzibar angalau basi kuwe na ofisi ambayo itafanya shughuli za Muungano kwa kuwakilisha zile shughuli za Zanzibar kule. Lakini matatizo tuliyonayo ni kwamba mpaka sasa hivi Zanzibar hatuna ofisi *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyosema, ilijengwa *fence* iliyotumia Shilingi milioni 200, lakini *fence* hii ika-*fail* kabisa na sasa hivi haijajulikana kama kuna mpango wowote, maana katika kitabu hiki hakuna. Sijui kama kuna mpango wowote wa kutaka kujenga hii ofisi tena au vipi. Hapo pesa zitakapopatikana, hebu Mheshimiwa Waziri atueleze ni vipi itajengwa tena na wakati gani. Kwa sababu tulishaharibu pesa hizo nyingi, thamani yake sina hakika nayo sana Mheshimiwa Waziri atatueleza hapa, lakini hizi Shilingi milioni 200 zilipotumika hawa waliokwenda kuanza kutaka kujenga hapa ni vipi hawakuangalia kwanza hapa mahali kama patafaa au hapafai? Ina maana walikwenda tu wakapavamia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule hakuna ofisi, kuna *Private Secretary* mmoja tu wa ofisi hii ya Makamu wa Rais na ninampongeza sana *PS* huyu kwa sababu ana juhudi sana katika utendaji wa kazi zote. Kazi zote zinazokwenda ziwe za kuondoa umaskini, yeye ndiye anayezikabili, ziwe za mambo ya mazingira, yeye ndiye anayezikabili na za Muungano pia ndiye anayezikabili. Mheshimiwa Waziri hebu tueleze, hivi kule Zanzibar hakuna watu wanaoweza kufanya shughuli za idara hizi tatu, au hakuna mishahara ya kuwalipa hawa watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze hilo kwa sababu hizi nazo pia ni kero za Muungano, wala si kidogo ni kero hasa za Muungano, zinatia doa kidogo katika mambo yetu ya Muungano. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atueleze matatizo haya yatapatiwa ufumbuzi lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa hapa kwamba huku tayari, fedha zimeshapatikana na michoro tayari. Je, kwa upande wa Zanzibar ni vipi? Atueleze baada ya ku-*fai*l ukuta ule uligharimu milioni 200. Sijui hata hiyo ofisi itakuja gharimu kiasi gani kama fence tu milioni 200 na tena muflisi haifai tena. Kule lini itapatikana ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na Idara zake zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, juu ya mambo ya Muungano tulikuwa tukihimiza Tume ya Pamoja ya Fedha iundwe. Kwa bahati nzuri, sasa hivi Tume hii tayari imeshaundwa, lakini imekuwa kama geresha tu kwa sababu haina fedha za kuendelea kutumia kwa kufanya vikao. Sisi tulikuwa tukihimiza Tume ya Pamoja iundwe ili kazi za Tume ile ziendelee, lakini kwa bahati mbaya Tume haiwezi kufanya kazi kwa sababu fedha hakuna. Sasa je, hii ni Tume au wamepewa kama kilemba cha ukoka tu? hakuna kazi yoyote inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nizungumzie kuhusu Utekelezaji wa Mkakati wa Kuondoa Umaskini. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, UKIMWI sasa hivi ni janga ambalo sasa hivi linaendelea kupunguza nguvukazi yetu katika maofisi mbalimbali na katika maeneo mbalimbali. Sisi tupo katika kupambana na UKIMWI, lakini ukitazama vitendo vyenyewe vinavyofanyika katika nchi yetu haviendani kabisa, ni tofauti na mambo ya kupambana na nasema baadhi ya hivi vyombo vya habari na siyo vyote. Sijui huwa hatuangalii Vyombo vya Habari au huwa, hatuna zile *Censor Board?* Mfano michezo ya kuigiza ukiangalia katika *TV* kama upo na mtoto wako wa kiume basi wewe utaona bora uondoke umpishe yeye au uwe na *TV* yako nyingine pembeni. Michezo yetu ya kuigiza, vikundi vyetu vya miziki mbalimbali na hata matangazo yetu ya kwenye *TV* au vyombo mbalimbali vya habari hayo tunayosema labda pengine ndiyo itakuwa kinga, lakini namna yanavyotolewa hayaendani kabisa na mambo ya kupambana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye upande wa mavazi, siye wazee tukisema huambiwa: "Nyie mmeishapitwa na wakati." Lakini wakati wa zamani na wakati wa sasa hivi ni tofauti sana. Kama tutasema wazee wameishapitwa na wakati vijana waendelee kuvaa mavazi yao yale yale itakuwa ni shida. Unaweza ukapishana na mtoto ukajionea haya wewe mwenyewe, yeye hata habari hana. Kama nguo fupi, ni kipande hasa hata siyo fupi tena na kama ya kubana basi kuvua pia tabu. Sasa katika kupambana na UKIMWI tunaelekea wapi? Ni lazima Serikali iingilie kati suala hili japokuwa mavazi ni hiari yake mtu atakavyovaa vyovyote ili mradi ajihifadhi tu, lakini siyo namna yanavyovaliwa mavazi siku hizi. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali iingilie kati katika kutatua tatizo hili kwa sababu hiki peke yake ni kishawishi. Kinachohamasisha mambo ya ngono na hasa tukizingatia wakati wa janga hili la Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nije kwenye maeneo mengine ya Mikoa yetu. Kuna maeneo mengine ya Mikoa yetu wanaume wana tabia ya kuhamahama kwenda Mikoa mingine au maeneo mengine kwa lengo la kufanya biashara au pengine kwa lengo la kutafuta maisha kama wanavyosema wao wenyewe. Sasa wanapoondoka pale husahau familia zao, husahau watoto wao kule wakifika pengine watakuwa na nyumba ndogo, kama watu wanavyosema siku hizi, hawana habari ya watoto wala mama.

Sasa, mama aliyebaki kule ana mzigo mkubwa sana wa kulea watoto matokeo yake watoto pengine wakose haki zao za kusoma kwa sababu mama hana pesa pengine ya kutafuta chakula na mtoto ana njaa hawezi kusoma. Watakaporudi wale watu, basi zawadi ya kwanza watakayoileta pale ni ya UKIMWI kwa wake zao. Matokeo yake ni kuacha watoto yatima katika hali ya umaskini. Kwa suala kama hili ninaiomba sana Serikali ingawa najua sheria zipo, lakini itafute namna basi ya kuwabana wale akina baba wanaopenda kuhamahama kwa shughuli za biashara au kwa shughuli za kutafuta maisha mahali pengine. Hatuwakatazi, lakini wawajibike na kukumbuka watoto wao kule watokako pamoja na familia zao. Sheria itungwe ya kuweza kuwabana hawa watu kwa sababu wanajulikana kule mikoani kwao au Vijijini. Wabanwe ili waweze kuwajibika na kule, wasiwaachie akina mama mizigo mizito namna hiyo peke yao, halafu baadaye wanawaletea zawadi ya kifo na kuacha watoto yatima katika hali ngumu ya umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *time* imeshakuwa kubwa, lakini nimalizie kwa kusema habari hii hii ya kuondoa umaskini. Kuna *NGOs* mbalimbali hupitapita huko vijijini kutoa mikopo midogo midogo kwa Wananchi. Kuna vikundi chungu nzima, vikundi hivi viratibiwe kwa sababu Wananchi wameshaanza kulalamika sana kwamba kuna *NGOs* nyingine huwaambia wajikusanye watano watano na kwanza watoe kiingilio halafu ndipo wapewe zile pesa pengine kama Sh.50,000/= za kuendesha miradi midogo midogo. Matokeo yake wakishazichukua zile pesa za viingilio hawarudi tena pale, huingia mitini kabisa. Akina mama wale walishatoa pesa zao ikiwa Shilingi elfu kumi kwa kikundi kwa kiingilio wanawaacha pale na matatizo yao ya umaskini yakiwa vile vile. Kwa hiyo, hivi vikundi viratibiwe, wasiachiwe tu kupita huko mitaani kusema watatoa mikopo kumbe ni uongo mtupu, ni matapeli ambao wanazidishia watu umaskini. Kwa kuwa *time* imeshamalizika sitaki niendelee na mpya, isipokuwa naunga mkono hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais na nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kuahirisha Bunge umekaribia, tukirudi mchana kwa sababu tuna Mawaziri wawili ambao itabidi wajibu hoja hizi, tutajadiliana mpaka saa 12.00 halafu tutawaachia nafasi Mawaziri waweze kujibu. Kwa hiyo, tutakapokuja mchana tutakuwa na Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Faida Bakar na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. Hawa mtaona kwamba ni wale ambao wameshazungumza mara moja tu, hii itakuwa ni mara ya pili. Wapo wengine ambao walizungumza mara mbili wako zaidi ya kumi, inaelekea hawatapata nafasi, hivyo waandike hoja zao kwa maandishi.

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo naahirisha kikao mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 06.59 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema Wizara hii ina Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, wawili kwa hiyo, muda wao wa kujibu

maswali itabidi wagawane kwa hiyo, tutakwenda mpaka saa 12 halafu Mawaziri wataanza kujibu hoja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya awali mchana huu, ili na mimi niweze kuchangia machache katika hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kabla sijaendelea kwa kuwa hii ni mara yangu ya pili katika uchangiaji safari hii, naomba nichukue nafasi hii kuwakumbuka marehemu Wabunge wenzetu, kwanza Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego Mbunge wa Mbeya Vijijini na vile vile Mheshimiwa Marehemu Capt. Theodos Kasapira Mbunge wa Ulanga Mashariki. Ninaomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu hawa mahali pema peponi. *Amen.*

Pili, naomba sasa nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Mawaziri wote wawili toka Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa na kuwasilisha asubuhi ya leo hotuba nzuri sana yenye mwelekeo mzuri ambayo imegusa maeneo yote muhimu ambayo yapo katika dira waliojiwekea katika ofisi yao. Kwa kuwa Wizara hii ni pana na inagusia mambo mengi nitaomba nijielekeze katika mambo machache na hasa suala la mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira kama tunavyofahamu ni pana sana linagusa sekta nyingi sana hapa nchini na si rahisi ukazungumzia masuala yote ya mazingira kwa siku moja kwa sababu kila moja lina details zake nyingi sana na kwa upana mkubwa. Kwa hiyo, nitagusia maeneo machache kwa sababu maeneo mengi yanagusa sekta za maliasili, maji, kilimo na mifugo, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengi ambayo sasa hivi tunayaona kuhusiana na suala zima la uharibifu wa mazingira au uchafuzi wa mazingira, ninavyoona mimi linatokana na tatizo la elimu duni kuhusu umuhimu wa mazingira. Wananchi wengi hasa sisi wenyewe tulioko katika rika hii, tuliomo humu ndani na wenzetu wengi walioko huko nje vijijini na kila mahali, tunakosa kabisa ule undani wa uelewa na kuona umuhimu wenyewe wa mazingira yetu kwa maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu lisije likachukuliwa juu juu, ninaelewa kabisa zipo *NGOs* mbalimbali hapa nchini zinazoshughulikia mazingira. Kuna Serikali yenyewe inashughulikia mazingira na sekta nyingine ambazo nimezitaja zinashughulikia mazingira. Lakini utaona kwamba uhamasishaji huo haujaenda ndani sana. Ni uhamasishaji wa juu juu tu. Kwa hiyo, ningeomba Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Mazingira pamoja na *NEMC* na *NGOs* tujizatiti zaidi katika suala hili kwa kina zaidi ili wananchi wetu waweze kuelewa maana ya mazingira. Ninapenda kushukuru sana kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, imeshafikia hatua nzuri katika kuandaa sheria ya mazingira nawapongeza sana Mawaziri wetu. *(Makofi)*

Ninaelewa kwamba sheria hii itatusaidia kwa sababu ni kweli kabisa kuna watu wazima ambao hata uwafundishe, hawafundishiki hasa kuhusu uchafuzi wa mazingira utaona watu wanachafua mazingira kwa makusudi kabisa wanatupa takataka ovyo tu,

wanatupa karatasi ovyo tu na hasa hii mifuko ya *plastic* watu wengi wameizungumzia na hata Kamati ya Mazingira imezungumzia hii mifuko ya plastic wanaitupa ovyo tu kiasi ambacho miji yetu ni michafu kweli kweli, vijiji ni vichafu kweli kweli, barabara zetu, mifereji ni michafu kweli kweli. *(Makofi)*

Lakini ni sisi kama watu wazima wengine ambao wamesoma shule kabisa tunafanya hayo yote. Sasa hiyo, sheria mimi naamini kabisa itakuwa na meno, itawapa *NEMC* au chombo chochote ambacho kitapewa kusimamia naamini itakuwa ni *NEMC.* Itawapa meno ya kuweza kuwaadhibu vikali kabisa wale ambao wanachafua mazingira kwa sababu kwa kweli ni tatizo kubwa. Naamini wengine hasa wakiona uchafu umezagaa mahali anaona si kitu. Lakini tuelewe kwamba usafi ni kivutio kimojawapo hata ukizungumzia suala la utalii lazima mazingira yawe safi, kama unawapeleka watalii kwenye maeneo machafu kwa kweli hawawezi kupendezewa kabisa kuendelea kuishi katika mazingira ya namna hiyo, kwa hiyo, naamini na ninashukuru kabisa kwamba sheria itakayoletwa hapa na mimi nitaiunga mkono kwa asilimia mia kwa kuwa itaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa kuwa nimesema kwa watu pengine inaonekana suala hili kulielewa ni vigumu, basi hiyo elimu ambayo inatolewa sasa mashuleni, kwani naamini inatolewa elimu ya mazingira mashuleni, naomba suala hili lisisitiziwe zaidi. Najua watoto wetu, wanafunzi wetu wanajifunza elimu ya mazingira. Lakini liende kwa undani zaidi ili hii generation mpya ambayo inakua sasa ije ichukie kabisa uharibifu wowote wa mazingira ambao utakuwa unawazunguka. Watakapokuwa watu wazima, mimi najua watakuta mazingira yote yameshaharibiwa kwa sababu ya sisi tulioko sasa hatujali kabisa kulinda mazingira yetu. Kupitia siku ya Mazingira Duniani najua Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa vizuri kabisa taratibu kama walivyojieleza wenyewe kwenye hotuba kwamba wanapanga mipango mizuri na siku hiyo inatumika vizuri sana katika kuelimisha jamii umuhimu wa utunzaji wa mazingira. Lakini siku moja tu katika mwaka haitoshi. Ni siku ya kuhamasisha sawa, lakini haitoshi. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema hali hii ya usimamizi wa mazingira iende sambamba na kuwafundisha vijana wetu mashuleni kuhusu utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila elimu tutakuwa tunatwanga maji katika kinu. Sasa nimetaja suala la mifuko ya *plastic* au chupa za plastic ni kweli sisi ni nchi maskini tunahitaji viwanda ambavyo vinatoa ajira kwa wananchi wetu. Lakini kupanga ni kuchagua hii mifuko pamoja na kwamba inaweza ikavuta *interest* za watu fulani fulani, lakini tuangalie je hatuwezi tukaingiza teknolojia nyingine ambayo itaweza ikafanyiwa utafiti na ikaweza kuzalisha mifuko ambayo inaoza na kwa hiyo, ikioza tutakuwa tumeepuka kabisa hili tatizo la kuzagaa ovyo mifuko huko na huko. *(Makofi)*

Lakini tumeona wenyewe Dar es Salaam leo hii tukiondoka hapa safari kwa magari kuelekea, Dar es Salaam hasa huko njiani vijiji vyote vimepambwa kwa mifuko ya *plastic* inatusaidia nini? Mingi inaingia katika mashamba ya watu na huko basi hakuna mimea inayoendelea kuota, watu wanazidi kulima kwa sababu elimu hawana wanazidi kulima, wanafukia ile mifuko wanapanda juu, hakuna kinachoendelea, kwa hiyo, hilo ni tatizo kwa hiyo, lazima tuliangalie vizuri sana. Ungeweza kusema ufanye *recycling,* sijui

kama *recycling* itaweza kufanyika kwenye mifuko, lakini naelewa kabisa kwa chupa inawezekana.

Mimi nimeona katika Mji wa Moshi eneo la *SIDO* kuna kiwanda ambacho kimeanzishwa na wawekezaji fulani ambao kazi yao ni kukusanya chupa mbalimbali za *plastic* na wana - *recycle* na kutengeneza mabomba ya *plastic* sasa hiyo ndiyo inatusaidia zaidi. Lakini hilo suala la kutupa ovyo ovyo takataka tu na bila kuwa na mipango yoyote wala hakuna anayestuka kukusanya kwamba walau basi tuiweke mahali fulani tubuni njia ya kui-*dispose* pamoja hakuna, basi ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* ni chombo ambacho kinafanya kazi nzuri lakini ukiangalia fedha iliyotengwa kwa ajili ya *NEMC* ni fedha kidogo sana, sijui watakwenda wapi na waache wapi ili kwenda kufanya uhamasishaji na fedha kidogo sana. Kwa hiyo, mimi ningeomba kama kweli *we are serious* kuona kwamba mazingira yetu tunahitaji kuyatunza na kuyaboresha zaidi na chombo hiki tumekiweka kisheria, tukipatie fedha ili kiweze kufanya kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la upandaji wa miti. Ofisi ya Makamu wa Rais, inahusika katika uratibu wake huo huo kuona kwamba suala la miti linapewa kipaumbele. Ni kweli kabisa Wilayani nyingi, Vijiji vingi hapa nchini vinapanda miti. Jana tulipokuwa tunapitia majedwali katika Wizara ya Maliasili na Utalii, tuliona takwimu zinazoonyesha maendeleo ya upandaji miti tangu mwaka 2002, 2003, 2004 na wakapongezwa wale ambao wamepanda miti kwa wingi. Mimi naona nadhani tubadilishe approach yetu ya kuangalia mafanikio kama haya.

Miti mingi inayopandwa haikui kabisa, rekodi zinaonyesha kwamba watu wamepanda miti, lakini ufuatiliaji wa kuona miti hiyo, kweli inakua ni mdogo. Kwa hiyo, mimi naona ili kupima mafanikio ya upandaji miti, basi mafanikio hayo yapimwe katika kuona miti iliyopandwa, miti iliyokua, basi kwa ile iliyokua ndiyo tuitolee maksi nzuri kwamba hawa kweli wamefanikiwa. Bila kufanya hivyo hamna maana kabisa. Kwa sababu ni kweli miti inapandwa kwa wingi kwa sababu watu wanaona ni sifa si wito wa taifa watu watapanda, baada ya hapo wanaisahau kabisa. Kwa hiyo, hilo nalo tuliangalie katika mtazamo mwingine kwamba tukipanda miti basi yule *assess, assess* ukuaji wake siyo upandaji haitusaidii sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa nizungumzie suala la Lake Jipe, napenda kupongeza sana jitihada kubwa sana aliyoionyesha Mheshimiwa Waziri Ntagazwa, katika kufuatilia kuona kwamba kweli anajihusisha na matatizo ya kukauka kwa Ziwa Jipe, nampongeza sana. Mimi nimekuwa nikimsumbua mara nyingi sana, nasema bwana tusaidiane. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nitangulie kwa kutoa salama za rambirambi kwa wenzetu hawa waliotutangulia mbele ya haki. Naomba nitume salamu kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego pamoja na Mheshimiwa Kasapira ambao tulikuwa nao hapa Bunge, kwa bahati wameshatangulia mbele ya haki. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu azijalie familia za marehemu hawa ziwe na subira kwani hiyo ndiyo hatma ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuzungumza hayo nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wa hotuba hii ambayo ipo mbele yetu. Katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, amejaribu kuongelea maeneo mengi tu ambayo yako katika ofisi yake. Lakini kuna maeneo ambayo kwa mtazamo wangu pengine ule ustahiki wake umekuwa ni mdogo ukilinganisha na ile portfolio hasa ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, imeanzishwa na Ibara ya 47 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo kazi yake kuu pale ukiangalia iliyotajwa ni Muungano, mengine ni atayoagizwa na Mheshimiwa Rais.

Lakini kiutendaji ukiangalia kitabu hiki masuala ya Muungano yameanzia ukurasa wa 4 mpaka ukurasa wa 9, Mazingira ukurasa wa 9 mpaka 65, Umaskini ukurasa wa 65 mpaka 87, *NGOs,* nazo amezianzia ukurasa wa 87 mpaka 90 na Utawala ukurasa wa 91 mpaka ukurasa wa 93. Ukitazama jina la Wizara inasema Wizara ya Nchi, Mazingira na Muungano kwa maana imeshapoteza mwelekeo hata ule wa Kikatiba.

Basi kama inaingia na mazingira pengine ingetangulia Muungano na Mazingira. Hata ukitazama hiki kitabu hiyo nafasi yenyewe ya Muungano pia ndiyo hivyo kama nilivyoeleza haikuguswa, imeguswaguswa tu ukurasa wa 4 mpaka 9. Ukitazama hasa yale maeneo ambayo ni nyeti na mazito yameachwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo tuliyonayo sasa hivi Tanzania, Tanzania ile tunaizungumza ya mwaka 1964 na leo ya mwaka 2004 ni mabadiliko makubwa ambayo tumekwenda. Ni jambo la kushukuru kwamba Muungano wetu umeendelea na unakua, lakini sasa hiki chombo ambacho cha kutuunganisha na kutuendeleza mimi naweza nikasema kiko dhaifu. Nasema hivyo kwa sababu ukiangalia hata hii hotuba ya mwaka huu na ukilinganisha na mwaka jana yapo mabadiliko ambayo kulikuwa kuna chain ionekane kwamba imeendelea kubakia kuwa ni chain lakini tayari imeshavunjika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 6 alizungumzia kwamba “ushirikiano umeongezeka kati ya Wizara zisizo za Muungano za

SMZ na SMT" hiyo nakariri iko ukurasa wa sita katika kitabu chake cha mwaka na akataja baadhi ya Wizara pale na akaendelea, ambapo ratiba imepangwa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka na tayari imeshafika vikao 15 tuliuliza afafanue vikao vilivyofanyika ni Wizara gani, wapi, tarehe gani hiyo haikuwa na jawabu, mwaka jana sasa sijui mwaka huu kama kutakuwa kuna jawabu. Humu hamjatajwa. Tatizo kubwa ambalo tulilonalo sasa hivi Tanzania tunapozungumzia hizi issue za Muungano hatuizungumzi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, hii iko moja kwa moja, hata Mheshimiwa Sarungi anapokwenda Zanzibar bado gari yake anabandika nembo zake zile zile. Inaonekana pale Waziri wa Ulinzi. Kwa Tanzania nzima Waziri wa Ulinzi yuko peke yake.

Sasa bado tuna matatizo zile Wizara ambazo si za Muungano ndipo matatizo yetu makubwa yako pale. Hapa ndipo tunapokuta mahali tukavutana hata watu wakashindwa kutufahamu. Sasa Wizara hii ilikuwa iwe ni kiungo kikubwa sana cha kutuunganisha pale. Katika kutuunganisha hapo ndipo pale hasa ile kuonekana kama Tanzania ni Taifa moja, pamoja na kwamba ni taifa moja, lakini hiyo ingelikuwa na sauti kubwa zaidi kuliko vile ambavyo inavyoendeshwa kupitia chombo hiki cha kutuunganisha. Hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taasisi, pengine ukiziangalia zimeanzishwa kwa madhumuni ya kutanzua haya matatizo, nitatoa mifano. Tunayo Tume ya Fedha ya pamoja, Tume ya Fedha ya pamoja imeanzishwa kwa sheria namba 14 ya mwaka 1996, lakini hiyo tume tumeunda hivi karibuni, siyo tatizo tumeshaunda tuanze kazi. Lakini mpaka hivi tunavyozungumza zaidi ya wale Makamishna hata wafanyakazi hakuna.

Sasa Makamishna sijui wanafanya kazi vipi. Mheshimiwa Shellukindo akishaandika ripoti zake hata sijui wa kumchapia nani, hawana ofisi inayoeleweka wana-*hang* ndiyo zinatajwa tajwa tu ofisi zinaanzishwa zinasubiri kitu gani, zinatafutwa furniture, hizi *furniture* zinatafutwa nchi gani? Sasa kwa hiyo, hayo ni miongoni mwa matatizo, sasa tume hii ingeliweza kutusaidia kutuunganisha katika zile *gape* ndogo ndogo ambazo tulizonazo, ambazo sasa zinakua ndizo zinapokuwa kubwa. *(Makofi)*

Tumezungumza kuna kero za Muungano, kuna vitabu tunabadilisha *cover* leo kijani, kesho *blue, solution* tunasuasua kwa nini twende hivi? Tunazungumzia kama taifa, Wizara ya Fedha pengine nayo kwa kushirikiana na ofisi hii ingeweza kutusaidia vizuri sana kujenga hii daraja ya ufumbuzi. Lakini nina wasiwasi hata katika Wizara ya Fedha kuna maofisa hii Tume wanaihofu pengine itawapunguzia ukubwa wa mkate wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hii sheria katika kifungu cha 7 naomba kunukuu, *function of the commission: "The Commission shall be a principle advisory organ to the Government on the physical system of the United of Republic in respect of revenue, expenditure, other moneys payable to the account by each government."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiki kitabu anazungumzia nafasi ya kuchangia Serikali mbili. Sasa hapa ninavyoelewa pia kidogo hapaendi sawa sawa pana matatizo.

Sasa sheria hii ingetusaidia kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu inazungumzia mapato, inazungumzia matumizi, inazungumzia na hayo ya kuchangia. Sasa hiki ni chombo muhimu sana kwa kutuunganisha na kuimarisha huu umoja wetu. *(Makofi)*

Sasa tatizo lilipo tunavyofahamu sasa humu wanasiasa na linaposhuka mpaka kwenda kwa wananchi huku ambao hawana *document* ndipo pale linapokuwa kubwa kwa sababu tafsiri ya hawa watu wa kawaida huku na tunavyoliewa sisi ni vitu viwili tofauti, huku litakuwa kubwa, huku tunaweza tukazungumza, mwisho wa mazungumzo yetu tukacheka, tukakaa tukanywa chai pamoja, lakini huku chini haiendi hivyo wanafika mahali wananchi wanaona kwamba hawa ndiyo source ya matatizo.

Sasa tusifike hapo, hapo ni pabaya, sisi tunavyozungumza Tanzania kama ni Taifa ni vizuri tukaendelea kuwa taifa. Kwa hiyo, hilo kuna haja ya kuliangalia kwa kina, tuna maeneo mengi tu ambayo yalikuwa yanahitajika ufumbuzi. Mfano tujiulize kama tunakusudia kukua tuwe na watalaam. Tuangalie mfano elimu, nikitoa mfano labda niondoke hapo, juzi tu ilikuwa Wizara ya Afya, ilitilia saini mkataba wa kusaidia katika masuala ya Ukimwi, Wizara zote mbili zilikwenda vizuri zilikwenda pamoja.

Sasa kulikuwa na kasoro ipi na kwa nini katika miradi mfano kama ya MMEM, MMES isiende pamoja, *Poverty Reduction Strategies,* haya mambo ya umaskini ilikuwa kuwaje, kukawa na *program* mbili tofauti, hata kama zilikuwa mbili basi zilikuwa ziende sambamba. Lakini tatizo tunalolifanya tunafika mahali Watanzania, tunakuwa tuna vitu kama vya aibu. Leo tumeenda kuomba, tunaomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano tunasaidiwa, kesho tunarudi tena kwa lile lile tunaomba Serikali ya Zanzibar hawa watu wanashindwa kutuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja mimi niliwahi kwenda katika mambo haya ya kuomba kwenye Ubalozi wa Japan, nilikuwa na Mheshimiwa mmoja humu humu ndani, kwa kuwa sijapata idhini yake simtaji. Akatuambia ninyi Watanzania hii miradi yenu mbona inakuja kama uyoga? Leo umeota hapa, kesho umeota hapa. Hebu wekeni *priority* halafu wale mnaowaomba watajua waanzie wapi kuwasaidia. Leo ukiomba maji, kesho unaomba njia ya kupitia maji, keshokutwa unakwenda kuomba sijui unataka na bomba za maji, keshokutwa unasema kuna wagonjwa huku, hawa wanashindwa kutuelewa. Kwa hiyo, ni matatizo ya kufanya kazi kwa pamoja. Hilo nimejibiwa mimi nilivyokwenda kuomba masuala ya Jimbo langu.

Sasa hata Serikali yanatukuta hayo hayo kwa sababu hatuna *working plan* kama Serikali, kujiwekea mipangilio tunapanga, kipi kinaanza, kipi kinafuata. Sababu yenyewe tatizo lililokuwepo kama ingelikuwa Mheshimiwa Waziri, anayehusika angetumia yale maelezo yake ya mwaka jana kuendeleza ule utaratibu wa kukutana wakazungumza wakapanga ikafuata utekeleza*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naelewa Mheshimiwa Rais Mkapa, hili analisisitiza sana lakini nina wasiwasi sijui askari wake wa miavuli wengine wameganda kwenye miti au vipi? Hapa sielewi. Katika makaratasi tunazungumza vizuri lakini utekelezaji *I don’t know what is wrong. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vema si vizuri kurudia haya siku na siku, tunajaribu ku-*control* huu uzungumzaji isitoe picha mbaya kwa sababu sisi wa Chama cha Mapinduzi, hizi ni Serikali zetu moja ya jukumu letu ni kuzitetea, kuzilinda kwa nguvu zetu zote. Sasa tusifike mahali tukawa tunazungumza kwa lugha moja na wapinzani haitapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huu mshikamano wa kitaifa tuna tatizo ambalo tutalikuta hapa mbele si muda mrefu. Sasa hivi tuna wa Umoja wa Afrika Mashariki, tuna Umoja wa *SADC countries,* kuna *AU,* kuna *AGOA,* kuna *NEPAD.* Sasa bila ya kukaa vyombo vyetu kwa pamoja vikazungumza kwa kina tutajikuta siku zote huyu anasema hivi, huyu anakwenda hivi, tunavutana tu.

Mfano wa wachangiaji waliotangulia wamezungumzia 4.5 kwa kiasi ninachoelewa hii tulipewa kama ni *temporary solution na world bank* kwamba *okay* kwa kuanzia, anzeni hapa ni vizuri tuanze hapo. Ndugu lazima wafike mahali wanazungumza kwa maelewano. Lakini *solution* yake hiyo, tungepitia pale pale kwenye ile tume lakini sasa ndiyo hivyo mambo yenyewe kama nilivyokwisha kueleza hakuna kinachokwenda katika mtiririko mzuri ambao unaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeliomba sana katika Wizara hii ifanye kazi yake zaidi ijielekeze nini Katiba ilichoiagiza kukifanya. Kwa sababu ukichukulia mazingira, umaskini, hii unaweza ukaihamishia Wizara nyingine bado ika-*fit*. Sisemi ihamishwe isipokuwa tu zile unaweza ukazungumza zikae pengine na zikafanya kazi vizuri sana. Lakini hata kama zinabakia hapo siyo tatizo, lakini ionekane ule utendaji. Hata ukiangalia hii Idara inayoitwa Kitengo cha Muungano, ukiangalia bajeti yake kifungu ambacho kina fedha angalau unaweza kusema za kufanyia kazi, ni kile cha safari tu nadhani kina milioni 5,200,000 kitu kama hicho. Sasa tujiulize hivi huu muda wa kuja Bungeni tu hapa mpaka akiondoka zaidi ya nusu ya fedha zile zilishatumika. Sasa hivi kazi nyingine watazifanyafanya vipi? Kwa kifupi ukiangalia hata bajeti nzima ya ofisi hii ile Wizara haikupewa umuhimu wake kama ambavyo inaonekana hata idadi ya watu wake ina watu wawili/watatu tu, itakuwaje kwa sababu bajeti yao ukiifanyia *breakdown* hukuti kwamba ina *manpower* ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY J. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Naomba pia niungane na wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kupotelewa na Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego. Naomba pia nitoe pole kwa wananchi wa Ulanga Mashariki kwa kumpoteza Mbunge wao mpendwa Marehemu Captain Kasapira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa basi kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Makatibu wake wakuu na watendaji wake wote kwa kutengeneza hotuba hii nzuri ambayo imezungumzia mahsusi kabisa jitihada na malengo ya Serikali katika kutunza na kuendeleza mazingira pamoja na kupunguza umasikini katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri, ningependa nitoe maoni yangu kidogo kwa nia nzuri ya kuboresha kwa sababu sisi wote tuna jukumu la kuhakikisha mazingira ya nchi hii yanakwenda vizuri pamoja na umasikini unapigwa vita kwa jitihada ambazo ni kamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumzie kidogo katika hifadhi ya mazingira. Mimi natoka Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro una milima mizuri sana inaitwa Milima ya Uluguru. Hii milima ilikuwa ina miti mizuri, ilikuwa ni vyanzo vya maji mengi sana, maji ambayo yanahudumia Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Dar es Salaam. Lakini kwa bahati mbaya kwa muda wa miaka 15 sasa ile milima imekuwa inaunguzwa moto na wananchi. Sio kwa sababu labda wanataka kupambana na mtu labda ni kwa sababu hawaelewi vizuri.

Serikali ya Mkoa wa Morogoro imejitahidi sana kutoa elimu na kuzuia uharibifu huo, lakini kwa bahati mbaya jitihada zote zinagonga ukuta. Tunafikia mahali tunajiuliza, kwa nini jitihada zote hizo zinagonga ukuta? Ningefikiri kwamba Wizara hii ingejaribu kufanya utafiti ili tuweze kupata ufumbuzi au tukajua ni kwa nini bado pamoja na elimu yote, pamoja na wananchi kukamatwa na kupewa adhabu, bado Milima ya Uluguru inaendelea kuungua moto na matokeo yake ni kwamba vyanzo vyote vya maji vinaanza kupungua mpaka inafika mahali sasa kwa muda ulio mrefu Mji wa Manispaa ya Morogoro tunakuwa na zamu za kugawiwa maji. Unaweza ukapata maji wiki hii mara mbili, wiki ijayo ukapata mara moja. Kisa ni kwamba vyanzo vya maji vimeharibiwa na kiwango cha maji tunachopata kinakuwa ni kidogo.

Sasa suala linakuwa sio Morogoro tu, nafikiri hata Mji wa Dar es Salaam, matatizo yake ya maji yanatokana pia na uharibifu wa Milima ya Uluguru. Kwa hiyo tunaona kwamba kuwepo na utunzaji wa mazingira ya Milima ya Uluguru ni uhai wa Mji wa Dar es Salaam, Mkoa wa Pwani na Miji ya Morogoro. Sasa Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, tungependa tuulize kwamba sijui kama wameshaona hilo tatizo na kwamba ni hatari kubwa, it is a time bomb. Tutafika mahali tuanze kulaumiana. Lakini naomba kusema kwamba Serikali Mkoani inafanya kazi, lakini tatizo liko wapi? Sisi uwezo wa kusema kwamba Serikali ya Mkoa wa Morogoro ifanye utafiti kuangalia ni kwa nini wananchi wa Morogoro wanaendelea kuunguza ile milima, huo uwezo hatuna kwa sababu tunahitaji input ya pesa.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia namna ya kushirikiana na Serikali yetu ya Mkoa kutafuta ni kwa nini lile tatizo linaendelea kuwepo au kutafuta ufumbuzi wa kufanya ile milima iwe ni hifadhi ya Taifa, maana yake ni kwamba zitafutwe pesa za kuweza kutoa compensation kwa wale wananchi wanaoishi kule milimani juu waweze kuhamishiwa katika sehemu nyingine na wasaidiwe kuanza makazi mapya ilimradi tu tukalinde yale mazingira ya ile milima tuweze kuendelea kupata maji.

La pili, nafikiri kila mmoja wetu anaposafiri kuja Dodoma, wanaotokea Dar es Salaam wanapita lile pori la Chalinze halafu wanaendelea wanakuja wanakuta tena kuna

pori lingine kati ya Chalinze na Morogoro. Kutokea Morogoro kuna pori kati ya Morogoro na Gairo. Haya mapori yote kila unapopita utakuta magunia na magunia ya mkaa barabarani, lakini miti inaendelea kuisha. Sasa unajiuliza kwamba huyo mtu wa Maliasili ambaye anatoa vibali tu na miti inakatwa hakuna mti unaopandwa, sasa tunaanza kujiuliza hivi sasa ni jukumu la nani? Ni jukumu la Wizara hii au ni jukumu la Maliasili?

Tunaomba Wizara hii ijaribu kuangalia na kuhoji Maafisa Maliasili katika hii Mikoa miwili kuwauliza wao wanakuwa na kigezo gani cha kutoa vibali tu vya kukata miti ilimradi wamepata pesa na Halmashauri zinapata kodi au ushuru kutokana na huu mkaa unaochomwa mle. Tunaona kwamba wao *interest* yao wanapita wanaangalia wewe una kibali? Kama huna kibali unanyang'anywa mkaa wako. Lakini nashangaa hawaulizi kwamba wewe unapokwenda kukata miti kule au hizi pesa wanapozipata miti inakatwa, wana jitihada gani za kuhakikisha kwamba hii miti inayokatwa kunakuwa na replacement? Kwa sababu kuna hatari kwa mfano huu msitu wa kati ya Morogoro na Gairo, kama pori la Dakawa kila siku wanakata miti. Ukiangali ni kwamba ile miti inaendelea kupungua. Kuna dalili za kuonyesha kwamba jangwa litakuwepo na dalili ni kwamba hata wale wenzetu wafugaji ambao wanalisha ng'ombe wao katika maeneo haya, inabidi mara nyingi wahame kwa sababu kunakuwa na ukame ambao umekithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hilo Waziri anayehusika aliangalie kwamba atashirikianaje na hizi Wizara nyingine kwa sababu hii haiwezi kuwa vita ya mtu mmoja. Ni lazima sasa kuwepo na *inter-ministerial collaboration* ili kuhakikisha kwamba haya mapori ambayo kila siku yanapukutika, tunaweza tukaangalia kwamba huu uharibifu unaanza kupunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba watu watafute *alternative source of energy*. Sasa hiyo *alternative source of energy* kwa Muafrika ambaye kipato chake ni kidogo haipo. Tukisema wapikie mafuta ya taa ndio yamepanda bei kweli! Sidhani kwamba wale ambao walikuwa wanapikia mafuta ya taa sasa hivi wataendelea kupikia mafuta ya taa, hata mkaa unapanda bei, watanunua kuni.

Kwa hiyo, hata vile vichaka vidogo vidogo vitaanza kufyekwa. Tukisema wapikie umeme, ni kwamba hata wale waliokuwa wanapikia umeme wanakaa magorofani inabidi wateremke chini watafute namna ya kupikia kwenye mafiga kwa sababu umeme umepanda bei kupita kiasi. Ndio sababu nasema kwamba, kuwepo *inter-ministerial collaboration,* waangalie kwa pamoja wanashirikiana vipi kuhakikisha kwamba mwananchi anaweza akapata *alternative source of energy* ya kupikia na kuwasha kibatari ndani ya nyumba yake bila kuendelea kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja pia kwenye suala la Bwawa la Mindu. Bwawa la Mindu mwaka huu mwanzoni ilibidi Mamlaka ya Majisafi na Majitaka iingie hasara kubwa sana ya kuweza kusafisha maji kwa sababu lile bwawa limejaa matope. Limejaa matope kwa sababu tatu muhimu. Sababu ya kwanza ni hii barabara ambayo inajengwa. Wale wamechimba mitaro yao, wamekusanya takataka zao karibu na bwawa

wakaziacha hawakusambaza wala hawakuzichukua kwenda kutupa mbali. Mvua iliponyesha, yote imekwenda kwenye bwawa. Hilo ni moja.

La pili, ni uharibifu wa ukataji wa miti hovyo katika Milima ya Uluguru, imefanya kumekuwepo na mmomonyoko wa udongo kwa hiyo lile bwawa likaanza kujaa na kuanza kupata visiwa vya udongo ambavyo vimeteremka kutoka milimani.

Tatizo lingine ambalo limekuwa ni kubwa linatokana na Wizara ya Nishati na Madini. Ninafikiri, kuna Ofisa wao mmoja ambaye amekwenda kuwabonyeza watu kwamba kuna dhahabu karibu na lile bwawa. Wameanza kuingilia, wamechimba na matokeo yake ni kwamba sasa kuna mashimo, kuna mmomonyoko na bado wanaendelea kuchimbachimba. Sijaona jitihada ya Wizara husika kuhakikisha kwamba inasaidiana na Mamlaka ya Maji na Serikali ya Morogoro pale Mjini kuhakikisha kwamba hawa watu wanaochimba kule hawachimbi. Kichekesho ni kwamba, walipoanza tu kuna wengine walikuja tayari wana hati za kumiliki vitalu.

Sasa tunashangaa huyu mtu ambaye anaona kwamba pa kuchimba dhahabu ni karibu na chanzo pekee kikubwa, 80% ya maji yanayotumika Morogoro Mjini yanatoka katika Bwawa la Mindu. Sasa ghafla tu kwa wiki moja walipokaa pale kulikuwa na watu zaidi ya 4000 na kwa mahesabu ni kwamba walikuwa hawana choo wala nini, tulifanya mahesabu tukakuta kwamba walifanya *contamination* ya kinyesi tani 800 kwa wiki moja tu katika lile bwawa. Matokeo yake ni kwamba Ilibidi Mamlaka ya Maji itumie pesa nyingi sana kununua dawa za kufanya super chlorination kupunguza mlipuko wa magonjwa katika Manispaa ya Morogoro.

Ninaomba Wizara hii ijaribu kuhimiza Wizara nyingine ambazo zinahusika katika lile bwawa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na *proper environmental security* kwamba machimbo yale yasitishwe mara moja pamoja na kwamba tunajaribu kuweka Polisi, utaweka Polisi mpaka lini? Lakini naomba hali kama hiyo basi, Wizara ya Nishati na Madini ihakikishe kwamba Maofisa wake wanawajibika pale ambapo wanakwenda kutoa information kwa watu *regardless* ya kwamba kama madini yapo lakini kilichopo ambacho kinawasaidia wananchi ni nini? Ni yale maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie usafi katika Miji yetu. Nakwenda katika Miji hii midogo midogo hata Dar es Salaam, unakuta Maofisa wa Afya wanapita wanahimiza watu wachimbe majalala ya takataka kandokando ya barabara karibu na nyumba zao na kama huna lile jalala basi unapewa adhabu. Sasa mimi najiuliza, haya majalala yakijaa aidha wanachoma pamoja na mifuko ya *plastic* kwa hiyo unakuta *the whole surrounding* inakuwa na harufu ambayo inafanya watu wanakohoa na mengineyo. Wengine wanayafukia, baada ya muda wanakuja wanayachimbua. Kwa hiyo, takataka zote zinazagaa. Sasa tungeomba kwamba Wizara hii iweze kukishauri Wizara ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwamba wahakikishe kwamba wanawaagiza Watendaji wao katika Halmashauri kwamba kuwepo na *alternative way* ya *disposal* ya *hard rubbish* yaani taka ngumu zisiwe zinachimbiwa mashimo kando kando ya barabara Mijini katikati. Lazima kutakuwepo na *solution* tu kwamba sasa hawa watu waelimishwe

namna gani ambavyo watatupa takataka zao kwa njia ambayo haitatoa athari kwa mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaomba nizungumzie sasa jitihada za Wizara na Serikali katika kupunguza umasikini. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba umasikini unaendelea kukithiri. Hiyo ni hali ya kukatisha tamaa. Lakini ni vizuri tukajiuliza ni kwa nini huu umaskini unaendelea kukithiri? Sijui kama Mheshimiwa Waziri alituzungumzia ni kwa nini umasikini unaendelea kukithiri pamoja na jitihada zote ambazo zinafanywa na Serikali yetu. Nafikiri Mheshimiwa Waziri atatueleza. Sasa kama bado hajui ni kwa nini unaendelea kukithiri, basi tunakuomba aelekeze jitihada zake katika kufanya utafiti kwa sababu bila kufanya utafiti tujue ni kwa nini unaendelea kukithiri, naomba nielezee kwamba we can not have a permanent solution kama hatujui ni kwa nini.

Tunazungumzia tu umasikini unaendelea kukithiri, umasikini unakuwepo, tunazungumzia kwamba watu wapate mitaji, wafanye nini lakini wapate mitaji ya kufanya nini? Ni vizuri kila mtu katika maeneo yake ambako yeye yupo asaidiwe hapo alipo lile ambalo linafanya kazi Dar es Salaam la kuuza kanga, kuwa na *Viosk* na Mama Ntilie, haliwezi likafanya kazi katika maeneo ya Vijijini.

Sasa umasikini unakithiri zaidi Vijijini kwa sababu watu wanategemea kilimo cha mkono, jembe la mkono, wanamwomba Mwenyezi Mungu wapate mvua. Tukitenda dhambi sana Mwenyezi Mungu akitunyima mvua basi, njaa inakithiri tunakosa mazao. Sasa ningeomba kwamba sasa hivi basi tuwe na kitu ambacho tunasema kwamba ni *focused approach*. Iwe *tailored* kwa kufuatana na mazingira ya yule masikini ambaye ni mwananchi anayeishi Kijijini, anayeishi katika slums za Miji yetu. *(Makofi)*

Naomba kusema kwamba vijana wengi sasa hivi, kuna vijana ambao wamesoma, wana ujuzi lakini bado hawana namna ya kuweza kupata hiyo mitaji tunayoizungumzia. Huyo kijana atakwenda kukopa wapi ikiwa yeye hana nyumba anaishi kwa baba yake, hana kitu chochote cha kupeleka Benki kwenda kufanya *collateral.* Hata kama akienda kukopa hizi pesa wengine wanazi-*misuse* kwa sababu hawana ujuzi wa kuweza kufanya shughuli ambayo inakuwa ni *very productive* na ambayo ni *profitable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba elimu aliyozungumzia kwenye ukurasa wa 78 kwa kutumia Redio Tanzania, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kuna kipindi kinachoitwa Tujikomboe. Redio Tanzania inafika wapi? sehemu nyingi haifiki! Kwa hiyo tunaomba kwamba pamoja na kutumia Redio Tanzania kutoa elimu hiyo, tunaomba basi atumie na zile *community radios* ambapo Redio Tanzania haisikiki. Mheshimiwa Waziri pia amezungumzia kuhusu Gazeti la Mapambano. Hili gazeti sijui kama mimi nimeshawahi kuliona, lakini hata kama litakuwepo tutalipeleka kwa wananchi wangapi? Utahitaji pesa nyingi sana kuanza kuchapisha gazeti kama hilo. Sasa tujaribu kutoa elimu kwa Viongozi wote katika ngazi za chini waelimishwe Wenyeviti wa Mitaa, elimu hii itolewe mashuleni wanafunzi wanapokuwa wanaendelea kusoma basi, kile kipindi ambacho tunasema ni cha Maarifa ya Nyumbani, basi wafundishwe namna ya kuweza kujitegemea, sio kufikiria tu kwamba nikimaliza Shule

nakwenda kupata kazi. Wengi wa watoto wa Tanzania wanamaliza Shule wakifika Darasa la Saba. Mtoto anamaliza Darasa la Saba lakini hajui maana ya kujitegemea. Tunaomba sasa mfumo wa elimu yetu sasa, katika syllabus...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kukushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, naomba kutoa salam za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Kasapira, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi, *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa rambirambi hizo, napenda kuwapongeza Mawaziri wetu wawili, Mheshimiwa Ntagazwa na Mheshimiwa Maokola Majogo kwa kazi zao nzuri za ushirikiano za kuiongoza Wizara hii. Vile vile napenda kutoa pongezi kwa hotuba nzuri ambayo wametuletea leo hii na yote hayo yasingekuwa isipokuwa kwa ushirikiano wao mzuri na wataalam wao ama wataalam wetu wote, kwa hiyo napenda kuwapongeza kwa hotuba nzuri na kabla sijasahau ninapenda kuwaunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baada ya kutoa pongezi kwa Mawaziri na wataalam napenda vile vile kuipongeza Ofisi yetu ndogo ya Makamu wa Rais iliyoko Zanzibar na Watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na vile vile kwa ushirikiano mkubwa na wananchi tukiwemo sisi Wabunge. Kwa kweli wanafanya kazi vizuri, wao ndio tegemeo letu. Sisi tukienda pale kwa mambo yote ya kupata ufumbuzi kwa mambo ya Muungano kwa kweli wanatusaidia, wanatuongoza vizuri, tunawashukuru sana na tunawaomba wasichoke. *(Makofi)*

Lakini pia pongezi za pekee napenda kumpongeza Makamu wetu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Shein kwa kazi yake nzuri ambayo anaiongoza nchi hii kwa ushirikiano mkubwa na viongozi na wananchi. Mheshimiwa huyu hachoki, mchana usiku kwa kweli anaitembea Tanzania nzima kama wenzangu walivyosema katika kutafuta matatizo ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi kwa ushirikiano mkubwa na viongozi wenzake akiwemo Rais wetu Mheshimiwa Mkapa. Kwa kweli hapa Mheshimiwa Rais Mkapa amechagua kiongozi shupavu, nampongeza sana na Mwenyezi Mungu amjalie Mheshimiwa huyu awe na uwezo mzuri zaidi wa ushirikiano na ampe umri zaidi azidi kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda sasa kuchangia hoja. Kwa sababu sitasema maneno mengi, napenda kwanza nisije nikasahau niende moja kwa moja kwenye mradi wa *TASAF* maana huu mradi wa *TASAF* una mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Rais wetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wetu wa Zanzibar kwa kuleta mradi huu katika nchi yetu ya Tanzania na kutusaidia. Wananchi wa Tanzania tulikuwa mbali sana kwenye umasikini mkubwa sana na tulikuwa tunajiuliza tufanye nini ili tuokoke na umasikini, lakini Mwenyezi Mungu akawapa nguvu Waheshimiwa Marais wetu ukaletwa mradi huu wa *TASAF* na kwa kweli mradi huu umetukomboa Tanzania. Mradi huu umetukomboa kwa sababu umelenga sana wananchi, sio kama Maafisa wanajifanyia peke yao, hapana. Wanakwenda Vijijini, wanafanya kazi vizuri, wanashirikiana na wananchi bega kwa bega, wananchi wanaibua miradi yao ambayo inawakera sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda kushukuru sana kwa mradi huu wa *TASAF,* ila kuna moja. Huu mradi wa *TASAF* ni mzuri, lakini kama alivyozungumza mwenzangu Mheshimiwa N'hunga asubuhi nilimpongeza sana kwa sababu yale aliyozungumza na mimi kwenye Jimbo langu halikadhalika ndiyo hivyo hivyo. Sijui hata nisemeje! Huu ni mwaka wa nne niko Bungeni hakuna asiyeniona nikitetea kila siku kwenye maswali yangu ya kawaida asubuhi hapa, nikichangia natetea kuhusu *TASAF* katika Jimbo langu; huko Jimboni tukiwa kwenye Mikutano, lakini Mradi wa *TASAF* napenda kusema kwamba mpaka leo bado sijapata mradi kwenye Jimbo langu. Kwa kweli inasikitisha sana! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Lia! lia! Pole! *(Kicheko)*

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kusema sana nitalia, usione kama ninacheka, rohoni nina uchungu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona uchungu kwa sababu gani? Mwaka wa mwanzo tuliambiwa viongozi twende kuhamasisha wananchi Majimboni mwetu. Tukaenda kuhamasisha. Mimi nikaenda katika Vijiji vyote, ukapatikana mradi katika Kijiji cha Mvumoni Kilimahodi na vile vile mradi mmoja wa Wara wa Ujenzi wa Shule kule Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika mahali mpaka nikawa naogopa tena kwenda kule Kijijini. Nikienda wanasema, uko wapi huo mradi? Uko wapi?! Watu tunataka maji! Watu wana matatizo hasa wanawake jamani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri sasa anataka niwe mkali. Mheshimiwa Waziri, mradi wa *TASAF* katika Jimbo langu sijapata na sijui kwa nini sijapata au nafikiri kuna ubinafsi ndani yake katika utendaji. Haiwezekani Majimbo mengine yana miradi mitatu mitatu na nina ushahidi kamili, Pemba ile ile kuna miradi. Au kwa sababu Vijiji vingine vina Mawaziri? Lazima tuseme hiki kitu! Watu wengine wanauharibu mradi wa *TASAF.* Rais wetu Mkapa kwa imani yake ametuletea Mradi wa *TASAF* kwa imani nzuri ili wananchi waondokane na umasikini, kwa nini vinachaguliwa Vijiji vingine miradi mitatu, Vijiji vingine hatujapata mpaka leo? Naomba baadaye wakati Waziri akifanya majumuisho anijibu, kwa nini Jimbo langu la Wawi na Vitongoji mpaka leo hatujapata mradi? Majimbo yote Pemba yamepata miradi ya *TASAF,* kwani sisi tumekosa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani Vijijini huko wanasema, wanakuja kutudanganya tu, hakuna mradi, hakuna nini! Au njooni wenyewe kule vijijini muwaambie kwamba mradi huu haukubaliki hapa. Lakini kwa nini mnatutuma sisi tukawaambie watu wahamasike wachague miradi yao, pesa imeshatengwa; maana pesa mpaka imeshatengwa lakini huu mwaka wa nne nasogezwa mbele. Kwa nini wengine tusogezwe mbele? Mimi nafikiri kuna ubinafsi ndani yake au kuna namna fulani wanataka watufelishe, lakini sisi hatutafeli, watafeli wao. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo kwenye Mradi wa *TASAF* naomba kwenda kwenye Mradi wa *NAGP.* Kila siku nalizungumza suala hili hapa na Mheshimiwa Majogo ananiahidi kila siku. Kule Pemba ulikuwepo mradi huu wa *NAGP* ambao unashughulika na mambo ya ukulima wa chumvi. Vijana, wanawake na akina baba hawana kazi za kufanya kule. Unajua kule Visiwani wanashughulika na mambo ya biashara ya chumvi. Biashara ya chumvi, chumvi bila kuitia iodine huwezi kuitumia, hawawezi kupata soko la nje. Nikaambiwa hapa kwamba wataleta mashine. Katika Jimbo langu la Wawi ikatolewa nyumba maalum ikatengenezwa iwe ni kiwanda. Lakini mpaka leo hakuna kilichofanyika. Vijana wote wakawa wamehamasika katika Jimbo la Wawi au Pemba nzima kwamba angalau watapata ajira na watauza chumvi yao, watapata pesa; mpaka leo! Mheshimiwa Majogo kila siku unanidanganya. *(Kicheko/Makofi)*

Leo nasema hapana kudanganywa hapa! Tuambiwe ukweli! Mradi huu utarudi tena Pemba? Sasa sio Pemba peke yake na Zanzibar Chukwani huko na sehemu nyingine. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, maneno ya kudanganya itabidi uyaondoe kidogo. *(Kicheko)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, *I am sorry!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ukiahidiwa kitu hakitendeki naona maana yake ndiyo hiyo hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuchangia Mradi huu wa *SELF.* Hii *SELF* kila siku hapa tunaambiwa Pemba kuna *SELF,* mimi nataka niambiwe hii *SELF* iko kwenye eneo gani? Mimi sioni mradi wa *SELF* na wala sijui unashughulika na nini. Kwa hiyo, naomba sana Mradi wa *SELF* kwa kweli tusiambiwe kama huko Pemba hauko na kama uko, basi tuambiwe uko wapi. Wananchi wanapata shida, wanafanya miradi yao midogo midogo hawana msaada wowote, wanalia na sisi na sisi lazima tulie na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna hii sheria ya *SIDO* ya mwaka 1973. Mimi nazungumza hii *SIDO* sio eneo lake lakini ni eneo lake kwa sababu ni kuondoa umasikini. *SIDO* inaondoa sana umasikini katika nchi yetu, lakini sheria hii ilipotungwa hapa Bungeni mwaka 1973 ilikuwa ni ya Tanzania Bara tu. Tanzania Visiwani

haikuingizwa. Naomba sana Serikali itayarishe tena Muswada walete hapa Bungeni turekebishe ili *SIDO* nayo iwepo Zanzibar. Pemba na Unguja iwepo, watu wote, vijana hususan vijana wapate ajira. Vijana hawana ajira! Mara tunawaambia wanavuta bangi, wanakuwa wezi; wasiwe wezi vipi wakati hawana kazi za kufanya!?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Pride Tanzania* napenda kuishukuru kwa sababu imekuja Pemba na imetoa mikopo midogo midogo kwa wananchi wakiwemo wanawake na vijana na akina baba, tunaipongeza sana. Tunaomba isifikie hapo mwisho, iendelee mpaka Vijiji vya ndani. Hata Jimboni kwangu pia *Pride* imefika na wanawake na vijana wamenituma kuishukuru *Pride.* Lakini vile vile ipunguze riba. Riba ni kubwa! Tunaomba sana riba ipunguzwe kidogo kwa sababu hali za biashara kule Pemba sio nzuri sana. Unaweza ukafanya biashara siku nzima unapata Sh.5,000/=. Sasa riba hiyo utaipata wapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine vile vile napenda kuchangia kuhusiana na mambo ya Muungano wetu. Mimi napenda kuushukuru sana Muungano wetu. Kwanza napenda kuwashukuru Waasisi wetu wa Muungano, Hayati Baba wa Taifa, Julius Kambarage Nyerere na vile vile Hayati Sheikh Abeid Aman Karume kwa kuuasisi huu Muungano wetu. Sisi vizazi tuliopo sasa tunaupenda sana Muungano na sisi watu wa Zanzibar tunaupenda sana Muungano na tunaukiri kwa kweli. Labda asiyeupenda ni yule ambaye hapendi maendeleo ya nchi hii. Kwa hiyo, tunapenda tuudumishe Muungano wetu na vile vile tuutetee kwa sababu umeanzishwa na Waasisi wetu na kwa kweli Muungano hauna matatizo isipokuwa mambo madogo madogo ya kawaida na yakikaliwa kitako yanaweza kurekebishwa. Jamani tusiuchukie Muungano, tuupende ili tuweze kuendeleza nchi yetu kwa umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwenye tatizo la Ukimwi. Tatizo la Ukimwi linapunguza sana nguvu kazi ya Taifa letu. Ukimwi ni tishio kwa dunia na hapa kwetu Tanzania kwa kweli kila tukienda mbele tunasema unapungua lakini ndio kwanza unaongezeka.

Kwa hiyo, tumwombe Mwenyezi Mungu atuondolee tatizo hili na sisi wenyewe tukijitahidi kwa sababu bila kujitahidi kila siku tunapiga kelele Ukimwi Ukimwi lakini mambo yote yanayopelekea Ukimwi tunayatenda, kwa kweli hatutaondokana na Ukimwi. Lazima tujitahidi hasa viongozi kuelimisha wenzetu tukiwemo sisi wenyewe ili matatizo haya yapungue. Ukimwi hauna dawa.

Kwa hiyo napenda sana kwa wale wenzetu ambao wameshaathirika tuwapende, tuwasaidie, tusiwanyanyapae. Vile vile watoto yatima inasikitisha sana kuona mtoto anazaliwa mfano hana baba, hana mama, wazee wake wote wameshakufa. Nyumba unakwenda kuiona, mimi nimeona kwenye *TV Makete* sijui sehemu gani, yaani inasikitisha sana. Yaani nyumba imefungwa wako watoto watupu ndani ya nyumba.

Kwa kweli Serikali yetu isaidie kuwapatia misaada watoto yatima. Watoto yatima sio waliofiwa na wazee wao waliokufa kwa Ukimwi tu, lakini vile vile watoto yatima wote ili na wao waone kwamba wako katika maisha ambayo ni ya faraja kwa

sababu kuna tabia ya *NGO* nyingine ni briefcase *NGOs*, wanasema Ukimwi Ukimwi halafu wanachukua hela wanakula wao. Hawapendi kupeleka misaada hiyo kwa walengwa.

Tunaomba Serikali yetu isimamie suala hili ili *NGOs* hizi zenye tabia hizi ziondolewe au zifutwe. Tunapenda sana watu katika nchi hii tupendane. Ukishamwona mwenzako ana Ukimwi sio tena umcheke au umseme. Ni mambo ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Nakushukuru Mwenyekiti, kwa kuniruhusu ili niwe mmojawapo katika kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri safi pamoja na wataalm wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuzungumzia kuhusu *TASAF*. Napongeza sana kuhusu mradi huu wa maendeleo ya *TASAF* na nashukuru sana kwa sababu kwenye Jimbo langu umeshaingia katika sehemu mbili, Shehiya mbili, Shehiya ya Maungani kwa kujenga skuli moja safi kubwa na Shehiya ya Kibondeni. Kwa hiyo kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Mwera nampongeza na natoa shukrani za dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nazungumzia kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Ndiyo! Hivi kuna ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar. Lakini Ofisi hiyo hivi sasa haiendelei kujengwa na ime-stopishwa. Kwa hiyo ningependa nijue itaanza lini na Ofisi hiyo kwa bahati nzuri iko kwenye jimbo langu la Mwera. Lakini kwa bahati mbaya na ya kusikitisha kabisa kabisa wakati kinaandaliwa kiwanja au sehemu ya kujenga palikuwa na vipando, siyo magari, yaani mihogo, viazi vitamu, migomba ya wananchi. Vyote vimeng'olewa na wananchi wale hawakupata fidia hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mazao, palikuwa na jengo moja la maskani ya CCM ambayo tayari lilikuwa lina kozi nne, linaendelea kujengwa nalo limebomolewa nao vile vile hawakupata fidia yoyote. Kwa hivyo nalo hili ningeomba nifafanuliwe leo, vipi watalipwa watu wale. Lakini la kuskitisha zaidi ni kwamba sehemu ile ilikuwa linapita bomba kubwa la maji ambayo yanasambaza maji kwa wananchi na baada ya ujenzi huu kufika bomba lile limekatwa na wananchi wanapata matatizo ya maji pale, hivi sasa wanapata maji masafa marefu sana na mpaka leo hawajaunganisha na ujenzi umesimamishwa. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwera nataka maelezo au kama litaungwa tena kwa ajili ya kupata wananchi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naendelea kuchangia mambo ya Muungano. Muungano mara ya kwanza ulikuwa unazungumziwa chini chini kwa yule ambaye haupendi muungano anakaa nyumbani kwake anasema kwamba muungano huu haufai sijui vipi. Lakini sasa hivi Muungano unazungumzwa dhahiri kwamba muungano haufai. Kwenye majukwaa ya kisiasa, kwenye magazeti, kwenye redio, mtu anayo haki ya

kuukosoa muungano na chombo kikubwa cha kufanya ili muungano uwe nzuri ni Ofisi ya Makamu wa Rais. Tunaweza kusema kwamba Ofisi hii ni Ofisi ya uhamasishaji ili muungano uwepo na udumu, ili kuuhamasisha muungano uwepo na udumu ni lazima uende sambamba na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa sababu kule ndiko kunako upinzani mkubwa kwamba muungano hautakiwi. Kwa hiyo, kama Ofisi ya Makamu wa Rais itakuwa ina kigugumizi kwa baadhi ya mambo kule Zanzibar watatuweka pabaya Zanzibar na hasa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hawa wanaokaa wakasema kwamba muungano haufai ni vyama vile ambavyo vina sababu zake. Sasa ili sababu zile tuziondoe hizi kasoro ndogo ndogo ambazo alizozisema Mheshimiwa Waziri leo ambaye amemnukuu Mheshimiwa Rais wetu basi kasoro hizi na sababu hizi na matatizo haya wasimamizi wakuu ni Ofisi ya Makamu wa Rais, hakuna mwingine tena. Kwa hivyo, la kwanza tunaomba chombo hiki moja kwa moja kwa mambo ya muungano na mambo yaliyoko yasiyo ya muungano lakini yanaweza kusaidia Zanzibar yaende sambamba na Wazanzibar pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lazima tuelewe kwamba kuna usemi ambao unasema kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini vile vile naweza kusema kwamba na Tanganyika ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu nchi hizo zote mbili zimetoa nchi zao kwao kwa niaba ya kuunda muungano. Kwa hivyo, wakati nchi hizi zote zimetoa sehemu zao za nchi na kuwa muungano mmoja ni lazima wakati nchi ya Zanzibar ni ndogo muuilee vizuri sana.

Natumaini muungano wetu wa Chama Cha Mapinduzi ulifanyika 1977. Lakini Mwalimu Nyerere, Baba wa Taifa alithbutu kusema, nashangaa sana na Wazanzibar, nchi ndogo kama hii kukubali na hawakuogopa kwamba watamezwa na kanchi kakubwa kama kale na wamekubali kutoa nchi yao kuwa chama kimoja, kujitia kwenye muungano, nawapongeza sana Wazanzibar. *(Makofi)*

Na nitajitahidi sana kuhakikisha simeezi Zanzibar na mojawapo ili kuhakikisha Zanzibar isimezwe, Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuilea na hasa katika mfumo huu wa vyama vingi. Hivi sasa kila mmoja akija Zanzibar hazungumzi kwamba Tanzania Bara tutapata au Serikali ya Muungano au Jamhuri ya Muungano tutachukua. Anayekuja yeyote akiwa mpinzani anasema ah! Zanzibar tutapa ushindi. Hawasemi kwamba Tanzania Bara au Serikali ya Muungano tutapata ushindi, wote wameelemea Zanzibar tutapata ushindi kwa hivyo mashirikiano ya pamoja na hasa ilivyokuwa chama tawala ndicho kinachoendesha Zanzibar na Tanzania Bara lazima twende sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mpango wowote unaokuja Zanzibar ikiwa Ofisi, kama hivi sasa tunajenga Ofisi ya Bunge na tuliambiwa mwezi wa tano inaanza. Nathubutu kusema kwamba walahi Ofisi ile itakuwa na kigugumizi. Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar itakuwa na kigugumizi, na zile ndizo kasoro kubwa. Wazanzibar lazima tuwe tunajinafsi kabisa kabisa kwenye Serikali yetu ya Muungano. Na vyombo vyetu vya muungano. Wenye vyombo vya muungano kule Zanzibar na Ofisi ya Makamu wa Rais wapate Ofisi yao watanue, wajisikie, watembee kifua mbele, twende pale

tufurahi kabisa kabisa, wajitanafasi pale tutasema muungano tayari. Lakini wakati huo huo na Ofisi ya Bunge nayo iwe vile vile. Jambo lingine ambalo nataka kulisemea ni kuhusu Ofisi za Wabunge Zanzibar. Wabunge Zanzibar immetufanya kama watoto yatima tena watoto yatima wenyewe wa ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wanaona wao wanaogopa pengine wana ukimwi. Kwa hiyo, naomba mpango huu uondoshwe, Ofisi ya Waziri Kiongozi, uletwe kwenye Ofisi yetu hasa Ofisi ya Makamu wa Rais washughulikie. Kwa sababu Ofisi ya Waziri Kiongozi hivi sasa inalea watoto wawili, Wawakilishi na Wabunge. Wawakilishi nadhani wao hawana Ofisi, sisi tutatafutiwa Ofisi kweli? Mtoto wote kawazaa mwenyewe, na tukitaka tusitake, SMZ, wenzake Wawakilishi, kweli watatoa Ofisi, hawatoi. Kwa hiyo, nawaomba hili litafutiwe ufumbuzi mpya na sisi tuwe na Ofisi zetu, tusikaye chini ya miembe na sisi ni Wabunge, kama wenzetu walivyokuwa Wabunge. *(Makofi)*

Sisi Wabunge wa Chama Tawala wote hatuna matatizo na muungano wala hatuna matatizo na hotuba hii. Matatizo yetu ni yale yale kwamba kwenye kasoro tupakosoe kwa uadilifu na pale pazuri tupasifie kwa njia zote na tutumie vile vile vikao vyetu vya kukosoana kama tunavyokosoana, siyo kwenye hadhara.

Baada ya hayo Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi isipokuwa naunga mkono hoja asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF* ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii kwa maana kwamba, unalenga katika kuondoa kero kwa Wananchi kwa kuwapatia huduma mbalimbali kama vile barabara, shule, zahanati na kadhalika. Huduma hizi kwa kweli huwa zinawagusa moja kwa moja Wananchi. Kwa umuhimu wake *TASAF* ilikuwa kwa vyovyote iwe inaendesha miradi yake kwa kuwashirikisha kwa kiwango cha kutosha, Wawakilishi wa Wananchi kama sisi Waheshimiwa Wabunge. Hii ni kwa kuwa Wabunge ndio wanaopaswa kuyaelewa sana mahitaji ya Wananchi na pale penye matatizo wao ndiyo wa kwanza kuyaelewa na pia kuwa wa kwanza katika kujua namna ya kuyatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kwa upande wa Pemba pale kwetu Wilaya ya Chake Chake, Maofisa wa *TASAF* hawatushirikishi kabisa sisi Wabunge. Mfano, mimi mwenyewe huu sasa ni mwaka mzima tokea niwe Mbunge, sijaitwa na Afisa yeyote wa *TASAF* wala sielewi kitu gani kinaendelea katika suala zima la *TASAF*. Kwa namna hiyo, ushauri wangu ni muhimu sana katika kuanzisha miradi Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaona mambo makubwa yakifanyika kimzaha mzaha kana kwamba, jambo lenyewe linafanywa na mtu mnyonge tena wa mawazo na fedha pia. Kwa mfano, nimeona ujenzi wa barabara mbili Jimboni mwangu zinazojengwa na Mfuko wa *TASAF.* Barabara hizo moja ni ya Shungi, Tundaua na

nyingine ni ya Chanjamjawiri Limani. Barabara hizi zote ni za kiwango cha kifusi. Magari huteremsha kifusi kilichojaa mawe makubwa kidogo. Badala ya Wananchi kupatiwa gari la kutandaza na kushindilia kifusi hicho, utawaona Wananchi wenyewe wakifanya shughuli hizo. Kutokana na ukweli kuwa mkono mtupu hauwezi kuwa kifaa bora cha ujenzi wa njia, ni dhahiri kuwa ujenzi huo huwa wa ovyo sana. Mawe hayakkti sawasawa kwenye ardhi, kifusi hakichuwami sawa sawa pia na kwa hivyo njia nzima huwa ya muda mfupi sana kwani haihimili upepo wala mvua. Hali ya hewa yoyote ni tatizo kwa barabara hizo, kwani upepo hupeperusha kifusi na mvua kuhamisha kabisa kifusi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapungufu hayo, kazi inayofanywa na *TASAF* huwa ya bure na fedha itolewayo haileti faida katika kiwango kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuonesha kuwa Serikali iko *very serious* katika miradi ya *TASAF,* ninaishauri Serikali kwa dhati kabisa kuwa, miradi ya *TASAF* itushirikishe Wabunge kikamilifu badala ya kuangalia mambo kama wapita njia na hali sisi hasa ndio wadau wakubwa sana wa miradi ya Wananchi hasa majimboni mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 mwezi wa Aprili, ulianza kwa vishindo na kwa kutawaliwa na utashi wa kisiasa. Kwa wakati ule tunaweza kusema kuwa kwa utashi huo wa kisiasa na mazingira ya wakati ule, pengine ndiyo ilikuwa ndiyo sababu ya Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jaji Nyalali kupitia Tume yake ya mfumo wa chama kimoja au vyama vingi vya siasa hapa nchini, Jaji Nyalali alipendekeza kuwa, lazima mfumo wa vyama vingi vya siasa uanzishwe hapa nchini. Kwa kuanzishwa kwa mfumo huo, ambapo kutakuwa na uwezekano wa vyama tofauti vya siasa kushinda na hivyo kushika hatamu katika pande tofauti za Muungano, jambo hilo kwa mujibu wa Jaji Nyalali, linaweza kusababisha mtafaruku au mkanganyiko mkubwa wa utawala na kuondoa yale mazowea ya watu kukaa pamoja na kusemezana pale linapoibuka tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usemi wa asiyesikia la mkuu huvunjika guu, umelisibu Taifa letu. Siasa za wakati huu hazikubaliani kabisa na mfumo wa Muungano wa Serikali mbili. Mfumo huu unalazimisha utawala wa chama hicho hicho katika pande zote za Muungano hata kama upande mwingine chama hicho hakikupata ridhaa ya kutawala kutoka kwa Wananchi walio wengi wa upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo linasababishwa na ukweli kuwa, Muungano tulionao *purely* ni wa kisiasa ambao maslahi ya kisiasa pekee ndiyo yanayotawala katika kuendesha Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasababisha kukosekana kwa demokrasia kwa kiwango kikubwa na cha kutisha sana kwa upande wa Zanzibar. Wananchi waliojiunga na chama cha siasa halali cha *CUF* wamekuwa wakiporwa ushindi wao kwa hila tokea pale mwaka 1995 na mwaka 2000, mambo yakawa mabaya zaidi pale Chama cha Mapinduzi baada ya kugundua kuwa kimeshindwa vibaya katika uchaguzi wa mwaka

kikatumia Serikali yake katika kuviamrisha vyombo vya dola kama vile polisi, jeshi la wananchi, KMKM, JKU na kadhalika. Vyombo hivyo vilipita katika vituo vya kupigia na kuhesabia kura, wakawatisha Mawakala wa Chama cha *CUF* na wa vyama vingine vya Upinzani kwa kufyatua risasi ovyo ovyo juu. Baada ya kuona kuwa hali ilikuwa ya kuwaruhusu kufanya wapendavyo, walivibeba visanduku chini ya mtutu mkali wa bunduki na kuvipeleka katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya bila ya Mawakala wa Vyama vya Upinzani kuelewa hatima ya visanduku hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wiki nzima ndiyo Tume ya Uchaguzi ikatangaza matokeo ya Uchaguzi kama ilivyopenda yenyewe peke yake. Mgombea wa Urais wa Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamad, akaibiwa kura zake kupita kiasi na Majimbo yakagawiwa ushindi wa Ubunge na uwakilishi kama njugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chini ya mfumo wa vyama vingi na wa Muungano wa Serikali mbili, jambo hilo siku zijazo litasabatisha madhara makubwa kwani *CUF* hawako tayari kuona wakiporwa tena ushindi wao kwa njia yoyote iwe ya hila au ya mabavu, kwa mantiki hiyo kama vile alivyosema Jaji Nyalali, njia pekee ya kutatua tatizo hilo ni kuanzishwa kwa Mfumo wa Muungano wa Serikali tatu, ya Tanganyika, Zanzibar na ya Shirikisho. Kinyume chake tuwe tayari kushuhudia matatizo makubwa zaidi na zaidi na safari hii ya kutisha sana ikiwa demokrasia haitaachwa ikatembea kupitia mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu inaonekana kuwa uhai wa Muungano huu ni kikwazo kikubwa cha demokrasia ya kweli Zanzibar. Serikali ya Muungano bado inaweza kuendelea kukilinda Chama cha Mapinduzi na kukiweka madarakani hata kama watu wote watakikataa kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya Uchaguzi wa mwaka 2000, merikebu za kijeshi zilikuwa zikimimina mamia kwa mamia ya Wanajeshi ambao hatimaye yalisaidia kubeba visanduku vya kura na kuwatisha Wananchi. Ili hali hiyo iondoke na watu wapate matunda ya demokrasia, lazima mfumo wa Muungano ubadilike ili uchaguzi uwe wa haki na huru.

**MHE. SHARIFA MBAROUK KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kukubali kushughulikia mifuko ya *plastic* na kufikiria kupiga marufuku uingizaji na utengenezaji wa mifuko hiyo. Naiomba Wizara hatua hizo zichukuliwe haraka sana ili kuiokoa nchi yetu katika madhara ya mifuko hiyo, hasa ukizingatia baadhi ya Wananchi wetu huitumia mifuko hiyo kwa kuwashia moto bila ya kuelewa madhara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie masuala ya Muungano, pamoja na kwamba, Wizara inajitahidi kuondoa kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika Muungano. Naomba kueleza yafuatayo:-

Kwanza, ingawa Ofisi ya Makamu wa Rais ina nia ya kujengwa Zanzibar, hata hivyo, jengo hilo linaelekea kuchelewa kujengwa kutokana na ufanisi wake kuwa wa pole pole mno. Aidha, sehemu iliyotarajiwa kujengwa inaonekana kutokubalika kuanza ujenzi na kushauriwa kutafutwa eneo lingine. Je, uamuzi huu umetekelezwa na lini ujenzi utaanza?

Pili, Wizara zote za Muungano zianzishwe Ofisi zake Zanzibar ili kuondoa usumbufu.

Tatu, kwa zile kero ambazo zimeorodheshwa na Ofisi ya Waziri Kiongozi na kuwasilishwa katika Ofisi yako, hatua ya kutekeleza kero hizo zimefikia wapi, naomba maelezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nichangie suala la Ukimwi kama ifuatavyo:

Kwanza, Semina na makongamano yapunguzwe na badala yake wasaidiwe kupatiwa dawa waathirika. Pili, ndoa zisiruhusiwe hadi pale watakapoonyesha vyeti vya kupima Ukimwi. Tatu mila na desturi zifuatwe zenye kuelekeza malezi bora.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kutoa rambi rambi zangu kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa kifo chake cha ghafla na pia kwa Wananchi wa Ulanga Mashariki, bila kusahau, chama chake cha CCM. Poleni sana kwa ujumla wenu. Naomba Mwenyezi Mungu, mwenye huruma, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kujikita kwenye suala zima la umaskini. Umaskini ulio kithiri wa Watanzania wote hasa wale walala hoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mipango ya muda mrefu ya kuondokana na umaskini kama vile *TASAF* kujenga mashule, ili watu waondokane na umaskini kupitia elimu. Kwa misingi hiyo naomba Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAF* ifike nchi nzima, siyo wengine tuwaache wakiwa watazamaji. Wote tushiriki na tuondokane na umaskini, kwani maskini aliyeelimika siyo sawa na ambaye hajaelimika. Suala hili nililipigia debe sana katika hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuhakikisha jamii yote ya Tanzania inapata maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini, mimi nashangaa sana, tunasema tunapiga vita umaskini, ila ni jambo la kushangaza mno, ikitokea dalili ya kuukwepa/kuondokana na umaskini, Serikali inapiga chenga. Nasema hivyo kwa sababu, ardhi ni mali na ni mtaji namba moja wa kutokomeza umaskini. Mfano, madini, ardhi hii ambayo ina madini ni matongo ya babu zetu tangu enzi zao, wakati watu wala hawajui kama kuna madini, sasa la kushangaza ni kwamba, ardhi hii ikionekana ina mali, yaani ina madini mfano, dhahabu, almasi na kadhalika, pale pale mwenye ardhi hiyo toka kwa wazazi wake anaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli tunataka kweli watu wetu waondokane na umaskini kidhati kweli? Kwa nini tusiwaelimishe wafanye *Joint Venture* na wawekezaji, ili nao wawe matajiri na kuondokana na umaskini kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawatakia mema hawa! Kila mtu hula *Altareni* kwake. Hawa wamejaliwa ardhi yenye madini, Serikali nayo itapata toka kwenye kodi. Mimi naamini wakiachiwa, umaskini sehemu hiyo ya madini umekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko pale pale kwenye ardhi. Iwapo mkulima atapewa ardhi ya mababu zake, amiliki ardhi hiyo pasipo kugharamia fedha nyingi kama ilivyo sasa kuzidi uwezo wake, alime, apange bei ya mazao yake kama pamba, tumbaku, chai, kahawa, korosho na kadhalika. Kufuatana na gharama alizotumia, mfano, madawa, *fertilizers* na kadhalika na hata kuweka *labour charges* pamoja na faida yake. Naamini kabisa naye atajikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa naye atajikwamua. Kamwe hatakuwa maskini, ili mradi apate elimu hii na pia awe na hatimiliki, aweze kupata mikopo mikubwa na midogo kwa biashara zake. Mkulima huyu atajikwamua. Pia ajue kuweka chakula cha familia yake. Mimi naamini atakuwa amejikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondokana na umaskini huku ndiyo kunakotakiwa kwa haraka na hivyo kubaki na mapesa mfukoni kwake. Hii ndiyo mipango ya muda mfupi ya kuondokana na umaskini. Lakini vinginevyo, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuwape wakulima wajipangie bei za mazao yao. Wanaweza sana hata kujiwekea akiba ya uzeeni, wakishauza mazao yao. Kwa misingi hiyo, hivi lini Mkulima wa Tanzania atapewa fursa hizo nilizozielezea? Nashauri wapewe ili waondokane na umaskini uliokithiri mmoja mmoja awe na mapesa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la mazingira, katika *level* ya chini kabisa ya jamii vijijini *(grassroot).* Naomba ushirikishwaji wa wanawake katika suala zima la mazingira. Sababu wanawake ndiyo watumiaji wa kuni, mkaa, hivyo wanahitaji sana elimu ya mazingira huko huko wanakoishi. Wanatakiwa kuelezwa ukataji wa miti na uhusiano wake na mvua. Mvua na kilimo cha chakula na mazao ya biashara na suala zima la mazingira, wanawake wanatakiwa kupewa elimu ya majiko mbadala, majiko yanayotumia mkaa mchache, kuni chache kwa kupia na haswa kuelimishwa kupanda miti kandokando ya nyumba zao kwa ajili ya kuni na kadhalika. Wanawake wakipata elimu hii kwa ajili yao sasa na kwa ajili ya vizazi vijavyo, watafanya na watabadilika na hivyo jamii nzima itabadirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri elimu hii iwafikie wote pamoja na mapungufu yote ya sheria ya mazingira ili tusiendelee kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utumiaji wa *Biogas* toka kwenye samadi ya ng'ombe, mbuzi na kadhalika. Hata takataka za nyumbani za kila siku. Naomba elimu hii iwafikie akina mama hasa wanaotoka kwa wafugaji. Bila kusahau majiko yanayotumia pumba na mionzi ya jua. Hebu fanyeni hili ili kuzuia uharibifu wa mazingira

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia samadi ya wanyama kama ng'ombe/mbuzi na hata kuku ni mbolea safi sana, hata ya takataka za nyumbani. Kwa taarifa yenu, Ulaya sasa hivi wanahitaji vyakula vilivyolimwa bila kutumia mbolea za kemikali, hivyo mbolea ya samadi hizi zikiwekwa shambani, mazao bora yatapatikana na soko lipo nje na ndani ya nchi na hivyo watu watapata pesa bila tatizo yaani kwa ulaini hivyo kuondokana na umaskini. Kuptia kilimo, hebu toeni elimu hii kote nchini. Elimu hii ya majiko mbadala itatengeneza ajira kwa vijana hivyo pia kuondokana na vijana wasio na kazi nao pia watakuwa na mapesa. Tukipungumza kukata miti kwa ajili ya kuni, mkaa na kadhalika, tutakuwa na mazingira mazuri yanayovuta mvua kwa ajili ya kilimo, hivyo, nchi itakuwa na neema, ina chakula na mazao ya biashara, wote shibe na mapesa umaskini utakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la Muungano. Katika suala la Muungano kuna Wizara zisizo za Muungano, sasa kulikoni zinaingizwa kinyemela? Mwenyekiti, lazima tusifumbie macho suala hili. Si sahihi na wala sio haki kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vitu/mali/haki yao na kuna pia vitu/mali/haki zetu Tanganyika, mfano masuala au Wizara ambazo haziko kwenye Muungano ambazo ni Wizara za Tanganyika peke yake na kuna Wizara zilizo kwenye Muungano ambazo ndiyo zetu, hivyo kuna chao, chetu na vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane, wanayoona wanaonewa nasi tunayaona si sahihi, tungumze ili yaishe, kwani watu wakikaa pamoja lazima watagongana. Ni sahihi kutumia hekima na busara zetu kuzungumza na kufikia muafa. Zamani sisi wanawake tulikuwa hatuna haki ya kumiliki mali, sasa hivi tunamiliki mali, ardhi na kuwa na chetu sababu ya kupigia kelele na kwa kuwa ni haki tumepata. Ni vizuri basi suala la Muungano lizungumzwe ili kila mtu aridhike au tukubaliane siyo vitu vinakwenda kinyemela tu kwa kuzimwa zimwa. Zamani tulikuwa tunachaguliwa mume/mke, siku hizi haiwezekani nani umchagulie mume/mke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la muafaka lisiwe tu wa *CUF* na CCM, liwe kwa vyama vyote kwani vyote ni vya Kitaifa na pia uchaguzi wa Wawakilishi tu ndiyo wa Zanzibar peke yao, lakini Wabunge ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kulikoni, hebu tukubaliane kwa nguvu ya hoja siyo hoja ya nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muafaka huo huo vipi Wabunge watano toka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wote ni kutoka CCM kwa nini? *CUF* haina Wawakilishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hawa Wabunge watano ni wa nini hawa baada ya kuingia mfumo wa vyama vingi, kwani tuna Wabunge katika kila Majimbo ya Uchaguzi Tanzania nzima, ambao wanawakilisha kwenye Bunge la Tanzania na Tanzania ni Tanganyika na Zanzibar, hivyo, uwakilishi upo, sasa nini tena? Tunagharamia bure tu. Kwa kuwa bajeti kila mara ni finyu, mnaonaje hawa wakaondolewa ili tu-*save* pesa kwa ajili ya shughuli nyingine za Kitaifa?

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuitumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo, kwa hotuba yao nzuri juu ya Mazingira na Muungano, kuondoa umaskini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Vivyo hivyo, nawapongeza Viongozi na Watumishi wote waliomo katika Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu wao, Ndugu O. S. Mollel, kwa kazi nzuri wanazozifanya ambazo matokeo yake ndiyo hotuba hii nzuri. Nawapongeza.

Napenda pia nitumie fursa hii kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya Wananchi na Wapiga Kura wa Jimbo la Kwimba, niishukuru sana Serikali ambayo kupitia Wizara hii tumeshirikishwa katika mpango wa *TASAF.* Mfuko huu umesaidia sana katika kuleta maendeleo na katika juhudi ya kuondoa umaskini katika Wilaya na Jimbo la Kwimba. Majengo ya Shule na Zahanati yaliyojengwa na Wananchi kupitia Mfuko huu yamekuwa ni chanzo na ya kuigwa hata katika kufanikisha mpango wa MMEM Wilayani humo. Utaratibu uliotumika katika uibuaji wa miradi ulikuwa mzuri na muafaka kwa Wananchi wetu. Ni kupitia Mfuko huo, watu wamehamasika hata katika ujenzi wa shule za sekondari za Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mnapowasikia Waheshimiwa Wabunge wengi wanapiga kelele na kulalamikia sana ni kwa nini Mfuko huo haujapelekwa kwenye maeneo yao, ni kwa kuwa wamesikia kule Mfuko ulikofikishwa Wananchi wameupokea vizuri na kufanikisha. Hivyo, kelele na lawama hizo zisiwakatishe tamaa. Vyote hivyo ni ushahidi kuwa mfuko huo kama ukipokewa vizuri ni mfuko mzuri sana, hivyo mjione kuwa mnapongezwa. Ni vizuri kwa hivyo nikatumia fursa hii kuzipongeza Wilaya chache zilizoupokea vyema mpango huu wa *TASAF,* kwani kama zimefanya vyema Wilaya zingine sasa zaweza kwenda kujifunzia huko zikiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo ombi moja tu katika Wilaya yangu kuna shule za Sekondari zinazojengwa kwa msaada wa *TASAF.* Wananchi wamejenga hadi kufikia hatua nzuri, kinachowashangaza Wananchi ni kuona kuwa mchango wa *TASAF* bado haujafika. Wananchi wangelipenda shule zao zifunguliwe mwanzoni mwa mwaka kesho lakini bila msaada wa *TASAF* kufika mapema huenda ikashindikana, hivyo, ninachokiomba ni mchango wa *TASAF* kupelekwa mapema ili kufikia azma ya Wananchi hawa wenye uchu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba ndiyo yenye Mashirika yasiyo ya Kiserikali machache sana yanayoshughulikia mazingira na Ukimwi. Kupitia kwako Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, anayeshughulikia eneo hili

aiangalie Wilaya hii pia ili kwa ushauri wake nasi tunufaike na michango ya Mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwimba, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipeleka maombi yangu ya kujengewa daraja lililovunjika kwa Mradi wa *TASAF*, nimeahidiwa na Mkoa wangu na hakuna kilichofanyika. Ahadi hiyo, *TASAF* ina watu wake labda. Daraja liko Mpona (Kwale).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifikiriwe, daraja hilo ni *shortcut* ya kwenda Kaskazini. Wananchi wanapata tabu na watoto ni hatari kwao. *Please help.*

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa utendaji kazi wake mzuri pamoja na watendaji kazi wake wote wa Wizara yake. Pia ninaipongeza hotuba yake jinsi ilivyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nianze na uchafu uliotuzunguka wa mifuko ya plastiki nchi nzima, kwa kweli hili ni tatizo la muda mrefu sasa tunalipigia kelele, hivi Serikali hailioni au kele zetu hamzisikii kwani huu ni uchafu usiooza na mifuko hii kila mmoja na anavyoitumia wengine wanafanya ndiyo vyoo kuweka kinyesi na kutupa mahali popote pale, wengine huwashia moto na kuathiri afya zao na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifuko ya plastiki ipigwe marufuku kuingizwa nchini na hata kama kuna kiwanda kinachotengeneza mifuko hii hasa ile midogo midogo myepesi ambayo ukienda dukani hununua kitu unapewa bure, viwanda hivyo visimamishwe kwani katika nchi yetu imekuwa kero sana, huu uchafu wa mifuko au kama kuna uwezekano wa kukusanya mifuko hii nchi nzima na kuirejesha tena kiwandani basi ninaiomba Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Wizara ya Fedha, basi ifanywe hivyo, kukusanya mifuko yote ambayo inatupwa ovyo na kurejeshwa tena kiwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiwanja ambacho kilitegemewa kiendelezwe kujengwa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais kimefelishwa na kwa kuwa kwenye bajeti hii limetengwa fungu la fedha kwa ajili ya ujenzi huo, je, kiwanja kimeshapatikana kingine na kama kimepatikana ni wapi? Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho anijibu na kama kimeshapatikana ninamwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya bajeti kupita asicheleweshe ujenzi kwani jengo hilo na nyumba ya makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ni muhimu kuwepo Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango wangu huo, ninaunga mkono hoja hii kwa dhati kabisa kwa asilimia kwa mia.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa Muungano wa Tanzania unaendelea kukua kila kuchapo, hata hivyo, kukua huko pia matatizo lazima nayo yataendelea kujitokeza. Naamini kwamba, msingi mkuu wa matatizo ya Tanzania ya leo ni uchumi duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Fedha ya pamoja ni kiungo muhimu sana katika kupunguza matatizo yetu ya Muungano, cha kusikitisha ni kwamba, mpaka hii leo, Tume hii Ofisi zake bado hazijakamilika, hazina wafanyakazi hata *office structure* haipo, kwa hiyo, ofisi hii bado inayumba na haijaanza kazi na kikwazo zaidi ni Wizara ya Fedha ambayo inaiona Tume kama itamega kazi zake, hivyo, tatizo hili ni vyema lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *international relation* ni suala la Muungano lakini bado Tanzania haijawa na mtazamo wa pamoja katika kutafuta misaada hasa ile misaada ya msingi mfano elimu, umaskini, lakini miradi hiyo Tanzania imefanyika bila ya ushirikiano, hali kama hiyo pia ipo katika *EAC, SADAC* au *AGOA NEPAD* na kadhalika. Ofisi hii mwaka 2003 ilituambia kuwa inaimarisha vikao vya ushirikiano kati ya Wizara zisizo za Muungano na Wizara za SMZ, hata hivyo, bado hatuna ufafanuzi ni Wizara zipi zilizokutana na mafanikio ni yepi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, atupatie ufafanuzi wa ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 ujenzi huu ulitengewa Sh.454,699,700/= lakini kazi iliyofanyika ni ujenzi wa ukuta wa uzio wa ofisi hiyo, je, ni shilingi ngapi zimetumika kwa kazi hiyo na kama zimebaki zimefanyiwa kazi gani, hata hivyo, zipo tetesi kuwa eneo hilo halifai kwa ujenzi huo, hivyo, naomba tueleweshwe hatua au maendeleo ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa hongera Mawaziri na Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Wakuu wa Idara za Umaskini na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *NGO* moja ya kuhifadhi mazingira Kata za Kiroka, Kinole, yaani Milima ya Urugulu lakini inawekewa vikwazo kuandikishwa na viongozi fulani fulani Wilayani hawatoki kwa sababu baadhi ya Viongozi wana *NGO* yao iko mjini bila ya kushirikisha wanavijiji wa Kata hizo. Badala yake *NGO* hiyo inafyeka mazao ya Wananchi maeneo ya Bamba, Kinole na Kiroka. Naomba msaada wa ushauri ili niwaambie Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini maeneo ya Muungano yasiongezwe ili kuimarisha badala ya kubakia na hayo hayo tu tangu 1964? Tuimarishe?

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Ofisi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba *TASAF* ikamilishe miradi viporo au ile ambayo imekamilika nusu kabla ya kuanza mipya katika awamu ijayo. Miradi hiyo ni kama Mradi wa Maji Nyabibuye, Mradi wa Barabara ya Rumashi - Kabare na Zahanati ya Kazilamihunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hasa msimamo wa Serikali ya Muungano kuhusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa na bendera yake? Nini hatima ya mtazamo wa jumla wa Muungano huu?

Kuna tatizo la Muafaka wa Vyama vya CCM na *CUF* kuonekana kuwa ni *binding* kwa Serikali zote mbili. Ni vyema vyama hivi na Wananchi kwa ujumla, wakaelimishwa kuwa Muafaka wa vyama si kwamba ni Muafaka wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *SELF*, kwa kuwa mtaji ndio mpango muafaka wa uwekezaji rasilimali watu katika kuondoa umaskini na kwa kuwa tayari wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wameunda *SACCOS* zao katika kila Wilaya, ni kwa nini Mfuko wa *SELF* haujaona umuhimu huu wa kuwakopesha wanawake hao mtaji wa kuinua *SACCOS* zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni namna gani Idara ya Kuondoa Umaskini inaunganisha juhudi za Kitaifa za kuondoa umaskini mfano, jitihada za Kisekta, jitihada za Kiwizara na jitihada za Kijamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, isingekuwa busara kuwa na Madawati Maalum ya Kikata/Kiwilaya na Kimkoa yatakayokuwa yana-*co-ordinate* juhudi hizi za kupambana na umaskini chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nguvu gani ya hoja kwa hoja inayotoka Idara ya Kuondoa Umaskini inayowafikia maskini moja kwa moja? Ukiachia mbali miradi ya Kitaifa ya *SELF* na ya mazingira ambayo inashuka kijumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo ya zana bora za kilimo na ushirikishaji kaya katika kuelewa tatizo la umaskini na kujua mbinu za kuondokana nazo. Tunao watafiti wengi katika Wizara na idara mbalimbali katika kuona namna ya kuboresha mfano zana za kilimo kwani zana hizo bado haziwafikii walengwa maskini kuboresha uzalishaji wenye tija. Nini kazi ya Idara ya Kuondoa Umasikini katika kufuta *gape* toka kwa watafiti mbalimbali na wazalishaji na watumiaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani mwenye wajibu wa kuzisaidia familia kujielewa na kujianzishia mawazo yakinifu ya kutambua tatizo la umaskini hasa wa hali na kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yepi ni majukumu ya kimahusiano ya kiutendaji katika hilo, mfano, tuna siku ya familia ni namna gani unawekwa utaratibu wa kimahusiano ya

kiutendaji kutumia mianya hiyo kukuza mahusiano ya kifamilia katika kutambua tatizo la umaskini na kulichukulia hatua toka kaya mpaka Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri utaratibu wa kuzielimisha familia ni wa msingi.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo inatoa matumaini makubwa. Ninawapongeza Mawaziri wote wawili, pamoja na Makatibu Wakuu wao na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kwa ushauri mzuri sana iliyoutoa kwa Serikali juu ya uharibifu wa mazingira unaofanywa na makaratasi na mifuko ya plastiki nchini kote. Mifuko hii ya plastiki imezagaa kote nchini na inaleta maafa makubwa kwa wanyama na kuharibu ubora wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haionyeshi dalili yoyote ya kukerwa na kero hii kubwa na kusubiri Wazungu waje kutoka Ulaya au Amerika kutoa Semina juu ya athari ya uchafu huu wa plastiki. Hivi Serikali haitambui kwamba, uharibifu wa mazingira unaosababishwa na plastiki unaongeza umaskini na magonjwa mbalimbali kwa Wananchi. Hivi Serikali inahitaji *World Bank* itoe mikakati ya kuondoa uchafu wa mifuko hii ya plastiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Serikali kwa mafanikio makubwa ya Mradi wa *TASAF.* Mradi huu ni ukombozi mkubwa kwa Wananchi kwani umesaidia sana kupunguza umaskini usio wa kipato. Barabara zimelimwa, visima vya maji vimechimbwa, madaraja yamejengwa, zahanati zimejengwa, pamoja na kukarabatiwa. Vilevile mashule yamejengwa kutokana na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Wilaya yangu ya Kyela, miradi ya jamii 29 na miradi ya ujenzi saba, yote yenye thamani ya zaidi ya Sh.630,780,000.00/= imejengwa. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kubuni Mradi huu wa *TASAF* na atakumbukwa na Watanzania wote milele na milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kupunguza umaskini ni pamoja na kazi zote za maendeleo zinazofanywa na Serikali. Uboreshaji wa huduma za jamii tunaoushuhudia hivi leo nchini Tanzania, ndiyo njia kuu ya kupunguza umaskini. Ukitaka kumsaidia maskini kupunguza umaskini wake ni kumsomeshea mtoto wake, kumjengea barabara, kumpa maji safi na tiba nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kazi kubwa iliyoko mbele ya Serikali katika vita dhidi ya umaskini ni kuleta mikakati ya kumfanya kila Mtanzania afanye kazi. Uvivu ni ugonjwa mbaya kuliko Ukimwi. Uvivu ndiyo chimbuko la umaskini, ujinga na maafa mbalimbali.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wa Mifuko iliyo chini ya Wizara na Watendaji, kwa kuandaa hotuba nzuri, inayoeleweka na kutia matumaini ya utekelezaji wa malengo ya Wizara iliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nichangie machache tu kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu Idara ya Kuondoa Umaskini, niseme tu inajitahidi kufanya kazi vizuri kwa kutumia Mfuko wa *TASAF* na *SELF,* ambayo husaidia kuendeleza miradi mingi inayolenga kuwakomboa Wananchi. Hata hivyo, naomba ufafanuzi ni kwa kiasi gani huduma za mifuko hii imewashirikisha jamii ya watu wenye ulemavu katika kufaidika na miradi hiyo. Nimeomba ufafanuzi huu kwa sababu katika taarifa za *TASAF* ilisemekana kuwa *TASAF* ina majukumu ya kushughulikia miradi ya jamii ya watu wenye ulemavu, wazee na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kuhusu suala la vifaa (mifuko) ya *plastics,* ambayo inaharibu mazingira na ardhi ambayo inachakaa na kwamba, haitaweza kustawisha mazao. Hii ni hatari sana kwa Wananchi na ustawi wa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Serikali kwa kuhakikisha kuwa, kituo cha utafiti wa viumbe wa bahari cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa miongoni mwa vituo vinne duniani vilivyoteuliwa kuwa *Centre of Excellence.* La msingi ni kwa Tanzania kuendelea kuhakikisha kuwa inatimiza vigezo vyote vinavyohitajika ili kituo kidumu katika uteule wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja na kuwatakia kila la kheri Wizara katika utekelezaji wa majukumu waliyojiwekea.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kutoa pongezi kwa hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na Wataalam wote walioandaa hotuba hii safi na yenye kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia hotuba kwa kuanza kwenye Mfuko wa Jamii wa *TASAF.* Mimi na Wananchi wangu wa Jimbo la Mwera, tunashukuru sana Mfuko wa *TASAF* kwa kuweza kutujengea shule mbili za Kibondeni na Maungani. Kwa niaba ya Wananchi wangu, nizidi kutoa shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naendelea kuchangia kuhusu ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais huko Magogoni ndani ya Jimbo langu la Mwera Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa jengo hilo haliendelei kujengwa kwa sababu haieleweki kabisa na kwa mimi naomba maelezo kwa nini jengo hili ambalo ni muhimu kwa kule Zanzibar haliendelei kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia juu juu kuwa eti sehemu hiyo imefeli kuwepo ofisi hiyo kwa sababu za kiusalama, je, hili ni kweli au la?

Cha kusikitisha kwa eneo hilo la ujenzi, palikuwa na makonde ya Wananchi ambayo walipanda mihogo, migomba, viazi vitamu na kadhalika, pia palikuwa na sehemu ya kiwanja cha maskani ya CCM, ambayo ilikuwa imeshajengwa hadi kozi nne, lakini vipando hivyo vimeng'olewa, jengo la Ofisi ya maskani ya CCM limebomolewa, hadi leo Wananchi hao wakiwa Wapiga Kura wangu wanahangaika hawakupata malipo yoyote yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kuwa, sehemu hiyo inayojengwa ofisi hiyo pamepita bomba la maji. Bomba ambalo linapeleka maji masafa marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hayo yote nataka maelezo. Je, wenye makonde yao watalipwa lini pamoja na maskani iliyobomolewa?

Je, Ofisi ya Makamu wa Rais iko tayari kusimamia bomba ambalo linapeleka maji kwa Wananchi ili lifanye kazi kikamilifu kupeleka maji kwa Wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais ni chombo kikubwa sana, kwa hiyo, ikiwa kinafanya mambo kama haya si vizuri kwa Wananchi. Kwa hiyo, nataka maelezo kamili kwa yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi napenda kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kuhusu bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile natoa mkono wa rambirambi kwa jamaa wa Marehemu, Wabunge wenzetu wawili waliofariki hivi karibuni wakati tukiwa hapa hapa kikaoni Dodoma. Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Mawaziri wa Nchi wote wawili wanaoshughulikia masuala ya Muungano, mazingira na kuondoa umaskini, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, kwa juhudi zao za kuiongoza kwa umakini Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 26 Aprili, 2004, Jamhuri yetu ya Muungano ilitimia miaka 40 ya Muungano. Kwa bahati nzuri kilele cha Sherehe ya Muungano kilifanyika *Amani Stadium* Mjini Unguja. Kwanza, nachukua nafasi hii kuisifu Kamati ya Itifaki kwa shughuli za kupokea wageni uwanjani pale. Kamati ya Itifaki hii naisifu kwa kupanga utaratibu mzuri wa kuwapokea viongozi wetu jinsi walivyopangiwa kuingia

na kuondoka. Watu wengi walikuwa wakiangalia Rais Amani Abeid Karume ataingia baada ya Kiongozi gani Kimuungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kumpangia Rais Amani Abeid Karume, kuingia pale uwanjani kama Rais kimekata kidomodomo cha wachochezi wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa ni Mjumbe wa Kamati hii ya Maliasili na Mazingira, Kamati hii imepata nafasi ya kutembelea Mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara, Wilaya ya Bagamoyo, Kisarawe, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara zetu kote huko tumepata fursa ya kuangalia mambo yanayohusu mazingira na kuangalia mikakati ya kuondoa umaskini. Vilevile naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kushughulikia na kutatua baadhi ya kero za Muungano kwa kuanza kujenga jengo la *Bank of Tanzania* kule Gulioni Zanzibar. Pia kuweka jiwe la msingi la Ujenzi wa Ofisi Ndogo ya Bunge kule Tunguu Zanzibar, pamoja na kuanza kujenga Kituo cha Uchunguzi wa Viumbe wa Baharini kule Buyu Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yote yalikuwa ni baadhi ya kero za Muungano na hivi sasa yanatekelezwa. Jambo hili linatia moyo sana, lakini ujenzi wa nyumba ya Makamu wa Rais na Ofisi yake bado ni kitendawili. Tunaomba Serikali ifanye juhudi za kutafuta eneo na kuanza kujenga Ofisi ya Makamu kabla ya kufika mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza hotuba hii na naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wao wote, waliotayarisha hotuba hii kwa umahiri mkubwa. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapa pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kuchangia hoja iliyo mbele yetu kama ifuatavyo:-

Kwanza, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi hiyo kwa upande wa Zanzibar haipo kabisa, iliyopo ni Idara ya Huduma za Makamu wa Rais *(Private Office)* inayoongozwa na Naibu Katibu. Inasikitisha kuwa na hali kama hiyo ambayo inasababisha baadhi ya kazi za utekelezaji wa mambo ya Muungano yasifanyike kutokana na ukosefu wa kutokuwa na Idara na Wakuu wa Idara kiutendaji. Ujenzi wa Ofisi ya Makamu, hilo ni

wazo zuri lakini utendaji wake unasuasua, kilichofanyika ni kujenga uzio tu hatujui lini ujenzi wa Ofisi utaanza na kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua za ujenzi ambao umeshaanza wa Ofisi ya Benki Kuu, Ofisi ya Bunge na *Marine Science,* baada ya miaka 40 hayo ndiyo yameanza, hata hivyo, nashauri na Ofisi nyingine ziige mfano huo kwani huduma zao pia zinahitajika Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bima ya Afya, kwa upande wa Unguja wanapata tiba Taasisi za Muungano lakini kipande anapewa mtu mmoja wakati sheria ni vipande sita, yaani baba, mama na watoto wanne. Kwa upande wa Pemba bado hawajaanza kupata huduma hizo wakati fedha wanakatwa kwenye mishahara. Je, ni lini wataanza kupata huduma hizo za tiba? Naomba lishughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, mimi binafsi naipongeza Hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kuiunga mkono mia kwa mia. Ila naomba nichangie yafuatayo: Kwanza, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Itakumbukwa kwamba, kwa kipindi cha miaka 40 sasa ya Muungano wetu hakuna Ofisi mahsusi kwa ajili ya Makamu wa Rais huko Zanzibar, jambo ambalo limepigiwa kelele sana na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele za Wabunge zilisaidia kwa kupatikana kiwanja kwa ujenzi wa Ofisi hizo. Wahusika wote walikitembelea kiwanja hicho na kuridhika nacho. Ilifurahisha kuona fedha kiasi cha Sh.454,699,700/= zikitengwa na kiwanja husika kilizungushiwa ukuta. Sasa je, fedha hizo zote zilitumika kwa kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sasa ilikuwaje kiwanja hicho kutamkwa kuwa hakifai? Je, hizo fedha Sh.421,699,700/= zilizopangwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 zitafanya nini? Naomba nipate maelezo ya kina.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo, kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaongeza vilevile wataalamu wote wanaosaidia Mawaziri kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu za dhati kwa Serikali kwa kubuni na kutekeleza Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF).* Mradi wa *TASAF* umeonyesha mafanikio makubwa na kusaidia kwa vitendo kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mradi wa *TASAF* uendelezwe na kuimaishwa zaidi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mkenge. Naomba Serikali ipokee shukrani za dhati kwa kuwapelekea Mradi wa *TASAF*. Wananchi walipokea vizuri mradi huo na wameshiriki kwa nguvu zote na kufanikisha miradi walioibua kulingana na taratibu za utekelezaji wa miradi ya *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa changamoto kwa Serikali kuendelea kubuni miradi mingi zaidi inayofanana na Mradi wa *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, mia kwa mia.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Mafia, kwa Mawaziri walio chini ya Ofisi hii ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo na kuwapongeza pia Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais na Makatibu Wakuu, upande wa Mazingira na Kuondoa Umaskini na Wakurugenzi wote wa Idara zilizo chini ya Ofisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu *TASAF,* sisi watu wa Wilaya ya Mafia, *TASAF* tunaisikia tu, hivi kweli huo mgawanyo wa kila Mkoa hivi hawakuiona Wilaya ya Mafia kuwa ni Kisiwa hatuna Miradi yoyote ile ya kimaendeleo? Naomba sana hivi sasa kabla ya huo mwaka 2005 kule Mafia tuna miradi miwili ya kimaendeleo mmoja ni Ujenzi wa Shule ya Sekondari Kirongwe na Mradi wa Maji wa Kijiji cha Jibondo. Tunaomba Miradi hiyo *TASAF* iione na kuipa msaada maana hiyo shule nia yetu ifunguliwe Januar, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuoneeni huruma tuko kisiwani tumetengeka kijiografia tu siyo kwa makusudi, ni hali aliyoiweka Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba tu ombi langu hilo lifikiriwe, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi kadhaa katika Jimbo la Nanyumbu ambayo inafadhiliwa na *TASAF* haijakamilika hadi sasa. Mradi wa kwanza ni wa Maji wa Ndwika - Mangaka, ambao umekwama baada ya kuishiwa mabomba kilometa chache kabla ya kufika Mangaka Mjini. Hali hiyo ilisababishwa na ukadiriaji mbaya wa mabomba uliofanywa na wataalamu ngazi ya Wilaya. Tayari maombi yameshatumwa *TASAF* Taifa, lakini majibu bado kutolewa, hivyo, mradi huo umekwama hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ihakikishe mradi huo unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi mingine iliyokwama ni ya uchimbaji wa mabwawa saba katika maeneo mbalimbali. Sehemu ya kwanza ni katika Kijiji cha

Maratani. Bwawa hilo limeshafanyiwa *survey* lakini tangu wataalamu waondoke, hakuna hatua yoyote inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ni katika Kijiji cha Namasogo ambapo *survey* imefanywa na hakuna shughuli inayoendelea hadi sasa. Sehemu ya tatu ni katika Kijiji cha Mpwahia ambapo survery imefanywa lakini tangu wataalamu waondoke hakuna kitu Kinachoendelea hadi sasa. Sehemu ya nne ni katika Kijiji cha Maneme ambapo *survey* imefanywa na hakuna maendeleo zaidi hadi sasa. Sehemu ya mwisho ipo katika Kijiji cha Mpombe ambapo *survey* imefanywa lakini hapo hakuna kingine kinachoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hiyo ni muhimu sana katika kuondoa au kupunguza matatizo katika upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo katika maeneo husika. Wananchi walihamasika vya kutosha na walishiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za miradi hiyo. Hivyo, kuendelea kukwama kwa miradi hiyo kunawakera sana Wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ihakikishe kuwa miradi hiyo inamalizika kujengwa..

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuondoa umaskini katika Jimbo la Nanyumbu, ningeomba Serikali ianzie kwenye uimarishaji wa kilimo cha korosho. Karibu kila mwananchi katika Jimbo la Nanyumbu anategemea zao la korosho kwa kujipatia fedha hivyo kuondokana na umaskini. Mwaka ambao korosho zinazaa sana, hali za watu huboreka kuanzia kujijengea nyumba bora hadi mavazi na chakula. Hivyo, kuboresha zao la korosho ndiyo njia kuu ya kuondoa umaskini Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kutambua umuhimu wa zao la korosho, bado Serikali haijachukua hatua thabiti ya kulikuza zao hilo. Bado suala la pembejeo kwa zao la korosho ni kitendawili kwani hazipatikani kwa wakati, wingi na ubora, wakulima wengi hawazipati kwa kukosa uwezo kifedha na Viongozi wa Serikali hungojea tu kukata fedha za ushuru wakati wa mauzo lakini kusaidia kwenye maandalizi ya zao la korosho hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ihakikishe kuwa, mkulima wa korosho anawezeshwa katika kupata pembejeo mapema na kwa wingi na ubora unaotakiwa. Hivyo, Wananchi wakopeshwe pembejeo mapema ili zitumike vizuri kama inavyotakiwa. Kwa njia hii, nina hakika umaskini ndani ya Jimbo la Nanyumbu utaondolewa baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu huu, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, iliyochambua Bajeti ya Makamu wa Rais, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, kwa hotuba yao lakini pia kwa

ushirikiano wao na Kamati na kwa ujumla kwa utendaji wao. Hapa sijasahau kazi nzuri ya Makatibu Wakuu, Ndugu R.l Mollel na Ndugu Mary Mushi na Watendaji wote walio chini yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya Muungano, kero za Muungano, mimi huwa sielewi. Tunaposema mgao wa asilimia 4.5 ni kutokana na nini? Kunapokuwa na madai mbalimbali, je, tunajua mchango wa kila upande wa Muungano katika shughuli mbalimbali kwa mfano ni kiasi gani kinachangiwa na Zanzibar kuwahudumia Wabunge toka huko? Je, idadi ya Wabunge (Majimbo) ni asilimia ngapi ukilinganisha na Majimbo ya Bara na ukubwa wa nchi (Tanganyika)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kero ziko upande wa Zanzibar tu? Je, iwapo upande wa bara nao wakiamua kueleza kero, Muungano utakuwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba majibu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa hotuba zao nzuri na kazi zao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utunzaji wa mazingira ni muhimu sana kwa maisha ya siku hadi siku pamoja na jitihada za kupambana na umaskini. Sote tumeshuhudia athari mbaya za uharibifu wa mazingira, hasa ukame na kukauka kwa mito na vianzio vingine vya maji. Ukame na njaa ni miongoni mwa athari, hivyo pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa kulinda mazingira, bado jitihada kubwa zaidi kielimu na kiudhibiti zifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya sheria ndogo na Kanuni mbalimbali zilizopo, hapana budi Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji kuwa wakali zaidi dhidi ya wachafuzi wa mazingira hasa misitu na hifadhi za bahari. Hatua kali zaidi zinahitajika dhidi ya uchomaji mkaa na uvuvi haramu. Aidha, udhibiti mkali unahitajika dhidi ya uchomaji ovyo wa misitu na matumizi mengine mabaya ya maliasili na rasilimali zetu mbalimbali hasa kuambatana na shughuli za migodi. Katika jitihada hizi, hatuna budi kuongeza ushirikishwaji wa Wananchi wenyewe kama walinzi wa mazingira na rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi maalumu kwa Serikali, Wahisani na Wananchi, kwa jitihada zao kubwa katika kupambana na umaskini chini ya mipango mbalimbali shirikishi, hasa *TASAF*. Kupambana na umaskini ni shughuli muhimu na ya kudumu. Hapana budi kuwahamasisha zaidi Wananchi kushiriki katika mipango shirikishi kwa bidii zaidi ili kupata mafanikio ya baraka zaidi na endelevu katika vita hii kubwa ya kupambana na umaskini

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mkinga, natoa shukrani kwa misaada mingi iliyotolewa na Serikali na wahisani katika kupambana na

umaskini Jimboni Mkinga. Hata hivyo, kutokana na hali duni ya uchumi na ustawi Jimboni Mkinga, ninaomba kurudia kusisitiza tena na tena kuhusu umuhimu wa kuongeza kiwango cha misaada kwa Jimbo la Mkinga ili lisiendelee kuwemo katika hali duni kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maombi mengine zaidi ya kuongeza kiwango cha misaada ni kutazama uwezekano wa kupunguza viwango vya michango ya wanavijiji, ambao mara nyingi wanashindwa kuchangia kiwango wanachotakiwa kutokana na umaskini wao. Fedha za misaada kwa ajili ya miradi zifikishwe kwa wakati muafaka ili miradi hiyo isichelewe na kukatisha tamaa Wananchi. Pia *DCs* wasijichukulie maamuzi ya kubadili miradi/mipango bila kuhusisha wadau wengine, hasa wadau. Vilevile jitihada za makusudi zifanyike kuepusha urasimu mwingi na ucheleweshaji katika ufunguzi wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa hotuba yake. Nawapongeza pia Mawaziri wote wawili, kwa maelezo yao yaliyomo katika kitabu cha hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya Ofisiya Makamu wa Rais kwa Mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na Wabunge wenzangu, kutoa mchango wangu kuhusu Ofisi hii ya Makamu wa Rais, juu ya mambo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muungano. Kulingana na maelezo yaliyomo katika kitabu na hotuba ya Waziri, mimi naona suala la Muungano na kero zake, bado halijapewa uzito unaostahili. Naona katika kitabu limegusiwa juu juu tu na sikuona suala lolote la Muungano lililozungumzwa kwa umaskini wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kero, Waziri hakuzungumza juu ya kero yoyote na ufumbuzi wake zaidi ya kukiri kwa kunukuu Hotuba ya Rais kuwa kero zipo. Kukubali kero zipo ni suala moja na kuzitafutia ufumbuzi wake ni suala lingine, jambo ambalo halionekani katika kitabu wala Hotuba ya Waziri. Tabia hii ya kuyaweka matatizo au kero za Muungano upande bila ya ufumbuzi, ni hatari sana kwa Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue suala la kuundwa Tume ya pamoja ya Fedha. Kitabu cha Waziri kinataja tu kuwa Wajumbe wa Tume waliteuliwa mwaka 2003, ingawa sheria ilipitishwa 1996. Lakini hatuelezwi kwamba, mpaka sasa Tume imefanya nini au inafanya nini. Maelezo ya Waziri hayatoshelezi. Naomba katika majumuisho, angalau Waziri alieleze Bunge kuwa, Tume hiyo kwa mwaka huu wa matumizi imepangiwa kiasi gani cha fedha ili kutimiza shughuli zake. Inaonekana Tume hii ipo kama geresha tu, lakini kwa udhati haina inalofanya kwa sababu haijawezeshwa kufanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano, lakini suala zima la namna masuala ya Muungano yanavyoshughulikiwa, ni la kuchekesha. Mtu akiuliza shughuli za Muungano zinazoshughulikiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kule Zanzibar ziko wapi, hakuna jibu. Hata hiyo Ofisi ya Waziri Kiongozi inayosemekana inaratibu shughuli hizi, haiwezi kujibu suala hili maana hazipo. Hivi kwa jambo kubwa kama la Muungano, kuna ugumu gani wa kuwepo Wizara kamili inayoratibu shughuli za Muungano badala ya utaratibu wa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kuwa, matumaini yangu ni kuwa utakapoletwa Muswada wa Marekebisho ya Katiba ya Muungano, ambayo yanatarajiwa kuwasilishwa Bungeni katika kikao kijacho, mzaha wa kupigana chenga kunakoonekana katika hotuba za bajeti za kila mwaka na katika majibu ya maswali yanayohusu Muugano, kutaachwa. Muswada huo tunategemea ujielekeze kwenye mambo ya msingi na kujibu hoja za kero za Muungano, ambazo tumedumu nazo kwa miaka 40 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo ninaunga mkono hoja hii kwa matumaini hayo.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuweka hapa mpaka leo hii. Nataka nimpongeze Makamu wa Rais, pamoja na Ofisi yake, kwa hotuba yao nzuri yenye matumaini makubwa kwetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu binafsi na Wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani kwa kutoa mkono wa rambirambi kwa Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niupongeze Mradi wa *TASAF* sana kwa juhudi yao kubwa ya kuweza kutuondolea baadhi ya kero kwenye majimbo yetu. Lakini ningeiomba *TASAF* ifanye juhudi zao kubwa sana ili ifikapo mwaka 2005, angalau iwe imekwisha maliza ile miradi ambayo hivi sasa tayari wameshahamasishwa Wananchi na tayari wameshaanza kutoa michango yao. Lakini mpaka muda huu tunapata maswali makubwa na hata tunashindwa kuyajibu au wanashindwa kutuelewa nini tunawaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza programu ya uvuvi endelevu na ufungaji wa samaki. Naipongeza programu hii kwa sababu kwanza inawasaidia sana akina mama kimapato na kiafya pia. Ninaiomba Ofisi hii ifanye *(coordination)* mpaka Zanzibar, ili Wananchi wa Zanzibar nao wafaidike na programu hii, ukizingatia kwamba, lengo kubwa la Serikali hii ni kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwapongeze Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, pamoja na Watendaji wa Ofisi hii, kwa kazi nzuri wanayofanya kusimamia shughuli za Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa juhudi zake za kuimarisha Muungano, kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na kusimamia vizuri shughuli za mazingira na kuondoa umaskini hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti kwa umahili mkubwa. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango mdogo tu katika hotuba hii kuhusu hali ya mazingira nchini Tanzania. Napenda niseme kwamba, tatizo letu kubwa la uharibifu wa mazingira, ni matumizi makubwa ya nishati ya kuni na mkaa, ukilinganisha na matumizi ya nishati ya umeme, makaa ya mawe, nguvu za upepo na jua. Takwimu zinaonyesha kuwa kuni na mkaa, vinachukua asilimia 90 ya matumizi ya nishati, mafuta yanachukua asilimia nane, umeme unachukua asilimia 1.2 na makaa ya mawe, jua na upepo vinachukua asilimia 0.8. Jumla yote ni asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza uharibifu wa mazingira utokanao na matumizi ya nishati, Serikali haina budi kuweka Mpango Maalum wa utekelezaji wa kuwapatia Wananchi vijijini (ambao hutumia asilimia 85 ya nishati hapa nchini), nishati ya umeme, nguvu za jua na upepo, matumizi ya majiko sanifu ya kuni, upandaji miti na uvunaji miti kwa njia endelevu na kuharakisha utungaji wa sheria mama ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni juu ya kuondoa umaskini. Hatima ya Mtanzania katika kuondoa umaskini, iko katika mkakati wa kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025. Mkakati wa kuondoa umaskini, unayo nadharia nzuri sana, lakini unahitaji tafsiri rahisi ya utekelezaji, inayoelewekwa kwa Wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni uwezeshaji Wananchi kwa vitendo kama ilivyoanza kufanywa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, kwa mpango wake wa kujenga na kukabidhi kwa wajasiliamali, machinjio ya kisasa na chuo cha kufundisha jinsi ya kuchinja na kukata nyama kisasa hapa Dodoma. Chuo hiki kitaendeshwa na *VETA.* Uwezeshaji wa namna hii ukifanywa kwa mpangilio sawia katika Wizara zote za uzalishaji wa biashara na kuenezwa kote nchini, ni dhahiri kuwa Watanzania wataondokana na umaskini ifikapo au kabla ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni juu ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvamizi wa wachimba madini wadogo wadogo katika vyanzo vya maji katika maeneo ya milima ya Wilaya za Muheza, Korogwe na Lushoto.

Tunaiomba Ofisi ya Makamu wa Rais, iingilie kati mpango wa Wizara ya Nishati na Madini wa kutoa hati za uchimbaji madini katika maeneo haya, ili usiathiri vyanzo vya maji na kuhatarisha maisha ya Wananchi kwa kukosa maji au kutumia maji yaliyochafuliwa na zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kishapu linakabiliwa na hali ya kuenea kwa hali ya jangwa na ukame. Hivyo, hata upandaji miti unakabiliwa na tatizo la upatikanaji maji. Hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais isaidie suala la upatikanaji maji katika Jimbo la Kishapu, ili itusaidie kupanda miti na kuirejesha Kishapu katika hali ya kijamii. Serikali inaweza kusaidia kuungana na nguvu za Wananchi, kwa kuchimba mabwawa makubwa ambayo yatasaidia umwagiliaji wa miti na kunywesha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Kimataifa la Kilimo *(IFAD),* katika Wilaya ya Kishapu, linaendesha shughuli zake katika kijiji kimoja cha Ikoma. Ninaomba Shirika hili lipanue shughuli zake katika vijiji vingine vilivyo katika Kata ya Itilima, ambako mradi uliko, ili kupunguza tatizo la ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuondoa umaskini, kwa upande wa Wananchi wanaotegemea kilimo cha mazao ya biashara, Ofisi ya Makamu wa Rais, ihakikishe bei ya mazao ya biashara haiteremki kiasi cha kumwumiza mkulima. Bei ya mazao kama itaendelea kuwa nzuri, wakulima watalima kwa bidii na pesa watakazozipata zitawasaidia kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa uchumi duniani, hauna haki. Bei za mazao hupangwa na nchi tajiri. Jambo hili linaumiza nchi maskini. Utafutwe utaratibu mzuri kwa kutumia vyombo vilivyopo *AU, SADC,* Jumuiya ya Afrika Mashariki na *UNO,* kuhakikisha haki inatendeka katika suala zima la bei za mazao duniani. Wajibu wa kila Mtanzania kufanya kazi kwa bidii, utalisaidia Taifa letu kupunguza au kuondoa kabisa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Muungano. Muungano huu wa Tanzania ni wa nchi mbili, yaani Tanganyika na Zanzibar. Hivyo, ni vyema ikaeleweka kuwa kila upande una haki sawa kwa masuala yanayohusu Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi hasa kutoka kwa Wananchi wa Zanzibar kwamba, Zanzibar imekuwa haifaidiki ipasavyo kutokana na mapato ya Muungano. Ni vyema basi Serikali ikaliangalia suala hili kwa umuhimu wake, ili kama si kuondoa kabisa, basi angalau kupunguza kwa kiasi kikubwa

malalamiko hayo.  Hili likifanyika, litaimarisha kwa kiasi kikubwa Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali za kuondoa umaskini, bado hali ya umaskini ni ya kutosha katika nchi yetu.  Asilimia kubwa ya Watanzania hasa vijana, bado wako katika dimbwi kubwa la umaskini.  Naishauri Serikali kupitia Ofisi hii, kubuni mikakati madhubuti ya kuwashirikisha vijana katika sekta binafsi ili kwa kiasi fulani kupunguza ukosefu wa ajira, ambao utapunguza umaskini.  Pia naishauri Serikali kupitia Ofisi hii, kutoa kipaumbele kwa Mikoa na Wilaya zilizokithiri kwa umaskini kama Mikoa ya Kisiwani Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwapongeza *TASAF,* kwa juhudi zao za kuwapatia huduma ya maji Jimboni kwangu Ziwani katika Kijiji cha Wesha. Naomba sasa waangalie tatizo sugu la maji katika Kijiji cha Kukuchuni katika Jimbo la Ziwani.  Hali ya maji katika kijiji hiki ni mbaya sana kiasi cha watu kutumia maji ya mto, ambayo ni machafu na ni hatari kwa afya ya binadamu.  Naomba *TASAF* waende kijijini hapo ili wakaone hali halisi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafi wa mazingira ni jambo muhimu sana.  Utupwaji ovyo wa mifuko ya plastiki, unachafua kwa kiasi kikubwa usafi wa mazingira.  Naishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kuandaa mpango kamambe wa kupambana na utupwaji wa mifuko ya plastiki.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:**  Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Ofisi yake mbele yetu kwa ufasaha zaidi na kuonyesha nia na azma ya Serikali katika kushughulikia matatizo ya Wananchi ambao ndi wadau wakubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Wananchi wetu kwa kweli ni duni sana na wanahitaji kusaidiwa kwa njia moja au nyingine ili waweze kupunguza umaskini miongoni mwao, kwani kusema kuondoa kabisa umaskini, si suala la mchezo.  Kwani tunaelewa uwezo wetu katika Serikali kuwa ni mdogo.  Lakini pamoja na hayo, iko haja ukawepo mtazamo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *TASAF,* mpaka sasa kwa kusikia na kuona utendaji wake, unaendelea vizuri sana hapa nchini.  Lakini jambo la kusikitisha, ni baadhi ya majimbo fulani tu ndiyo yaliyofaidika na mfuko huo.  Kwani ndani ya Jang'ombe, bado tunausikia tu mfuko huo na kwa kuwa hivi sasa nasikia *TASAF* inaingia katika awamu ya pili, basi ningelishauri Mfuko huo sasa utusaidie sisi ambao kwa awamu ya kwanza hatujafaidika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mazingira katika nchi yetu siyo nzuri na hii inatokana na sisi wenyewe Wananchi kuyaharibu mazingira yetu kwa kufanya uchafuzi wa makusudi katika maeneo yetu tunayoishi kwa kutupa taka ovyo na kwa kuzagaa kwa mifuko ya plastiki nchi nzima, kiasi ambacho hujui umlaumu nani kati ya Serikali na

Wananchi, kwani Serikali bado haijaona athari ya mifuko ya plastiki, kwani hadi hii leo inaendelea kutoza kodi na Wananchi bado wanaendelea kuitupa ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. REMIDIUS EDINGTON KISSASSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzipongeza Ofisi hizi mbili kwa kazi nzuri zinazofanywa, ili kupunguza umaskini katika nchi yetu. Pamoja na hayo, napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *project write-up formats.*Napenda kupendekeza kuwa ni vizuri zikatengenezwa *standard formats* za kujaza/kuandika na kuombea miradi kutoka katika mifuko iliyopo katika Ofisi hii hasa *SELF* na *TASAF.* Hii itapunguza urasimu wa baadhi ya maeneo/majimbo kukosa mikopo hii ya nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Chumvi - Chukwani. Ninasikitika sana kuwa kwa kipindi cha miaka mine sasa mfululizo, mradi huu umeshindwa kuendelezwa kwa sababu mbalimbali, pamoja na jitihada zangu za kuonana na Viongozi wa Ofisi hii, *NIGP* na Wizara ya Fedha. Kwa vile sijaridhika na namna mradi huu unavyoendeshwa, basi nakusudia kutoa Shilingi wakati muafaka utakapowadia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Mfuko wa *SELF* haujajitangaza vyema Zanzibar na taratibu na uendeshwaji wake bado haueleweki. Nashauri waje kutufanyia semina Zanzibar ili tuuelewe na tuweze kunufaika nao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naupongeza sana Mfuko wa TASAF, umejibeba vizuri na unaeleweka kwa wananchi na viongozi wengi Zanzibar, na wengi tumenufaika nao. Napendekeza baadhi ya miradi ya Serikali zetu mbili, ambayo inawagusa wanajamii moja kwa moja, iibuliwe kwa mtindo wa TASAF, yaani shirikishi jamii. Viongozi wengi tunaufurahia mfuko huu, ingawa baadhi ya wakati kuna ukorofi wa baadhi ya viongozi kutaka kuchelewesha baadhi ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu na nangojea majibu muafaka. Ahsante.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina pingamizi na hotuba hii hata kidogo, ila nina machache tu ambayo ninahitaji kuyasemea na kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na mambo ya Muungano kwa kusema kuwa, Muungano wetu uzidi kudumu kwa amani na upendo, ila kasoro zilizomo ndani ya Muungano huo ni vyema zikaliwe kitako kwa ajili ya kurekebishwa kasoro hizo ambazo ni kero kubwa kwa Watanzania. Muungano ni makubaliano ya nchi mbili mbalimbali ambazo ni Zanzibar na Tanganyika. Waasisi wetu wakakaa na kukubaliana uwe wa miaka mingapi ya kuanzia kwa Muungano wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mfuko wa pamoja wa fedha, ni vyema nao pia uwe na uwiano wa Wajumbe katika mfuko huo wa pamoja. Pia ningependa kujua nani ana dhamana ya kulipa iwapo moja kati ya Serikali, itakopa fedha hizo. Kwa mfano, Serikali ya Zanzibar ikikopa fedha hizo kutoka mfuko wa pamoja, nani ana jukumu la kurudisha deni hilo, ni Serikali ya Muungano au Serikali ya Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais huko Zanzibar, ni vyema iwepo tena katika kipindi hiki kifupi kabla ya mwaka 2005, kwa sababu Muungano kwa sasa hivi una umri mkubwa wa miaka 40. Kwa hiyo, kutokuwepo kwa Ofisi hiyo huko Zanzibar, ni kuwa tumechelewa kuwepo kwa Ofisi hiyo huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi za Wabunge wa Zanzibar kuwa tutapewa ofisi hizo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar. Jambo hili la kupewa Ofisi na Kiongozi huyo, basi ni ndoto tu. Wabunge kutoka Zanzibar, hawawezi kupata Ofisi hizo kwa sababu ya hali ya uchumi huko Zanzibar na ukata wa fedha Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu UKIMWI. UKIMWI ni balaa kuliko balaa na UKIMWI pia hata wageni wanausambaza sana. Kwa hiyo, wageni ambao watahitaji kuingia nchini, basi kwanza wapimwe afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi nzuri na kubwa wanazozifanya katika shughuli za hifadhi ya mazingira, kuondoa umaskini na kudumisha Muungano wetu. Hata hivyo, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa *TASAF*. Programu ya kuondoa umaskini kupitia Mfuko wa *TASAF,* ni moja ya hatua kubwa na inayoleta manufaa makubwa nchini. Inatia moyo kuwa mpango huu mwaka 2005 utafika katika Wilaya zote nchini. Pongezi sana. Hata hivyo, *cut off point* kwa *TASAF, phase I* badala ya kuwa Oktober, 2004, iwe Desemba, 2004. Hii itatoa nafasi nzuri kwa Wananchi husika kukamilisha miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa *SELF,* huu ni mpango mwingine wenye umuhimu mkubwa katika kusaidia Wananchi kupata mitaji kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali. Wilaya ya Manyoni imo katika mpango huu, lakini haijaanza kunufaika kwa kuwa haikuwepo *a local NGO* ya kuendesha Mfuko huu Wilayani Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Shirika la SHIVU la Singida limekubali kuhudumia pia Wilaya ya Manyoni, Shirika hili limekwisha pata Wanachama Wilayani Manyoni, limepata Ofisi pale Manyoni na limepata Afisa wa kuendesha shughuli Wilayani Manyoni. Lakini pamoja na kutimiza masharti yote, bado fedha kwa ajili ya Manyoni hazijatolewa. Kwa nini? Tunaomba sana kuwa zile Wilaya zilizochelewa

kupata manufaa ya *SELF* kama Manyoni, pale zinapotimiza masharti zianze kupata manufaa hayo mapema bila ucheleweshaji mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema tena kuwa, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2004/2005 katika masuala ya mazingira na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi na kwa niaba yangu mimi mwenyewe, natoa kwa masikitiko makubwa sana, salamu za rambirambi kwa familia, rafiki na Wananchi wa Majimbo ya Ulanga Mashariki na Mbeya Vijijini, kwa misiba ya wenzetu waliotoka wakati wa kikao hiki cha Bunge la Bajeti, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Hotuba hii siyo tu imegusa masuala yanayohusu maisha, mazingira na mwelekeo wa Wananchi wa Taifa letu, bali uhusiano wa binadamu na ulimwengu wake. Kusema kweli Tanzania inahitaji dhamira ya uhakika katika kulinda mazingira na kupambana na umaskini wa mali na pia umaskini wa akili. Ni muhimu kuwa Taifa letu lionyeshe kwa dhati kabisa mikakati ya kulinda au kuhifadhi mazingira Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi kwa sasa Ofisi ya Makamu wa Rais, iendelee kulenga maeneo mbalimbali ya kulinda/kuhifadhi mazingira na kupambana na umaskini, pasipo kuweka wazi mikakati na mipango inayomulika Taifa zima katika kila sekta na jamii na hasa katika maeneo yote kikamilifu *(comprehensive national plan and strategy approach for environmental protection and poverty elimination).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa suala la Hifadhi ya Mazingira linalenga maeneo machache ambayo yana umaarufu kiuchumi na kimaendeleo kama vile mito mikubwa, milima na mabonde makubwa, maziwa makubwa na pwani za bahari. Kwa sasa maeneo yanayoathirika na uharibifu wa mazingira ni yale ya ukame, mimomonyoko ya udongo, maeneo yanayoanza kuwa majangwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuelekeza juhudi za kuondoa umaskini kwenye maeneo, Mikoa na Wilaya ambazo zina unafuu kimaendeleo na kutelekeza kabisa maeneo, Mikoa na Wilaya zenye umaskini uliokithiri hasa mikoa ya ukame kama Singida, Dodoma, Tabora, Shinyanga, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama mipango ya maendeleo kiuchumi na kijamii, Mikoa hii niliyoitaja imetelekezwa kabisa, kwani hata katika kuelekeza misaada na fedha za bajeti za Serikali, Mikoa hii haipewi upendeleo maalum. Kwa mfano, utazame miundombinu kama barabara, viwanja vya ndege, madaraja, huduma za afya, elimu, usalama; vyote huwezi kulinganisha na Mikoa, Wilaya na vijiji vya maeneo ambayo Serikali na Mashirika *(NGOs),* yanaendelea kumwaga misaada ya kila namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza umaskini uliokithiri, ni kwenye maeneo yenye uharibifu mkubwa wa mazingira, ambao sasa maeneo haya yanazidi kuharibika kimazingira. Mahali pote duniani, inapoonekana kuwa hali ya mazingira na umaskini uliokithiri, ni kawaida kabisa Serikali yoyote kuona umuhimu wa kutoa upendeleo maalum katika kugawa rasilimali na mikakati katika kupambana na umaskini na kuhifadhi mazingira. Kwa sasa Serikali ione wazi kuwa maeneo au mikoa na wilaya zilizoathirika na umaskini na uharibifu wa mazingira, yapewe upendeleo maalum katika kuelekeza mikakati na rasilimali kibajeti na kisera kusudi kulinda na kuokoa kimaendeleo, kiuchumi na kijamii kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi; na isitishe kumwaga au kuelekeza/kuzidisha maendeleo kwenye maeneo/mikoa iliyokwishaendelea na inazidi kuendelea at the expenses of poverty-stricken regions/districts/villages of this nation.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni yetu wote na wote tunalazimika kuona umuhimu wa kuhakikisha kuwa Mikoa/Wilaya/Vijiji vyote vipate maendeleo, kutokomeza umaskini wa mali na akili na tuhifadhi mazingira. Sera ya Taifa iwe kuipa upendeleo maalum Mikoa/Wilaya/Vijiji vyenye umaskini mkubwa/uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Kuondoa Umaskini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali), Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Makatibu Wakuu na Watendaji wote, walioshiriki katika kuandaa mpango wa bajeti hii yenye mwelekeo wa kuleta maendeleo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, napenda nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada na mikakati kwa maeneo mengi katika utekelezaji wa Sera na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, napenda nitoe ushauri na mapendekezo katika maeneo kadhaa, nikianza na Sera ya Taifa ya Upandaji Miti. Pamoja na azma nzuri ya Serikali ya kuhamasisha sera hii ya upandaji miti kwa kutenga siku maalum kwa kila mwaka kuhakikisha nchi nzima inatumia siku hiyo kuwa ni siku ya upandaji miti, lakini pamekuwa hakuna mikakati endelevu kwa Wananchi chini ya usimamizi wa watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ihakikishe imekuwa na mikakati endelevu kwa Wananchi chini ya usimamizi wa watendaji, kuona kwamba, suala la kupanda miti ni la siku zote na wala si la siku moja kwa mwaka kama ilivyo sasa, wakikumbuka Agizo la Serikali lisemalo "Kata Mti Panda Mti". Ni matumaini yangu

kwamba, Serikali ikikubaliana na mimi, itakuwa imesaidia sana nchi yetu kutokumbwa na jangwa pamoja na njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Serikali itafakari kwa kina, kutafuta njia mbadala au nishati mbadala ya matumizi ya jikoni, badala ya kutumia kuni au mkaa, ambayo sasa hivi imemaliza misitu kwa kiasi kikubwa na kupoteza kabisa sura ya nchi. Kwa kuwa sasa hivi Serikali ina kasi ya kupeleka umeme hadi vijijini, naishauri Serikali ione uwezekano wa kupunguza gharama za umeme ili iweze kuwa njia mbadala ya matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwani imekuwa ikihamasisha Halmashauri zetu katika suala zima la usafi wa mazingira kwa kushindanisha Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya na kutoa zawadi kwa washindi. Naishauri Serikali ili zoezi hili liweze kuzaa matunda. Naomba Halmashauri zinazoshindwa kwa kiasi kikubwa, Watendaji pamoja na Halmashauri husika, watafutiwe kiboko cha kuwachapa ili waweze kuongeza juhudi kwa awamu inayofuata, kuliko wanavyoachwa tu bila karipio lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mazingira yetu yanachafuliwa sana na takataka zisizooza, ama mitaa kutokuwa na dampo la kuhifadhia takataka, mfano mifuko ya Rambo, chupa za plastiki za maji na hata ndoo za plastiki, naishauri Serikali itafute vyombo vingine kwa matumizi ya kila siku. Kwa mfano, vikapu vya asili vinavyotengenezwa na akina mama kwenye miradi yao ya maendeleo, vitasaidia sana kuondokana na matumizi ya mifuko hii ya plastiki, ambayo pia ni ya hatari kwa wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu kwa kuanzisha mfuko wa kukopesha Wananchi wenye nia ya kuondokana na umaskini. Kwa kuwa mfuko huu umekuwa siyo wazi sana kwa Wananchi walio wengi na kwa kuwa Wananchi sasa hivi wengi wao wanaondokana na biashara ndogo ndogo na kuanzisha miradi mkubwa, naiomba Serikali iweke Ofisi ndogo mikoani, zitakazosimamia maombi, kuhamasisha na kutoa elimu, hususan kwa akina mama, namna ya kupata mikopo kutoka mfuko huo, kuliko ilivyo sasa, kwani Ofisi yake iko mbali sana na Wananchi na kuwafanya wakate tamaa kuomba mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa, Serikali ikitumia ushauri huu, Wananchi watanufaika na Serikali yao kwa kuendesha miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipongeza Halmashauri zote, kwani zimekuwa na hifadhi ya miti ambayo inakuwa chini ya usimamizi wa Halmashauri. Naishauri Serikali kuwa hifadhi hizi za miti ziwe chini ya usimamizi/umiliki wa Serikali zetu za Vijiji ili hifadhi hizi ziwe na uangalizi wa karibu, kuliko ilivyo sasa kwa watu kukata miti ovyo kwa kuwa na vibali vya udanganyifu kwamba wameruhusiwa na Maafisa Misitu wa Halmashauri, kumbe si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naomba niungane na wenzangu kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia kwa mia. Mungu awape nguvu na mshikamano ili waweze kutekeleza au kutimiza azma yao.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninachukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wa Ofisi hii ya Makamu wa Rais, pamoja Watendaji na Wafanyakazi wote wa Ofisi hii, kwa kazi zao nzuri wanazozifanya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. Kabla sijaanza kuchangia hotuba hii, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kumteua Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyeiiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote, Viongozi mbalimbali wa Serikali, Watendaji wote na Wananchi wote wa Tanzania, kwa mashirikiano yao makubwa wanayompatia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein katika kutekeleza majukumu yake ya kazi kwa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu ni kuwa Watanzania wameona uwezo na ukweli wa Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa Taifa hili la Tanzania na kwa Watanzania wote. Ofisi hii ndiyo kiungo na mhimili mkubwa wa Muungano wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu wa mwaka 1964, haukuasisi umoja wetu, bali ulirejesha umoja wetu Watanzania. Kwa hiyo, ni vizuri kwa Watanzania wote tukalielewa hili na kuendeleza Muungano wetu kwa kuwa na umoja, amani na usalama wa nchi yetu na kwa Wananchi wote na kuondoa tofauti ndogo ndogo ambazo baadhi ya wakati huwa zinajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulifanikisha hili, ni vizuri sera iliyopitishwa na Serikali mnamo mwezi Oktoba, 2003 ya Habari na Utangazaji nchini, itumike kuwapatia Wananchi taarifa mbalimbali zinazohusiana na suala zima la Muungano wetu na umuhimu na malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii inasema kuwa, Sekta ya Habari na Utangazaji ni moja ya sekta ya huduma ya jamii nchini. Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama ilivyotamkwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 18 ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona umuhimu wa Wananchi kupata habari mbalimbali za nchi yao na viongozi wao, pamoja na jamii yote ya Watanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, suala la Muungano wetu, ni vyema sasa Wananchi wakaelimishwa juu ya Muungano wao ili kuwawezesha kuelewa vizuri zaidi suala la Muungano wetu na umuhimu wake, tofauti na unavyoelezewa vibaya na baadhi ya Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waasisi wetu walifanya kazi kubwa na ya msingi kujenga msingi muhimu wa umoja wa Taifa letu na Wananchi wote wa Taifa hili bila ya kuwepo ubaguzi wa rangi, jinsia, majimbo, ukabila, udini na maeneo, jambo ambalo ndani ya miaka ya hivi karibuni yalianza kujitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Ni vizuri Watanzania kuendelea na umoja wetu, amani na upendo ambao ndiyo misingi sahihi ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika suala zima la Muungano wetu, hatuwezi kupata maendeleo ya kweli kama hatutaimarisha umoja, amani na usalama hapa nchini petu, pamoja na kuondoa tofauti ambazo zinaonyesha kujitokeza miongoni mwetu sisi Watanzania wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimnukuu Mheshimiwa Rais katika hotuba yake aliyoitoa Uwanja wa Amani Zanzibar, tarehe 26 Aprili, 2004, alisema kuwa: "Niliapa kulinda Katiba ya Nchi, Katiba isemayo wazi kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Taifa moja huru na lenye muundo wa Serikali mbili. Ninawajibika kwa dhati kuutetea na kuulinda Muungano huo na zaidi mimi mwenyewe ninaamini kwa dhati kuwa Muungano wetu na mfumo wake ndiyo sahihi".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa maelezo yake hayo ya msingi kabisa kwa Taifa letu hili la Tanzania na ninamwunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa, Rais atakayekuja wa Awamu ya Nne, mbali ya kuwa ataongozwa na Katiba na Sheria za nchi yetu, lakini pia maeneo haya ya hotuba ya Mheshimiwa Rais, haitakuwa vibaya akiyaelewa na kuyafuata pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaiunga mkono Serikali yetu ya Muungano, kwa uamuzi wake wa kununua magari ya aina ya *VX* na *SX* kwa matumizi ya viongozi na watendaji mbalimbali wa Serikali hapa nchini.

Nchi yetu ni kubwa na Wananchi muda wote wanahitaji huduma mbalimbali toka kwa viongozi wao wa nchi. Pia magari haya yameiwezesha Serikali yetu kuwatumikia Wananchi ipasavyo na kuweza kutawala nchi nzima bila ya kuwepo eneo au jimbo lililotengwa au lililojitawala lenyewe kama ilivyokuwa baadhi ya nchi za Kiafrika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninarudia kuiomba Serikali ya Muungano kuipatia msaada wa fedha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili iweze kunijengea barabara zangu tangu zenye urefu wa kilomita 24 tu. Barabara hizi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kutoa pongezi nyingi kwa hotuba ya Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi,

Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) na hotuba ya Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Kuondoa Umaskini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali). Kwa kuwa hotuba ni nzuri na zina mwelekeo wa matumaini, hivyo naziunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pamoja wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa ushirikiano na Nchi za Malawi na Msumbiji kwa mwaka 2003/2004, hakuna lililofanyika kwa sababu Benki ya Dunia imesimamisha kufadhili miradi yote ya mazingira katika nchi ya Malawi. Katika hali hii, Tanzania na Msumbiji tumekosa kufadhiliwa kutokana na matatizo kati ya Malawi na Benki ya Dunia. Tatizo hili litaendelea hadi lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa, huu ni mwaka wa kumi, Mradi huu unabaki katika makaratasi au mpango usiotekelezeka. Naomba Mheshimiwa Waziri, aelezee hatima ya Mradi huu. Kama hauwezi kutekelezeka, basi hakuna amradi wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mradi wowote umebuniwa nchi hii Wilaya ya Mbinga ikaingia katika awamu ya kwanza. Mara zote inapangwa mipango katika awamu ya tatu, ya nne au awamu ya mwisho, wakati mradi unafutwa. Hali hii itaendelea hadi lini? Kwa nini Wananchi wa Wilaya ya Mbinga wanakuwa watazamaji au wasindikizaji wa miradi yote ya maendeleo kama umeme, maji, kilimo, *TASAF* na mingineyo, kama miradi ya mabonde ya maziwa (Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu *TASAF* itaingia lini Mbinga? Wananchi wa Mbinga wanapenda kufahamu ni lini miradi ya *TASAF* itawafikia? Ahsante sana.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kutamka kwamba, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, naomba kuchangia kama ifuatavyo katika eneo linalohusu mazingira:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa idadi ya ongezeko la Watanzania linaongezeka kwa kasi kubwa na kwa kuwa matumizi makubwa ya nishati ya ongezeko hili la Watanzania bado litaendelea kutumia kuni, ipo haja kubwa suala la hifadhi ya misitu yetu likaangaliwa upya. Najua upo msemo wa Kata Mti Panda Mti. Mimi sikubaliani na msemo huo kwa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miti inayokatwa mara nyingi huwa na umri wa zaidi ya miaka 20. Miti hii mara nyingi hustawi sana katika vyanzo vya chemchemi za vyanzo vya mito yetu. Miti hii inapokua, mizizi yake huenda katika kina kikubwa na kufikia kwenye miamba au majabali. Mara nyingi mizizi hiyo hujenga ufa au mwanya au upenyo kwenye majabali haya na hivyo kuwezesha maji yaliyo chini ya miamba hiyo kupenya katika mianya iliyojengeka na mizizi ya miti hiyo na kuwezesha kupatikana kwa chemchemi na kuanzisha vyanzo vya mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hii, msemo unaopigiwa kelele wa Kata Mti Panda Mti, hauna mahusiano yoyote ya kuendeleza vyanzo vya mito yetu kwa sababu miti inayokatwa huwa mara nyingi ina umri wa zaidi ya miaka 20 na mti unaopandwa huwa bado haujaanza ku-*develop roots* za kuwezesha ku-*maintain* mianya iliyojengeka na miti iliyokatwa. Kwa maoni yangu, Sera ya Kata Mti Panda Mti, itapelekea nchi yetu ikose vyanzo vya mito na hivyo kusababisha mito yetu kukauka kwa sababu mizizi ikikauka, mianya inajifunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hii ya utunzaji wa mazingira yetu, nashauri Serikali itamke kisheria miradi yote ya maendeleo, *economic cycle* yake itamke wazi kuwa katika *cycle* hiyo, *environmental impact* ya mradi huo iwe sehemu ya *economic cycle* ya mradi huo husika. Ni vizuri *assessment* yake ihusishwe kifedha ili fidia ikidhi haja ya kuwezesha kulipa fidia ipasavyo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine, nashauri Serikali ikubali katika suala hili la mazingira, mfumo wa matumizi ya *balance sheet.* Mara nyingi watu wanapozungumzia *balance sheet,* wanahusisha na mipango ya kifedha. Nashauri Serikali ikubali sasa kuanzisha matumizi ya *balance sheet* katika utunzaji wa mazingira yetu, hasa miti ya misitu yetu. Napendekeza hivyo, kwa kuwa *balance sheet* inaweza pia kutumika katika *physical accounts.* Mifano tunayo katika nchi za Norway, France, Canada na Great Britain. Matumizi ya *balance sheet* yanawezesha Serikali *at a given time,* kujua ni kiasi gani cha miti iliyokatwa na miti mingapi iliyopandwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa sina hakika kama Wizara inayohusika na mazingira, inajua idadi ya misitu tuliyonayo na sina hakika kama inajua idadi ya miti tuliyonayo na pia sina hakika kama Serikali ina utaratibu wa kujua uwiano wa ukataji wa miti na upandaji wa miti. *Introduction of balance on environment will enable our government to realize at any given time to know* idadi ya miti na misitu yetu na uendelezaji wa upandaji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Wataalam wake, kwa kutuletea hotuba nzuri ambayo kwa kiwango kikubwa imechambua Dira na Mwelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Rais, pamoja na majukumu yake. Nitachangia sehemu mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Ofisi kwa kwa jitihada zake za kuboresha kazi nzuri inayofanywa na Baraza la Mazingira *(NEMC),* katika kupambana na uchafuzi wa mazingira, hususan katika miji na uharibifu wa vyanzo vya maji, unaofanywa na wafanyabiashara na wachimba madini. Ukosefu wa sheria mama ambayo ingeliainisha majukumu ya wahusika wote katika kulinda mazingira, ikiwa ni pamoja na *NEMC,* unaifanya kazi hiyo kuwa ngumu. Kisheria, *NEMC* ni taasisi ambayo haina meno ya kisheria na hivyo kuwafanya washindwe kuwauma kisheria waharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kuwa rasimu ya sheria mama ya mazingira ifanyiwe kazi haraka ili ipitishwe Bungeni, ili ianze kufanya kazi bila kuchelewa. Kwa vile naambiwa jirani zetu katika ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kenya na Uganda tayari wanayo sheria kama hiyo. Kwa vile mazingira haya mpaka utekelezaji wa shughuli za mazingira kwa pamoja ni njia pekee ya kupata mafanikio mazuri, kama ilivyojionyesha katika suala la kupambana na magugu maji katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kero ya mifuko ya plastiki, limezungumzwa kwa muda mrefu. Lakini inaelekea Serikali inakuwa na kigugumizi katika kuchukua hatua za kusitisha utumiaji wa mifuko ya plastiki kama inavyopendekezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira. Kama kulikuwa na hoja ya kuwepo kwa mifuko ya plastiki ili kukidhi mahitaji ya Taifa, sasa nadhani sasa wakati ni muafaka wa kuchukua hatua. Hili linawezekana likienda sambamba na ufufuaji wa Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo, kiwanda hicho kitaweza kutoa malighafi kukidhi mahitaji ya viwanda vinavyotengeneza mifuko. Inawezekana wahusika watakiwe kuelekeza viwanda vyao huko, pengine kwa kubadili mifuko ya viwanda vyao ili waweze kutumia malighafi hii isiyo na athari kwa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa *TASAF* umekuwa na mafanikio makubwa ya kuleta maendeleo ambayo kwa kweli yanalenga katika kupunguza makali ya umaskini uliokithiri. Kusuasua kwa kusambaza mfuko wa *TASAF* katika wilaya zilizobaki, kunaleta wasiwasi. Ni mwaka 2003 tu ilifanywa tathmini ya pamoja kati ya Serikali na Benki ya Dunia, wanaofadhili mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini hiyo, Benki ya Dunia ilimwaga sifa nyingi kwa mafanikio yaliyopatikana. Aidha, ilitolewa kauli kwamba, awamu ya pili ya mradi wa *TASAF,* ambayo ingelipelekea kusambazwa kwa mradi huo nchini kote kabla ya mwisho wa mwaka 2003. Lakini tangu hapo, uanzishwaji wa mradi huu katika Wilaya zilizobaki, unazidi kupigwa tarehe mpaka leo, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Waziri. Kisiasa, wacha kiuchumi, inazifanya wilaya ambazo hazina mradi huo, zimeanza kuzitazama Wilaya zilizopo kwa jicho la husuda, kwa vile wanaona wenzao wanapeta kimaendeleo wakati wao wamebaki wamegubikwa na wimbi la umaskini. Ninakubali kuwa Serikali inatoa misaada ya kifedha za bajeti katika Wilaya zote bila ubaguzi au kwa usawa, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa Wilaya zilizomo katika Mradi wa *TASAF*, zinaenda kwa kasi zaidi kwa vile fungu la fedha za Serikali linatunishwa sana na mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mfuko huu umeanzishwa au kuasisiwa kutokana na juhudi za Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, Benki ya Dunia inatumia ujanja fulani *(Buying Time),* wakisubiri ang'atuke na hivyo kupata fursa ya kusitisha Mradi kwa kudai kuwa anayefuata kuongoza Tanzania labda siyo mwadilifu. Ni lazima Serikali ichukue hatua za kufuta hisia hii mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. LAWRENCE. M. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri sana ambayo imefanyika katika kuandaa hotuba hii ambayo ni ya kina na yenye kuleta matumaini katika kukabiliana na tatizo hili la uharibifu wa mazingira katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Wataalam wake ambao wamemsaidia Waziri katika kiwango cha kuandaa hotuba hii ambayo imekidhi matazamio yetu sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kwamba, tangu Ofisi hii ianzishwe, kumekuwa na mabadiliko makubwa hapa Tanzania katika suala hili la mazingira. Wananchi sasa wako *aware* katika utunzaji wa mazingira hasa katika suala la ukataji na uchomaji wa miti na misitu. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma uko katika hali nzuri, lakini dalili za kuharibu misitu imeanza kuonekana hasa katika Wilaya ya Mbinga. Kama hatua kali hazichukuliwi hivi sasa, kwa siku za baadaye kunaweza kutokea balaa. Mheshimiwa Waziri, atafute nafasi ya kutembelea Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kushauriana namna ya kufanya ili kuikabili hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla ya kusema haya niliyo nayo, nitumie nafasi hii kwa kupongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kazi nzuri anayoifanya kulinda amani na utulivu wakati wote Mheshimiwa Rais anapokuwa nje ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri wote wawili, kwa kazi nzuri wanayoifanya wakisaidiwa na Katibu Mkuu na Watumishi wao wote. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Yapo mambo mawili yanayonikera, ambayo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri, ayatolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hatima ya kuanzisha mpango kamambe wa Hifadhi ya Bonde la Ziwa Rukwa, ikiwa ni pamoja na ziwa lenyewe la Rukwa? Kulikuwa na wazo la Serikali la kuiomba Serikali ya Italia kuandaa mpango huo. Eneo hili karibu litakuwa ni jangwa kutokana na utitiri wa mifugo. Ziwa nalo karibu litakauka kutokana na *silting* inayosababishwa na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, aweke kipaumbele cha kuona namna ya kuendeleza jitihada za Baba wa Taifa katika kufanya Mji Mdogo wa Butiama na vitongoji vyake katika suala zima la Hifadhi ya Mazingira. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere alikuwa mfano wa dunia katika suala zima la kutetea hifadhi ya mazingira. Kwa nini Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, pamoja na heshima ya kuwa Rais wa Mazingira Duniani, asitafute njia kokote duniani, kumuenzi Baba wa Taifa kwa kukifanyia yale Mwalimu aliyoyaenzi kijijini Butiama!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, aliahidi kukisaidia kijiji hicho. Kila Wizara ingemsaidia Rais kutekeleza azma hiyo ya Rais kwa heshima ya Baba wa Taifa. Hili linanisononesha na ninaomba Waziri aendelee kulisimamia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba pia Mheshimiwa Waziri anayehusika na *TASAF,* anihakikishie kama Halmashauri za Miji, ambazo zote zina vijiji vinavyozunguka miji. Naomba hilo kwa sababu kila mara miradi ya Wilaya inasahau kuwa miji yetu pamoja na Dar es Salaam, ina vijiji ambavyo havifaidi matunda ya Jiji halisi, kutokana na umbali wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado namwomba Mheshimiwa Waziri, aweke bayana sheria inayotoa madaraka ya kuadhibu na kukemea kwa chombo cha Taifa cha Hifadhi ya Mazingira *(NEMC).* Niliomba mwaka 2003 kuwa kama *NEMC* hawawezi kukemea na kuwachukulia hatua wanaotuharibia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na kumwombea Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kama Rais wa Mazingira Duniani, aitumie vyema nafasi yake hiyo kwa manufaa ya Watanzania.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, kwa hotuba nzuri ambazo wamezitoa asubuhi hii. Nawaunga mkono na ninawatakia kila la kheri na fanaka katika utekelezaji wa Sera na Ilani ya CCM ya 2000 na *vision* ya kupambana na umaskini na kuuondoa ifikapo 2025.

Aidha, nachukua fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kuhusu ombi la Siha kwa Ofisi ya Makamu wa Rais la kutusaidia kumpata mhisani au wahisani ambao watatusaidia katika suala la kukarabati mazingira yetu ambayo yameharibika sana na hivyo kuhatarisha hata upatikanaji wa maji. Kama nilivyouliza hapa Bungeni na kuainisha katika hotuba yangu, Siha inakaribia kugeuka jangwa kama hatua mahsusi hazitachukuliwa kwa kupanda miti hasa kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeandaa *write-up* kama nilivyoongea na Mheshimiwa Ntagazwa na nitaomba nimkabidhi ili aone namna anavyoweza kutusaidia katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Kwa heshima kubwa, naunga mkono hoja hii. Asante.

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza kuhusu *TASAF.* Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuanzisha Mfuko huu wa *TASAF* kwa baadhi ya majimbo. Kitu nilichokiona kina upungufu katika Mradi huu ni kwamba, una ubaguzi sana. Kwamba, fedha za Mradi zinatolewa kwa Wabunge wa Majimbo tu, Wabunge wa Viti

Maalum wamesahauliwa kabisa. Wanawake pia wanahitaji kusaidiwa ili wapate maendeleo na waondokane na umaskini. Ofisi ya Waziri Mkuu inashughulikia mambo ya kuondoa umaskini, lakini panapotolewa fedha, wanawake wanasahauliwa kabisa. Umaskini utakwisha vipi kwenye upande wa wanawake? Naomba sana Mradi huu wa *TASAF* ufikirie sana wanawake. Wabunge Wanawake tunahitaji hizi fedha ili tuwasaidie wanawake waliokuwepo kwenye majimbo yetu.

Hoja ya pili ningependa kuzungumzia kuhusu mazingira. Miji yetu imechafuka sana, utaona takataka zimejaa ovyo hasa kwenye miji mikubwa. Mifuko ya plastiki inachafua sana mazingira. Ombi langu ni kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu ishirikiane na Halmashauri za Miji kuiweka miji yetu mikuu iwe katika hali ya usafi ili tuepukane na maradhi ya milipuko ya kipindupindu, kuhara na kuhara damu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Waziri na Wataalam wake, kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Haya ambayo yameandikwa yakifuatiliwa na kutekelezwa vizuri, ni mategemeo yetu kwamba, mambo yataenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia tatizo kubwa la kuzagaa kwa mifuko ya plastiki. Mimi ninatoka Wilaya ya Kilolo (Iringa), iliyopo katika barabara kuu ya Tanzania/Zambia. Hivyo, kandokando ya barabara hiyo, kumezagaa sana mifuko ya plastiki ambayo inasababisha vifo vingi vya wanyama, yaani ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kama lisipovaliwa njuga, kuna hatari kubwa inakuja. Nitaomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anajibu hoja za Wabunge, alitolee ufumbuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mweyekiti, ninaomba nitoe pongezi kubwa kwa kazi kubwa inayofanywa na *TASAF*. Kazi iliyofanyika ni kubwa sana na hii ndiyo pekee ambayo itasaidia sana kupunguza makali ya umaskini. Lakini Kilolo au Iringa, *TASAF* wana tatizo la gari. Je, ni lini gari litapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa mawasilisho mazuri katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu umuhimu wa matumizi ya *Biotechnology* kwenye juhudi za kupambana na umaskini kupitia Kilimo. Bado Wizara ya Sayangi na Teknolojia hawajatoa Sera ya *biotechnology* na matumizi yote ya *genetic engineering* kwa kuzingatia *Biosafety Frameworks* ambazo kwa sasa Ofisi ya Makamu wa Rais inazifanyia kazi.

Wakazi wa Mbeya kwa mfano, wanataka kulima *Bt. Cotton,* lakini hapa nchini mwetu bado hatuna sera wala sheria wala taratibu zinazohusiana na matumizi ya sayansi hii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, wanaoshirikiana kuongoza Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa unadhifu na maendeleo ya hali ya juu. Hali kadhalika, nawapongeza Makatibu Wakuu, Watendaji wote nchini, kwa ushirikiano wa kikazi hadi Mawaziri wanapata nguvu ya kuongoza kwa maendeleo. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa upande wa *NGOs* na *SACCOS.* Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, aweke utaratibu wa kudumu wa kuzielimisha ili zielewe jinsi ya kuendeleza miradi yao ambayo kwa sasa mingi inalegalega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, namwomba aweke utaratibu wa kufanya tathmini ya ziara tulizofanya Kamati ya Mazingira na Kuondoa Umaskini, ili kuona tunarekebishaje yale tuliyoyaona na kuyaleta Wizarani. Kwa mfano, masuala ya vyura na magugu maji kwenye Maziwa ya Jipe, Victoria na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono tena hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ndiye alikuwa msemaji wetu wa mwisho, kama nilivyosema waliohusika leo ni wale tu waliochangia mara moja. Kwa hiyo, utakuta wengine mliomba hapa na hakuna aliyepewa zaidi ya yule aliyechangia mara moja. Kwa hiyo, naomba sasa Mawaziri waanze kujibu. Namwita Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, nasimama mbele yako ili niseme kwamba, ningependa na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge walionitangulia, kutoa rambi rambi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu wawili waliotuaga hivi karibuni hapa Dodoma, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego. Pia ningependa nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na watoto wao na pia wale ambao wamefiwa na wazazi wao. Wote hao nasema waliotangulia mbele ya haki nasema, Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nasimama hapa ili niungane na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri mwenzangu, katika hoja hii ya ubia na namwunga mkono kwa yale ambayo ameyasema kwa niaba yetu sote na yeye atachukua

nafasi ya kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa kusema hapa Bungeni, pamoja na wale ambao wametoa michango yao kwa maandishi. Niseme tu kwa ujumla kwamba, nitaungana na Waziri mwenzangu na Wataalamu wetu, Katibu Mkuu Mwandamizi, katika kuzifanyia kazi hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi kwamba, asubuhi pengine watu walikuwa hawajaamka sawasawa, lakini michango ya jioni hii imeleta changamoto kubwa sana na hasa kwa jinsi walivyochangamka zaidi wakiongozwa na dada yangu, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitakwenda moja kwa moja kwenye sekta ambayo ninaisimamia, nayo ni kuondoa umaskini, halafu shughuli za vyama au taasisi hizi za *NGOs* na ndani ya kuondoa umaskini kuna mifuko hii ya kuondoa umaskini. Ninafurahi sana kusema kwamba, michango ya Waheshimiwa Wabunge, imetuongezea ari yetu ya kufuatilia suala zima la kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowahi kusema hapa kwamba, suala la kuondoa umaskini ni pana na sisi tunaongozwa na mkakati wa kuondoa umaskini ambao ulipitishwa mwaka 2000. Tulijiwekea vipaumbele kwa upande wa Elimu, Barabara, Utawala Bora, Kilimo, Maji, Ukimwi na afya. Hivyo, ni vipaumbele ambavyo tulijiwekea kwenye mkakati huo na hivi sasa mkakati unafikia mwisho wake. Mwisho wake ni mwezi Desemba, 2004. Kwa hiyo, yote yanayotekelezwa na Serikali yetu, Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwa inaratibu tu katika Wizara mbalimbali yanalenga katika kuondoa umaskini kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawashukuru Mawaziri ambao wametoa hotuba zao zikiwa zimeelezwa kwa kina nini kinachofanywa katika suala hili zima la kuondoa umaskini. Lakini napenda niseme kwamba, kwa hivi sasa kutokana na tuliyojifunza na utekelezaji wa nyuma, Serikali hivi sasa inatathmini ushiriki wa Wananchi na wadau wote katika uandaaji wa mkakati wa kuondoa umaskini awamu ya pili. Jambo hili ni muhimu, kwa sababu umiliki na utekelezaji wa mkakati unatakiwa uwe wa Wananchi wenyewe na Serikali yao. Maandalizi ya mkakati wa awamu ya kwanza ya mwaka 2000 na matukio yanayofanyika sasa kwa madhumuni ya kuandaa mkakati wa pili na tumewashirikisha wadau wote mkiwepo ninyi Waheshimiwa Wabunge yanalenga katika kuandaa Mkakati wa Kuondoa Umaskini wa pili. Hivi sasa kama nilivyosema, tuko kwenye mchakato wa kuandaa mkakati wa pili ambao tunategemea kuukamilisha mwishoni mwa mwaka huu wa 2004 ili uanze mwaka 2005. Tunatumia njia za mjadala, warsha, vipeperushi na kadhalika. Hivyo, ningependa nitoe tena wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kutoa mchango kwa sababu nia yetu ni kuona makosa tuliyofanya nyuma yasirudiwe ili tuweze kuboresha zaidi mkakati unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta mbalimbali ziko nje kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walivyosema, suala la umeme vijijini halipo kwenye vipaumbele. Suala la madini halipo kwenye vipaumbele na Sekta nyingine, kwa hiyo, tutatazama na tutakubaliana namna ya kufanya ili tufanye vizuri zaidi. Niseme hapa

katika mikutano mingi tunayohudhuria ya ndani na nje, kwa kweli Tanzania inasifiwa kwa kuweka mkakati wake ambao tunautekeleza mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondoa umaskini kuna umaskini wa kipato na kuna umaskini usio wa kipato. Usio wa kipato ndiyo ule unaohusu miundombinu mbalimbali. Kwa upande wa umaskini wa kipato ningeweza nikasema tu kwamba, tunayo mifuko hii ambayo imesemewa hapa. Lakini kabla ya hapo niseme tu kwa ujumla kwamba, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge ambao tangu Bunge hili lianze na hata leo wamesema kwamba, kwa kweli kuondoa umaskini ambao umekithiri zaidi vijijini lazima tulenge katika kutekeleza mradi ambao unawasaidia Wananchi wengi, asilimia 87 ya Wananchi wetu wanategemea kilimo na kwa hiyo, sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais, tunategemea sana kwamba, kilimo kikiwekewa mikakati inayofaa zaidi, ndicho kitakachokuwa ukombozi wa kumwondoa mwananchi kwenye umaskini hasa wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa maeneo mengi wanauza pamba. Pamba itamwondolea mwananchi umaskini. Kuna mazao mbalimbali, mazao ya korosho, mazao ya chai, hayo ndiyo yatakayoweza kumwondolea mwananchi umaskini na kwa hiyo, mimi ningependa nitoe mwito hapa kuanzia sisi viongozi tuwe tunaonyesha waziwazi kabisa kupenda kilimo. Mara nyingi tunazungumza tu kilimo lakini hatujakiendea kwa undani zaidi tukianzia upande wa viongozi. Naungana ana Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, asubuhi aliposema anashangaa kwa nini watu wanapiga makelele wakisikia kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana mashamba. Inawezekana kama asipolima yeye na sisi Wabunge tukaonyesha mfano, basi umaskini hautaondoka hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati fulani Rais Nyerere aliwahi kusema kwamba, kiongozi ambaye hatakuwa na shamba la mfano, mwaka huo mwaka 80 asingestahili kuchaguliwa mwaka 80. Kwa hiyo, nasema kilimo kipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mifuko ya kuondoa umaskini. Mfuko wa kwanza mmojawapo ni Mfuko wa *TASAF*. *TASAF* imesemewa na Waheshimiwa Wabunge karibu wote waliochangia. Ningependa nitoe majibu ya ujumla kwamba, *TASAF* imekuwa ikisaidia sana Wananchi kutekeleza miradi katika Wilaya 40 za Bara, Pemba na Unguja. Mfumo wa kiuendeshaji ambao umetumiwa na *TASAF* umetoa mamlaka kwa Wilaya pamoja na Ofisi ya Waziri Kiongozi kule Zanzibar, kuteua maeneo kwa vigezo vinavyokubalika kama vile uhaba wa huduma za jamii na chakula, hali duni ya maisha ya Wananchi wakilinganishwa na wenzao. Hivyo, Mfuko huu unalenga zaidi maeneo yaliyokidhi vigezo hivyo.

Maeneo yote yaliyoteuliwa kwa ajili ya kusaidiwa na Mfuko huu, huridhiwa na Kamati ya Uendeshaji ambayo Wajumbe wake ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. Kwa hiyo, kwa kuwa Wabunge ni sehemu ya jamii na viongozi wawakilishi, ni vizuri wakajihusisha zaidi katika kuibua hii miradi na kuisimamia. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, siyo maeneo yote yaliyokidhi vigezo hivyo katika zile Wilaya ambazo zilichaguliwa kutekeleza Mradi huu wa *TASAF*, yamepewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii yote ambayo inaendelea sasa hivi na kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali letu la hotuba, inatarajiwa kukamilika kabla ya awamu hii ya kwanza ya *TASAF* haijamalizika muda wake tarehe 31 Desemba, 2004. Hata hivyo, Wilaya zimehimizwa kuweka bidii kumaliza miradi yao kabla ya Oktoba, 2004 ili kutoa nafasi kutayarisha taarifa ya utekelezaji kwa ajili ya wadau wote. Aidha, awamu ya pili ya *TASAF* inatarajiwa kuanza mapema Januari, 2005. Kwa hiyo, Wilaya zote zitafaidika bila hata kuacha Wilaya moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunatazamia *TASAF* iendeshe semina kwanza kwa Waheshimiwa Wabunge wote, mara maandalizi yote ya awamu ya pili yatakapokamilika ili kueleza Mfuko wa utekelezaji na uendeshaji utakavyofanya kazi. Kwa hiyo, natazamia kikao kijacho cha Bunge tutaombe siku ambayo tutaeleza awamu ya pili. Maandalizi yake ni vitabu hivi hapa tayari vimekwishakamilika, kilichobaki ni kufanya Mkataba na *World Bank* ili malalamiko ya Wabunge kwamba, katika maeneo yao hakuna *TASAF,* yasiwepo kuanzia pale tunapoanza awamu ya pili. Sasa tutakapofika huko tutaondokana na makosa au matatizo tuliyokumbana nayo wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza na kwa yale maeneo ambayo *TASAF* haijakamilisha miradi yake aidha kwa kupungukiwa fedha au kwa matatizo mengine, tunategemea kwamba, awamu ya pili itakapoanza, miradi hiyo itakuwa imepatiwa fedha kwanza ya kumaliza miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyojitokeza kwanza Viongozi wanatofautiana wakati mwingine na matakwa ya Wananchi yanayotokana na pembuzi shirikishi jamii. Baadhi ya Viongozi kama Wananchi wanaamua mradi fulani, Kiongozi fulani kwenye Wilaya, anasema siyo mradi huu, twende mradi huu. Hiyo nayo inacheleweshа. Nautoa mwito, Waheshimiwa Wabunge, wahakikishe kwamba, ile miradi iliyochaguliwa na Wananchi wenyewe siyo na Viongozi, ndiyo ipewe pesa na itekelezwe. *(Makofi)*

Vilevile uchambuzi wa makadirio ya gharama ya pili huwa inakosewa kutokana na Watendaji wa Wilaya kutokuwa na sifa zinazotakiwa. Tutalirekebisha hilo. Tatu, uzembe katika utekelezaji unasababisha kuchelewa kukamilishwa mradi hadi bei ya vifaa vya ujenzi inapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, walivyotoa maelezo na wengine hapa kwa upande wa Zanzibar, Miradi ya *TASAF* inasimamiwa au inafuatiliwa na kuratibiwa na Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Kiongozi. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe, ni vizuri haya yaliyosemwa hapa yakafikishwa kwenye Ofisi husika ambayo inasimamia kwa upande wa Zanzibar. Ni matumaini yangu kuwa yaliyosemwa hapa kama yana ukweli na bila shaka yana ukweli, yatafanyiwa kazi. Hakuna sababu ya kuleta upendeleo. Nia ni kufikisha Mradi huu kwa Wananchi ili waondokane na umaskini. Kwa hiyo, mimi sitaingilia moja kwa moja lakini bila shaka Ofisi yangu, itatoa sehemu ya *Hansard* kumfikishia Waziri mwenzangu asikie au apate moto, sehemu ya moto uliokuwa unawaka humu ndani kuhusiana na hili la *TASAF* Zanzibar ili marekebisho husika yafanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine wa kuondoa umaskini ni *ANIGP*. Huko Zanzibar-Pemba kuna mradi wa chumvi Chukwani, pamoja na ule wa Pemba ambao unatekelezwa chini ya programu ya *ANIGP* na ilianzia Juni, 1997.

Programu hiyo imesimama kwa sababu wafadhili walisimama kutoa fedha. Lakini tumefanya mazungumzo na sasa hivi hata *UNICEF* wameonyesha nia ya kumalizia miradi hii na tayari ukamilishaji wa jengo la Ofisi lililopo Wawi Pemba umeshaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *UNICEF* imesaidia kutoa mashine ndogo ndogo za kuchanganya chumvi pamoja na kutoa mafunzo kwa wazalishaji chumvi na mradi huu utakamilishwa pindi utaratibu wa upatikanaji wa fedha utakapokamilika.

*SELF* ni Mfuko wa Kuondoa Umaskini. Lakini SELF sio ndiyo inayotoa fedha kwa wale walengwa mmoja mmoja. *SELF* ni Shirika mama tuseme kwa *SACCOS*. *SELF* inatoa fedha kwa *SIDO* na *SACCOS* mbalimbali kama ilivyoonyeshwa kwenye ukurasa wa 57 wa hotuba yetu, ambamo tumeonyesha fedha zilitolewa na *SELF* kwenye hizo asasi ambazo zinatimiza masharti katika mikoa ile ambayo tumesema iwepo hiyo Miradi ya *SELF*. Kuhusiana na maelezo kwamba riba iko juu ukitazama juu ya riba, riba kwa kweli ukilinganisha na mabenki na taasisi nyingine za fedha ambazo zinafikia mpaka asilimia 30 sisi tuko asilimia 11 tu.

Hata hivyo, tutaendelea kutazama jambo hili na kadri biashara inavyochanganya, natumaini *SELF* wanaweza kulitazama jambo hili la riba ili kuwawezesha wakopaji kupata unafuu katika Mfuko huu.

Mpaka sasa kama tulivyosema kwenye hotuba, mikoa ambayo inafaidika na *SELF* ni Singida, Dodoma, Morogoro, Pwani, Lindi na Mtwara na katika mwaka huu kwenye hotuba tumesema tunaongeza Mikoa ya Mara, Mwanza, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Ruvuma, Iringa na Mbeya.

Nia yetu baadaye tuendelee kuchukua Mikoa mingi zaidi ili kusudi jambo hili liweze kuchukua watu wengi ili waweze kufaidika katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hoja nyingi zipo kwa maandishi na natoa ahadi, nitashirikiana na Waziri mwenzangu katika kuzifanyia kazi pamoja na kutoa majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge waliotoa rai kwamba, kuna haja ya kuongeza kasi ya juhudi zetu za kushirikiana na Wananchi katika kuondoa umaskini. Lakini kama siku zote tunavyosema, umaskini lazima uondokane kwanza na Wananchi wenyewe mmoja mmoja kuuchukia umaskini, kama usipochukia umaskini sio rahisi kwa Serikali kukuondolea umaskini wako. Kazi kubwa ya Serikali ni kuweka mazingira mazuri kama hivyo, kuwa Vyama vya Kuweka na Kukopa, kuhakikisha kwamba Mabenki yanakopesha watu mbalimbali ili washughulike katika

shughuli zao za kuondokana na umaskini wa kipato. Ofisi ya Makamu wa Rais haina mfuko au fedha za kutoa kwa wanaombaji mikopo moja kwa moja. Nasema haya kwa sababu mara nyingi tunaandikiwa barua na watu mbalimbali na hata Makamu wa Rais, wakisema mimi nina mradi fulani, naomba uniongezee shilingi milioni tatu, nne, ili niondokane na umaskini. Ofisi ya Makamu wa Rais haina fedha za kutoa na kumpa mtu mmoja mmoja lakini tunayo hiyo mifuko ambayo inaweza kufikiwa kwa njia hizo tulizozieleza kwa kupitia hiyo mifuko ya kukopeshwa ili tuondokane na umaskini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za usoni ninavyoona mimi, mkakati unaokuja utajielekeza zaidi katika kuhakikisha kwamba, umaskini wa kipato ndio unapigwa vita zaidi. Tumefanya vizuri sana katika kuweka miundombinu lakini huku kwenye mfuko namna ya kumwezesha mtu aondokane na umaskini huo ndio jambo muhimu lifanyiwe kazi kubwa na ndio maana sasa hivi tunalifanyia kazi suala zima la kutambua mitaji mfu. Watu wale ambao wana nyumba nzuri mijini lakini hawatambuliwi kwa sababu hawana hatimiliki na wanasema wao hawawezi kukopeshwa kwa sababu hawatambuliwi kisheria, jambo hili kwa maelekezo ya Rais, hivi sasa linafanyiwa kazi tukitumaini kwamba, wengi ambao wananyimwa mikopo ya kujiendeleza kwa sababu tu mitaji yao haitambuliki itaweza kutambulika baada ya sheria husika na sera mbalimbali kutazamwa ili kumwezesha kila mtu anayetaka kujiondoa kwenye umaskini afanikishe azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana wote waliochangia katika sekta inayonihusu na mimi nimalizie tu kwa sababu hii ni nafasi yangu ya kwanza kabisa kikao hiki, mbali na kujibu maswali machache niliyojibu safari hii, nitoe shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano ninaopata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge katika kushughulika kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kama Mbunge wa kuanzia mwaka 1975, ningependa nitoe shukrani kwa zawadi niliyopewa hivi karibuni mimi na Mheshimiwa Jackson Mwakwetta ya begi nadhani nitaweka mle kumbukumbu zote za Bunge, nawashukuru sana kwa heshima hiyo mliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kusema kwamba, hapa Bungeni ili kudumisha Utawala Bora, ushirikiano, Wabunge wote kwa uzoefu wangu, wanatakiwa washirikiane na washauriane, hilo ni jambo muhimu sana. Hivi karibuni, kwa mimi niliyekaa muda mrefu, nimeona mambo ambayo sikuwa nayaona nyuma hususan Mbunge mmoja kumshambulia Mbunge mwingine. Hilo jambo sio la Kibunge hata kidogo. Wabunge wanatakiwa wawe pamoja ni kama wawindaji wanakwenda kuwinda pamoja lakini wewe katika kikundi cha uwindaji ukianza sasa kumzomea mwenzako uliyefuatana naye, hamtafanikiwa kuua mnyama huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mimi kama Waziri, nilishindwa kuingilia hapa Bungeni alipokuwa anasema jirani yangu Mheshimiwa Raynald Mrope kwamba, Mradi wa Mbwinji ambao nimeufanyia kazi muda mrefu na ni mradi mmojawapo wa kuondoa umaskini kwa sababu maji ni muhimu kwa Wananchi. Mradi wa Mbwinji ni mkakati mmojawapo wa kuondoa umaskini katika Wilaya ya Masasi na Nachingwea na

nimeufanyia kazi karibu miaka 25 haukufanikiwa mwaka huu umefanikiwa, namshukuru Mwenyezi Mungu. Kwa ushirikiano wa Mheshimiwa Edward Lowassa, nampongeza sana kwa jinsi alivyoshirikiana na mimi katika miaka minne iliyopita na nimemshirikisha Mheshimiwa Raynald Mrope, jirani yangu, ili watu wa Masasi wapate maji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kushuhudia nikiwa Naibu Waziri wa Maji, Bwawa la Masasi likiwa linakauka, nilikuta vyura wanakufa, kambale wanakufa, kwa hiyo, maji sio ya uhakika lakini mradi huu utawezesha Mji wa Masasi na Nachingwea kupata maji ya uhakika kwa miaka 30 ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Raynald Mrope, kama tulivyokuwa marafiki wa muda mrefu, uniunge mkono ili Wananchi wetu waondokane na kero hii ya maji. Sina matatizo naye kwa sababu kwanza, aliwahi kuwa *RDD* wangu nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi na pia shamba lake la mikorosho liko Nachingwea, hatuna matatizo. Nasema hivyo kwa sababu watu wengine walikuwa wanauliza kwani una matatizo na Mheshimiwa? Nikasema hatuna matatizo isipokuwa na yeye alikuwa anatoa hoja zake, ana hoja kwamba, Masasi Magharibi wapate maji. Katika hilo tutapeana mawazo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoa maji Mbwinji yanafika barabara kuu itokayo Mtwara kwenda Masasi na ikifika barabara kuu, bomba moja kubwa litakwenda Masasi na kwa hiyo njiani kutoka kwenye eneo hilo nilivyoambiwa na watu wa maji vijito vya Liputu, Ndanda, Mwena, Chikundi, Chigugu, Liliyo upande wa Masasi utaingiza maji kwenye bomba hilo kutunisha maji ya Mbwinji kwa upande wa Masasi na upande wa pili yatakwenda Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize kipindi hiki cha 2000 -2005 nikiwa na Mradi wa Maji Wilaya ya Nachingwea kwa sababu hiyo ni kero yangu kubwa na ni kero ya Masasi. Kwa hiyo, tutashirikiana katika suala hilo na hatuna shaka Mungu atatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na naunga mkono hoja iliyotolewa na Waziri mwenzangu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya muda kama wa nusu saa kwa mujibu wa kanuni ili nijaribu kupitia na kutoa maelezo kwa baadhi ya masuala yaliyojitokeza kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu ni dhahiri kabisa katika muda huo nilioutaja, si rahisi kutoa maelezo kwa kila hoja iliyojitokeza kwa sababu Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuzungumza wako 13, waliochangia kwa maandishi wako 46. Kwa hiyo, hata ungechukua dakika moja moja kwanza hata waliochangia kwa maandishi haitoshi kwa muda tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, niseme wakati nikiwashukuru tumepata mwongozo, mawazo ya kufanyia kazi katika kipindi chote kuanzia mafungu tunayoomba yaidhinishwe yatakapokuwa yameidhinishwa na kama tunavyosema mawazo yao na yale waliyoyataka tutawapelekea kwa maandishi. Napenda kutanguliza dibaji hiyo.

Nimesema hoja zilizojitokeza ukizihesabu moja moja nazo ziko kama 41 ambazo unaweza ukachukua muda kuzungumzia moja moja. Ndio maana nasema nitazungumzia baadhi ya zile hoja kuu zilizojitokeza na zingine tutazifanyia kazi na maelezo tutawapelekea kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwashukuru waliosema hapa Bungeni, nikianza na Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, kwa niaba yako Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Karim Said Othman, kwa niaba ya Mheshimiwa Ali Said Juma, ambaye ndiye Msemaji Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais upande wa Mazingira, Mheshimiwa Salim Omar Aali, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi, Mheshimiwa Mohammed Abduly Ally, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Hilda Ngoye na Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Mwaka Abrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Thadeus Luoga, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Bujiku Sakila. Naomba radhi kama kuna ambaye tumesahau kumtaja lakini katika majibu yetu ya maandishi kwa vyovyote majina yatatoka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hoja ziko 41 lakini ukiangalia zile zilizozungumziwa hapa kwa nguvu na kutiliwa msisitizo unaweza kusema liko suala la

Muungano, hili linahitaji kutolewa maelezo hata kama sio jawabu la matatizo yaliyopo. Vilevile limezungumziwa suala zima la mifuko ya plastiki, hili nalo ni la msingi. Pia imezungumziwa Sheria Mama ya Mazingira na suala la elimu ya mazingira kusudi tusiendelee kuharibu mazingira yetu na hivyo kuhatarisha uhai wa Taifa letu kwa maana ya kwamba, mazingira ndimo tunamofanyia shughuli zote za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Yapo mengine ambayo nitayazungumzia hapa, suala la UKIMWI, sidhani kama kuna haja ya kusisitiza kwa sababu tunafahamu ni kweli kabisa linatunyang'anya nguvu kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili suala la Muungano na napenda kusisitiza na kurejea ile nukuu iliyoko katika hotuba yetu ya Mheshimiwa Rais wetu aliposema kwamba na haya ni maelezo ya nukuu ile, maneno yangu kwamba, Muungano wowote ule na nafikiri aliwahi kutuambia hivyo Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kwa sababu sisi binadamu sio wakamilifu na Muungano huu ni wa binadamu na ni Muungano wa kisiasa, mkafika mahali mkakuta hakuna dosari au kasoro ndogo ndogo basi mnapaswa kujipongeza kwamba mnakaribia umalaika lakini kwa Muungano ambao ni wa binadamu, kisiasa kasoro ndogo ndogo hazitakosekana. Kama alivyotuasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wajibu wetu sio kuzikuza hizi kasoro ndogo ndogo ni kutafuta namna ya kuziondoa ili kudumisha Muungano wetu. Najua kinachosemwa hapa kwamba hizi dosari mbona mwaka nenda mwaka rudi haziondoki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu kwa mfano tusingekuwa tunazungumzia uchumi ambao hautoshelezi mahitaji ya Taifa letu, wala migogoro hii na kasoro ndogo ndogo zisingekuwa zinapewa umuhimu kama tunavyofanya hivi sasa, tungeweza kutekeleza na kuondosha kasoro ndogo ndogo hizi zikabaki zile kasoro zinazotokana na ubinadamu wa binadamu kama alivyoumbwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, mimi nakubali kwamba, katika Muungano wetu, zipo kasoro lakini kasoro hizi zinazungumzika na kwa utaratibu wa nchi na Taifa letu, tunao utaratibu wa kuzungumzia matatizo yetu ili kuyatafutia ufumbuzi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba, ni vizuri basi tunapokuwa tunazungumzia matatizo haya ya Muungano na hasa tunapogusia maeneo ya utekelezaji tukazingatia kwamba tatizo la msingi linatokana na hali ya uchumi wa Taifa letu sio kwamba kuna mchawi au mtu mwenye roho mbaya asiyependa kuona dosari hizi zinaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika lakini ilitolewa kauli kwamba, baadhi walikuwa katika *G55*, ndio na mimi nilikuwa katika *G55*. Lakini niseme wakati wa *G55* tulikuwa tunawasiliana na Marehemu Baba wa Taifa na tunazungumza naye na tunakunywa naye chai. Kwa hiyo, lilikuwa sio kundi ambalo halikuwa na mwelekeo na katika *G55* tulikuja kugundua kwamba, ukisema unataka Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano *virtually* unazungumzia Serikali tatu. Namshukuru sana kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni, siku moja alisema ukishakuwa na Serikali tatu utaua Muungano. Kwa hiyo, kidogo ilinisononesha kurejea *G55* lakini pengine ulimi uliteleza, sina hakika kama ilikuwa ni kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ni muhimu tukakumbushana hapa, Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo wakati ule iliyofanya utafiti na kuainisha kasoro hizi ndogo ndogo zinazoleta kero katika Muungano yapo maeneo ilisema Muungano wetu ni nchi mbili zilizoungana na tunayo Katiba ya Jamhuri ya Muungano na pia tunayo Katiba ya Zanzibar na ziko Ibara katika Katiba ya Zanzibar ambapo Tume ile ilipendekeza ili kupunguza huu utata unaozungumzwa vifungu vile virekebishwe. Kwa mfano, Katiba yetu inasema kama sheria ni ya kutumika pande zote za Muungano, Tanzania yote ikishatamka hivyo ndio imetamkwa. Katiba ya Zanzibar inasema sheria hiyo lazima kwanza ipelekwe kwenye Baraza la Wawakilishi. Sasa sijui ataipeleka nani kutoka katika Mawaziri wanaotaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano, sijui? Lakini inaendelea kusema na Baraza la Wawakilishi liridhie. Mimi sipendi niseme kwamba, ukiyasoma haya pengine unaweza kuwa na mawazo kwamba, niachie hapo. Nilitaka niseme kwamba, hakuna mtu mwenye roho mbaya ambaye hataki kuondosha hizi kero za Muungano, hili lilikuwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo linaendana na suala la Muungano, ni suala la ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Limeulizwa swali hapa Ofisi ya Makamu wa Rais iko wapi? Kikatiba inasema kutakuwa na Makamu wa Rais halafu unaweza kuzungumzia ofisi kama hizi Ofisi za Bunge, majengo haya tuliyonayo. Ni kweli tumeliona hili, kusisitiza Muungano wetu na umoja wa Taifa letu lakini tunapokuwa tunafanya jitihada hizi na hata Bunge hili Tukufu likatenga fedha, napenda niseme tu kwamba, mnapokuwa mmefanya uchunguzi wa udongo *(Soil Snalysis),* mkaanza na mipango ya kujenga mkakutwa na mambo mawili balaa la njaa katika nchi yenu, mafuriko na vitu vya namna hiyo, mpaka mkashauriwa kiusalama kwamba, msimuweke kiongozi mkuu eneo lile, hivi kama anavyosema Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, mnaenda kichwa kichwa tu na mnaendelea kujenga, si lazima mrudi nyuma kidogo ili muone mtajenga wapi kwa umoja wenu?

Hili nilifikiri nilisema hivi na nimeulizwa swali mmeshapata kiwanja? Kiwanja hatujapata lakini tutashauriana na wenzetu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, watupe kiwanja mahali ambapo wenzetu vyombo vya usalama watasema hapa panafaa kuweka ofisi na makazi ya Kiongozi Mkuu wa nchi. Kwa hiyo, ndio maana tunaomba yatakapokuja mafungu tupewe fedha kwa sababu ujenzi ni kama wanavyosema kwa Kiingereza, *Rome was not built in a day,* tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mifuko ya plastiki. Naishukuru sana Kamati ile nyingine ambayo wewe ni Mwenyekiti wake. Kwa kweli wametupa ushauri mzuri sana, wametupa agizo ambalo Serikali inalifanyia kazi. Kama tulivyosema, tunapenda kufanya uamuzi wa pamoja na tufikie hatua kwa misingi ya kisayansi. Tunaishi katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia, hatuwezi tukakurupuka tukasema basi lakini ninachopenda kusema hapa ninashukuru sana kwa Kamati yako kuona umuhimu wa kusisitiza suala hili na ili Serikali tufikie uamuzi wa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nigusie si kwamba nawahisha shughuli za Bunge kwa sababu haipo kwenye *Order Paper,* katika hotuba nilisema *insallah* kabla hatujaondoka tunaweza kupata Muswada ule wa Sheria Mama ya Mazingira. Mtaona

ndani ya Muswada ule ni jinsi gani Serikali imezingatia suala la kushughulikia mifuko ya plastiki. Katika Muswada ule mtaona adhabu kwa uchafuzi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kutupa mifuko hii ya plastiki iwe ni nyumbani kwa mtu mmoja au katika ardhi ya umma na uchafuzi wa mazingira niseme na sitaki kuchekesha ni pamoja na kwenda haja ndogo ovyo, adhabu inayopendekezwa ni kiasi kisichopungua shilingi milioni moja. Kwa hiyo, aliyesema kuwe na adhabu kali huko ndiko tunakokwenda na tunaraji tutaungwa mkono kwa dhati. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la Muungano kulikuwa na hoja kwamba, sasa hivi tuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar tuko vipi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? Ukishakubali kwamba Tanganyika na Zanzibar ziliungana kuunda Jamhuri ya Tanzania na Tanzania ni mwanachama katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, sasa namna ya kusema Zanzibar inaingia vipi, mimi nadhani unapouliza swali hili jawabu unalo labda ukatae kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la elimu, ni muhimu sana tukalisisitiza. Katika Ofisi ya Makamu wa Rais, nawashukuru kwa kuwapongeza wataalam na viongozi wetu, Katibu Mkuu Mwandamizi, Katibu Mkuu na wengine wote. Ni kweli pale pana hazina ya ujuzi katika masuala haya ya mazingira. Kwa kweli wataalam hawa wameijengea sifa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko baadhi ya mikutano ukienda utaulizwa na naomba Bunge lako liniruhusu nitaje baadhi ya watumishi, kwa mfano, unapokwenda kwenye mikutano inayohusu hifadhi ya mazingira ya Pwani na Bahari utaulizwa Dr. Ngoile yuko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda katika mikutano inayohusiana na mabadiliko ya tabia nchi *(Climate Change),* mambo haya ya *Kyoto Protocol,* ongezeko la joto katika dunia yetu linalotishia kama baadhi yenu mliona *BBC* leo asubuhi, kuendelea kuwako nchi ambazo ni visiwa kama *Maldives* kule Kusini mwa India, unapokwenda kwenye mikutano hiyo ya Kimataifa utaulizwa umefuatana na Richard Muyungi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunao wataalam na tunayo hazina ya wataalam katika nchi yetu. Tunachopaswa kumshukuru Mungu ni kwamba, tuna kiongozi pia wa Taifa letu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Viongozi Wakuu wa juu ambao wamejenga heshima na sifa ya nchi yetu. Mimi binafsi nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema asubuhi wakati natoa shukrani na niliwaambia marafiki zangu wana habari hivi kama isingekuwa sifa ya nchi ya Tanzania kule Korea nani angemjua Mheshimiwa Arcado Ntagazwa wa Nyarugusu? Ile ilikuwa ni kwa sababu ya tiketi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunayo matatizo mengi tu kwa sababu ya hali ya uchumi wetu lakini ni vizuri tukajipa moyo, yako mambo tunafanya ambayo hata

Jumuiya ya Kimataifa inatambua. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hili linapohusiana na tuliposema *NEMC* nikiwataja baadhi ya watumishi lakini niseme pia katika Muswada wa Sheria Mama ya Mazingira mtaona tunapendekeza kufuta Sheria ya *NEMC* iliyopo kwa sababu tulikuwa tunaambiwa *NEMC* wana meno butu au ya plastiki au ni vibogoyo kabisa. Kuhusiana na suala la Bajeti Ndogo ya *NEMC* katika mapendekezo ya Muswada wa Sheria Mama ya Mazingira, tunapendekeza *NEMC* ifanye kazi ya udhibiti. Katika suala la mazingira kuna msemo unaofahamika Kimataifa *"Polluter Pays",* mchafua mazingira lazima alipe. Sasa katika malipo hayo kutakuwa na sehemu itakwenda *NEMC* kuongezea kile tunachowapa katika mkutano kama huu tunapopitisha vifungu. Matarajio yetu ni kwamba, hali ya *NEMC* itaimarika na watafanya kazi yao ya udhibiti na *enforcement* kama tunavyotarajia katika suala la mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia masuala ya hifadhi ya mazingira ya bahari na pwani ni pamoja na kuzingatia kilimo cha mwani alichokizungumzia Mheshimiwa Salim Omar Ali, wakati mwingine huwa wanamtania wanamwita Mrema lakini jina lake ni Mheshimiwa Salim Omar Ali. Kilimo cha mwani ni kweli kinasaidia sana kupunguza umaskini na tunapozungumzia juu ya hifadhi ya mazingira ya bahari na Pwani tunalenga kwa rasilimali hizi, zisitoweke kwa sababu ya uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magari mengi kule katika mradi wetu wa Ziwa Victoria, napenda niseme kwamba, magari yale ni kwa watenda kazi lakini tunavyo vyombo pia vya kufanya usafiri majini. Najua tunacho chombo cha kisasa ambacho kinaweza kutoka Mwanza kwenda Bukoba katika muda usiozidi saa nne. Ukiondoka kwa meli zetu za kawaida unaondoka saa tatu usiku, unafika Bukoba saa kumi na mbili alfajiri. Lakini sio hivyo tu, chombo kile wanasema *echo sounder,* maana kule tunajua kuna miamba na mawe, lakini chombo kile kinakuonyesha hapa chini kuna mwamba au kina cha hapa ni kiasi gani. Kwa hiyo, vyombo vya majini kwa madhumuni mahsusi ya majini vipo, lakini pia lazima tukubali mradi ule ni kwa Mikoa ya Mara, Mwanza na Kagera. Wale watumishi katika mradi ni lazima waweze kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine kuona kama shughuli zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nizungumzie suala ambalo limezungumzwa kuhusu maeneo ya madini na uchafuzi wa vyanzo vya maji. Hili nalo tutaona katika Muswada wa Sheria Mama ya Mazingira kwamba, tunasema ili uweze kutekeleza mradi lazima kwanza ifanyike tathmini ya athari kwa mazingira kwa sababu tunapozungumzia mazingira lengo kuu ni kuhakikisha kwamba, shughuli yoyote ile ya maendeleo haina hatari au kama kuna hatari, hatari ile inapunguzwa kwa mazingira yenyewe na binadamu hasa afya ya binadamu. Kwa hiyo, nalo hili tutaliona huko tunakokwenda tutakapofikia katika Muswada wa Sheria Mama ya Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengine yalikuwa yamezungumzwa, kwa mfano, hili la uchimbaji wa madini katika Bwawa la Mindu. Unaweza ukasema Milima ya Uluguru sasa hivi ni vipara. Sasa juzi nilipokuwa najibu swali la hapa Dodoma nilisema Ibara ya 27 ya Katiba yetu inatuhimiza, inasema kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano na mimi nimepiga mstari pale maliasili ya

Jamhuri ya Muungano ambayo ni pamoja na misitu na vilima vyetu na hasa safu ya Milima ya Mashariki *(Eastern Arch Mountains)* ambayo ina mradi mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na ibara ndogo ya pili ya ibara hiyo hiyo ambayo naamini inazungumzia *sustainability* ya rasilimali zetu kwa maana ya kutunza mazingira inasema watu wote wanatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja na kupiga vita aina zozote za uharibifu na ubadhirifu. Nina hakika inalenga kwenye suala la hifadhi ya mazingira. Kwa hiyo, pana haki na wajibu. Sisi tuliomo hapa wote ni viongozi. Watanzania wanatudai haki ya mazingira safi, sisi tunawajibu wa kuona kwamba ni kweli wajibu wetu ni kuwahakikishia mazingira safi na salama lakini pia na wao wana wajibu, kusudi kwa kufanya hayo mawili, haki ya kuishi katika mazingira safi itendeke. Haiwezi kuwa upande mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, si rahisi kuyajibu yote yaliyojitokeza katika michango ya Waheshimiwa Wabunge na kwa mfano, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, anasema hakusikia jina lake, nilisema kama halikusikika, tumetanguliza kuomba radhi, lakini lipo katika orodha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie hili la Tume ya Pamoja ya Fedha. Imeelezwa vizuri sana na mchangiaji na ni mwaka 2003 tu imeundwa kwa mujibu wa sheria kutekeleza Katiba. Lakini pia ningeomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu, tunapokuwa tunazungumzia suala la Tume hii kufanya kazi, pia tuone vikwazo vilivyopo kwa maana moja ile ya hali yetu ya uchumi. Lakini ningeomba pia tuisome Katiba ya Zanzibar kwa sababu ipo ibara inayosema hata kuchangia uendeshaji wa shughuli za Muungano iwepo Tume hii. Tunashukuru ipo tangu mwaka 2003 lakini uchambuzi utakaofanywa na Tume hii upelekwe kwanza Baraza la Wawakilishi ili liridhie. Mimi nina hakika nayo haya ni matatizo na pengine si madogo, basi tuyafanyie kazi halafu njia itakuwa nyeupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Waheshimiwa Wabunge watataka kutumia muda mwingi zaidi kwenye Kamati. Kwa hiyo, ni vyema tukaacha muda huo ili tujaribu kutoa maelezo kwa sababu muda wa nusu saa kujibu hoja arobaini na moja za Waheshimiwa Wabunge hamsini na tisa, uwezekano wa kufanya hivyo kwa ufanisi *within human limitations* haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hapa Bungeni kwa kusema na kwa maandishi. Lakini pia nisiwe mtovu wa fadhila, naomba nikushukuru wewe vilevile na kwa kweli nafarijika kwa sababu ni Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua mafungu haya na leo pia ni Mwenyekiti wa shughuli zetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 26 - Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration and General ... ... ... ... ...* Sh. 1,483,900,700/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia hapa kuna Ofisi ya Makamu wa Rais. Sasa kama mnataka kumnyang'anya mshahara Makamu wa Rais, tukubaliane hiki kifungu cha 26 ni Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, mtakapokuja kwenye fungu la 31 ndiyo mshahara wa Waziri. Kwa hiyo, naomba tuelewane hapo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 - *Administration and General ... ... ... ... ...* Sh. 2,430,150,900/=

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilikuwa naomba ufafanuzi. Wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumza kwanza kuhusiana na hili jina, kuita jina Mazingira na Muungano wakati hii Ofisi imeundwa kwa mujibu wa Katiba na katika Katiba ile kazi kuu ya Ofisi hii ni suala la Muungano. Nikataka Mheshimiwa Waziri, anipatie ufafanuzi ni sababu ipi ya msingi ambayo ipo hivi na katika maelezo yangu nilizungumza kwamba, hili suala la mazingira unaweza hata kuliweka Wizara ya Kilimo, Maji au kwingineko na likaenda lakini Muungano haliondoki lipo pale pale. Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niliulizia kuhusu masuala haya ya vikao vya pamoja. Mwaka 2003 alizungumzia kuhusu hivi vikao vya pamoja, akasema kwamba, utaratibu umepangwa, mwaka huu kimya, sikuliona katika hotuba yake. Sasa lile lingesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza yale matatizo ya Muungano. Sasa majibu yake anasema umaskini. Sidhani kama Tanzania ni maskini mpaka kwenye kufanya vikao, hilo siafikiani nalo. Uwezo wa kufanya vikao naamini tunao na ndani ya vikao naamini mengi yangetanzuka kuliko hata hilo tatizo la fedha ambalo Mheshimiwa Waziri amelizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tulipozungumzia hili suala la kwamba tunaingia vipi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile Jumuiya zingine nilizozitaja, hiyo haina mashaka kwamba, tunakwenda kama Taifa la Tanzania, suala la Utaifa halina matatizo. Tatizo lililopo, kuna masuala pale siyo ya Muungano, mfano, tunapokwenda kwenye suala la elimu, hivi tunategemea kitu gani tutakwenda kwenda na sura ipi? Hivi vitu

viwili vipo tofauti, tunapokwenda na suala la kilimo kama nchi za Afrika Mashariki tunakwenda kwenda nalo vipi? Kwa vyovyote itabidi lazima tuwe na sura, tunaingia pale kama Taifa moja, tunawasilisha hoja yetu katika sura mbili ambazo bado zinalenga Taifa moja? Hicho ndicho nilichokuwa nataka ufafanuzi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, anipatie ufafanuzi kwenye hayo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Muungano kuwa pamoja na suala la mazingira na anasema suala la Muungano ni la Kikatiba, nakubaliana naye. Lakini vilevile ni suala la Katiba na madaraka ya Rais kusema *portfolio* hii iwe wapi na namshukuru mchangiaji mmoja, alisema labda anayeamua yawe hivyo ndivyo. Lakini kwa hili la kwanza ni suala la Kikatiba na ni madaraka ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikutano kuzungumzia masuala ya hizi dosari, kero na matatizo ya Muungano, wataalam wetu wanakutana na wanaendelea kukutana. Ningependa nitumie mfano mmoja tu ambao ni wa dhahiri, walipokutana ngazi ya Makatibu Wakuu tulipokuwa tunazungumzia maandalizi ya Muswada wa *Marine Shipping.* Kwa hiyo, wataalam wanaendelea kukutana, wakifika mahali yakafika masuala ya ngazi ya Mawaziri wanaleta na ikizidi ngazi ya Mawaziri ikahitaji viongozi wetu Wakuu wa Taifa tunafanya hivyo, kwa hiyo, mikutano inafanyika. Kama hatukulisema katika hotuba yetu, sawa hiyo tunakiri, lakini kwa sababu halikuwa ni tatizo lililojitokeza kwamba kulikuwa na haja ya kusema wataalam wameleta jambo kwetu na tukawa hatukulizingatia. Ningependa niseme hivyo kuwa wataalam wetu wanakutana na itakapofika hatua ya Mawaziri linakuja na sisi likitushinda, tunalipeleka kwa viongozi wetu. Tutaendelea kufanya hivyo ili kudumisha Muungano wetu daima dumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala yasiyo ya Muungano yanapojadiliwa katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nakubaliana naye kama nilivyosema, tunakwenda kama Taifa la Tanzania na Taifa la Tanzania huwezi ukaiweka pembeni Zanzibar. Kwa hiyo, yale yatakayojitokeza ambayo yana sehemu ambayo si ya Muungano lakini ni ya manufaa kwa Zanzibar ambayo ni sehemu ya Tanzania, upo utaratibu wa kuyafikisha. Ningeomba niachie hapo.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nikikizungumzia kuhusiana na vikao vya pamoja, ameeleza kwamba vinafanyika. Nilitaka atufafanulie kwamba, vimefanyika mara ngapi na wapi kwa sababu taarifa tulizonazo hivi karibuni kabla ya kuja Bungeni, mwezi wa tano sisi tulifanya ziara katika ofisi mbalimbali hazipungui ofisi kumi, karibu nyingi zinalalamikia tatizo la mawasiliano. Ndio sababu hilo suala likaja hapa.

Halafu unapokuja kwenye suala la ofisi kuwa ni maamuzi ya Rais, hilo sipingani nalo, naelewa hayo ni mamlaka ya Rais kuhusu hii ofisi, lakini katika Katiba kilichotajwa ni suala lile la Muungano, Mazingira na vinginevyo, hayo ni mamlaka yake mwenyewe Rais. *Point* yangu ilipo ile ni Wizara ya Muungano na hayo mengine yanafuata, lakini sasa hapa imetangulia Mazingira, Muungano ukafuata ndiyo *point* yangu ilipo. Sasa namna ya ku-*pronounce* hilo jina ndio tatizo lilipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili suala tunapokwenda huku nje, kwa mfano, *East Africa,* upungufu uliokuwepo vile vikao vya kabla, tunapoondoka kama Tanzania tunaondoka na kitu kimoja sisi kama Taifa, tunaingia hapa na sura ipi? Si vizuri tukafika pale tukaanza huyu anasema hivi, huyu hivi, *point* yangu ipo hapo na ndiyo nataka ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mawasiliano, sioni kama lipo baina ya wataalam wetu kuhusu kuzungumzia masuala ya Muungano. Labda lipo tatizo kwamba, wataalam wetu hawaripoti kwetu sisi Wabunge, upo utaratibu wa Kiserikali, wanapokutana wataalam wawasiliane na nani. Kwa hiyo, yawezekana lipo tatizo hili la mawasiliano linavyochukuliwa kwamba waripoti kwa nani, kama tunawatarajia waripoti kwetu Waheshimiwa Wabunge au tupate taarifa, mimi nadhani kufanya kazi Kiserikali kuna utaratibu wake. Kwa hiyo, mimi sioni kama kuna tatizo la mawasiliano baina ya wataalam wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kweli ni mamlaka ya Rais kama nilivyosema na anavyokubali, lakini anapata tatizo la namna ya kutamka. Sasa jamani kama namna ya kutamka ni tatizo, basi tuangalie kinachofanyika, *what is in a name?* Maana kama tatizo ni kutamka Mazingira na Muungano au Muungano na Mazingira, sasa sijui unaweza kusema vip! kuhusu tunavyokwenda kwenye vikao vya Afrika Mashariki tunakwenda na sura ipi, tunakwenda na sura ya Kitanzania na huwa tunafanya mawasiliano kabla hatujakwenda ili tuwe na msimamo mmoja. Tunapokwenda kwenye mkutano ule tunakuwa na vikao na mimi nashukuru niseme huwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa anatuita na tunakutana ili kuweka msimamo wa pamoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, nadhani hatutafanya ubishi, tunafanya mara mbili.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kidogo tu.

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu moja naona Mheshimiwa Waziri labda amelisahau, niliuliza hivi vikao vyetu vya ndani, vile vya ushirikiano, kama tunakutana mara ngapi, lini na wapi? Hili hakunijibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani Waziri hawezi kujibu kwa sababu wanaokutana ni Wizara mbalimbali na wataalam wa Wizara mbalimbali. Hii Wizara tunayoshughulika nayo ni ya *coordination.* Kwa hiyo, kama lingekuwa limefahamika mapema basi angekuwa ame-*coordinate* na Wizara nyingine.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho, ninalo suala dogo tu. Kwa kuwa kuvuta hewa safi ni haki ya binadamu na kwa kuwa hivi sasa imezuka tabia ya watu kuchoma takataka katikati ya Miji na kuchafua hewa, kwa hiyo, watu badala ya kuvuta *oxygen* wanavuta *carbon monoxide* ambayo ni hatari sana katika maisha ya binadamu. Je, Mheshimiwa Waziri, ana maelezo gani na je, ipo sheria ya kuzuia hilo au kama hakuna mtatunga sheria ili kudhibiti hali kama hii?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaandaa sheria hiyo na itakaposomWa mara ya kwanza hapa Bungeni, sijui kunako tarehe 6, nadhani au kabla ya hapo, Mheshimiwa George Lubeleje ataona Muswada ule unajielekeza kwenye *air quality standards* ili kujihakikishia kwamba, Wananchi wetu wanavuta hewa safi na kwa viwango vya Kimataifa.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilichangia kwa maandishi mambo mawili, matatu. Lakini kwanza ningeomba tu Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi kutokana na kauli yake alipokuwa akijibu hoja mbalimbali alipozungumzia kuhusu sheria ambazo zimepitishwa na Bunge letu halafu akatoa tamko akasema sheria zile kama ni Muungano inabidi moja kwa moja na Zanzibar zitekelezwe, mimi sikatai hayo. Lakini anavyotuuliza sisi hapa Bungeni kwamba, Katiba ya Zanzibar nayo inasema ipelekwe Baraza la Wawakilishi, akasema sasa sijui niseme nini, akasema niache hapo. Sasa yeye atufafanulie tufanye nini kwa sababu ulikuwa ni wajibu wake. Naona leo Waziri alikuwa *hot*, mimi namwomba awe *cool* kama alivyokuwa Waziri Mkuu, alitujibu vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi nilichangia kuhusu ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, nadhani katika mtu aliyelifuatilia suala hili mimi ni wa kwanza kuliko wote. Tulifanya ukaguzi na wataalam wake katika jengo moja la Mji Mkongwe, wakasema halifai kwa kulikarabati kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Tukaenda tukatafuta kiwanja na mimi ndiye niliyewaongoza watu wa Zanzibar na wataalam kutoka huku, tukawaonyesha eneo la Mwanakwerekwe, tukawaona watu wa Wizara ya Zanzibar na Bara, wakaja wataalam na watu wote wanaohusika na Ofisi ya Makamu wa Rais wakakubali. Baada ya kukubali wakapelekewa barua, wakajibu kwamba, eneo wanalitaka, wakapewa hatimiliki. Cha kusikitisha fedha zilitengwa Sh. 454,699,700/= kwa ajili ya Ofisi hiyo ya Makamu wa Rais, lakini cha kusikitisha zaidi fedha za umma zimejengewa ukuta, shilingi milioni mia mbili na kitu. Halafu tunaambiwa eneo halifai! Tunaomba tupate maelezo ya kina kabisa kwa sababu kiwanja hicho tulikitafuta kwa bidii tukakikabidhi na shilingi milioni mia mbili hizi zimefanywa nini, ukuta kweli uliozungushiwa kiwanja shilingi milioni mia mbili, inashangaza! Tunataka jawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu milele hautovunjika na yeyote anayesema Muungano uvunjike, basi mimi nasema Mwenyezi Mungu atampa maradhi ya kifafa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema nchi za wenzetu viongozi wetu wa zamani, Waasisi wa Vyama na Waasisi wa nchi wanaheshimiwa sana. Mheshimiwa Abeid Amani Karume, Muasisi wa Chama, alianzisha Muungano huu na amezaliwa Kijiji cha Kiongoni, lakini inashangaza tangu kufa kwake maji yalikatika eneo la Kiongoni, Pongwe, Koani, Mwera, lakini tukajaribu kadri tuwezavyo miaka yote kupeleka Mradi wa *TASAF,* haujakubalika mpaka leo, hivi Karume leo hajulikani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza alilouliza Mheshimiwa Haroub Said Masoud na si kwamba nimehamaki, kwa kawaida wanasheria hatuhamaki ila tunasema kitu ambacho kipo kwa maandishi na sasa nitamsomea Ibara ya 132(1) ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, nanukuu: "Hakuna sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na pia ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na hii ni Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano masharti yake".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 132(2): "Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika". Sheria imetungwa hapa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, Waziri anayehusika aipeleke mbele ya Baraza la Wawakilishi, ndicho nilichokisema, sikuwa *hot* kama yeye alivyojaribu kusema. Jengo lililokuwa Mji Mkongwe ni kweli kwamba, wataalam walikwenda kuliangalia na wakakubaliana kwamba, gharama za kukarabati jengo lile achilia mbali suala zima la usalama wa Kiongozi Mkuu wa Taifa letu, ilionekana hapafai. Kuhusu kiwanja cha Mwanakwerekwe, nashukuru kwamba, wewe binafsi umepata fursa ya kufika pale na kukiona kiwanja kile. Sasa kwa maelezo ya Mheshimiwa Haroub Said Masoud ni kweli kwa sababu tunamuenzi Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pengine kulikuwa na shauku ya kupata jengo na ofisi ili kudhihirisha haya wanayoyasema Waheshimiwa Wabunge kwamba, Muungano na umoja wetu udhihirike kwa mambo kama hayo. Sasa inawezekana katika shauku ukasahau mambo fulani fulani ambayo ni ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposikia kiwanja kipo Mwanakwerekwe kabla ya kufika, nimefika pale mara tatu, nilikuwa najua ni Mwanakwerekwe kule ilipo Ofisi ya muda ya Ofisi za Bunge ambako mwaka 1984, tulijenga majengo ya maonyesho kuadhimisha miaka ishirini ya Muungano wetu. Lakini nilipokwenda kuona kumbe ni Mwanakwerekwe kwenye korongo na mafuriko. Sasa wenzetu wa usalama wakasema jamani hivi mnampenda huyu Makamu wenu wa Rais, hadhi yake na mahali hapa na hasa hasa suala la usalama, wakatuambia basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo ndiyo maelezo ya kwamba imekuwaje na kiasi cha fedha ni kweli kimetumika na kama ulivyojionea hata wewe mahali ambapo ni oevu *(wetland),* kuweka jengo si kazi ndogo. Kuna masuala ya kuondoa udongo ule chepechepe na kuweka udongo mwingine. Lakini kwa taarifa nilizonazo ni kweli fedha ya umma imetumika. Taarifa tulizonazo Ofisi ya Makamu ni shilingi milioni 110 si shilingi milioni 200, lakini ni kweli fedha zimetumika. Lakini tumeambiwa hapafai

pengine tulifanya shauku na ninashaukuru kwamba, Mheshimiwa Haroub Said Masoud anasema alihangaika na kushughulika sana kupatikana kiwanja kile. Tulikuwa na shauku hatuzingatii suala la moja la msingi na sijui kwa nini watu wa usalama hatukukumbuka kwamba wana kazi kubwa ya kufanya kwa viwanja vinavyotakiwa kujengwa majengo ya Viongozi wetu wakuu.

Napenda ninakubaliane naye kwamba, Muungano wetu hautavunjika. Ningependa ninukuu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 26 Aprili, 2004 kwamba, wale wanaofikiri Muungano utavunjika na ningependa ninukuu na ninaanza: "Kama yupo atakayefaidika kwa kuudhoofisha Muungano, achilia mbali kuvunjika, bila shaka ni yule anayefukuzia mazigazi, mimi wa Kibondo sijui neno mazigazi, lakini Zanzibar bila shaka wanalifahamu. Anayefagilia masilahi binafsi na ukubwa wa kibinafsi." Ninakubaliana naye, Muungano utadumu daima milele. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefurahi kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini bado nina utata wa jawabu la kiwanja. Kama kweli Ofisi kubwa kama ile ina wataalam wazuri, shauku gani hiyo ya kuvamia na kutumia shilingi milioni 110 pahali ambapo wanasema kwamba, hapafai kwa jengo. Mimi sikatai shilingi milioni 110 kama zimetumika, shilingi milioni mbili na shilingi milioni tatu. Lakini hao wataalam wa aina zote walifika pale shauku gani hiyo ikiwa ni hivyo watatupeleka mahali pabaya. Mimi nasema bado jawabu la Mheshimiwa Waziri, halijaniridhisha na hilo alilosema ninakubali inawezekana hapafai, lakini si kama hapafai kwa kujenga majengo, kiusalama inaweza pakawa hapafai lakini kwa nini ikafanywa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili labda ningepata nafasi kuliendeleza vizuri mradi niliokusudia mimi ni Mradi wa *TASAF*. Mchanganuo tuliufanya vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge *TASAF* ni mpya.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si mpya hiyo niliichangia

**MWENYEKITI:** Wapi?

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Hapa niliitamka hiyo.

**MWENYEKITI:** Mara hii ya mwisho ulipopewa nafasi ulizungumzia Katiba. Naomba ukae. Ulizungumzia Katiba, Ofisi ya Makamu na Muungano ndiyo mambo matatu uliyozungumza. Ukileta *TASAF* tena itakuwa si kweli.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza suala la Karume alipozaliwa Mwera na maji yalikatika mara tu baada ya kufa. Nikasema tulichanganua mchanganuo wetu kwa ajili ya Mradi wa *TASAF,* sikuwahi kumaliza nikapigiwa kengele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki yangu bado ninayo kwa mujibu wa kifungu. Sasa kama niendelee niambie kama unanikatili ninaomba radhi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana ulisema hotuba kwa hiyo, *TASAF* hukusema. Sisi tulielewa kwamba ni habari ya Muungano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA - MAJOGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema, awamu ya kwanza inakamilika mwezi Desemba, 2004 na miradi ambayo imetekelezwa ni sehemu tu ya ile ambayo ilikwishapitishwa na Wananchi. Kwa hiyo, ningependa kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hili kama nilivyosema, tutawasiliana na Ofisi ya Waziri Kiongozi Zanzibar ili ile miradi ambayo haikupata fedha katika awamu ya kwanza, iwe ya kwanza kupata fedha katika awamu ya pili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Dakika 10 zimebaki.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina moja tu, nimefurahi sana kwa jawabu zuri la Mheshimiwa Waziri na ninaomba tu kwa kumtukuza Marehemu Abeid Amani Karume, mchanganuo upo, Mradi wa *TASAF* anitamkie kwamba, mara tu fedha zikipatikana zitapelekwa huko Kiongoni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani hilo tumeambiwa wote kwamba, miradi ile ambayo haikuwepo katika awamu ya pili kila mahali patapewa mradi na pale ambapo ilianza wataanzia huko kwanza. Nadhani nilielewa hivyo.

Kwa mujibu wa kanuni zetu, tatizo tunalokuwa nalo, ukipewa nafasi ya kuuliza bahati mbaya mnaendelea kushindana kama mara tatu, nne, kwa hiyo, mwisho wake inafika haiwezekani watu wote kumalizika kwa muda uliopo. Kwa hiyo, kwa mujibu wa kanuni hii inasema: "Kama utafika wakati wa kusimamisha shughuli za Bunge itakuwa katika Kamati ya Bunge zima au Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti atasimamisha shughuli za Kamati hiyo na kwa hiyo ataamua dakika 10 kabla kufanya *guillotine*." Labda kama mtu mmoja angesimama akaomba muda tungerudi kule juu, halafu tungeongeza muda, lakini hakuna aliyeomba. Kwa hiyo, *guillotine.*

| | |
|---|---|
| Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... | Sh. 63,911,900/= |
| Kifungu 2001 - *Union Secretariat* ... ... ... ... ... | Sh.12,051,600,500/= |
| Kifungu 3001 - *Poverty Eradication* ... ... ... ... | Sh. 1,815,240,500/= |
| Kifungu 4001 - *Non-Government Organizations* ... ... | Sh. 68,901,200/= |
| Kifungu 5001 - *Environment* ... ... ... ... ... ... | Sh. 885,307,700/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

| | |
|---|---|
| Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... | Sh. 421,699,700/= |
| Kifungu 3001 - *Poverty Eradication* ... ... ... ... | Sh. 6,952,757,700/= |
| Kifungu 5001 - *Environment* ... ... ... ... ... | Sh 3,668,614,000/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge zima, imepitia Makadirio ya Ofisi ya Makamu ya Rais, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo ya Kamati sasa ikubaliwe.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 29 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*